Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 19 Novemba, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini juu ya Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi Nchini**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana jioni wakati tunafikia kuahirisha shughuli za Bunge, Mwenyekiti hapa alikuwa ameita mtu kutoka Serikalini ili aweze ku-*respond*. Kwa hiyo, sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri M kuu, Sera, Uratibu na Bunge ili awez3e ku-*respond.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kwa niaba ya Serikali, niipongeze sana Kamati ya Nishati na Madini inayoongozwa na Mheshimiwa January Makamba, kwa kufikiria na kuazimia, Kamati hiyo iunde Kamati Ndogo ya kuchunguza juu ya sekta muhimu ya gesi.

Napenda pia nilipongeze Bunge hili na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa kuridhia uundwaji wa Kamati hii Ndogo ya Kamati ya Nishati na Madini ili ifanye kazi hii iliyoifanya ya kuchunguza, kuangalia ukweli wa Mikataba na mambo yote ambayo yanahusiana na gesi ambayo ni rasilimali kubwa hivi sasa katika nchi yetu, Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakushukuru sana wewe kwa kukubali kwa sababu Bunge lililopita tuliarifiwa rasmi kwamba Kamati ya Nishati umeipa kibali ili iweze kuchunguza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote 10 waliochangia jana. Wachangiaji 10 wamechangia kwa kirefu, lakini wametoa mchango mkubwa sana. Taarifa hii, wote tumeipata jana na sisi kama Serikali tumeipata jana. Lakini kubwa zaidi, tunakiri kwamba taarifa hii imeandikwa vizuri na ndiyo maana tunawapongeza wajumbe wa Kamati waliofanya kazi hii. Kwa sababu Serikali hii ni ya watu na sisi tumewekwa na watu na hii rasilimali ni ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka kukiri kwa niaba ya Serikali, kweli Kamati hii imefanya kazi kubwa na inawezekana kazi hiyo imeisaidia Serikali sana na imeirahisishia Serikali katika kufanya mambo fulani fulani na mengine pengine kama Serikali, imetusaidia katika kutuamsha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa niaba ya Serikali nataka kusema yafuatayo:- Kwamba sisi tunaomba Bunge lako Tukufu likubali kwamba Tunakiri kwamba tunaipokea hiyo taarifa na tunapokea yale maazimio 26 kama tulivyoyasikia wote jana, na tunaomba Bunge lako tukufu litupe muda, maana leo tukianza kumwita Waziri wa Nishati aanze kujitetea hapa kwa niaba ya Serikali, tutakuwa hatulitendei haki Bunge hili na wala hatutendi haki Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ndani mle ya ripoti kumeonekana kuna ukwepaji wa kodi ambalo ni faida kwa Serikali na ni faida kwa Umma. Kuna ukiukwaji wa mikataba, kuna ukiukwaji wa masharti. Kwa siku moja hii tusingetarajia

kwamba Serikali tuwe tumeishaipitia ile taarifa na kuifanyia uchambuzi na kuchukua hatua ambazo Kamati imependekeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu Bunge lako Tukufu likubali kwamba Serikali tunapokea yale Maazimio yote kama yalivyo na mtupe muda, twende tukayafanyie kazi, Bunge lijalo, Serikali ije itoe taarifa. Sisi hatuna matatizo, hata Bunge likiamua kujadili tena taarifa ya Serikali kuunganisha na hii, hatuna matatizo. Lakini, tunaomba tu hapa mbele yako tupokee maazimio haya, mtukubalie. Kwa sababu lengo ni hilo, wamegundua upungufu wa mikataba ambayo ilisainiwa kati ya Serikali na wawekezaji. Kwa hiyo, Serikali tunaomba tupokee hiyo taarifa ili tuje tuitolee taarifa Bunge lijalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijamalizia, nataka niseme kwamba kuna karatasi ilikuwa inaonyeshwa hapa kama *E-Mail*, bahati nzuri Mheshimiwa Mnyika alisema kuwa alitumia maneno yake kwamba ile karatasi wawekezaji wanaweza kuwa wameisambaza kwenye mtandao ili kututisha Wabunge tusijadilijadili hivi kwa sababu wametiatia na majina ya wakubwa humu. Mimi kama Serikali, nataka niseme kwamba, kwanza tunakataa ile *E-Mail*, siyo karatasi sahihi wala siyo karatasi rasmi.

Nataka niungane na Mheshimiwa Mnyika kwamba Waheshimiwa Wabunge wala msikwazwe na lolote kutokana na ile karatasi na bahati nzuri hamkukwazwa, mmejadili pamoja na yale yaliyoandikwa kwenye *E-Mail* kwamba haya maazimio tulikubaliana na Waziri Ngeleja, sijui tulikubaliana na nani, hayana maana. Ile karatasi siyo karatasi rasmi na wote hatukuipata kupitia Kamati, kuna mtu ameileta.

Kwa hiyo, nilitaka kusema tu kwamba ile karatasi siyo karatsi ya Serikali na wala Serikali hatukubali. Tunachokikubali ni taarifa ya Kamati hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba kutoa hoja!

**SPIKA:** Huna hoja! Unauunga mkono tu! Huna hoja hapa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja! Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JANUARY Y. MAKAMBA – MWENYEKITI WA KAMATI YA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nakushukuru kwa fursa ya kuhitimisha hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kutoa kibali kwa Kamati yangu kuunda Kamati Ndogo ya Kuchunguza Uendeshaji Sekta Ndogo ya Gesi. Tunashukuru kwa ofisi yako kutuwezesha tuweze kuifanya kazi hiyo kwa namna ambayo imeridhisha na kutupa muda na kutuongezea muda pale ambapo tumeomba. Kwa hiyo, tunakushukuru sana na utayari wako na *vision* yako ya kuona umuhimu wa Bunge letu kushiriki katika kurekebisha mambo yanavyoenda, ndiyo imefanya tufikie hapa tulipo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani vile vile kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii jana na naomba niwataje. Kwanza; Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Yusuph A. Nassir, Mheshimiwa Mohammed Habibu Juma Mnyaa, Mheshimiwa Charles J. P. Mwijage, Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mheshimiwa Saidi M. Mtanda, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla na Mheshimiwa John M. Shibuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Wabunge waliona, taarifa yetu ilikuwa ni ndefu, ni kubwa na bahati mbaya sana, kama alivyozungumza Waziri wa Nchi, Wabunge walipata taarifa hii wakati taarifa ndiyo inasomwa.

Tunakiri kwamba kutokana na kuipata katika muda mfupi, wasingeweza kuchangia kwa namna ambayo ingeweza kuwafanya wachangie katika namna ya kuiboresha zaidi. Na hoja za Wabunge katika kipindi cha jana cha jioni kwamba wanahitaji muda zaidi wa kuweza kuichangia, zilikuwa ni hoja sahihi na hoja za kweli.

Mheshimiwa Spika, sasa, katika maazimio yetu haya 26 ambayo tunaomba Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu liyaridhie na kuyakubali, tunapenda kuongeza vile vile Azimio la ziada kwamba Serikali itakapoleta taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati, basi Waheshimiwa Wabunge waruhusiwe au wapate fursa ya kujadili taarifa hiyo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zimejitokeza hoja nyingi jana wakati wa mchango, na nitatumia muda mfupi tu kupitia baadhi ya hoja kwa kifupi.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu nchi yetu ina rasilimali nyingi:- gesi, madini na rasilimali nyinginezo. Tumekuwa tunakosea katika kuvuna na kufaidika kwenye rasilimali hizi nyingine. Sasa Bunge lako lifike mahali, liweke, lichore mstari kwenye mchanga kwamba tumekosea huko nyuma, sasa tusikosee kwenye gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu sasa hivi ina gesi ambayo inakadiriwa kuwa futi za ujazo trilioni 1. Uchimbaji wa gesi unaendelea kwenye Bahari Kuu, baada ya miezi michache kutatokea tangazo tutasikia lingine ambalo litaongeza gesi ambayo imevumbuliwa kufikia trilioni 3 na labda tutafikia trilioni tano (50).

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nchi nyingi Duniani zinaangalia ukanda huu wa Afrika Mashariki na hasa Tanzania kwamba ndiyo sehemu mpya ya uchimbaji na utafutaji wa gesi. Iko mifano ya nchi nyingi ambazo zimekuwa na gesi, zimekuwa na rasilimali hizi, lakini ukitazama watu wake ni maskini wa kutupwa, pamoja na rasilimali zilizokuwepo.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu isikubali na sisi tufikie huko kwamba lazima tuwe tayari kitaasisi, tuwe tayari kirasilimali watu na tuwe tayari kisheria na taratibu za kuweza kunufaika na rasilimali gesi ambayo iko kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, yapo mengi kwenye ripoti yetu kama nilivyosema. Kwenye taarifa yetu kuna ambayo yanahitaji utekelezaji wa haraka na jambo kubwa hasa ni hili la uvunjaji wa mikataba kama alivyosema Waziri wa Nchi, tunawaachia waende wakayatazame, sisi tumeazimia na watakuja watatupa taarifa.

Mheshimiwa Spika, cha mwisho ambacho nataka nizungumze, kwa sababu nataka nizungumze kwa ufupi, tupate fursa ya kujadili taarifa ile nyingine, ni kwamba dhambi kubwa ambayo imefanyika kwenye suala la gesi ni kuifikisha nchi yetu mahali pa kutumia fedha nyingi za kigeni kuagiza mafuta kuweza kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme. Kwenye nchi ambayo ina gesi kama ya kwetu, ni *scandal* kubwa kwamba itakapofika Desemba mwaka huu, zaidi ya MW500 zitakuwa zinazalishwa kwa mafuta ya kuagiza nje ya nchi, kama siyo mafuta ya ndege, basi *diesel*, kama siyo *diesel*, basi mafuta mazito. Sasa, leo zinatumika karibu shilingi bilioni 2 kila siku kuzalisha umeme wa kuendeshwa kwa mafuta.

Mheshimiwa Spika, nchi yenye gesi kama hii na gesi ambayo imevumbuliwa mapema miaka ya nyuma, haiwezekani tukawa tumewakabidhi wenzetu, sisi ndiyo wenye gari, tumewakabidhi funguo, tumewakabidhi usukani, tumewakabidhi gari waendeshe wanavyotaka na hatuwezi kuwatoa, na hatuwezi kubadilisha njia kwamba piteni huku, tunataka kwenda huku, wakati rasilimali ni zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo linasikitisha sana. Kamati yetu sisi, tunashukuru kwamba Wabunge wameiona na Wabunge wenzetu mmetuunga mkono kwamba ifike mahali sasa mwelekeo tunaoenda naokwenye suala la gesi lazima tuubadilishe.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa tu kuongeza uelewa wa Wabunge, ni kwamba mradi huu, maana kampuni ni moja tu iliyokuwa inaongelewa ya *PAN-AFRICAN,* lakini kuna kampuni nyingine ambayo inafanya biashara na *PAN-AFRICAN* inaitwa *SONGAS.* Mtakumbuka kwamba kwenye miaka ya 1980, gesi ya Songosongo ndipo ilipogunduliwa.

Baada ya kugundulika, ikazibwa isitumike kwa sababu miaka ya nyuma gesi ilionekana kama haina kazi, kila mtu alikuwa anatafuta mafuta. Sasa, baada ya gesi hii kupatikana, wakaziba. Tulipoamua sasa tunataka kuitumia kutokana na ushauri wa Benki ya Dunia, akatafutwa Mwekezaji, Benki ya Dunia iliamua kuikopesha Serikali zaidi ya Dola milioni 200.

Lakini ikatoa masharti kwamba tunawakopesha hizi pesa, lakini tunataka mradi huu utekelezwe na sekta binafsi. Kwa hiyo, pesa zile zinazoendesha mradi huu wa sasa ni pesa ambazo tumekopa sisi Serikali. Kwa hiyo, ni kama wewe umekaa unaendelea na shughuli zako, anakuja mtu anakwambia Dola milioni 200 hizi, nenda katekeleze mradi huu. Na kwenye biashara ya ukopaji, kitu kikubwa ni *risk* ambayo ina-*determine interest rate*.

Sasa *risk* sisi ni ya *sovereign*, ni ya kwetu. Kwa hiyo, *interest* ni ya chini sana. Ule mradi wa ukopeshaji unaoendeshwa pale, unaendeshwa kwa fedha ambazo *risk* ni ya kwetu. Katika biashara hamna jambo tamu kama mtu anakuletea pesa na *interest* ya chini sana kwamba fanya kazi. Ni kweli wanavyozalisha wanatulipa na sisi tunalipa Benki ya Dunia. Lakini sasa, mradi huu ni wa miaka 20, unaisha mwaka 2024.

Mheshimiwa Spika, sasa wenzetu wameamua kupanua mradi huu na tumeandika kwenye taarifa yetu kwamba wanaingiza fedha Dola milioni 120 kupanua uwezo wa kuleta gesi Dar es salaam kwa kiwango cha futi za ujazo milioni 35 kwa siku. Sasa, swali la kujiuliza ni kwamba kama mradi huu una *structure* yake tayari kwamba *TANESCO* wana asilimia 9, *TPDC* wana asilimia 29 na wale *SONGAS* wana zilizobaki, ndiyo *structure* ya mwanzo ya mradi wa miaka 20 kwa fedha ambazo tumekopeshwa na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Spika, sasa mwenzenu anapoenda sekta binafsi kuomba mkopo wa Dola milioni 120, kinachotakiwa kwanza awaombe ninyi, kwamba jamani sisi tuko pamoja kwenye huu mradi, tunaenda kukopa kwenye sekta binafsi Dola milioni 120 ambayo *interest rate* yake ni kubwa zaidi kuliko mradi uliopo sasa. Tuliuliza *TPDC,* tuliwauliza *TANESCO.* Je, mlipata taarifa au mlipata maombi kwamba tunataka kwenda kukopa kwenye sekta binafsi ili tuzitie kwenye mradi huu ambao upo tayari? Majibu yao ni kwamba, hapana! Tuliwauliza Serikali.

Je, kwenye mradi huu ambao unaendeshwa kwa fedha za mkopo, anapokuja mbia anaweka pesa kutoka sekta binafsi kwa *interest rate* tofauti, *implication* yake kwa *shareholding structure* ni ipi? Je, ni mkopo kwa *partnership?* Au Je, *share* zenu zinashuka chini? Bahati mbaya watu wa Serikali walikuwa hawajalitafakari na kujua *implication* yake ni nini. Lakini wale wenyewe ambao wanaziingiza hizi fedha uelewa wao ni kwamba watakapoingiza fedha hizi kutoka sekta binafsi, ule ukubwa wa mkopo unaingia kwenye gharama za uwekezaji. Lakini, kubwa zaidi ni kwamba kunakuwa na *dilution* za *share* za Serikali, kwamba badala ya asilimia 9 za *TANESCO,* badala ya asilimia 29 za *TPDC* zinakuwa chache zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa kikubwa cha kutazama hapa ni *timing*. Huu mradi ulikuwa unatengeneza hasara. Katika miaka ya sasa, mwaka jana, mwaka huu na mwaka ujao, una-*breakeven*, unaanza kutengeneza faida. Kwa mujibu wa mkataba, ni kwamba gawio litatolewa kwa yule mwenye *share* nyingi kwanza. Sasa, unapoingiza fedha za sekta binafsi ambazo zina-*dilute share* za Serikali, maana yake ni kwamba wenzetu wametu-*time* kwamba mwaka watakaoanza kutengeneza faida, sisi tusipate kitu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunaomba wenzetu wa Serikalini kwamba haya myatazame na myajue na myazingatie.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa mchango, kwa kuikubali taarifa yetu. Tunatarajia mwezi Februari tutapata fursa tena ya kujadili kwa kina pamoja na taarifa ya Serikali kuhusu taarifa yetu. Lakini tunachosisitiza ni kwamba katika Bunge lijalo Serikali, tafadhali tafadhali, njooni na sheria ya gesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunachofahamu ni kwamba Muswada upo toka mwaka 2009 na tumeambiwa upo kwenye ofisi ya Mwanasheria Mkuu, sasa kama Muswada upo toka mwaka 2009 kwanini usiletwe Bungeni ili tupitishe Sheria hiyo, ili tuweze kuvuna rasilimali zetu kwa manufaa ya umMa.

Licha ya hivyo, sijawahi kuona nchi Duniani yenye gesi, lakini haina *Gas Master Plan.* Tanzania haina *Gas Master Plan*. Sasa zile fikra za pamoja za mkakati wa kuitumia gesi hii kwa maendeleo ya nchi hazipo. Kwa vyovyote tunaomba *Gas Master Plan* itengenezwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, lakini tunafahamu kwamba *TANESCO* inao mpango unaitwa *Power System Master Plan* toka mwaka 2009-2033, tumeambiwa na wenyewe unafanyiwa marekebisho, lakini huwezi kufanya marekebisho ya *Power System Master Plan* bila kuzingatia hali halisi ya gesi.

Kwa hiyo, tunachopendekeza cha ziada, tusisitize tu kwenye taarifa yetu ni kwamba kutengeneza G*as Master Plan* uende pamoja na hii *update* ya *Power System Master Plan*, kwa sababu hii mikakati miwili inaendana, hauwezi kutengeneza *Power System Master Plan* tofauti na *Gas Master Plan.* Kama tunayo gesi ni lazima tuondokane na kuzalisha umeme kwa mafuta na vile vyanzo vingine vya maji tuvitumie kwa wakati wa dharura.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru tena kwa fursa hii, nashukuru sana kwa kutuwezesha kufanya kazi hii, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuchangia hoja hii, naishukuru Serikali kwa kupokea maazimio haya na kuyafanyia kazi. Tunapendekeza sasa taarifa ya Serikali ije Bungeni tuijadili tena, taarifa ya Serikali ya utekelezaji wa maoni haya.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba kurudia tena kukushukuru na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya mnapaswa kuunga mkono kwa sababu hoja ni ya kwenu, lakini imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge tunachotaka kuwahoji ni kwamba yale maazimio 26 myakubali lakini mnakubali hoja kwamba katika hoja kwamba katika Mkutano wa Sita Bunge lijadili utekelezaji wa maazimio haya na Serikali na ninyi wenyewe mtakuwa tayari mmeelewa undani wa taarifa hii ya Bunge. Kwa hiyo, nitawahoji kwamba taarifa ya Serikali ya utekelezaji iweze kuwasilishwa katika Mkutano wa Sita wa Bunge hili.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Nishati juu ya Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi nchini Ilipokelewa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote mmeafiki na tunaiagiza Serikali kuchukulia taarifa hii ya Kamati ya Nishati kwamba ni kitu ambacho tunazungumzia uhai wa nchi hii, ina mambo ya kutekeleza dhahiri kama hizo *dividend* zilizochukuliwa, kuna mambo ya kisera hapa, tunategemea Serikali mtakuja na mambo ambayo Bunge litaridhia na kuagiza kwamba yaendelee kutekelezwa. Baada ya kusema haya tunaendelea.

## KAMATI TEULE YA BUNGE

### Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge Iliyoundwa Kuchunguza Uhalali wa Utaratibu wa Wizara Kuchangisha Fedha kwa Ajili ya Kupitisha Bajeti Bungeni.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI - MWENYEKITI WA KAMATI TEULE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua na kuitumia fursa hii ya mwanzo kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia sisi sote afya na uzima na kwa kutuwezesha kumudu changamoto zetu za maisha ya kila siku hii ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa shughuli zetu kama Wabunge.

Aidha, namshukuru Mungu kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wote wa Kamati Teule kwa kutuewezesha kukamilisha kazi hii ngumu na yenye changamoto kubwa na nyingi. Lakini kwa mapenzi yake ametusimamia, ametuongoza na kutuelekeza hadi kufikia hatua hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni Kamati teule ya kwanza katika Bunge la Kumi na kwamba mimi kwa niaba ya Wajumbe wenzangu nimesimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara yangu ya kwanza kabisa katika historia ya Bunge hili. Hivyo pamoja na kutambua maelekezo kwamba muda wa kupeana pongezi unapaswa kuwa umeisha rasmi, bado niombe angalau kwa sentensi niwape pongezi Viongozi wote waliopata nafasi mbalimbali za Uongozi katika Taifa letu kwa kuchaguliwa na kwa kuteuliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kutaja wachache naanza na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda Waziri Mkuu, Mheshimiwa Anne Semamba Makinda, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Waheshimiwa Wabunge wote, Mawaziri na wengineo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tatu napenda kutumia nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Wapiga kura na wananchi wote kwa ujumla wa Jimbo langu la Tunduru Kaskazini, kwa uelewa wao na uvumilivu wao wa kutambua, kuheshimu na kuthamini umuhimu wa jukumu hili nililopewa na kunikubalia nilitekeleze kwa kuwa wameweka utaifa na uzalendo kwanza na mbele.

Nawaahidi kwamba ratiba yetu ya awali kama wanavyoijua imesogea tu mbele na sasa wakati wake umefika nawaambia niko njiani nakuja.

Mheshimiwa Spika, nne na mwisho lakini siyo kwa umuhimu na kwa namna ya pekee kabisa nawashukuru na kuwapongeza Mke wangu na wanangu wote kwa uvumilivu na ushirikiano walionipa katika kipindi chote hasa kwa kukosa uwepo wangu miongoni mwao kwa muda unaokaribia nusu ya mwaka mzima tangu Bunge la Bajeti, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pongezi na shukrani nilizozitoa hapo juu pia ziende kwa familia na wananchi wa majimbo yafuatayo kwa wale ambao ni wanakamati wenzangu katika Kamati Teule hii. Kwanza ni Mheshimiwa Martha Umbulla, Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Jimbo la Karatu, Mheshimiwa Godbless Blandes, Jimbo la Karagwe na Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Jimbo la Gando. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ina kurasa 150, viambatisho *appendix 17,* na nyongeza *annex 32* ambazo ni *Hansard* za siku 32 za mahojiano na majadiliano na watu 146. viambatisho na nyongeza vitapatikana kwa utaratibu utakaowekwa isipokuwa kuwa tu kwa *appendix* ambazo mmegawiwa, Vinavyobaki havikuwa rahisi kuvileta mbele ya Bunge lako Tukufu vikiwa vimefungashwa na taarifa hii kutokana na ukubwa wa fungasho hilo kama tungevifunga pamoja. Pia kutokana na changamoto ya muda nitafanya mawasilisho tu ya taarifa hii lakini kwa ajili ya ukamilifu na usahihi wa kumbukumbu nitaomba *Hansard* irekodi taarifa nzima kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, Utangulizi> Katika Kikao cha 56 cha Mkutano wa Nne wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 26 Agosti, 2011 ukirejea Azimio la Bunge lililopitishwa katika Kikao cha 54, tarehe 24 Agosti, 2011, uliunda Kamati Teule ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni 2(2) na 117(4) za Kanuni za Bunge, Toleo la 2007.

Kamati Teule iliundwa kwa ajili ya kuchunguza uhalali wa utaratibu wa Wizara kuchangisha fedha kwa ajili ya kupitisha Bajeti na kubainisha endapo kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kutoa Taarifa kwa Waandishi wa Habari juu ya uchunguzi wa suala la fedha zilizokuwa zikichangishwa na Wizara ya Nishati na Madini kimeingilia au kuathiri Madaraka ya Bunge. Kamati Teule imekamilisha kazi hiyo na ifuatayo ni Taarifa kamili kwa mujibu wa Kanuni ya 119.

Mheshimiwa Spika, Chimbuko. Taarifa Rasmi (*Hansard*) ya Majadiliano ya Bunge ya Kikao cha 27 cha Mkutano wa Nne, tarehe 18 Julai, 2011 inaonyesha kwamba wakati wa Mjadala wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, miongoni mwa Waheshimiwa Wabunge waliopata fursa ya kuchangia ni Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, (Mbunge). Katika mchango wake, pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, (Mbunge) aliweka Mezani kwa Spika kivuli cha barua aliyoitolea maelezo kama ifuatavyo:-

Kwamba barua hiyo ilisainiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu David Kitundu Jairo, ilielekezwa kwa Wakuu wa Taasisi, Vitengo na Idara zilizo chini ya Wizara kuwataka wachangie kufanikisha mawasilisho ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara Bungeni.

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mbunge, alisema kuwa anadhani fedha hizo zinazidi Sh.1,000,000,000.00 kwa hiyo akahoji zimekwenda wapi wakati kwa utafiti alioufanya Taasisi zimejigharamia zenyewe katika ushiriki wake zoezi la Bajeti ya Wizara Bungeni Dodoma.

Aidha, alihoji ukusanyaji wa fedha nyingi kiasi hicho na kupelekwa kwenye akaunti ya Taasisi ya GST iliyoko chini ya Wizara na ambayo Makao yake ni Dodoma. Pia aliuzungumzia ukusanyaji wa fedha kiasi hicho na matumizi yake akilinganisha na changamoto kadhaa zilizoko katika Sekta ya Umeme nchini. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, (Mbunge) alitamka kusudio lake la kutaka kutoa hoja mahsusi kuhusu masuala ya umeme na changamoto zake likiwemo hili la uchangishaji, baadaye kabla Mheshimiwa Waziri hajahitimisha Hoja yake.

Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, (Mbunge) alikuwa miongoni mwa wachangiaji katika Hoja ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Katika mchango wake pamoja na mambo mengine alichangia kuhusu ukusanyaji wa Shilingi 50,000,000.00 kutoka kwa kila Idara iliyo chini ya Wizara ya Nishati na Madini na akahoji fedha hizo zilikuwa ni kwa matumizi yapi? Alielezea mashaka yake kuwa huenda umma wa Watanzania wakahusisha fedha hizo na uvumi uliokuwepo wa uwepo wa kile kilichoitwa mgao wa fedha usiokuwa rasmi.

Mheshimiwa Ole-Sendeka naye alishtushwa na kiwango hicho cha fedha kuwa kikubwa na hasa akihoji matumizi yake. Akasisitiza kuwa Waziri Mkuu amuagize Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi wa dharura. Mheshimiwa Ole-Sendeka, aliahidi kumuunga mkono Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, wakati atakapotoa Hoja yake kuhusu masuala haya.

Mheshimiwa Spika, Kuundwa kwa Kamati Teule; Jumatano Agosti 24, 2011, kabla ya Kipindi cha Maswali, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge, aliomba Mwongozo wa Spika. Akitoa maelezo ya Mwongozo, alirejea tukio la Jumanne, Agosti 23, 2011 ambapo Katibu Mkuu Kiongozi alitoa taarifa kwa umma juu ya suala la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuchangisha fedha Taasisi zilizo chini ya Wizara yake kwa ajili ya kuwezesha maandalizi na uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara hiyo Bungeni.

Akifafanua alisema Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi inaonyesha kwa umma wa Watanzania kwamba tuhuma zilizotolewa na Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo, Mbunge wa Kilindi, dhidi ya Katibu Mkuu wa Nishati na Madini Ndugu David Kitundu Jairo, hazipo kwa kuwa hazikuweza kuthibitishwa. *(Makofi)*

Akihusisha uamuzi huo na kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge; na akirejea kauli ya Katibu Mkuu Kiongozi kuhusu uwezekano wa Wabunge kushtakiwa kwa "*defamation*", Mheshimiwa Kabwe Zitto, (Mbunge) alisema kuwa hadhi ya Bunge imeingiliwa na hivyo akatoa Hoja kwamba Bunge lisitishe kujadili Shughuli za Serikali hadi Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali itakapoletwa mbele ya Bunge ili ijadiliwe.

Mheshimiwa Kabwe Zitto, alitoa Hoja hii kwa mujibu wa Kanuni ya 51 ya Kanuni za Kudumu za Bunge inayohusu Haki za Bunge ikisomwa pamoja na Kanuni ya 55(3)(f) inayohusu Hoja ambazo zinaweza kutolewa bila taarifa ikiwemo jambo lolote linalohusiana na haki za Bunge.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa William Lukuvi, alisimama na alipopewa nafasi ya kuzungumza, pamoja na kukiri kuwa jambo hili lilivuta hisia za Umma wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, (*public interest*), alizungumzia Kanuni ya 51(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na akataka kujua kama masharti ya Kanuni hii yalizingatiwa katika kufikia Hoja hiyo kutolewa na kuungwa mkono. Mheshimiwa William Lukuvi, (Mb.) aliisoma Kanuni hiyo kama ifuatavyo:-

Nanukuu: *"Mbunge anayetaka kuwasilisha jambo ambalo anaamini linahusiana na haki za Bunge atafanya hivyo wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa Shughuli za Bunge uliowekwa na Kanuni hizi na atakuwa amemwarifu Spika mapema kuhusu kusudio lake hilo na jambo ambalo anataka kuwasilisha."* Mwisho wa kunukuu.

Akitoa majibu kwa Mheshimiwa William Lukuvi, Naibu Spika Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, alitoa maelezo kwamba wakati Kikao cha siku hiyo kinaanza alipokea taarifa fupi ya maandishi kutoka kwa Mheshimiwa Kabwe Zitto, ya kusudio la kutaka kutoa Hoja hiyo, na akasisitiza kwamba Hoja imetolewa kiutaratibu na imeungwa mkono na Wabunge wengi.

Hata hivyo, akakiri kwamba Hoja ya kuahirisha Shughuli za Bunge ni nzito na hawezi kuitolea uamuzi yeye peke yake, hivyo akawaomba Wajumbe wa Kamati ya Uongozi wakutane muda huo kwa ajili ya kujadili jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kipindi cha Maswali kumalizika, Naibu Spika alitoa taarifa ya kikao cha dharura cha Kamati ya Uongozi, ambapo pamoja na mambo mengine alisema.

Nanukuu: *"Kamati ya uongozi imepima Hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Kabwe Zitto na kuiona ni Hoja ambayo inahitaji kupata fursa ya kusikilizwa na Bunge. Kwa maana hiyo sasa namwomba Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto achukue fursa hii kutuweka sawa anasema nini kuhusu jambo hili sasa..."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Kabwe Zitto, alitoa maelezo kufafanua Hoja yake na baadaye iliungwa mkono na Wabunge wengi. Hoja hii ilichangiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, na Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu, Wakati akichangia Hoja hii Mheshimiwa Ole-Sendeka, alitumia fursa hiyo pia kutoa Hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ambapo pamoja na mambo mengine alisema.

Nanukuu: *"... Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge hili liniunge mkono kwa kutoa Hoja kwa mujibu wa Kanuni ya 117 fasili ya (1), (2) mpaka ya (4) ambayo inaweka masharti ya utaratibu wa kuundwa kwa Kamati Teule na hii itasaidia sana kuitendea haki Hoja hii na kulinda hadhi ya Bunge lako Tukufu na ndiyo maana nimesimama hapa kutoa Hoja. Naomba kutoa Hoja na naomba mniunge mkono Waheshimiwa Wabunge."* Mwisho wa kunukuu.

Hoja hii iliungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wengi na katika kuhitimisha, Naibu Spika akasema.

Ninanukuu*: "... katika kujadili Hoja hii ambayo imeibuliwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, sasa Mheshimiwa Ole-Sendeka ameiboresha kwa kutoa hoja ya kuundwa Tume Teule [Kamati Teule] ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeiunga mkono kwa wingi sana kwa kutumia Kanuni ya 117 ambayo inasema. "...Kamati Teule inaweza kuundwa na Bunge kwa madhumuni maalum kwa hoja mahsusi itakayotolewa na kuafikiwa". Hoja hii imetolewa na imeafikiwa na kwa jinsi hiyo mimi ninakubaliana na jambo hili. Kwa jinsi hiyo kufuatana na Kanuni hii ya 117 Bunge hili litaunda Tume Teule [Kamati Teule] kwa ajili ya kulichunguza jambo hili....."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Wakati hatua hii ikifikiwa, Mheshimiwa Nimrod Mkono, aliomba Mwongozo wa Spika akitumia Kanuni ya 68 na kurejea Ibara ya 15(6) [13(6)] ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayohusu usawa mbele ya Sheria. Katika rejea hii Mheshimiwa Nimrod Mkono, alitaka kujua ikiwa Bunge halikiuki Katiba kwa kumhukumu Ndugu David Jairo, bila kumpa nafasi ya kujitetea.

Naibu Spika, alitoa ufafanuzi kwamba mpaka wakati ule bado hakukuwa na hukumu yoyote na kwamba kuundwa kwa Kamati Teule ni mojawapo ya hatua muafaka za kutenda haki kwa kuwa Kamati Teule itakuwa na madaraka kamili na uhuru wa kuita watu mbele yake na kuwahoji akiwemo mtuhumiwa anayetajwa, hivyo itakuwa ni jambo linalofaa ikiwa Ndugu David Kitundu Jairo atatumia fursa hiyo kujibu hoja ama kuuliza maswali na kutoa utetezi.

Mheshimiwa Spika, Hadidu za Rejea, Wajumbe wa Kamati Teule na Muda wa Kazi; Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kwa Azimio la Bunge la tarehe 24 Agosti, 2011 ilipewa Hadidu za Rejea Tano kama ifuatavyo:-

(a) Kuchunguza utaratibu uliobainika wa kukusanya fedha kwa ajili ya kukamilisha uwasilishwaji wa Hotuba za Bajeti za Wizara Bungeni.

- Uhalali wa utaratibu huo Kisheria/Kikanuni.
- Iwapo fedha hizo huwa zinakasimiwa katika Bajeti husika.
- Matumizi halisi ya fedha zinazokusanywa.

(b) Kupitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu uchunguzi alioufanya kuhusiana na agizo la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuchangisha fedha Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kwa ajili ya kufanikisha uwasilishwaji wa Bajeti ya Wizara hiyo Bungeni.

(c) Kuchunguza Mfumo wa Serikali kujibu hoja zinazotolewa Bungeni na taratibu za kuliarifu Bunge matokeo ya utekelezaji wa Hoja hizo. Katika kufanya hivyo pia ichunguze:-

- Usahihi wa utaratibu uliotumiwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwa suala la Ndugu David Kitundu Jairo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini.
- Kubaini kama utaratibu huo umeathiri dhana ya Haki na Madaraka ya Bunge.

(d) Kuangalia nafasi ya Mamlaka ya Uteuzi kwa ngazi ya Makatibu Wakuu, katika kushughulikia masuala ya nidhamu ya anaowateua.

(e) Kuangalia mambo mengine yoyote yenye uhusiano na masuala haya.

Kamati Teule iliundwa na Wajumbe watano kama ifuatavyo:-

(i) Mhe. Eng. Ramo Matala Makani, Mbunge;

(ii) Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mbunge;

(iii) Mhe. Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge;

(iv) Mhe. Mch. Israel Yohana Natse, Mbunge; na

(v) Mhe. Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge.

Mheshimiwa Spika, Mara baada ya Kamati kuundwa, Wajumbe walikutana kumchagua Mwenyekiti wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 117(4) na hivyo Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti. Aidha, kwa kuona umuhimu wa kuwepo kwa Makamu Mwenyekiti, Wajumbe walimchagua Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Kamati Teule ilianza kazi rasmi tarehe 5 Septemba, 2011 huko Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilikuwa na Wajumbe wa Sekretarieti wafuatao:-

(i) Ndugu Nenelwa Mwihambi-Wankanga;

(ii) Ndugu Lukago Alphonce Madulu;

(iii) Ndugu Asia Paul Minja; na

(iv) Ndugu Mswige Dickson Bisile.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilipewa muda usiozidi Wiki Nane kukamilisha kazi hii na pia ilitakiwa kuwasilisha taarifa yake Bungeni wakati wa Mkutano wa Tano wa Bunge kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 119 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, njia zilizotumika katika kukamilisha kazi. Kamati Teule imezifanyia kazi Hadidu za Rejea Tano ilizopewa kwa kufanya yafuatayo:-

(a) Kusoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Sheria mbalimbali na kuzichambua kwa kuziwianisha na Hadidu za Rejea. Sheria zilizohusika ni pamoja na:-

(i) Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002 na Kanuni zake za mwaka 2003;

(ii) Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009, Toleo la Tatu;

(iii) Sheria ya Fedha za Umma, 2001 na Kanuni zake za mwaka 2001;

(iv) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 na Kanuni zake za mwaka 2009;

(v) Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, 1988;

(vi) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007;

*(vii) The Government Loans, Grants and Guarantees Act, 1974*,

(viii) Waraka wa Katibu Mkuu - Hazina Namba 3 wa Machi, 2011;

(ix) Waraka wa Utumishi wa Serikali Namba 2 wa Mwaka 2010; na

(x) Kanuni za Fedha na Mipango Mikakati ya Taasisi nne zilizochangishwa fedha, na kadhalika.

(b) Kupitia maoni kwa njia ya maandishi kutoka Mabunge ya Australia (*House of Representatives*) na Uingereza (*House of Commons*).

(c) Kupitia maoni kwa njia ya maandishi kutoka Wizara 26 za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(d) Kupitia Taarifa zilizotolewa kwa Vyombo vya Habari kwa maandishi kuhusiana na suala la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu David Kitundu Jairo na kusikiliza sehemu ya Taarifa hizo kama zilivyotolewa kwenye vituo mbalimbali vya luninga.

(e) Kusoma na Kuchambua Taarifa ya Ukaguzi Maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kufanya mahojiano na watu mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, (Mb.) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(ii)Katibu Mkuu Kiongozi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(iii) Spika Mstaafu wa Bunge, Mheshimiwa Pius Msekwa.

(iv) Mheshimiwa William Ngeleja, (Mbunge), Waziri wa Nishati na Madini.

(v) Mheshimiwa William V. Lukuvi, (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, (Mb.), Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, (Mb.).

Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Cyril Agust Chami, (Mbunge), Waziri wa Viwanda na Biashara na Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, (Mbunge), Waziri wa Maliasili na Utalii.

(vi) Waheshimiwa Wabunge 17 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(vii) "*Senior citizens*" wakiwemo Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu. Mheshimiwa Dkt. Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu Mstaafu na Mheshimiwa Cleopa David Msuya, Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu.

(viii) Watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini wakiwemo Katibu Mkuu, Ndugu David Kitundu Jairo, Kaimu Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Mkaguzi Mkuu wa Ndani na Mhasibu Mkuu.

(ix) Watendaji na Taasisi saba (7) zilizo chini ya Wizara ya Nishati na Madini, wakiwemo Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi husika, Watendaji Wakuu na Wakuu wa Idara za Sera na Mipango, Rasilimali Watu, Ukaguzi wa Ndani na Fedha.

(x) Watendaji wa Wizara mbalimbali katika ngazi tofauti hususan Makatibu Wakuu, Wakurugenzi katika maeneo ya Sera na Mipango, Rasilimali Watu, Ukaguzi wa Ndani na Fedha.

(xi) Watendaji wa Taasisi tisa (9) zilizo chini ya Wizara za Fedha, Ujenzi, Maji, Viwanda na Biashara na Maliasili na Utalii katika maeneo ya Sera na Mipango, Rasilimali Watu, Ukaguzi wa Ndani na Fedha.

(xii) Wakongwe wa Siasa za Tanzania na Watu waliobobea katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya Katiba, Sheria, Bunge, Serikali, Mahakama, Utumishi wa Umma, Utawala Bora, Uongozi na Rasilimali Watu na kadhalika, wakiwemo Makatibu wa Bunge Wastaafu na Makatibu Wakuu Wastaafu.

(xiii) Wanazuoni waliobobea katika taaluma za Katiba, Sheria, Elimu ya Sayansi ya Siasa na Utawala na Utumishi wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Mzumbe.

(xiv) Wawakilishi wa Asasi mbalimbali za kiraia zikiwemo *Policy Forum*, *TGNP* na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

(xv) Wawakilishi wa Jukwaa la Wahariri.

Orodha kamili ya waliohojiwa na waliopata nafasi ya kuishauri Kamati Teule ina jumla ya watu 146 na imeambatishwa kama Kiambatisho II kwenye Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Utaratibu Uliobainika wa Kukusanya Fedha Kwa Ajili ya Kukamilisha Uwasilishwaji wa Hotuba za Bajeti za Wizara Bungeni, Hadidu ya Rejea ya Kwanza iliitaka Kamati Teule kuchunguza utaratibu uliobainika wa kukusanya fedha kwa ajili ya kukamilisha uwasilishaji wa Hotuba za Bajeti za Wizara Bungeni kwa kuchunguza mambo matatu yafuatayo:-

(a) Uhalali wa utaratibu huo Kisheria/Kikanuni.

(b) Iwapo fedha hizo huwa zinakasimiwa katika Bajeti husika.

(c) Matumizi halisi ya fedha zinazokusanywa.

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha jukumu hili, Kamati Teule ilifanya yafuatayo:-

(a) Kupitia Katiba, Sheria, Kanuni, Miongozo na Nyaraka mbalimbali.

(b) Mahojiano na Katibu Mkuu Kiongozi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Watendaji wa Wizara na Taasisi mbalimbali, Wanazuoni, Wabunge, Viongozi Wastaafu, Jukwaa la Wahariri na wawakilishi wa baadhi ya asasi za kiraia.

(c) Kukusanya taarifa mbalimbali kwa njia ya Dodoso kutoka Wizara zote.

(d) Kupitia Taarifa ya Ukaguzi Maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu jambo hili.

Uchunguzi kuhusu Utaratibu Uliobainika wa Kukusanya Fedha kwa ajili ya Kukamilisha Uwasilishwaji wa Hotuba za Bajeti za Wizara BungeniMheshimiwa Spika, Utaratibu uliokuwa ukichunguzwa na Kamati Teule ni ule uliotumiwa na Wizara ya Nishati na Madini kuchangisha fedha kwenye Taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya kuwezesha maandalizi na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti yake Bungeni. Aidha, ili kukidhi haja ya Hadidu ya Rejea hii, Kamati ilifanya uchunguzi katika Wizara zote nchini ili kubaini kama utaratibu huo pia upo katika Wizara nyingine na vile vile kuweza kubaini kama ni wa kawaida, na kwa kiasi gani.

Uchunguzi wa Kamati Teule ulibaini kuwa Wizara ya Nishati na Madini ina jumla ya Taasisi na Mashirika saba ambayo ni: *Tanzania Petroleum Development Corporation (TPDC), Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO), Rural Energy Agency* (REA), *State Mining Corporation (STAMICO), Geological Survey of Tanzania (GST), Tanzania Minerals Audit Agency (TMAA)* na *Mineral Resources Institute* (MRI).

Kati ya Taasisi hizo ni *REA, TPDC* na *TANESCO* tu ndizo ziliombwa michango kwa kuzingatia uwezo wao wa kifedha. Taasisi ya *EWURA* ambayo kiutawala iko chini ya Wizara ya Maji iliombwa mchango kwa sababu baadhi ya majukumu yake katika udhibiti wa nishati, yapo chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Taasisi nne zinazobakia hazikuombwa kuchangia kwa maelezo kwamba hazina uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 21 Juni, 2011 Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini aliwaandikia barua Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yake kuchangia gharama kwa ajili ya kukamilisha maandalizi na uwasilishwaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mwaka 2011/2012 Bungeni Dodoma. Kila barua aliyoandikiwa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ilielekeza kwamba fedha hizo zitumwe *Geological Survey of Tanzania (GST)* kwenye

Akaunti Na. 5051000068 *NMB* Tawi la Dodoma na kuwa baada ya kutuma fedha hizo Wizara ipewe taarifa kupitia Ofisi ya *DP* kwa uratibu.

Taasisi zilizoandikiwa barua kuombwa kuchangia, viwango walivyoombwa na mwitikio wa maombi ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1 na Jedwali Na. 2 kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 1: Taasisi zilizoandikiwa barua kuombwa kuchangia**

| Na. | Taasisi | Kiasi Kilichoombwa(Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania *(TANESCO)..* | 40,000,000/= |
| 2. | Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA)..* | 40,000,000/= |
| 3. | Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)* ........................... | 50,000,000/= |
| 4. | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)...* | 50,000,000/= |
| | **JUMLA ........................................................** | **180,000,000/=** |

**Jedwali Na. 2: Mwitikio wa maombi ya Michango kutoka katika Taasisi**

| Na. | Taasisi | Kiasi Kilichoombwa(Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania *(TANESCO)...* | 40,000,000/= |
| 2. | Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA)** | — |
| 3. | Wakala wa Umeme Vijijini *(REA)*................................ | 50,000,000/= |
| 4. | Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)*...... | 50,000,000/= |
| | **JUMLA ..........................................................** | **140,000,000/=** |

*——*EWURA* haikuchangia kiasi cha Sh. 4 0,000,000.00 kama ilivyoombwa, badala yake iligharamia chakula cha mchana kwa siku tatu (Sh.3,656,000.00) na tafrija ya tarehe 18 Julai, 2011 (Shilingi 6,141,600.00) siku ambayo Bajeti ya Wizara ilitarajiwa kupitishwa. Kwa maana hiyo *EWURA* ilichangia jumla ya Sh. 9,797,600.00.

Mheshimiwa Spika, Fedha zilizokusanywa toka Idara za Wizara na jumla ya fedha zote zilizoingizwa katika Akaunti ya GST ni kama inavyoonekana katika Jedwali 3 na Jedwali 4 kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 3: Fedha zilizokusanywa toka Idara za Wizara**

| Na. | Idara | Kiasi Kilichokusanywa(Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Uhasibu ...................................... | 150,720,000/= |
| 2. | Sera na Mipango ............................. | 278,081,500/= |
| | **JUMLA .......................................** | **428,801,500/=** |

**Jedwali Na. 4: Jumla ya Fedha zote Zilizoingizwa katika Akaunti ya GST**

| Tarehe | Stakabadhi | Mlipaji | Kiasi (Sh.) | Madhumuni |
|---|---|---|---|---|
| 14/6/2011 | 02427 | Wizara ya Nishati na Madini | 50,143,500/= | Shughuli za Bunge (Idara ya Sera na Mipango) |
| 24/6/2011 | 02429 | Uhasibu) | 150,720,00/= | *Kikao cha kazi/Semina |
| 25/6/2011 | 02428 | Nishati na Madini *(OC)* | 171,542,000/= | Bajeti |
| 25/6/2011 | 02428 | Sera na Mipango) | 56,396,000/= | Bajeti |
| 4/7/2011 | 02432 | *TPDC* | 50,000,000/= | Shughuli za Bunge |
| 13/7/2011 | 02431 | *REA* | 50,000,000/= | Shughuli za Bunge |
| 18/7/2011 | 02430 | *TANESCO* | 40,000,000/= | Shughuli za Bunge |
| | **JUMLA** | **..............................................................................** | **568,801,500/=** | |

* … Jumla ya Sh.150,720,000.00 ziliingizwa kwenye Akaunti ya GST kwa ajili ya gharama za vikao vya kazi na semina. Kwa hiyo, kiasi cha Sh.418,081,500.00 ndicho kilikuwa mahsusi kwa ajili ya shughuli za uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Ili kuweza kuuchunguza vema uwepo na ukawaida wa utaratibu huu ndani ya Wizara za Serikali, Kamati Teule ilifanya mahojiano na watu mbalimbali na kutuma Dodoso kwa Makatibu Wakuu wa Wizara 25.

(a) Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu Mahojiano.

(i) Ndugu Ludovick Utouh, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kamati Teule ilizingatia ukweli kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndiye Mwangalizi Mkuu wa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma Serikalini kwa niaba ya Bunge. Hivyo ilikuwa ni muhimu sana kupata kauli yake kuhusu utaratibu huu kama umebainika katika Kaguzi zake katika vipindi vilivyopita. Majibu yake yalikuwa ni kwamba utaratibu huu siyo wa kawaida. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali alisema.

*"…*Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema ni kwamba nime-*instruct* ukaguzi wa wizara zote za mwaka huu, tu-*dig into this issue* ili tuweze ku-*establish extent* ya tatizo lilivyo kiserikali in totality…lakini *the other reason also* ambayo iko kwenye ripoti, ile kwamba *most of these institutions they don't budget for contribution* ya kuchangia, *unless institutions* ziwe zinajua *from the time go, kwamba they have an obligation* ya kuchangia katika ku-*process* Bajeti ya Wizara ili wa- *make that provision".1*

(ii) Mheshimiwa Mustafa H. Mkulo, (Mb.), Waziri wa Fedha Lengo la Kamati Teule kufanya mahojiano na Waziri wa Fedha kuhusu jambo hili ilikuwa ni kupata kauli yake kama amewahi kuuona utaratibu huu katika usimamizi wake wa matumizi ya fedha za umma Serikalini. Waziri wa Fedha alitamka: -

*"…the whole transaction, the whole issue, haikuwa issue ambayo ni proper within the accounting system, within the monetary systems* za kiserikali*, ilikuwa nje ya utaratibu proper* wa kiserikali".

(iii) Mheshimiwa John M. Cheyo (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali. Lengo la Kamati Teule kufanya mahojiano na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ilikuwa ni kupata kauli yake kama Kamati yake imewahi kukutana na matumizi ya aina hii kwenye taarifa za hesabu za Wizara, naye alisema:-

*"…katika miaka yote mimi nimekuwa chair wa Public Accounts Committee (PAC), sijaona hata siku moja miscellaneous income, because hii exercise ya kwenda Bungeni ni ya kila mwaka, kila mwaka Wizara lazima iende Bungeni kupata idhini ya kutumia fedha, that means budget session; sijaona hata wakati mmoja pamekuwa na miscellaneous income ambayo ni fedha hiyo.*

*Kwa hiyo, question number one becomes; wewe unayekusanya hizo fedha unazipeleka wapi? Kama unatumia Mfuko Mwingine basi ndiyo kusema kuna non-disclosure ya funds ambazo zinakuwa collected na Serikali, kitu ambacho pia kihasibu siyo sawasawa."*

(iv) Ndugu Philemon Luhanjo, Katibu Mkuu Kiongozi Kamati Teule iliona ni vema kufanya mahojiano na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye ni Mkuu wa Utumishi wa Umma na Katibu wa Baraza la Mawaziri. Kwa kuwa katika Mkutano wake na Vyombo vya Habari alitoa kauli kuwa "huu ni utaratibu wa kawaida", alipoulizwa swali kwamba utaratibu aliousema kuwa ni wa kawaida unatumika katika Wizara ngapi, alisema:-

*"…* siwezi kusema Wizara ngapi, hiyo siyo rahisi sana, kwa sababu kwanza kwanini uchangishe, *issue* inaanzia hapo, kwa nini uchangishe… utaratibu huu siyo *formalized as such,* ni mpango unaofanywa kiutawala kwa maana shughuli ipo mbele yako huna *resources*, lakini unazo Taasisi unazoweza kuzi-*pull together* mkaweza kushirikisha.

Kwa hiyo, mtu ukiwa na shida unakwenda Hazina kuomba kwamba nimetindikiwa na fedha nipeni fedha.

(v) Makatibu Wakuu wa Wizara mbalimbali. Baadhi ya Makatibu Wakuu waliohojiwa ni kutoka katika Wizara za Ujenzi, Maji, Viwanda na Biashara, Nishati na Madini na Fedha (Naibu Katibu Mkuu). Lengo la Kamati kuwahoji Makatibu hawa Ilikuwa ni kujiridhisha na uwepo wa utaratibu huu pamoja na ukawaida wake. Isipokuwa

kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Makatibu Wakuu wa Wizara zilizotajwa walisema kuwa utaratibu huu haupo katika Wizara zao.

(b) Barua/Dodoso. Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilituma Barua/Dodoso kwa Makatibu Wakuu wa Wizara 25 za Serikali ili kuweza kubaini kama Wizara hizo zinaendesha uchangishaji katika Taasisi zao kwa ajili ya kuweza kuwasilisha Hotuba za Bajeti zao Bungeni. Makatibu Wakuu wa Wizara zote 25 zilizoandikiwa barua walisema kuwa utaratibu wa kuzichangisha Taasisi zilizo chini yao kwa ajili ya kupata fedha za kuisaidia Wizara kuwasilisha Hotuba za Bajeti Bungeni haupo. Makatibu Wakuu hao walijibu kuwa Bajeti zao zina kasma maalum kwa ajili ya uwasilishaji wa Hotuba za Bajeti za Wizara zao Bungeni. Na kwamba endapo limetokea tatizo la kasma kutokuwa na fedha kwa ajili ya shughuli iliyokusudiwa Wizara hufanya uhamisho wa fedha (*reallocation*) katika vifungu vyake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Fedha za Umma.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Makatibu Wakuu wa Wizara 25 zilizohojiwa kwa njia ya mazungumzo na Dodoso walikataa kuwa na utaratibu wa kuchangisha fedha kwenye Taasisi zilizo chini ya Wizara zao kwa ajili ya kuwezesha uwasilishaji wa Hotuba za Bajeti zao Bungeni, na kwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali alikataa kuwahi kuona matumizi ya namna hii kwenye Taarifa za kila Mwaka za Hesabu zinazokaguliwa za Wizara mbalimbali, na kwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia alikataa kuwahi kuliona jambo hili na kuahidi kuwa ataanzisha Ukaguzi Maalum kwenye Wizara kwa ajili ya jambo hili tu kwani katika Ukaguzi wa kawaida halijabainika kuwepo, hivyo basi Kamati Teule imejiridhisha kuwa huu siyo utaratibu wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Uchunguzi kuhusu uhalali wa utaratibu wa uchangishaji Kisheria na Kikanuni, Ili kuweza kuchunguza uhalali wa utaratibu huu Kisheria na Kikanuni, Kamati Teule ilirejea kwa kina Sheria ya Fedha za Umma, 2001 pamoja na Marekebisho yake ya Mwaka, 2004 na Kanuni za Fedha za Umma, 2004. Miongozo mingine iliyorejewa kwa kina ni Mipango Kazi ya Taasisi zilizochangia na Mpango Kazi wa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011.

Lakini pia, Kamati ilifanya mahojiano na wadau mbalimbali wakiwemo Waziri wa Fedha, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na Mheshimiwa Cleopa D. Msuya, Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu.

Mheshimiwa Spika, Msingi wa Kikatiba, Ibara ya 136 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inatamka wazi kwamba, hakuna fedha itakayotolewa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, isipokuwa tu fedha hizo ziwe ni kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa na Bunge. Hii pia ni kwa mujibu wa Ibara ya 137 ambayo inahusu utaratibu wa Serikali kuandaa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka na namna Makadirio hayo yanavyopaswa kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge.

Uchunguzi wa Kamati Teule ulibaini kuwa ni kweli fedha zilizochangishwa ziliidhinishwa na Bunge katika Bajeti ya Serikali katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011 lakini siyo kwa matumizi ya kuichangia Wizara ili iweze kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni bali ni kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya Taasisi zenyewe kama Taarifa hii itakavyoendelea kufafanua.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 4(4) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001, Mahojiano kati ya Kamati Teule na Watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini yaliifanya Kamati kuelewa kwamba Wizara ya Nishati na Madini ilifikia uamuzi wa kuomba michango kwenye Taasisi zake kwa sababu Kifungu wanachokitumia kwa shughuli za Bajeti yaani *Project Coordination and Monitoring* kilikuwa kimebakiwa na Sh.35,500,000.00 tu wakati makisio ya gharama za kukamilisha mchakato wa maandalizi na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ilikuwa ni Sh.207,042,000.00 *(*Tazama Kiambatisho VI*)* na kwamba Fedha za *Other Charges* (OC) kwa robo ya nne ya mwaka zilikuwa hazijapatikana hadi kufikia tarehe 21 Juni, 2011 hivyo kuleta hofu ya kukamilika kwa zoezi zima la uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule haikubaliani na sababu zilizotolewa na Wizara kwa kuwa endapo kunatokea mahitaji na kasma inayohusika haina fedha ama hakuna kasma utaratibu unaopaswa kufuatwa umeainishwa katika Kanuni ya 4(4) kama ifuatavyo:-

"*…The Appropriation Act shall allocate funds by vote and any variation in such allocation shall be approved by the National Assembly in a further Appropriation Act(s). The division of the funds by sub-Head and item shall be*

*controlled by the Minister under the authority of Section 5(1) (b) of the Public Finance Act and any variation in the amount allocated to a sub-head or item by such division shall have a prior approval of the Minister."*

Mheshimiwa Spika, Uchunguzi wa Kamati Teule ulibaini kwamba Kanuni hii haikuzingatiwa, kwa sababu mtiririko wa maelezo ya Wizara kuhusu uchangishaji ulitakiwa kuishia katika mabadiliko ya vifungu vya Bajeti ya Wizara yenyewe na mabadiliko hayo yalipaswa kupata idhini ya Waziri wa Fedha badala ya kuamua kuzichangisha Taasisi. Ndiyo maana katika mahojiano Waziri wa Fedha alisema:-

*"…kama Wizara ina shortfall, kuna utaratibu maalum wa Afisa Masuuli kumwandikia Mlipaji Mkuu wa Serikali na kuelezea tatizo la hiyo shortfall limetokea namna gani, kwa nini halikuwepo kwenye Bajeti na umuhimu wa hicho ambacho kina shortfall na kwa nini wanaomba Wizara iongezewe fedha… Waziri wa Fedha anatoa kibali kwamba, okay, sawa, hebu pelekeni hizo fedha huko kunakotakiwa… kwa hiyo, hakuna popote panaposema kwamba kama una shortfall mahali fulani unaweza kwenda kuwaambia watu fulani wakuchangie ili uweze kufidia shortfall, bado nasisitiza kwamba the whole thing was not proper… ".5 (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya ya Kanuni ya 4(4) ambayo yameungwa mkono na maelezo ya Waziri Mwenye dhamana ya Fedha, Kamati Teule imejiridhisha zaidi kuwa utaratibu huu siyo halali na wala siyo wa kawaida. (*Makofi*)

Aidha, sababu zilizoifanya Wizara kuchangisha fedha haziwezi kutiliwa maanani kwa sababu hadi kufikia tarehe 25 Juni, 2011 Wizara ya Nishati na Madini ilikwishakupata mahitaji yote ya fedha za uwasilishaji wa Bajeti baada ya kupokea Sh.171,542,000.00 za *Other Charges (OC)* kutoka Hazina. Hivyo Wizara haikuwa na sababu yoyote ya kuendelea kukusanya michango ya fedha toka kwenye Taasisi zake. Ukweli wa maelezo haya ulithibitishwa na Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Nishati na Madini ambaye ndiye mratibu wa kazi za Bajeti. Katika mahojiano na Kamati Teule alipoulizwa endapo kulikuwa na haja ya kuendelea kukusanya michango kutoka Taasisi hata baada ya kupokea fedha za OC Sh.171,542,000.00 alijibu kwa mkazo kuwa "ni kweli hakuna haja"6.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 53(1) na (2) ya Kanuni ya Fedha za Umma, 2001.

Kimantiki, Kanuni hii inaweka utaratibu kwamba fedha zinapokuwa zimeidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ndani ya Taasisi ya umma, inapaswa fedha hizo zionekane kwenye *Appropriation Accounts* za Taasisi hiyo kwa namna zilivyoingia na kutumika katika mwaka husika. Kanuni hii inatamka kuwa:-

*"53(1) The Government account shall be kept on a cash basis in order that the amount of cash spent on a particular service be compared with the amount authorized by the National Assembly.*
*(2) "…for purposes of sub-regulation (1) all actual receipts and payments made during the financial year shall be recorded in the Appropriation accounts."*

Uchunguzi wa Kamati Teule ulibaini kuwa Wizara ya Nishati na Madini ndiyo iliyochangisha fedha hizi na kuzitumia lakini mapato na matumizi ya fedha hizi hayatapatikana kwenye vitabu vya Hesabu vya Wizara. Mmoja wa wataalam wa masuala ya fedha Serikalini alitoa ufafanuzi ufuatao kuhusu utaratibu huu: -

*"… System* ya *payment ambayo ni ya Wizara ya Fedha inatumika katika Wizara zote na inategemea Bajeti ambayo imepitishwa na Bunge. Bunge likisema kwamba tumepitisha milioni moja kwa ajili ya safari there is no way ukatumia Milioni moja na nusu. Kwa sababu Bajeti ile inakuwa tayari imefungwa kwenye system, kwa maana hiyo, ili uweze kutumia milioni moja na nusu ni lazima Wizara ya fedha wapanue ceiling na Wizara ya fedha kupanua ceiling ni mpaka kibali cha Bunge …"7 (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu huu wa Wizara kuchangisha Taasisi na kuelekeza fedha hizo kuingia kwenye Akaunti ya GST ni dhahiri kuwa katika Hesabu za Mwaka, Bunge halitaweza kuona wala kuhoji ongezeko la sh. 140,000,000.00 na matumizi ya fedha hizo katika Fungu 58 la Wizara ya Nishati na Madini. Kwa maana hiyo utaratibu huu siyo halali kwa sababu unachochea matumizi ya fedha za Umma kinyemela bila ya usimamizi wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, Waraka Na. 3 wa Mwaka 2011 wa Katibu Mkuu Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Kamati Teule ilipitia na kuchambua Waraka Na. 3 wa Mwaka 2011 wa Katibu Mkuu - Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa Makatibu Wakuu wa Wizara na Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma kutoa Mikopo kwa Wizara. *(Makofi)*

Msingi wa Waraka huu ni Sheria ya *The Government Loans, Guarantees and Grants Act, 1974* na unaweka masharti kwa Wizara kuhusu kupata mikopo, dhamana na misaada kutoka kwenye Taasisi chini ya Wizara. Katika utafiti wake Kamati Teule imebaini kuwepo kwa mitizamo miwili tofauti kuhusu tafsiri ya Waraka huu kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Slpika, michango siyo sehemu ya mikopo, ruzuku au dhamana.

Mawazo ya wanaosema kwamba michango si sehemu ya mikopo, ruzuku au dhamana kulingana na Waraka yanajengwa katika Hoja kwamba kilichoombwa na Wizara ya Nishati na Madini kwa Taasisi hakikuwa mkopo, ruzuku, wala dhamana bali ni michango.

(b)Michango ni sehemu ya mikopo, ruzuku na dhamana kwa hiyo, waraka huu ni mahususi na waraka ungetumika basi Wizara isingeweza kuchangisha fedha kama ilivyoweza kuchangisha.

Mawazo ya wanaosema kwamba michango ni sehemu ya mikopo, ruzuku au dhamana kulingana na Waraka yanajengwa katika Hoja kwamba kilichoombwa na Wizara ya Nishati na Madini kwa Taasisi kilikuwa ni ruzuku kwa sababu ruzuku ni aina ya msaada. Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, (Mb.) alisisitiza hili kwa kusema:-

*"…* nadhani tulichozoea ni kwamba msaada lazima uwe unatoka *World Bank* lakini msaada unaweza kutoka kwa Mheshimiwa Mkulo, naweza kutoa shilingi milioni moja zangu za mwezi na tunafanya pale na tunasema Wabunge wote changieni. Ule ni msaada, kwa hiyo walichokifanya wao kina-*fit in* kwenye ile ya pili, misaada…"

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inasisitiza kwamba uchangishaji uliofanywa na Wizara ya Nishati na Madini ulipaswa kuwa chini ya Masharti ya Waraka huu kutokana na uchambuzi ufuatao: -

(i) Kilichoombwa na Wizara siyo mkopo kwa kuwa hapakuwekwa makubaliano ya urejeshaji.

(ii) Kilichoombwa na Wizara siyo dhamana kwa kuwa Wizara ilikuwa haidhaminiwi kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni.

(iii) Kilichoombwa na Wizara ni msaada kwa kuwa haikuwa na fedha za kutosha kukamilisha jukumu lake la kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni, na hapakuwa na makubaliano ya kurejesha fedha mara baada ya matumizi. Ndiyo maana hata zile fedha zilizokuwa zimebaki hazikurejeshwa kwa Taasisi zilizochangia kwa sababu zilitoa msaada kwa Wizara.

(iv) Waraka ulielekezwa kwa Makatibu Wakuu wa Wizara na Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma Tanzania Bara. Uchunguzi wa Kamati Teule ulibaini kwamba Waraka huu ulipokelewa kwenye Wizara ya Nishati na Madini tarehe 15 Machi, 2011 na kutolewa maelekezo ya kusambazwa kwenye Mashirika na Taasisi za Wizara hiyo tarehe 16 Machi, 2011. Maelekezo hayo yalitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu David Kitundu Jairo mwenyewe. Hivyo, Katibu Mkuu aliyeendesha uchangishaji huu alikuwa na taarifa za kutosha kuhusu kuwepo kwa Waraka huo. (*Makofi*)

(v) Wizara, Mashirika na Taasisi wanaandaa na kuidhinishiwa Bajeti zao kila Mwaka na inatakiwa Bajeti hiyo izingatiwe. Uchunguzi wa Kamati Teule ulibaini kwamba Taasisi zilizochangishwa hazina Kasma mahsusi kwa ajili ya kuichangia Wizara ili iwasilishe Hotuba ya Bajeti yake Bungeni. Hivyo, kitendo cha Taasisi kutoa fedha zake kuichangia Wizara hakikuzingatia sharti hili.

(vi) Wizara huandaa na kupewa Bajeti zake kwa mujibu wa majukumu na malengo yaliyopangwa na kuidhinishwa. Uchunguzi wa Kamati Teule ulibaini kuwa Wizara inayo Kasma mahsusi kwa ajili ya kuweza kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni. Hivyo, hili lilikuwa ni jukumu la Wizara yenyewe siyo jukumu la Taasisi.

(vii) Waraka unasisitiza kwamba: -"…Endapo kutatokea mahitaji yatakayolazimu kutumia fedha kutoka katika Mashirika ama Taasisi za umma chini ya Wizara ni lazima kupata kibali cha Waziri wa Fedha baada ya kushauriwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) na Msajili wa Hazina."

Hivyo, Wizara hazipaswi kupewa fedha za ziada kupitia Mashirika na Taasisi zilizo chini yake. Lakini Wizara ya Nishati na Madini inaonekana ilipata fedha za ziada kutoka kwenye Taasisi zake kupitia uchangishaji huu. Hii ni kinyume na masharti ya Waraka huu.

Mheshimiwa Spika, Ili kujielimisha zaidi, Kamati ililazimika kufanya mahojiano na Waziri wa Fedha ambaye kwa mujibu wa Waraka huu ndiye mtoa kibali. Akitoa maelezo yake mbele ya Kamati Teule, Waziri wa Fedha, Mhe. Mustafa Mkulo, (Mb.) alisema kwamba baada ya kuonekana kuna matatizo mengi ya Wizara mbalimbali kuomba fedha kutoka kwenye Taasisi zilizo chini yao, Baraza la Mawaziri lilijadili suala hili na kuazimia kwamba itafutwe namna ya kudhibiti matumizi, dosari na matatizo, ndipo ikakubalika kwamba Hazina itoe Waraka wa kudhibiti mambo haya. Waziri wa Fedha alifafanua zaidi juu ya Waraka huu kwa kusema:-

"…(Katibu Mkuu) hakuutoa yeye kama mtu binafsi, alitoa ule Waraka mimi kama Waziri nikiwa na *full knowledg*e na Rais akiwa na *full knowledge* kwamba tuweze ku-*control* matumizi ya ajabu ajabu ambayo hayahusiki.

Kwa hiyo, kilipokuja kutokea kile ambacho kilitokea Bungeni hata sisi Hazina kwa kweli ilitushangaza kwamba kuna kitu kama hicho kimetokea."

Baada ya kukamilisha uchunguzi wake kuhusu jambo hili Kamati Teule ilibaini kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, hakuomba kibali cha Waziri wa Fedha ili kupata ridhaa ya kuchangisha hivyo alikiuka masharti ya Waraka huu.

Uchunguzi iwapo taasisi zilizochangia zina Kasma kwa ajili ya Uchangiaji huu.

Mheshimiwa Spika, Ili kuweza kukamilisha jukumu hili, Kamati Teule ilipitia Mipango Kazi na Bajeti za Taasisi zilizochangia kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011. Nyaraka hizi zilibainisha kuwa Taasisi husika *(TANESCO, REA, TPDC* na *EWURA)* hazina kasma mahsusi kwa ajili ya kuichangia Wizara iweze kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni. Uchambuzi zaidi ulikuwa kama ifuatavyo.

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC),* Taasisi hii ilichangia kiasi cha sh. 50,000,000.00 kutoka kasma ya mapato ya Gesi ya Serikali (*Government Gas Revenue*). Kasma hii, kama inavyojieleza yenyewe ni ya mapato ya gesi ya Serikali na siyo kasma ya kuchangia Wizara kuwasilisha Hotuba ya Bajeti.

Kamati ilipitia Kanuni za Fedha za *TPDC,* 2008 zikisomwa pamoja na Mwongozo wa Ukomo wa Mamlaka ya kuidhinisha malipo mbalimbali (*Powers of Authority*). Nyaraka hizi zinaonyesha kuwa katika matumizi yote yanayohusiana na mitaji, miradi na mapato mengineyo, mamlaka ya Mtendaji Mkuu hayana ukomo kwa matumizi ambayo yamepitishwa na Bodi. Hata hivyo, matumizi yote ambayo hayajapitishwa katika Bajeti yatafanyika kwa idhini ya Bodi tu.

Mheshimiwa Spika, katika mahojiano na Watendaji wa *TPDC,* Kamati ilibaini kuwa *TPDC* ililazimika kuchanga fedha hizo bila idhini ya Bodi kama inavyotakiwa na Kanuni zake za Fedha na *Powers of Authority* ili kutii maagizo ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini. Kwamba *TPDC* walilazimika kuchanga kinyume na utaratibu kwa kuhofia kuitwa wakaidi kutokana na uzoefu waliokwishaupata siku za nyuma.

Hali hii ilijidhihirisha zaidi kupitia maombi ya Menejimenti ya *TPDC* kwa Bodi (*Board Paper*) yaliyoandaliwa ili kupata idhini baada ya matumizi (*Retrospective Approval*) kama ifuatavyo:-

*"Management thought that it did not have any choice in the matter since in its view, failure to make the contribution might cause untold consequences. However, since the Corporation has no money, and this item not having budgeted for, Management saw it fit to pay the money requested out of Government Gas Revenue."*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Nishati ya Umeme Vijijini *(REA),* Kiasi kilichochangwa na taasisi hii cha Sh. 50,000,000.00 kilitoka kwenye kasma ya kuandaa Mpango Kazi na Bajeti ya *REA* (*Preparation of REA Business Plan and Budget*). Kasma hii ilikuwa na Sh.37,500,000.0010, hata hivyo, tarehe 15 Aprili, 2011, kasma hiyo ilikuwa na bakaa ya Sh.7,792,425.00 tu, lakini ikaongezewa Sh.75,177,575.00 kwa utaratibu wa kuhamisha fedha *(reallocation)* hivyo kufanya kasma ya kuandaa Mpango.

Kazi na Bajeti ya *REA* kuwa na jumla ya Sh.82,970,000.0011. Hatua ya kuchangia Sh. 50,000,000.00 na wakati katika kipindi kifupi kilichotangulia REA ilishachangia Sh. 22,000,000.00 hivyo kufanya jumla ya michango kwa Wizara kuwa Sh.72,000,000.00 kutoka katika kasma iliyotengewa Sh.82,970,000.00 inaonyesha wazi kuwa kasma hii isingeweza kutekeleza jukumu lililokusudiwa kwani ilibaki na Sh.10,970,000.00 tu ambayo ni sawa na asilimia 13 ya kasma yote.

Kamati Teule ilipitia Mwongozo wa *REA* wa matumizi ya fedha ambao umezingatia Sheria na Kanuni mbalimbali zikiwemo Sheria ya *Rural Energy Act, 2005*, Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake na Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake na kubaini kuwa Kifungu cha 16.4 cha Mwongozo wa Fedha na Matumizi (*Financial Accounting Manual*) kinachohusu *unplanned activities or expenditure* kinaweza kutumika vibaya kwa kuidhinisha matumizi yasiyo na tija. Kifungu hicho kinasomeka:-

*"No activity may be carried out or expenditure be incurred without its prior inclusion in the annual plan and budget, except approval has been obtained from the DG or Board* ***".***

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kuwa uamuzi wa *REA* kuchangia ulifanyika kwa idhini ya Mkurugenzi Mkuu kwa kutumia Kifungu hiki cha Mwongozo. Kamati Teule ina maoni kwamba maudhui ya Kifungu cha 16.4.1 yanatoa mwanya kwa matumizi mabaya ya fedha za Umma kwa shughuli ambazo hazikupangwa na Taasisi. *Discretionary powers* za namna hii zisipowekewa mipaka ni mojawapo ya mambo yanayoweza kusababisha kudhoofisha Mashirika na Taasisi zetu za Umma**.**

Mheshimiwa Spika, Shirika la ugavi wa Umeme Tanzania *(TANESCO).* Shirika hili lilitumia Kasma ya *Donations and Subscriptions* kuchangia Sh.40,000,000.00. Tafsiri isiyo rasmi ya kasma hii ni Michango ya Kijamii na ada za Uanachama. Katika Bajeti ya *TANESCO* ya Mwaka 2011, kasma hiyo ilikuwa na Sh. 200,000,000.00 ambazo ziko ndani ya mamlaka ya Mkurugenzi Mtendaji. Hapo ndipo fedha za kuichangia Wizara ili iwasilishe hotuba ya Bajeti yake Bungeni zilipochukuliwa. Lakini kuichangia Wizara kwa ajili ya kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni siyo shughuli mahsusi iliyolengwa katika kuisaidia jamii wala siyo ada ya uanachama katika Wizara. Akitoa maelezo yake mbele ya Kamati Teule, mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa *TANESCO* alisema:-

*"… kwa jinsi ninavyoelewa mimi ni kwamba, kasma hiyo haipo kwa nia hiyo. Kunaweza kuwa na kasma kwa ajili ya donations na subscriptions, lakini sidhani kama kuna kasma ya kutoka ndani ya kampuni kwenda Wizarani… Kasma ambayo naijua ambayo inaitwa donation na subscription, labda kwa Kiingereza tungeiita kwa ajili ya philanthropic activities ambayo inakuwa ni ya donations za kutoa misaada katika vikundi, makampuni na shughuli za kijamii. Nataka nitofautishe shughuli za kijamii na shughuli ya kusaidia Bajeti ipite…."*

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati Teule kwamba kasma ya *Donations and Subscriptions* haikutumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji *(EWURA)* Mamlaka hii iko chini ya Wizara ya Maji kimuundo ingawa baadhi ya majukumu yake yapo chini ya Wizara ya Nishati na Madini.

Katika suala hili la kuichangia Wizara ya Nishati na Madini, *EWURA* haikuwa tayari kuchanga Sh.40,000,000.00 badala yake wakaomba wachangie kwa kulipia gharama za chakula na vinywaji (Sh.3,656,000.00) na tafrija siku ya kuwasilisha Bajeti (Sh.6,141,600.00) gharama ambazo zilifikia jumla ya Sh.9,797,600.00. Fedha hizi zilitolewa katika kasma ya Elimu kwa Umma.

Kutokana na mahojiano na Watendaji wa *EWURA* msingi wa ombi hili la kuchangia chakula na tafrija ni kuwa maombi ya Sh.40,000,000.00 kutoka Wizarani hayakuainisha mchanganuo wa matumizi. Hivyo walipima wenyewe na kutumia busara kwamba badala ya kupeleka fedha hizo Wizarani watagharamia chakula na tafrija wao wenyewe. Kwa hali hiyo, busara ya *EWURA* ilisaidia kuokoa Sh. 30,202,400.00.

Hata hivyo, Kamati Teule ilipitia *Financial and Accounting Manual* ya *EWURA* na kubaini uwepo wa Kifungu cha 16.4.1 ambacho kinaweza kutumika vibaya. Kifungu hicho kinasomeka:-

***"****No activity may be carried out or expenditure be incurred without its prior inclusion in the annual plan and budget, except approval has been obtained from the DG or Board".*

Uamuzi wa *EWURA* wa kulipia gharama zilizotajwa kwa Sh.9,797,600.00 badala ya kuchanga Sh.40,000,000.00 kama walivyoombwa uliwawezesha kufanikiwa kudhibiti matumizi na hivyo kuokoa fedha za Taasisi. Vilevile umewezesha uwekaji wa kumbukumbu za fedha kuwa kwenye mamlaka yao. Hata hivyo hali hii haihalalishi uchangiaji walioufanya kwa sababu kasma ya Elimu kwa Umma, kama jina linavyosomeka, siyo mahsusi kwa ajili ya kuichangia Wizara kwa ajili ya maandalizi na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Uchunguzi kuhusu Matumizi Halisi ya Fedha Zilizokusanywa Katika mahojiano na uchambuzi wa nyaraka za bajeti na matumizi ya Wizara juu ya fedha zilizochangishwa, Kamati Teule ilibaini kuwa mahitaji halisi ya maandalizi na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti yalikuwa Sh.207,042,000.00 ambayo Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini aliyaridhia. Kati ya Sh.207,042,000.00 zilizohitajika, Sh.35,500,000.00 zilitoka kwenye Kifungu cha *Project Coordination and Monitoring* cha Wizara. Kwa mantiki hiyo, Wizara ilibaki na upungufu wa Sh.171,542,000.00.

Kwa lengo la kuziba upungufu wa fedha ulioelezwa hapo juu, mnamo tarehe 25 Juni, 2011 Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini alituma kiasi cha Sh.171,542,000.00 kwa njia ya *TISS BOT* kwenye Akaunti Na. 5051000068 ya *GST* Dodoma. Fedha hizo zilipokelewa na GST Dodoma kwa stakabadhi Na. 02428 ya tarehe 25 Juni, 2011**.**

Hivyo, kufikia tarehe 25 Juni, 2011 Wizara ilikuwa tayari ina fedha za kutosha kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni bila ya kuhitaji michango kutoka kwenye Taasisi. Lakini pia, hiyo tarehe 25 Juni, 2011 ni siku tano tu (5) baada ya Wizara kutuma barua za kuomba michango kwenye Taasisi na ni siku 20 kabla ya Wizara kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni.

Hivyo Wizara ilikuwa na muda wa kutosha kuzuia michango isiendelee kama ingetaka kufanya hivyo, baada ya kuona fedha zilizokuwepo hadi wakati huo zilikuwa zinatosha kwa maandalizi na uwasilishaji wa Bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, Kama ilivyoainishwa katika maelezo chini ya Jedwali Na. 4 fedha zilizoingizwa katika Akaunti ya GST kwa ajili ya shughuli za uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti Bungeni ni Sh. 418,081,500.00. Kwa msingi huo, Kamati Teule ilijielekeza kuchambua namna Sh. 418,081,500.00 zilivyotumika kuanzia tarehe 14 Julai, 2011 siku moja kabla ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kusomwa hadi 20 Julai, 2011 siku ambayo fedha iliyobaki ilirejeshwa katika Akaunti ya *GST.* Uchambuzi wa matumizi hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Posho ya Kujikimu. Kamati ilibaini kwamba jumla ya watumishi 69 walilipwa posho ya kujikimu. Hii ni kwa mujibu wa orodha ya malipo ya posho ya kujikimu iliyowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati Teule. Jumla ya Sh.32,425,000.00 zililipwa kwa watumishi hao kwa muda wa siku saba (7), kuanzia tarehe 14 Julai, 2011 hadi 20 Julai, 2011.

(b) Posho ya Kikao. Malipo ya posho ya kikao yalifanyika kwa muda wa siku tano (5) kuanzia tarehe 14 Julai, 2011 hadi 18 Julai, 2011 kwa watumishi 243 ambapo jumla ya Sh.127,820,000.00 zilitumika. Hata Hivyo, Kamati ilibaini kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini alielekeza kuwa Maofisa sitini na mmoja (61) ndio waliotakiwa kwenda Dodoma kwa shughuli ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa watumishi 61 ndio walioidhinishwa kwenda Dodoma kwa shughuli ya Bajeti ya Wizara, Kamati ilishtushwa na ongezeko la watumishi 182 hadi kufikia 243 ambayo ni karibu asilimia 400 ya walioidhinishwa na Katibu Mkuu.

Kamati Teule ilipitia kwa kina mihtasari ya vikao ambavyo ndivyo vilikuwa msingi wa ulipaji wa posho ya kikao. Mihtasari ya vikao hivyo ni kuanzia tarehe 14 Julai, 2011 hadi 18 Julai, 2011; jumla ya vikao vitano (5). Kwenye mihtasari ya vikao vyote hivyo yafuatayo yalidhihirika:-

(i) Akidi ya kila kikao ni wajumbe mia moja na tatu (103).

(ii) Malipo ya posho ya kikao yalifikia wajumbe 243 kutoka 103, ziada ya wajumbe 140.

(iii)Hakuna yatokanayo na muhtasari wa kikao kilichopita.

(iv) Mihtasari yote haikuthibitishwa kuwa ni kumbukumbu sahihi za vikao vilivyopita.

Kamati Teule haikuweza kubaini ni mambo gani yaliyosababisha idadi ya walipwaji wa posho ya kikao kuongezeka kutoka 103 hadi kufikia 243. Muundo na maudhui ya mihtasari ya vikao vyote inaleta taswira kwa mtu wa kawaida kuwa iliundwa mahsusi kwa ajili ya kupata posho ya vikao.

(c) Chakula na Vinywaji. Mheshimiwa Spika, Kumbukumbu zilizowasilishwa kutoka Wizarani zinaainisha kuwa mnamo tarehe 19 Julai, 2011, Wizara ililipa kiasi cha Sh.17,480,000 taslim kwa *African Dreams Conference Centre Ltd.* ikiwa ni gharama ya chakula na viburudisho kwa watu 160 kwa siku tano za kazi.14 Malipo ya fedha hizo yalikiuka Kanuni Na. 86(1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2004. Kanuni hiyo inasema:-

*"86-(1) All disbursements of public money shall be properly vouched on the prescribed form of payment which vouchers must be typewritten or made out in ink or ballpoint pen and must contain or have attached thereto full particulars of the service for which payment is made, such as dates, numbers, distances, rates so as to enable them to be checked without references to any other document."*

Kwa mujibu wa Kanuni iliyonukuliwa hapo juu, dosari zinazotokana na malipo ya aina hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Hapakuwa na orodha ya watu mia moja sitini (160) waliopata huduma hiyo.

(ii) Malipo kufanyika kwa fedha taslim badala ya hundi.

(iii) Siku tano za kazi zilizoainishwa katika stakabadhi ya malipo hazibainishi tarehe husika kwani Bajeti ya Wizara iliwasilishwa tarehe 15 Julai, 2011 hadi 18 Julai, 2011 ambazo ni siku mbili (2) tu za kazi.

(iv) Kukosekana kwa Hati ya Madai na mchanganuo wa kuonesha jinsi madai hayo yalivyofikiwa.

(d) Mafuta ya Magari. Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilichambua stakabadhi za manunuzi ya mafuta yaliyotumiwa na magari 15 yaliyoshiriki katika shughuli ya uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini Bungeni Dodoma kama inavyoonekana kwenye Jedwali Namba 5.

**Jedwali 5: Orodha ya Magari ya Wizara ya Nishati na Madini yaliyotumika Dodoma kipindi cha Bajeti**

| Na. | Na.ya Gari | Tarehe | Lita | Shilingi | Jumla Ndogo | Jumla Kuu |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | STK 7925 | 13/7/2011 | 106 | 230,000.00 | | |
| | STK 7925 | 17/7/2011 | 106 | 210,000,00 | | |
| | STK 7925 | 17/7/2011 | 50 | 105,000.00 | 545,000.00 | 545,000.00 |
| 2. | STK 7920 | 13/7/2011 | 100 | 210,000.00 | | |
| | STK 7920 | 17/7/2011 | 100 | 210,000.00 | | |
| | STK 7920 | 18/7/2011 | 50 | 105,000.00 | 525,000.00 | 525,000.00 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3. | STK 3528 | 16/7/2011 | 50 | 105,000.00 | 105,000.00 | 105,000.00 |
| 4. | STK 8214 | 13/7/2011 | 100 | 210,000.00 | | |
| | STK 8214 | 17/7/2011 | 100 | 210,000.00 | | |
| | STK 8214 | 18/7/2011 | 50 | 105,000.00 | 525,000.00 | 525,000.00 |
| 5. | STK 5213 | 17/7/2011 | 100 | 210,000.00 | 210,000.00 | 210,000.00 |
| 6. | STK 8215 | 13/7/2011 | 23 | 40,000.00 | (DSM) | |
| | STK 8215 | 14/7/2011 | 109 | 230,000.00 | | |
| | STK 8215 | 16/7/2011 | 50 | 105,000.00 | | |
| | STK 8215 | 18/7/2011 | 100 | 210,000.00 | 585,000.00 | 585,000.00 |
| 7. | STJ 9429 | 13/7/2011 | 120 | 252,000.00 | | |
| | STJ 9429 | 17/7/2011 | 30 | 63,000.00 | | |
| | STJ 9429 | 17/7/2011 | 100 | 210,000.00 | | |
| | STJ 9429 | 17/7/2011 | 100 | 210,000.00 | 735,000.00 | 735,000.00 |
| 8. | STK 1801 | 13/7/2011 | 120 | 252,000.00 | | |
| | STK 1801 | 17/7/2011 | 50 | 105,000.00 | | |
| | STK 1801 | 18/7/2011 | 100 | 210,000.00 | | |
| | STK 1801 | | 30 | 63,000.00 | 63,000.00 | 630,000.00 |
| 9. | STK 8213 | 13/7/2011 | 120 | 252,000.00 | (DSM) | |
| | STK 8213 | 15/7/2011 | 50 | 105,000.00 | | |
| | STK 8213 | 17/7/2011 | 100 | 210,000.00 | | |
| | STK 8213 | - | 30 | 63,000.00 | 630,000.00 | 630,000.00 |
| 10. | STK 3525 | 18/7/2011 | 100 | 210,000.00 | 210,000.00 | 210,000.00 |
| 11. | STK 9868 | 13/7/2011 | 80.14 | 167,000.00 | (DSM) | |
| | STK 9868 | 16/7/2011 | 80.6 | 182,000.00 | 349,000.00 | 349,000.00 |
| 12. | STK 8186 | 21/7/2011 | 71.4 | 150,000.00 | 150,000.00 | 150,000.00 |
| 13. | STK 8184 | 21/7/2011 | 71.4 | 150,000.00 | 150,000.00 | 150,000.00 |
| 14. | STK 8191 | 17/7/2011 | 71.4 | 150,000.00 | 150,000.00 | 150,000.00 |
| 15. | STK 8189 | 21/7/2011 | 71.4 | 150,000.00 | 150,000.00 | 150,000.00 |

(d) Mafuta ya Magari. Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilichambua stakabadhi za manunuzi ya mafuta yaliyotumiwa na magari 15 yaliyoshiriki katika shughuli ya uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini Bungeni Dodoma, kama inavyoonekana kwenye Jedwali Namba 5.

Taarifa zilizoonyeshwa kwenye Jedwali Namba 5 zinadhihirisha yafuatayo:-

(i) Gari Na. STJ 9429 lilitumia kiasi cha lita 230 za mafuta kwa siku moja wakati kitabu cha kumbukumbu za safari (*Log Book*) hakionyeshi kama gari hii ilikuwa na safari ndefu nje ya Dodoma katika siku hizo.

(ii) Jumla ya magari 15 kutoka Wizarani peke yake inaashiria idadi kubwa ya watumishi walioshiriki kwenye zoezi la uwasilishaji wa Bajeti ambayo yanasababisha matumizi makubwa ya mafuta na matengenezo ya magari yasiyokuwa ya lazima.

(e) Vifaa vya Kuandikia. Shughuli hii ya uwasilishwaji wa Hotuba ya Bajeti Bungeni ilihusisha pia matumizi ya vifaa mbalimbali vya kuandikia. Vifaa Hivyo vilinunuliwa mjini Dodoma na Wizara kati ya tarehe 15 – 18 Julai, 2011 kwa gharama ya Sh. 625,020.00 kama ilivyoonyesha kwenye Kiambatisho.

(f) Takrima na Viburudisho. Kamati Teule ilipitia kwa kina nyaraka zinazohusiana na takrima iliyotolewa kwa Viongozi wa Wizara na pia viburudisho kwa wafanyakazi wa Wizara katika kipindi cha uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti Bungeni kati ya tarehe 14 - 20 Julai, 2011 kwa gharama ya Sh. 494,600.00 kwa ajili ya viburudisho na Sh. 8,000,000.00 kwa ajili ya takrima kwa Waziri na Naibu Waziri kama ilivyoonyesha kwenye Kiambatisho.

Mheshimiwa Spika, Kwa muhtasari, matumizi ya fedha zote zilizoingizwa kwenye Akaunti ya *GST* ni kama ifuatavyo:-Fedha zilizoingizwa Akaunti ya *GST* ....................... Sh. 418,081,500.00

**Matumizi:**
Posho ya kujikimu ................32,425,000.00
Posho ya kikao ................. 127,820,000.00
Chakula na vinywaji ............ 17,480,000.00
Mafuta ya magari...................... 754,000.00
Vifaa vya kuandikia .......... 625,020.00
Takrima na Viburudisho........ 8,494,600.00 .. ... Sh.192,598,620.00

Baki ...........................................Sh.225,482,880.00 Toa kiasi kilichorejeshwa Benki ............................Sh. 99,438,400.00
Salio halisi (fedha mkononi)...................................... Sh.126,044,480.00

Mheshimiwa Spika, Ukokotoaji wa matumizi ya fedha zilizoingizwa kwenye Akaunti ya *GST,* Dodoma umetokana na nyaraka zote za matumizi zilizowasilishwa na Wizara ya Nishati na Madini mbele ya Kamati Teule. Hata hivyo, nyaraka hizi hazikubainisha matumizi halisi ya kiasi cha Sh.126,044,480.00.

Kutobainika kwa matumizi halisi ya kiasi hicho cha fedha kuliifanya Kamati Teule imhoji tena kwa maandishi Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Nishati na Madini (Barua Kumb. Na.CBE.50/155/03A/94 ya tarehe 27 Oktoba, 2011). Maelezo yake ilikuwa ni kwamba matumizi ya Sh.126,044,480.00 yalikuwa kama ifuatavyo:-

(a) Sh. 50,143, 500.00 - Ziligharamia ukamilishwaji na marekebisho ya Randama kwa mara ya pili kwenye vikao vya Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini.

(b) Sh. 20,000,000.00 - Ziligharamia vikao vya Kamati Ndogo ya Wataalam waliobaki Dodoma kujibu Hoja za Wabunge baada ya vikao.

(c) Sh. 56,386,000.00 - Ziligharamia marekebisho ya *MTEF* ya Wizara baada ya mapendekezo ya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, maelezo yaliyotolewa na Mkurugenzi huyu hayakukubaliwa na Kamati Teule kwa sababu zifuatazo:-

(i) Hakukuwa na mchanganuo wowote wa matumizi na nyaraka za uthibitisho wa malipo.

(ii) Kiasi cha Sh.50,143,500.00 kilichoonyeshwa kama matumizi ya kurekebisha na kuwasilisha Randama kwa mara ya pili kwenye Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini iliyokutana Dodoma Juni, 2011 kimeonyeshwa mara mbili kwa matumizi yale yale.

Mheshimiwa Spika, kupitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu Wa Hesabu za Serikali Kuhusu Uchunguzi alioufanya.

Mwongozo kwa Kamati Teule kuhusu Hadidu ya Rejea ya Pili ulikuwa Kamati Teule ipitie Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Uchunguzi alioufanya kuhusiana na agizo la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuchangisha fedha Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kwa ajili ya kuwezesha maandalizi na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara hiyo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ili kukamilisha Hadidu ya Rejea ya Pili, Kamati Teule ilifanya yafuatayo:-

(a) Kupitia Katiba, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo na Nyaraka mbalimbali.

(b) Kupitia Taarifa ya Ukaguzi Maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(c) Kufanya mahojiano na mashahidi mbalimbali akiwemo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Watendaji wa Ofisi yake waliohusika katika ukaguzi huo na Katibu Mkuu Kiongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Majukumu ya Ofisi hii yameainishwa katika Ibara ya 143(2) ya Katiba.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008, Ofisi hii ina wajibu wa kukagua mahesabu ya fedha za Umma kwa niaba ya Bunge ili kuhakikisha kuwa Serikali inatumia fedha za Umma kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa namna yenye kuleta tija.15.

Mheshimiwa Spika, chini ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 200816 Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inafanya kaguzi zifuatazo:-

(a) Ukaguzi wa Kawaida (*Regularity Audit*);

(b) Ukaguzi wa Kiuchunguzi (*Forensic Audit*);

(c) Ukaguzi wa Ufanisi (*Performance Audit*); na

(d) Kaguzi Nyingine/Kaguzi Maalum (*Other Audits Special Audit*).

Kifungu cha 29(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008 kinaruhusu Taasisi yoyote kumwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi Maalum katika maeneo ambayo Taasisi hizo zinaona inafaa. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

*"The Controller and Auditor-General may, on request by any person, Institution, Public Authorities, Ministries, Departments, Agencies, Local Government Authorities and such other bodies to undertake any special audit."*

Kwa kutumia Kifungu hiki Katibu Mkuu Kiongozi aliona inafaa Ukaguzi Maalum ufanyike kwa kumtumia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ili kubaini uhalali wa utaratibu wa kuchangisha michango na kubaini matumizi ya fedha zilizochangishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalum wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama inavyofafanuliwa hapa chini:-

Namna Suala hili lilivyomfikia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Baada ya mahojiano kati ya Kamati Teule na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na baadaye mahojiano kati ya Kamati Teule na Katibu Mkuu Kiongozi; na kwa kutumia nyaraka mbalimbali za mawasiliano yaliyokuwepo kati ya Katibu Mkuu Kiongozi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati Teule ilibaini kuwa, Katibu Mkuu Kiongozi alimwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye Uchunguzi wa Awali *(Preliminary Investigation)* kwa kufanya Ukaguzi Maalum *(Special Audit)*. Katibu Mkuu Kiongozi alifanya hivyo kwa kutumia madaraka yake ya kisheria kwamba, yeye ndiye Mamlaka ya Nidhamu ya Katibu Mkuu aliyetuhumiwa, Ndugu David Kitundu Jairo.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kuipata nakala halisi ya Taarifa ya Ukaguzi Maalum, Kamati Teule ilizingatia Kanuni ya 81(a) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, 2009. Kanuni hii inaweka wazi utaratibu kwamba, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anapokuwa amekamilisha kufanya Ukaguzi Maalum aliyoombwa kwa maandishi, atakabidhi Taarifa yake ya Ukaguzi kwa aliyeomba. Katika suala hili, Katibu Mkuu Kiongozi ndiye aliyeomba kwa maandishi Ukaguzi huu Maalum ufanyike. Hivyo, Kamati Teule ilimwandikia Katibu Mkuu Kiongozi ili kupata nakala ya Taarifa hiyo na mnamo tarehe 9 Septemba, 2011 ilipata nakala ya Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa Kamati Teule ulibaini kwamba barua ya Katibu Mkuu Kiongozi kuomba kufanyika kwa Ukaguzi Maalum dhidi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa na Hadidu za Rejea mbili tu ambazo ni kuchunguza uhalali wa michango; na kuchunguza namna fedha hizo zilivyotumika. Hata hivyo, Taarifa ya Ukaguzi Maalum inaonesha kuwa palikuwepo na Hadidu za Rejea Kumi na Tano kama ifuatavyo:-

(i) Kufuatilia Wizara ya Nishati na Madini ili kupata idadi na majina ya Taasisi na Idara zilizoagizwa kuchangia fedha pamoja na kiasi husika.

(ii) Kuchunguza ili kujua namna uamuzi wa kuchangisha fedha kuziweka katika Akaunti ya *GST* ulivyofikiwa.

(iii) Kutembelea Taasisi na Idara zilizochangishwa fedha na kuangalia kama ziliagizwa kufanya hivyo na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini na upatikane ushahidi wa stakabadhi za kukiri mapokezi ya michango hiyo.

(iv) Kuulizia kutoka Taasisi na Idara zilizochangishwa fedha kama zililazimishwa kufanya hivyo au ilikuwa ni hiari na kama walitoa taarifa kwa mamlaka husika iwapo walilazimishwa.

(v) Kuchunguza chanzo cha fedha zilizochangwa na Taasisi/Idara na kuangalia kama zilikuwa katika bajeti zao za mwaka kwa kazi hiyo na kama malipo hayo ya michango yaliidhinishwa na Bodi za Wakurugenzi.

(vi) Kwa kila mchango, kufanya uhakiki wa nambari ya akaunti ya Benki na Tawi la Benki ambako fedha ziliwekwa.

(vii) Kupata Taarifa za Akaunti za Benki za *GST* na kufanya uhakiki wa usahihi wa taarifa hizo na kisha kukokotoa jumla ya fedha zote zilizochangwa na kuhamishiwa katika Akaunti ya *GST* – Dodoma.

(viii) Kuchunguza ili kubaini kama Wizara ilishawahi kuagiza michango ya namna hii kufanyika katika miaka ya nyuma na kufuatilia katika Taasisi na Idara zilizo chini ya Wizara ili kujua kiasi kilichochangwa. (Tanbihi: Maelezo yatakayotolewa yatasaidia uchunguzi wa kina kufanyika baada ya ripoti ya awali kuhusu tuhuma hizo kutolewa).

(ix) Kuuliza kwa mwenye akaunti ya Benki iliyopokea fedha *(GST)* ili kubaini kama aliagizwa kupokea fedha zilizochangwa na pia kama alipewa maagizo ya jinsi malipo yatakavyofanyika.

(x) Kupata maelezo ya malipo yaliyofanywa kutokana na fedha zilizochangwa na malipo hayo yaainishwe yakionesha madhumuni, majina ya waliolipwa na kiasi cha fedha kwa kila mmoja.

(xi) Kama sehemu ya kupata ukweli wa yale yaliyotokea, Maofisa waliohusika katika kadhia hii wafanyiwe usaili kwa kadiri itakavyoonekana inafaa.

(xii) Kuangalia kama malipo yaliyofanyika yamezingatia matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) na Kanuni zake za Mwaka 2005.

(xiii) Kuangalia kama waliolipwa huko Dodoma walikuwa wameshalipwa na Taasisi zao kwa kazi hiyo hiyo.

(xiv) Endapo malipo yaliyofanywa yatathibitika kuwa ni rushwa, taarifa itolewe kwa vyombo husika kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya Mwaka 2008.

(xv) Kuandaa Ripoti Maalum itakayowasilishwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi ikionesha matokeo ya uchunguzi pamoja na viambatanisho kwa kadiri itakavyoonekana inafaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia Hadidu za Rejea hizi Kumi na Tano, Kamati Teule ilipata mashaka, hivyo kuhoji kuhusu kutofautiana kwa idadi ya Hadidu za Rejea zilizopo kwenye barua ya Katibu Mkuu Kiongozi na zile zilizopo kwenye Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Alipohojiwa na Kamati Teule kuhusu tofauti ya Hadidu za Rejea hizo, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alijibu kwamba, Kanuni ya

80(1) inayohusu *Scope of Audit,* inampa mamlaka ya kurekebisha Hadidu za Rejea atakazopewa na aliyeomba Ukaguzi Maalum *(Special Audit).*

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya Kamati Teule na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:-

Swali: Labda tunaweza kuwa tunakaribia kwenye jibu lakini bado hatujafika. Ukurasa wa (v) na (vi) ni zile ambazo zimeitwa pale kuwa ni Hadidu za Rejea?

Jibu: Mheshimiwa Mwenyekiti ni *procedures.*

Swali: Mnabadilisha?

Jibu: *Yes!*

Swali: Ni *procedures* sasa, siyo Hadidu za Rejea?

Jibu: Ni *procedures.*

Swali: Kama zilivyoandikwa kwenye Ripoti, siyo Hadidu za Rejea ni *procedures*; kwa Kiswahili ni nini?

Jibu: Ni taratibu.

Kama inavyodhihirika katika sehemu hii ya mahojiano, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikiri kwamba, hizo hazikuwa Hadidu za Rejea kama alivyoeleza katika Taarifa ya Ukaguzi Maalum, bali ni taratibu.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilifanya pia mahojiano na Katibu Mkuu Kiongozi kuhusiana na kutofautiana kwa Hadidu za Rejea zilizopo kwenye barua ya agizo la kazi na zile zilizopo kwenye Taarifa ya Ukaguzi Maalum. Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano kati ya Kamati Teule na Katibu Mkuu Kiongozi:-

Swali: Sawa, halafu twende kwenye ukurasa wa pili wa *item number four*, unisomee neno linaloanzia 'pamoja na...'

Jibu: Pamoja na kuchunguza uhalali wa michango hiyo, pia uchunguze namna fedha hizo zilivyotumika.

Swali: Kwangu mimi hizi nadhani ndiyo Hadidu za Rejea ulizompatia?

Jibu: Ndiyo.

Swali: Ndizo ulizompatia hizi au kuna nyingine?

Jibu: Pamoja na zile za *details.*

Swali: Katibu Mkuu Kiongozi, naomba twende pamoja. Mimi nasoma barua yako ambayo umeandika, sijaona kiambatanisho hapa. Hii barua inajitosheleza, kwa hiyo, nilitaka twende pamoja tu na hapo nina *point* ya msingi sana. Sasa mimi nilitaka niulize, ndiyo hizi Hadidu za Rejea au unasema una nyingine tena kwa barua nyingine?

Jibu: Mheshimiwa Mwenyekiti, Hadidu za Rejea sijui ilikuwaje hapa... Hadidu za Rejea ambazo ni *detailed* ndiyo hizi. Nilitaka nikusomee hizi kwenye namba ambazo zipo *fourteen.*

Swali: Mimi bado; labda hujanielewa vizuri. Ulisema uliwasiliana na barua kwenda kwa Ofisi ya *CAG.* Sasa barua niliyonayo ndiyo hii ambayo tunaisoma wote kwa pamoja. Ambayo imeainisha Hadidu za Rejea, achana na Ripoti ya *CAG.* Mimi nazungumzia barua, kwenye Ripoti ya *CAG* tutakwenda baadaye. Sasa nilitaka niulize; kuna Hadidu za Rejea nyingine ambazo ulimwandikia mbali na barua hii?

Jibu: Sasa ndiyo nakwambia hivi; sijui imekuwaje katika *attachment,* lakini zilikuwa *detailed.* Hizi zilikuwa ni barua *summarized,* lakini zilikuwa *detailed* zile ambazo ziko kumi na nne… *I don't understand how it went about it…!*

Mheshimiwa Spika, katika mahojiano na Kamati Teule, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alisema kuwa alipewa Hadidu za Rejea mbili tu na zile zilizoandikwa kwenye ukurasa wa (v) – (vi) wa Taarifa ya Ukaguzi Maalum siyo Hadidu za Rejea bali ni taratibu zilizotumika kufanya Ukaguzi Maalum. Wakati huo huo Katibu Mkuu Kiongozi aliieleza Kamati Teule kwamba, alimpatia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Hadidu za Rejea kumi na nne. Huo ni mkanganyiko wa Hadidu za Rejea zilizotumika kufanya uchunguzi. Hata hivyo, Kamati Teule iliendelea kufanyia kazi Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Taarifa ya Ukaguzi Maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya suala hili, yapo masuala muhimu *(audit facts)* yaliyojitokeza ambayo aliyeomba kufanyika kwa Ukaguzi Maalum alipaswa kuyatumia kupima uhalali wa uchangishaji na namna fedha zilizochangishwa zilivyotumika. Mchanganuo wa masuala haya kutoka kwenye Taarifa ya Ukaguzi Maalum ni kama ifuatavyo: -

(a) Tarehe 9 Agosti, 2011, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikamilisha Ukaguzi wake na kukabidhi Taarifa ya Ukaguzi Maalum kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

(b) Kugharimia uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara Bungeni ni jukumu la Wizara yenyewe. Hivyo, Taasisi hazikupaswa kuchangishwa kwa sababu hazina kasma mahususi kwa ajili ya kuichangia Wizara inapowasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni; na kwamba, fedha zilizochangishwa zilitumika kwa ajili ya kulipia posho za vikao kwa Wajumbe 243 wa Wizara na Chakula cha Wajumbe kwa muda wa siku tano.

(c) Wizara imekuwa na utaratibu wa kuchangisha Taasisi zake kwa zaidi ya miaka miwili sasa.

(d) Jumla ya fedha zilizochangwa kwa ajili ya kuwezesha uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara Bungeni (2011/2012) ni Sh.418, 801,500.00. Ndani ya kiasi hicho, Taasisi zilichangia Sh.140, 000,000.00 na Wizara yenyewe ilichangia Sh.278, 801,000.00.

(e) Baadhi ya malipo yalifanyika pasipo kuzingatia matakwa ya kisheria katika maeneo yafuatayo: -

- Jumla ya Sh. 20,000,000.00 zililipwa kama *honoraria* kwa Watumishi wa Wizara kabla ya Bajeti kupitishwa Bungeni. Utaratibu huu ni kinyume na Kifungu Q.18 cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009, Toleo la Tatu.

- Kanuni ya 86(1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 zilizorekebishwa Mwaka 2004 zilikiukwa pale *EWURA* ilipotumia Sh.9,797,600.00 kwa kulipa fedha taslim badala ya hundi katika manunuzi ya chakula, malipo kutoonesha orodha ya watu waliohudumiwa, na hayakuonesha tarehe kamili za siku tano za gharama zilizolipwa.

(f) Ukaguzi Maalum haukuthibitisha kwamba Idadi ya Taasisi zilizochangishwa zilikuwa ishirini na kwamba jumla ya fedha zilizochangishwa zilikuwa Sh.1,000,000,000.00.

(g) Ukaguzi Maalum haukuthibitisha kuwepo kwa vitendo vya rushwa dhidi ya Waheshimiwa Wabunge kwa madhumuni ya kuwashawishi wapitishe Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kirahisi.

(h) Idadi ya Maofisa wa Wizara na Taasisi zake waliohudhuria mchakato wa kuwasilisha Hotuba ya Bajeti Bungeni Dodoma walikuwa kati ya 211 na 243 badala ya Maofisa 61 waliokuwa wameidhinishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini.

(i) Hapakuwepo na vikao vya makubaliano miongoni mwa Menejimenti za Taasisi zilizochangia na Uongozi wa Wizara kuhusu kiasi cha kuchangia.

(j) Kadhalika hapakuwepo na makubaliano kati ya Menejimenti za Taasisi zilizochangia na Bodi za Wakurugenzi wa Taasisi hizo kuidhinisha fedha kwa ajili ya shughuli iliyoombewa michango.

(k) Taarifa ya Ukaguzi Maalum juu ya suala la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuchangisha fedha kwenye Taasisi zake inaweza kubadilika baadaye endapo zitapatikana taarifa na vielelezo vya ziada.

(l) Mambo yaliyoibuliwa na ukaguzi huu maalum yatazingatiwa katika ukaguzi wa kawaida wa kisheria wa Fungu hili kwenye ukaguzi wa hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni, 2011 na kujumuishwa kwenye Ripoti ya Ukaguzi wa Wizara.

(m) Fedha zilizochangishwa zilitumika kwa ajili ya kulipia posho za vikao na chakula kwa Wajumbe kwa muda wa siku tano.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa yaliyojitokeza kwenye Taarifa ya Ukaguzi Maalum Kamati Teule ilifanya uchambuzi kwa yaliyojitokeza kwenye Taarifa ya Ukaguzi Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Mnamo tarehe 20 Julai, 2011 Katibu Mkuu Kiongozi alimwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi Maalum wa suala la uchangishaji wa Taasisi ndani ya Wizara ya Nishati na Madini. Ukaguzi huu ulikamilishwa katika muda wa siku kumi na tano kuanzia tarehe 25 Julai - 9 Agosti, 2011.

Kwa kuzingatia uzito wa suala hili na jinsi lilivyohusisha mifumo ya Kibenki na Taasisi mbalimbali ambazo zipo katika maeneo tofauti, Kamati Teule inaamini kuwa huu ulikuwa ni muda mfupi sana kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuweza kukamilisha jukumu hili kikamilifu. Hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alipohojiwa juu ya jambo hili, alikiri kwamba muda huu ulikuwa finyu kwake na kwamba alimjulisha Katibu Mkuu Kiongozi kwa maongezi ya mdomo juu ya ufinyu huo wa muda.

Madhara yaliyotokana na ufinyu huu wa muda ni kwamba, Taarifa ilitolewa kabla ya baadhi ya vielelezo muhimu kupatikana. Ndiyo maana Taarifa ya Matokeo ya Ukaguzi Maalum iliweka bayana kwamba "matokeo ya Ukaguzi huo yangeweza kubadilika endapo vielelezo vya ziada vingepatikana." Hii ni kwa sababu wakaguzi hawakuwa na muda wa kutosha kusubiri vielelezo.

(b) Taarifa ya Ukaguzi Maalum inaonesha kuwa Taasisi zilizochangishwa hazina kasma mahususi kwa ajili ya uchangiaji huu. Kamati Teule ilifanya uchunguzi katika Nyaraka za Mpango Kazi wa Mwaka 2010/2011 wa Wizara ya Nishati na Madini na kubaini kuwa Wizara ina Fungu lake la Bajeti linalojulikana kwa jina la Fungu 58 – 1003 - D01S04 *(to coordinate and prepare budget speech for the year 2010/11).* Kazi zilizokusudiwa katika Kasma hii ni pamoja na maandalizi ya Hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka husika.

Uchunguzi ulionesha pia kwamba Taasisi zilizochangishwa zinazo Kasma kwa ajili ya masuala ya maandalizi ya Bajeti za Taasisi zenyewe siyo kwa ajili ya kuichangia Wizara katika kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni. Ni kwa msingi huu ambapo Kamati Teule inaona kuwa Taasisi hazikupaswa kuchangishwa kwa sababu hazina Kasma Mahususi kwa ajili ya kuichangia Wizara inapowasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni. Maoni haya yapo pia kwenye Taarifa ya Ukaguzi Maalum. Haya ni miongoni mwa maoni ambayo Katibu Mkuu alipaswa kuyatumia kupima kuwepo ama kutokuwepo kwa kosa la kinidhamu katika utendaji wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini. Ni maoni ambayo Katibu Mkuu Kiongozi alipaswa kuyatoa pia kwenye Vyombo vya Habari ili "ukawaida" wa utaratibu wa uchangishaji uweze kupimwa vizuri.

Kuhusu Wizara kuwa na Utaratibu wa kuzichangisha Taasisi, Taarifa ya Ukaguzi Maalum imegusia kwamba Wizara imekuwa na utaratibu wa kuchangisha Taasisi zake kwa zaidi ya miaka miwili sasa. Kwa mfano, ili kuchangia uandaaji na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, Taasisi za *REA, TANESCO* na *TPDC* zilichangia jumla ya Sh.125,000,000.00. Yawezekana Katibu Mkuu Kiongozi aliuita utaratibu huu kuwa ni wa kawaida kwa sababu umekuwa ukitumika Wizara ya Nishati na Madini kwa muda wa zaidi ya miaka miwili sasa.

Ni maoni ya Kamati Teule kwamba hata kama utaratibu huu upo Wizarani kwa zaidi ya miaka miwili sasa, ni utaratibu ambao haujajengwa katika misingi ya Kisheria, Kanuni na Taratibu zingine za Fedha za Umma. Hivyo, ni utaratibu ambao hauwezi kuhalalishwa kwa kigezo cha kuwepo Wizarani kwa zaidi ya miaka miwili. Huu ni utaratibu unaopaswa kukomeshwa kabisa isipokuwa tu kwa kibali maalum kama ambavyo Waraka Namba 3 wa Machi, 2011 kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali unavyoelekeza.

(d) Uchunguzi wa Kamati Teule umebaini kuwa mnamo tarehe 14 Juni, 2011, Wizara iliandaa Bajeti kwa ajili ya kukamilisha zoezi la uandaaji na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti yake Bungeni. Zoezi hili lilikadiriwa kugharimu kiasi cha Sh.207,042,000.00. Hata hivyo, katika kipindi cha tarehe 14 Juni - 20 Juni, 2011, Wizara ilijitathmini na kuona kwamba kasma ambayo Wizara huitumia kwa shughuli za Bajeti *(Project Monitoring and Coordination)* ilibakiwa na Sh.35,500,000.00 hivyo kuwa na upungufu wa Sh.171,542,000.00. Ndipo tarehe 21 Juni, 2011 Wizara ikaamua kuziandikia Taasisi zake barua za kuomba michango ili kuziba pengo hilo. Hata hivyo, tarehe 25 Juni, 2011, kiasi cha Sh.171,542,000.00 kilitumwa na Wizara kwenye Akaunti ya *GST,* Dodoma kwa ajili ya shughuli za Bajeti yake kutoka kwenye Kifungu cha *OC.* Kwa mantiki hiyo, kuanzia tarehe 25 Juni, 2011 tayari Wizara ilikwishapata fedha za kutosha kukidhi gharama za mchakato wa uandaaji na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti yake.

Mahojiano kati ya Kamati Teule na Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Nishati na Madini katika eneo hili yalikuwa kama ifuatavyo:-

Swali: Kwa maana hiyo Mr. Swai, utakubaliana na mimi kwamba baada ya kupokea ile milioni 171...

Jibu: Ndiyo.

Swali: Kulikuwa hakuna haja kabisa ya kuwa na fedha nyingine kutoka kwenye Taasisi zenu, hilo nadhani tutakubaliana?

Jibu: Kama tungekuwa tumekwishazipata hizo fedha tungeweza kuwa na mahitaji, lakini siyo yale ya kusema kwamba lazima tuombe.

Swali: Hapa tunazungumza lugha moja!

Jibu: Ndiyo!

Swali: Kwamba, hapa kuna mtu alikuwa mahututi bin taaban anahitaji milioni 207.

Jibu: Ndiyo.

Swali: Akawa na wasiwasi kama atazipata.

Jibu: Ndiyo.

Swali: Lakini akatoa taarifa kwa wenzake, jamani eeh, naomba muwe tayari kunisaidia, ghafla fedha zake zinaingia, huyu mtu ana shida ya fedha tena?

Jibu: Ni kweli hakuna haja.

Swali: Kwa hiyo, ule umuhimu wa kuhitaji tena fedha za Taasisi ulikwisha kabisa?

Jibu: Ndiyo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo hapo juu, Wizara ilikuwa na fursa ya kuahirisha zoezi la uchangishaji kwa kuwa hakukuwa na mahitaji tena ya fedha kwa ajili ya matumizi ya zoezi la Bajeti, lakini kwa mshangao mkubwa haikufanya hivyo! Badala yake iliendelea kukusanya michango hiyo kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *REA* | Sh. | 50,000,000.00 |
| *TANESCO* | Sh. | 40,000,000.00 |
| *TPDC* | Sh. | 50,000,000.00 |
| Idara ya Mipango | Sh. | 278,081,500.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **418,081,500.00** |

Kipengele cha 2.4 cha Taarifa hii, kinaelezea namna fedha hizi zilivyotumika katika mchakato wa uandaaji na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara hiyo.

(e) Matokeo ya Ukaguzi Maalum yaliweka bayana pia kwamba, baadhi ya malipo kutokana na fedha zilizochangishwa yalifanyika pasipo kuzingatia matakwa ya Kanuni za Fedha za Umma katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kifungu Q.18 cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009 Toleo la Tatu, kinasomeka kama ifuatavyo:-

> *"Public Servants who make special contributions to the Service which lead to economy, or greater efficiency, or enhance reputation of the Service may be eligible for the payment of an honorarium of an amount which the Chief Executive Officer considers reasonable and justified under the circumstances."*

Kwa mujibu wa Kifungu tajwa hapo juu, mamlaka ya kuamua juu ya kiwango, sababu, wakati na namna ya kulipa honoraria yamewekwa kwa Mtendaji Mkuu. Hivyo, Mtendaji Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini ametumia Kifungu hiki kufanya malipo yanayozungumziwa licha ya kwamba hapakuwa na ufanisi ambao ungestahili malipo haya kwa kuwa Bajeti ya Wizara haikupitishwa.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati Teule kwamba, zoezi zima la Bajeti lingepimwa kwa kupitishwa kwa Bajeti ya Wizara Bungeni. Ni maoni ya Kamati Teule pia kwamba, Katibu Mkuu Kiongozi alitarajiwa kutumia Hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba malipo ya honoraria ya Sh.20, 000,000.00 yaliyofanyika bila tija kuwa ni kosa la kinidhamu.

(ii) Kwa kufanya malipo ya jumla ya Sh.9,797,600.00 kwa fedha taslimu, *EWURA* pia walikiuka Kanuni ya 86(1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 zilizorekebishwa Mwaka 2004 inayosomeka:-

> *"All disbursements of public money shall be properly vouched on the prescribed form of payment which vouchers must be typewritten or made out in ink or ballpoint pen and must contain or have attached thereto full particulars of the service for which payment is made, such as dates, numbers, distances, rates, so as to enable them to be checked without references to any other document."*

(f) Kamati Teule imeshangazwa na Hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyonukuliwa katika Taarifa ya Ukaguzi Maalum alioufanya na hatimaye kutumika na Katibu Mkuu Kiongozi katika uamuzi wake wa Uchunguzi wa Awali kwamba hakukuwa na uthibitisho wa idadi ya Taasisi zilizochangishwa kuwa ishirini na kwamba jumla ya fedha zilizochangishwa zilikuwa Sh.1,000,000,000.00.

Kamati Teule inaiona Hoja kubwa ni uhalali wa zoezi zima la uchangishaji wa Taasisi chini ya Wizara kwa madhumuni yaliyotajwa bila kuzingatia Sheria, Kanuni na taratibu, bila kujali idadi ya Taasisi zilizochangishwa wala kiwango cha fedha kilichochangishwa. Hata kama ingekuwa ni Taasisi mbili au tatu ndizo zilizochangishwa na fedha zilizochangishwa kuwa Sh.5, 000,000.00 au 10,000,000.00 bado suala la uhalali lingebaki pale pale.

Kamati Teule imepitia Hansard ya tarehe 18 Julai, 2011 na kuthibitisha kwamba hakuna mahali popote ambapo Mbunge yeyote alitaja idadi ya Taasisi kuwa ishirini. Hivyo, ili kufahamu Taasisi hizo 20 zilitoka wapi Kamati Teule ilimwuliza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na mahojiano yalikuwa kama ifuatavyo:-
Swali: …ume-*mention Hansard*, ni *Hansard* ya tarehe ngapi, ambako mimi *specifically* nataka unipeleke kwa Taasisi 20 maana *base* yako unasema …

Jibu: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi 20 *is very simple*, uki-*divide one billion by a 50 it gives you 20, mathematically.*

Swali: Naomba nijielekeze kwenye *Hansard. Hansard* hata ukikohoa inaandika umekohoa, ukicheka inaandika umecheka… Sasa tujielekeze pale hasa maana tusije tukatumia *logic.*

Jibu: Niseme tu kwamba, *the 20* kama ilivyokuwa *reported* na Vyombo vya Habari *it was mathematically derived, by dividing one billion by 50, it gives you 20.*

Swali: …umesema na *findings* zako umeonesha kwamba mmetumia *Hansard*…*concern* yangu hapo ni kweli kwenye *Hansard* zipo Taasisi 20 zilisemwa?

Jibu: Kwenye *Hansard* haioneshi moja kwa moja kwamba zipo Taasisi 20.

Swali: Labda kwa nyongeza hata ile *one billion* kwenye *Hansard* imeandikwa zaidi ya bilioni, *could be 10 billion!*

Jibu: … Hata magazeti yaliandika zaidi ya Taasisi 20.

Swali: Sasa nafikiri kwa sababu una-*refer* zaidi *Hansard* na ndiyo ambayo umeifanyia kazi kuliko magazeti twende na *Hansard*…

Jibu: Sawa.

Swali: Naomba tuangalie taarifa yako ya Ukaguzi, *page 15* ya Arabic. Naomba kama hutajali utusomee.

Jibu: "Kwa kuwa Ukaguzi Maalum haukupata uthibitisho wa kuwepo Taasisi 20 zilizotakiwa kuchangia fedha zilizofikia *one billion* kama ilivyorekodiwa …" Niseme tu kwamba nafikiri hapa *we erred.*

Swali: Kwa hiyo ilikuwa ni *error?*

Jibu: Yah!

(g) Kufuatia mahojiano na Waheshimiwa Wabunge na Watendaji wa Serikali, Kamati Teule iliridhika kwamba isingekuwa rahisi kwa wahojiwa hao kubaini vitendo vya rushwa. Yawezekana hata Ukaguzi Maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haukuweza kubaini vitendo hivyo vya rushwa kwa sababu Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi siyo Chombo Mahususi kwenye masuala ya rushwa. Utimilifu wa nadharia ya kuwepo kwa rushwa katika zoezi hili kwa kutumia fedha zilizochangishwa ungeweza kufikiwa endapo TAKUKURU kama Chombo cha Kisheria na chenye utaalam mahususi *(competent authority)* katika masuala ya rushwa wangehusishwa katika uchunguzi.

(h) Kamati Teule pia ilibaini idadi kubwa ya Maofisa wa Wizara na Taasisi waliohudhuria mchakato wa uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti Bungeni. Kwa mujibu wa Dokezo Sabili la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Wizara ilipaswa kupeleka Maofisa 44 na Maofisa 17 kutoka Taasisi zake na hivyo kufanya jumla ya Maofisa 61. Kinyume na agizo la Katibu Mkuu wa Nishati na Madini, Kamati Teule imebaini ongezeko la Maofisa 182 waliohudhuria mchakato wa Bajeti. Kama Bajeti ya uwasilishaji Hotuba ilikuwa kwa watu 61; ni dhahiri kwamba kuna matumizi yasiyo ya lazima ambayo ziada ya Maofisa 182 walilipwa.

(i) Kufuatia mahojiano na Watendaji wa Wizara na Taasisi, Kamati Teule inakubaliana na Hoja ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwamba hapakuwa na vikao vya maamuzi baina ya Wizara na Taasisi, wala Taasisi na Bodi kuhusiana na suala la michango, hivyo kukosekana kwa dhana ya ushirikishwaji. Hata hivyo, ni maoni ya Kamati Teule kwamba hata kama kungekuwa na ushirikishwaji bado kitendo cha kuchangisha kingekuwa kinyume na utaratibu.

(j) Katika kuchambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati Teule ilibaini kuwa taarifa hii inaweza ikabadilika kwa kuwa ilionekana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hakukamilisha taarifa yake kwa maelezo ya kukosekana kwa vielelezo vya ziada. Katika mahojiano, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikiri kuwa ni kweli kulikuwa na mashahidi walioahidi kuwasilisha kwake vielelezo vya ziada, jambo ambalo halikutimizwa hadi alipowasilisha Taarifa yake kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Ni dhahiri kuwa, endapo mashahidi watawasilisha vielelezo vya ziada, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaweza kubadilika. Hata hivyo, kwa nyaraka hizo tu zilizopatikana na kuchambuliwa na Kamati Teule pamoja na mahojiano yaliyofanyika baina ya Kamati Teule na mashahidi mbalimbali imebainika kwamba malengo ya uchunguzi kwa kiasi kikubwa yamefikiwa.

(k) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameeleza kwamba mambo yaliyoibuliwa katika Ukaguzi Maalum yatazingatiwa katika ukaguzi wa kawaida wa kisheria wa Fungu 58 kwenye ukaguzi wa Hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni, 2011 na kujumuishwa kwenye Ripoti ya Ukaguzi wa Wizara. Ni maoni ya Kamati Teule

kwamba Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ifuatilie utekelezaji wa maelezo haya itakapofika wakati wa kujadili Hesabu za Fungu 58 na Mafungu mengine.

(l) Taarifa ya Ukaguzi Maalum imebainisha kuwa Wizara ya Nishati na Madini ilikusanya jumla ya Sh.418, 081,500.00 kupitia Akaunti Na. 5051000068 ya *GST*. Kiasi hiki cha fedha kilikuwa ni kwa ajili ya kuwezesha uandaaji na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini Bungeni tarehe 15 na 18 Julai, 2011. Mapokezi ya fedha hizi katika Akaunti ya *GST* yalikuwa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| *REA* | Sh. | 50,000,000.00 |
| *TANESCO* | Sh. | 40,000,000.00 |
| *TPDC* | Sh. | 50,000,000.00 |
| Idara ya Mipango | Sh. | 278,081,500.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **418,081,500.00** |

Kiasi hiki kina ziada ya Sh.211, 081,500.00 kwa sababu fedha zilizokuwa zikihitajika kwa ajili ya kukamilisha zoezi hili zilikuwa ni Sh.207,042,000.00. Aidha, uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi Maalum unabainisha zaidi kwamba kati ya Sh.418,081,500.00, Sh.127,820,000.00 zilitumika kwa ajili ya malipo ya posho za vikao kwa Maofisa wa Wizara waliokuwepo Dodoma. Fedha zilizobaki benki ni Sh.99,438,380.00. Kwa maelezo yaliyotolewa hapo juu bakaa ya fedha hizi ilipaswa kuwa Sh.290,261,500.00 badala ya kuwa Sh.99,438,380.00. Kwa maana hiyo, Sh.190,823,120.00 bado hazijarejeshwa benki.

Kamati Teule ililazimika kuitisha nyaraka zaidi kutoka Wizarani kwa sababu ilibaini kwamba kwa kutumia Taarifa ya Ukaguzi Maalum peke yake kuna kiasi cha fedha (Sh.190,823,120.00) ambacho hakijulikani kilivyotumika na wala hakipo benki. Ni katika kuchambua nyaraka hizo ndipo Kamati Teule ilibaini kwamba yapo matumizi mengine ambayo Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali hakuyabaini. Matumizi haya yanafafanuliwa zaidi katika Kipengele cha 2.4 cha Taarifa hii.

Kuhusu Sh.99,438,380.00 zilizorejeshwa kwenye akaunti ya GST baada ya shughuli za kuwasilisha Bajeti, Kamati ilipata maelezo ya ziada kwamba Sh.68,000,000.00 zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa Jengo la *Rest House* na Ofisi ya Waziri na Naibu Waziri, Dodoma. Kamati ilihoji pia uhalali wa kutumia fedha hizi kwa shughuli za ujenzi na kupata majibu kwamba *GST* iliandika barua Wizarani kwamba kuna mkandarasi ana madai ya siku nyingi ndipo Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini akawapa kibali cha kulipa Sh.68,000,000.00 kati ya Sh.99,438,380.00 zilizokuwa zimerejeshwa benki.

Mheshimiwa Spika, upungufu uliojitokeza katika Hitimisho la Katibu Mkuu Kiongozi: Katika kupitia Taarifa ya Ukaguzi Maalum, Kamati Teule ilibaini kuwa Katibu Mkuu Kiongozi hakuyatumia ipasavyo maudhui ya Taarifa hiyo katika hitimisho lake. Mtazamo huu unatokana na sababu kwamba yapo masuala mbalimbali ambayo Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini alistahili kupewa notice ili kuyajibu kwa taratibu za kiutumishi wa umma kama ifuatavyo:-

(a) Kwa nini Wizara ilichangisha fedha kutoka kwenye Taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya kuwezesha uandaaji na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti yake Bungeni wakati ilijua kwamba Taasisi hizo hazina kasma kwa ajili ya uchangiaji huo?

(b) Kwa nini Wizara iliendelea kupokea michango na kuitumia wakati upungufu wa fedha uliokuwepo tayari ulikwishaondolewa kwa kuletewa fedha zake za OC?

(c) Ni kwa nini Wizara haikuandaa vikao vya makubaliano miongoni mwa Taasisi zilizotegemewa kuchangia ili kuridhia kiasi cha kuchangia na muda wa kuchangia? Aidha, Katibu Mkuu Kiongozi alipaswa kuyatumia maudhui hayo kupima uhalali wa utaratibu wa uchangishaji ulioendeshwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini. Ni kwa kufanya hivyo ambapo Katibu Mkuu Kiongozi angebaini kama kutenda jambo ambalo siyo halali ni kosa la kinidhamu au la kwa watumishi wa umma! Bahati mbaya Katibu Mkuu Kiongozi alitoa hitimisho ambalo halikutokana na matokeo ya Ukaguzi Maalum kuhusu uhalali wa uchangishaji na matumizi halisi ya fedha zilizochangishwa. Kwa maana hiyo, hitimisho la Katibu Mkuu Kiongozi halikuwa sahihi.

Mheshimiwa Spika, hitimisho la Katibu Mkuu Kiongozi kwa Vyombo vya Habari alipotoa Taarifa ya Matokeo ya Uchunguzi wa Awali kuhusu jambo hili ni kama ifuatavyo:-

"Sitaweza kuendelea na hatua ya pili ya kumpa taarifa ya tuhuma *(notice)* na Hati ya Mashitaka kwa sababu Bwana David Kitundu Jairo, hajapatikana na kosa la kinidhamu *(disciplinary offence)* kwa mujibu wa Taarifa ya Ukaguzi Maalum."

Hitimisho hili la Katibu Mkuu Kiongozi lilifuata baada ya maelezo ya utangulizi kutolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Vyombo vya Habari kama ifuatavyo:-

"Chimbuko la Ukaguzi huu Maalum lilijitokeza katika Kikao cha Bunge katika kujadili Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini tarehe 18 Julai, 2011. Katika kikao cha tarehe hiyo, Waheshimiwa Wabunge walihoji uhalali wa Wizara kuomba michango kutoka kwenye Taasisi zilizo chini ya usimamizi wake. Vilevile, Waheshimiwa Wabunge walihoji matumizi ya fedha hizo na kuzua hisia za rushwa zenye lengo la kuwashawishi baadhi yao ili Bajeti ya Wizara ipite kirahisi…

Ukaguzi huu Maalum ulifanyika kulingana na Hadidu za Rejea zilizokuwa na lengo la kutafuta ukweli kuhusu tuhuma za michango na matumizi ya fedha zilizokuwa zimechangwa na Wizara ya Nishati na Madini…

Ukaguzi Maalum umebaini kuwa idadi ya Taasisi zilizopelekewa barua za kuchangia gharama za kuwasilisha Bungeni Bajeti ya Wizara ni nne tu na siyo ishirini kama tuhuma zilivyodai. Vilevile Ukaguzi Maalum umebaini ya kuwa jumla ya fedha zilizochangwa kutoka kwenye Taasisi zilizochangishwa ni Sh.149,797,600 tu."

Mheshimiwa Spika, kauli hizi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinaeleza mambo ya msingi kwamba, Ukaguzi Maalum ulijengwa katika misingi ya Hadidu za Rejea alizokuwa amepewa na Katibu Mkuu Kiongozi. Hadidu za Rejea hizo zilikuwa ni kuhusu Uhalali wa Uchangishaji na matumizi halisi ya fedha zilizochangishwa. Lakini hitimisho lililotolewa kwa Vyombo vya Habari halikuwa na maelezo yoyote kuhusu kilichobainika katika uhalali wa utaratibu na matumizi halisi ya fedha zilizochangishwa. Ndiyo maana Kamati Teule inasema Katibu Mkuu Kiongozi hakupaswa kuizingatia Taarifa ambayo aliitoa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Vyombo vya Habari tarehe 23 Agosti, 2011, badala yake alipaswa kuzingatia Taarifa kamili ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama ilivyowasilishwa kwake tarehe 9 Agosti, 2011 kwa sababu hiyo ndiyo Taarifa ya Msingi aliyoiomba kwa maandishi na ndiyo iliyokuwa na majibu ya Hadidu za Rejea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipitia Taarifa ya Ukaguzi Maalum na kujiridhisha namna suala la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini lilivyomfikia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mawanda yaliyoandaliwa kukidhi ukaguzi na namna hitimisho la Mamlaka ya Nidhamu lilivyotolewa juu ya suala lenyewe, Kamati Teule ina maoni yafuatayo:-

(i) Mamlaka ya Nidhamu ilikuwa sahihi kumwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi Maalum juu ya suala hili kwa mujibu wa Kanuni ya 36 ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003 na kwa Mujibu wa Kanuni ya 79(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, 2009. Hivyo, tarehe 20 Julai, 2011 Katibu Mkuu Kiongozi aliiandikia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya uchunguzi kuhusu uhalali wa malipo yahusuyo mchakato wa kuwasilisha Bungeni Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini 2011/12. Hadidu za Rejea zilizokuwemo katika barua hiyo ni kuchunguza uhalali wa michango hiyo na namna fedha hizo zilivyotumika.

(ii) Katika mahojiano na Kamati Teule, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alisema kuwa Hadidu za Rejea zilikuwa mbili (Uhalali wa Michango na Matumizi) na kwamba zile 15 zilizoorodheshwa katika Taarifa ya Ukaguzi Maalum siyo Hadidu za Rejea bali ni taratibu. Bila kujali kama kulikuwa na Hadidu za Rejea 15 au taratibu 15, hitimisho la Taarifa ya Ukaguzi Maalum lilipaswa kueleza uhalali wa uchangishaji huo.

(iii) Taarifa ya Ukaguzi Maalum haikuweza kuelezea matumizi ya fedha zilizokusanywa kwa ukamilifu, kwa kuwa kati ya Sh. 418,081,500.00 zilizokusanywa, Taarifa hiyo ilifafanua matumizi ya jumla ya Sh. 227,258,380.00 tu ambapo Sh.127,820,000.00 zilitumika kwa ajili ya malipo ya posho ya vikao na Sh.99,438,380.00 zilirejeshwa Benki. Matumizi haya yanaonesha tofauti ya Sh.190, 823,120.00 ambayo Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali haikuielezea. Baada ya kubaini tofauti hii kubwa, Kamati Teule ikaitisha nyaraka na kufanya mahojiano na watendaji wa Wizara na hatimaye ikabaini matumizi ya ziada kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| Posho ya Kujikimu | Sh. | 32,425,000.00 |
| Chakula na vinywaji | Sh. | 17,480,000.00 |

| | | |
|---|---|---|
| Mafuta ya magari | Sh. | 5,754,000.00 |
| Vifaa vya kuandikia | Sh. | 625,020.00 |
| Takrima na viburudisho | Sh. | 8,494,600.00 |
| **JUMLA** | **Sh.** | **64,778,620.00** |

Kiasi hiki cha Sh.64,778,620.00 kikitolewa kutoka kwenye Sh.190,823,120.00 kinabaki kiasi cha Sh.126,044,500.00 ambacho Kamati Teule ilikihoji pia kama inavyoonekana katika Kipengele cha 2.4 cha Taarifa hii.

(iv) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikuwa sahihi kurejesha Taarifa ya Ukaguzi Maalum kwenye Mamlaka ya Nidhamu kwani ndiyo iliyomwomba. Hata hivyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 81(a) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma, 2009, angeweza kukabidhi Taarifa hiyo kwa Mamlaka nyingine ambayo angeona inafaa kuikabidhi.

(v) Taarifa ya Ukaguzi Maalum imeweka wazi dosari zilizokuwepo ikiwa ni pamoja na Wizara kuzitwisha Taasisi gharama za kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake wakati Taasisi hizo hazina kasma mahususi kwa ajili ya kuchangia. Ukaguzi Maalum ulipaswa kutoa angalizo kwamba Wizara zinapokuwa hazina fedha za kutosha kutekeleza mipango yao zinapaswa kuzingatia taratibu za kisheria mathalani Kanuni ya 4(4) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001. Ukaguzi Maalum ulipaswa pia kutumia kigezo cha Waraka Namba 3 wa Katibu Mkuu wa Hazina wa Mwaka 2011 kama mojawapo ya vigezo vya kupima uhalali wa utaratibu wa uchangishaji.

(vi) Katika sehemu ya ushauri na hitimisho, Taarifa ya Ukaguzi Maalum haikuzingatia yaliyojitokeza ndani ya Taarifa ili kutoa majibu kwa Hadidu za Rejea badala yake ushauri pekee unaonekana kuegemea katika idadi ya Taasisi kuwa 20 na kiwango cha fedha zilizochangwa kuwa Sh.1,000,000,000.00. Hatua hii imesababisha upotoshaji mkubwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi ambaye naye alitumia ushauri huu kama msingi wa Maamuzi yake katika Uchunguzi wa Awali alioufanya. Hata hivyo baada ya kukabidhiwa, Katibu Mkuu Kiongozi alipaswa kuitumia Taarifa ya Ukaguzi Maalum kwa ujumla wake badala ya kipengele cha ushauri ambacho ni upotoshaji.

Mheshimiwa Spika, Hadidu ya Rejea ya Tatu iliitaka Kamati Teule kufanya yafuatayo:-

(a) Kuchunguza mfumo wa Serikali kujibu Hoja zinazotolewa Bungeni na taratibu za kuliarifu Bunge matokeo ya utekelezaji wa Hoja hizo.

(b) Kuchunguza usahihi wa utaratibu uliotumiwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwa suala la Ndugu David Kitundu Jairo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini.

(c) Kubaini kama utaratibu huo umeathiri dhana ya haki na madaraka ya Bunge.

Katika kushughulikia Hadidu hii, Kamati ilifanya yafuatayo:-

(a) Kupitia Katiba, Sheria na Kanuni za Bunge.

(b) Kufanya mahojiano na mashahidi wa aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sura ya 2 inaelekeza kuwa, Bunge ndicho Chombo Kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kina madaraka kwa niaba ya Wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Vyombo vyake vyote katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba. Katika kutekeleza madaraka yake Bunge linaweza:-

(a) Kumwuliza Waziri yeyote swali lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake.

(b) Kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti.

(c) Kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano; na kutunga Sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.

(d) Kutunga Sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kuwapo Sheria.

(e) Kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Ibara ya 89(1) imetoa mamlaka kwa Bunge kutunga Kanuni za Kudumu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza shughuli zake. Kwa sasa Bunge linatumia Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Bunge zinaweka wazi kuwa zipo Hoja zifuatazo:-

(a) Hoja za Serikali ambazo hutolewa na Mawaziri kupitia njia kadhaa kama vile Miswada ya Sheria na Makadirio ya Matumizi (Hotuba za Bajeti).

(b) Hoja Binafsi zitolewazo na Kamati kama vile Miswada Binafsi ya Sheria au Marekebisho ya Miswada ya Sheria ya Serikali.

(c) Hoja Binafsi ambazo hutolewa kupitia Miswada Binafsi ya Wabunge na wakati wa mijadala kama vile kurekebisha Muswada uliowasilishwa Bungeni, kubadilisha Makadirio ya Matumizi wakati wa Kamati ya Matumizi, "kutoa shilingi" katika Bajeti ya Wizara, kuahirisha shughuli za Bunge zinazoendelea ili kujadili jambo linalohusiana na haki za Bunge.

(d) Hoja ambazo zinaweza kutolewa na Mbunge au Waziri kama vile kutengua Kanuni, kuahirisha mjadala unaoendelea Bungeni, kuahirisha shughuli za Bunge zinazoendelea ili kujadili jambo la dharura na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kama Katiba inavyoelekeza, Wabunge hujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mikutano ya Bajeti. Kanuni za Bunge zinaainisha taratibu za kujadili utekelezaji wa kila Wizara kwamba:-

(a) Mjadala huanza kwa Waziri kuwasilisha mapendekezo ya Bajeti ya Wizara yake na kuomba Bunge liyapitishe.

(b) Wabunge hupata nafasi ya kuchangia mmoja mmoja ambapo masuala mbalimbali huibuliwa.

(c) Mjadala ukimalizika Waziri mhusika hupata nafasi ya kuhitimisha Hoja yake kwa kutoa ufafanuzi wa masuala yaliyojitokeza.

(d) Bunge huingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi ambapo Wajumbe huhojiwa Kifungu kimoja baada ya kingine na kukipitisha.

Iwapo Mbunge aliuliza au kuzungumzia suala fulani wakati wa kuchangia mjadala wa jumla na Waziri hakulijibu au hakulijibu kikamilifu wakati anahitimisha Hoja yake, Mbunge huyo anaweza akahoji tena wakati wa Kamati ya Matumizi na asiporidhika na ufafanuzi wa Waziri ndipo taratibu za "kutoa shilingi" zinaweza kufuata.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali wakati Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, (Mb.) anachangia alihoji uhalali wa utaratibu wa Wizara ya Nishati na Madini kuzichangisha fedha Taasisi zilizo chini yake kwa ajili ya kufanikisha mawasilisho ya Bajeti.

Mitazamo ya watu waliohojiwa na Kamati Teule inatofautiana kuhusiana na iwapo suala hili lilikuwa Hoja mahususi ambayo ilitakiwa kujibiwa na Serikali. Kundi la Kwanza lina msimamo kwamba katika suala la Ndugu David Kitundu Jairo hakukuwa na Hoja mahususi ya Bunge ambayo Serikali ilitakiwa irudi Bungeni kuelezea utekelezaji wake kwa sababu liliondolewa Bungeni na kupelekwa katika mamlaka za juu ili lifanyiwe kazi kwa taratibu za kiutawala. Kundi la Pili lina msimamo kwamba suala hilo lilikuwa ni Hoja ambayo Serikali ilitakiwa kurudisha Bungeni majibu ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, waliotoa maoni katika Kundi la Kwanza wanaeleza kwamba ili Bunge liazimie kuwa suala fulani liende Serikalini ni lazima liwe katika mfumo wa Azimio la Bunge ndipo Serikali itabanwa na Ibara ya

63(2) kurudi Bungeni kulitolea majibu. Kwa suala la Ndugu David Jairo, Bunge halikuazimia kwamba baadaye Serikali irudi Bungeni kutoa majibu ya Serikali, hivyo hakukuwa na Hoja.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji katika Kundi la Kwanza waliendelea kusema kuwa shughuli za Bunge zinakwenda kwa misingi ya Hoja. Hoja inawasilishwa, inaungwa mkono, inajadiliwa na kisha inaamuliwa, na kama suala linahusu Serikali, basi Serikali inaliahidi Bunge kuwa italifanyia kazi na kutaja muda *(time frame).*

Kwamba kilichojitokeza Bungeni tarehe 18 Julai, 2011 wakati Wizara ya Nishati na Madini imewasilisha Makadirio yake ni Hoja za Wabunge wengi kuwa Serikali haijaonesha umakini wa kutatua tatizo la umeme katika kipindi cha muda mfupi. Ndipo Waziri Mkuu akatumia busara kuomba Hoja ya Waziri wa Nishati na Madini iahirishwe ili Serikali irudi kwenye *drawing board.*

Mheshimiwa Spika, Wakifafanua zaidi walisema kuwa Hoja zote zinazotolewa Bungeni zinaanza kwa kuwasilishwa, kuungwa mkono, kujadiliwa na mwisho wake Bunge linafanya Maamuzi. Suala la Ndugu David Kitundu Jairo lilizuka wakati Hoja ya Wizara ya Nishati na Madini inajadiliwa. Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, (Mb.) hakutoa Hoja binafsi, ilikuwa ni sehemu ya majadiliano ya Hoja ya Wizara. Mmoja wao alisema:-

> "… Waziri Mkuu hakusema naomba kutoa Hoja kwamba jambo hili liende sasa kwa Mheshimiwa Rais atakapolishughulikia litaletwa hapa Bungeni ili lifanyiwe uamuzi au liletewe taarifa …"

Mheshimiwa Spika, waliotoa maoni katika Kundi la Pili walieleza kwamba, kwa kuwa suala la michango liliibuka Bungeni, Waziri Mkuu akaomba kuliondoa na akakubaliwa na Wabunge karibu wote waliokuwemo Bungeni, hivyo hilo ni Azimio tosha lililohitaji kutolewa majibu na Serikali. Katika kufafanua zaidi, mmoja wao alisema:-

> "… hili jambo limetoka kwenye vinywa vya watu na likasikika nchi nzima, yule Mwananchi wa kawaida aliyesikia hajui juu ya utaratibu wako huo kwamba Azimio lazima liungwe mkono, watu wasimame kumi hajui, lakini anachojua; je, utaratibu ule ni wa kawaida? Unapaswa kuendelea au haupaswi kuendelea?"

Mheshimiwa Spika, Mtaalam mwingine aliyebobea katika masuala ya Bunge alisema kuwa kinachozungumzwa Bungeni na Hoja za Wabunge zinazotolewa wakati wa mijadala mbalimbali huelekezwa kwa Serikali ambayo nayo imo Bungeni, hivyo Serikali hutakiwa kutoa majibu humo humo Bungeni.

Wakisisitiza kuhusu msimamo wa Kundi la Pili, baadhi yao walisema kwamba ndani ya Bunge kuna mambo mengi yanayoibuliwa, lakini siyo lazima Wabunge wanyanyuke na kuunga mkono kila jambo. Kwa suala la Mheshimwa Beatrice Shellukindo, (Mb.) walifafanua kwa kusema:-

> "… Kauli aliyoitoa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, (Mb.) na *document* aliyoitoa mbele ya Bunge, *it was enough evidence* kuonekana kwamba Serikali lazima i-*intervene* katika hilo tendo, kwa vyovyote vile usingengoja tena Hoja ile ipanuliwe zaidi… Serikali iliyo makini ikisoma *mood* ya Wabunge, Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni anaweza akalichukua kama Bunge lina-*demand* hili jambo, bila ya kuingia utaratibu wa kuungwa au kutoungwa mkono…"

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imepitia Kanuni zinazoainisha Hoja zinazotolewa Bungeni. Zipo Hoja ambazo kabla ya kuwasilishwa Bungeni zinapelekwa kwanza kwenye Kamati inayohusika na zile ambazo hazipelekwi kwenye Kamati ya Bunge. Taratibu za kuwasilisha, kujadili na kupitishwa kwa Hoja za namna hii zimefafanuliwa katika Kanuni ya 53(6) na (7) kama ifuatavyo:-

(a) Hoja kutolewa na kuungwa mkono.

(b) Maoni ya Kamati husika.

(c) Maoni ya Kambi ya Upinzani au Serikali kama Hoja ni ya Kambi ya Upinzani.

(d) Mjadala wa jumla.

(e) Uamuzi wa Bunge.

Hata hivyo, wakati wa kuchangia mijadala mbalimbali Bungeni au kupitia Maelezo Binafsi ya Wabunge, Wabunge huibua masuala muhimu ambayo kwa uzito wake Serikali hulazimika kuyatolea ufafanuzi hapo hapo au kutoa ahadi ya kufuatilia au kulitolea maelezo mahususi siku nyingine kupitia Kauli za Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imebaini kuwa ipo mifano kadhaa ya kuthibitisha hili kama ifuatavyo:-

(a) Mwaka 2011 katika Mkutano wa Bunge la Bajeti, Wabunge mbalimbali waliochangia walionesha kutoridhishwa na ufinyu wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na matatizo ya Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA). Waziri Mkuu alilazimika kutumia sehemu ya Kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu tarehe 4 Agosti, 2011 kuliarifu Bunge kuwa Serikali imechukua hatua zifuatazo: -

(i) Imeongeza Sh.95,000,000,000.00 katika Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi; na

(ii) Imewaagiza *CAG, DCI* na TAKUKURU waanze uchunguzi mara moja kuhusiana na UDA.

Kwa maneno yake, Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Pinda alisema: -

"… yaliyojitokeza ni mambo ambayo yameonesha uzito na sisi Serikalini tukaona pengine ni vizuri …tuyaweke bayana mambo fulani fulani …jana, Serikali ililazimika kukutana na kuangalia uwezekano wa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi …kukutana kwa Serikali ilikuwa ni muhimu ili kuweza kujadili michango mingi mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge...

Kikao cha jana kimewezesha Serikali kufanikiwa kupata fedha kiasi cha Shilingi bilioni 95 ambazo zitatumika katika maeneo ya Reli ya Kati, Kampuni ya Ndege Tanzania na Usafiri wa Majini yaani Meli katika Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa...

...suala lingine lililoongelewa kwa hisia kali na Waheshimiwa Wabunge ni matatizo ya Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA). Serikali imesikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge na kwa sasa imeshawaagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkurugenzi wa Makosa ya Jinai na Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa kuanza uchunguzi mara moja…"

(b) Wakati huo huo wa Mkutano wa Bajeti mwaka 2011 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi nayo ilionekana kuwa imetengewa fedha kidogo na Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia walilalamikia hali hiyo kuwa kiasi cha fedha kilichotengwa hakiendani na hali halisi na changamoto zinazoikabili Wizara hiyo. Baada ya mjadala wa jumla kukamilika Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda, (Mb.) alisimama na kuliarifu Bunge kuwa kutokana na michango ya Waheshimiwa Wabunge, Serikali imeruhusu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi badala ya kuzipeleka Mfuko Mkuu wa Hazina fedha ambazo Wizara itazikusanya, Wizara hiyo izitumie fedha zote kwa ajili ya shughuli za Wizara. Waziri Mkuu alisema naomba kunukuu.

"…Michango ya Waheshimiwa Wabunge imegusa maeneo karibu yote ambayo ndiyo kero hasa kwa Watanzania. (Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi) amepata Bajeti ndogo kuliko hata mwaka jana… jana tukiwa kwenye Cabinet tumemwidhinishia huyu mama kwamba wewe mama ile fedha yote ambayo utakuwa unakusanya kutokana na shughuli zako za ardhi baki nayo yote, chukua yote ikusaidie wewe katika uendeshaji wa Wizara hiyo…"

Katika mifano yote hii utaratibu wa kuwasilisha Hoja, kuungwa mkono, kujadiliwa na hatimaye kupitishwa na Bunge haukufanyika, lakini kutokana na uzito wa masuala husika Serikali iliyafanyia kazi na kuliarifu Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imeridhika kuwa suala lililoibuliwa Bungeni na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, (Mb.) lilikuwa ni Hoja ambayo kwa uzito wake na kwa hisia zilizotawala mjadala huo, Serikali ilitakiwa kuifanyia kazi na kuitolea taarifa ya utekelezaji Bungeni hata kama haikushughulikiwa kufuatana na masharti ya Kanuni ya 53 na 54 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usahihi wa utaratibu uliotumiwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwa suala la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu David Kitundu Jairo: Kwa mujibu wa Katiba, Bunge lina sehemu mbili; Rais na Wabunge. Sehemu ya Pili ya Bunge *(National Assembly)* ina Wabunge wa kawaida na Mawaziri ambao

ndiyo wawakilishi wa Serikali. Hoja na kauli zote zinazotolewa na Wabunge wote katika kutekeleza majukumu yao Bungeni huelekezwa kwa Serikali ambayo nayo imo Bungeni. Vilevile Serikali hulazimika kujibu na kufafanua masuala yote yanayoibuliwa na Wabunge ndani ya Bunge hata kama masuala hayo yamewagusa moja kwa moja Watendaji wa Serikali ambao hawamo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Bunge zinaweka wazi utaratibu ambao Hoja za Wabunge zitajibiwa na Serikali. Kama ilivyoelezwa hapo awali, Hoja za Wabunge zinapotolewa wakati wa Mijadala huweza kujibiwa papo kwa papo na Waziri yeyote au Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na pia Serikali inaweza kutumia utaratibu wa Kauli za Mawaziri kujibu Hoja za Wabunge pale inapoonekana suala fulani limejitokeza na linahitaji kupatiwa majibu.

Kanuni ya 49 inayohusu Kauli za Mawaziri inasomeka:-

"49(1) Waziri anaweza kutoa kauli Bungeni kuhusu jambo lolote linaloihusu Serikali.

(2) Kauli za aina hiyo zinaweza kutolewa kwa idhini ya Spika katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa Shughuli za Bunge na zitahusu jambo mahususi, halisi na zisizozua mjadala na muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi thelathini.

(3) Waziri mwenye kutoa kauli atawajibika kutoa nakala ya kauli yake kwa Wabunge wote wakati anapoiwasilisha Bungeni."

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Hoja za Wabunge zinazotolewa wakati Bunge linajadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bajeti, Serikali ina nafasi mbili za kujibu Hoja hizo. Kanuni ya 99(9) inaelekeza kwamba, muda uliotengwa kwa ajili ya majadiliano utakapokaribia kwisha Waziri mtoa Hoja atapewa muda wa dakika 60 kuhitimisha Hoja yake kwa kujibu masuala yaliyojitokeza kutokana na michango ya Wabunge. Aidha, wakati wa Kamati ya Matumizi Serikali pia inapata nafasi ya kufafanua masuala mbalimbali kama yalivyohojiwa na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Agosti, 2011 wakati Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, (Mb.) anahitimisha Hoja yake hakuligusia kabisa suala la Ndugu David Kitundu Jairo. Vilevile, katika Kamati ya Matumizi Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, (Mb.) alipata nafasi ya kuomba ufafanuzi, lakini alizungumzia masuala mengine bila kugusia suala la Ndugu David Kitundu Jairo. Pia hakukuwa na Mbunge mwingine yeyote aliyezungumzia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imeridhika kwamba, kitendo cha Bunge kutohoji tena suala la Ndugu David Kitundu Jairo wakati wa Kamati ya Matumizi kilitokana na Bunge kuheshimu misingi ya utawala bora kwamba si vyema Mhimili mmoja kuingilia kati kwa kujadili suala ambalo linafahamika wazi kuwa linafanyiwa kazi na Mhimili mwingine, kwa kuwa. *(Makofi)*

(a) tayari kulikuwa na kauli na ombi la Waziri Mkuu kuwa Serikali ipewe muda wa kulifuatilia suala husika;

(b) tayari Katibu Mkuu Kiongozi alikwishatoa Taarifa kwa umma kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amepewa kazi ya kufanya Uchunguzi wa Awali kwa madai yaliyotolewa Bungeni;

(c) hadi siku hiyo tarehe 13 Agosti, 2011 wakati Bunge lilipokuwa linahitimisha Hoja ya Waziri wa Nishati na Madini hakukuwa na taarifa yoyote kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikuwa amemaliza kazi yake;

(d) Bunge lilikuwa na uhakika kwamba Serikali itakapokamilisha taratibu zake litaarifiwa rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usahihi wa Utaratibu uliotumiwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Philemon Luhanjo: Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002 na Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003 Katibu Mkuu Kiongozi ndiye Mamlaka ya Nidhamu kwa Watumishi wote wanaoteuliwa na Rais. Watumishi hao wameorodheshwa katika Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002 wakiwemo Makatibu Wakuu.

Katika Utumishi wa Umma kuna makosa ya kinidhamu ya aina mbili na yametajwa katika Kanuni ya 41 kama ifuatavyo:-

(a)Makosa mazito ambayo mtumishi akipatikana na hatia anaweza kupewa adhabu ya kufukuzwa kazi, kushushwa cheo au kupunguzwa mshahara *(formal proceedings).*

(b) Makosa mepesi ambayo mtumishi akipatikana na hatia anaweza kupewa adhabu ya onyo au karipio *(summary proceedings).*

Mheshimiwa Spika, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma vinaelekeza kwamba kabla Mamlaka ya Nidhamu haijachukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtumishi wa umma mamlaka hiyo itawajibika kufanya Uchunguzi wa Awali ili kujiridhisha kuwa mtumishi wa umma mtuhumiwa ana kesi ya kujibu.

Kanuni ya 36 inasomeka kama ifuatavyo:-

*"Where it is necessary to institute disciplinary proceedings against a public servant, the Disciplinary Authority shall make preliminary investigations before instituting disciplinary proceeding."* Mwisho wa kunukuu.

Madai haya yanaweza kuwa yamemfikia ama kwa kupelekwa kwake rasmi au ameamua mwenyewe kuyafanyia kazi *(suo motto)* kwa kuwa yamezungumzwa katika forum fulani na yanaonekana kuchafua hadhi ya Serikali.

Kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma endapo Uchunguzi wa Awali utathibitisha kuwa mtuhumiwa ana kesi ya kujibu itafuatia hatua ya mtumishi huyo kupewa Hati ya Mashtaka na Mamlaka ya Nidhamu itaanzisha Kamati ya Uchunguzi *(Inquiry Committee)* kwa hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua Sheria na Kanuni zinazotawala, Kamati Teule imebaini yafuatayo:-

(a) Katibu Mkuu Kiongozi ana mamlaka kisheria ya kuanzisha na kukamilisha mchakato wa kinidhamu kwa Makatibu Wakuu. Aidha, Uchunguzi wa Awali ungethibitisha kuwa Ndugu David Kitundu Jairo ana kesi ya kujibu, Kamati ya Uchunguzi ingeundwa na kama ingethibitisha tuhuma, Kanuni ya 48(6) imeelekeza kwamba nanukuu:-

*"Upon receipt of the record of proceedings and the report, the Disciplinary Authority after considering the evidence and such report of the Committee, shall make and record findings whether or not in his opinion, the accused public servant is guilty of the disciplinary offence with which he was charged, and shall inform the accused public servant of the decision within a period of thirty days."* Mwisho wa kunukuu.

(b) Sheria na Kanuni havijaainisha iwapo Katibu Mkuu Kiongozi, kabla ya kutoa maamuzi yake kama Mamlaka ya Nidhamu anatakiwa kupeleka taarifa yake kwa Mamlaka nyingine yoyote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, kupitia Nyaraka kadhaa na kufanya mahojiano na watu mbalimbali, Kamati Teule ina maoni yafuatayo:-

(a) Pamoja na kwamba Katibu Mkuu Kiongozi ni Mamlaka ya Nidhamu kwa Ndugu David Kitundu Jairo ni wazi kuwa alichukua hatua ya kuanzisha Mchakato wa Awali kutokana na Hoja za Wabunge tofauti na masuala mengine ya kinidhamu yanayoanzia kwenye mkondo wa kiutumishi wa Umma. Hivyo basi, baada ya kukamilisha Uchunguzi wa Awali, kwa busara ya kawaida Katibu Mkuu Kiongozi alipaswa kumshirikisha Waziri Mkuu ili kukubaliana namna bora zaidi ya kuliarifu Bunge. *(Makofi)*

(b) Hoja zote zinazotolewa Bungeni huelekezwa kwa Serikali na zinatakiwa kujibiwa Bungeni na Serikali hata kama suala husika linahusu Mtendaji wa Serikali nje ya Bunge. Hata suala la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini lilielekezwa kwa Serikali hivyo lilitakiwa kujibiwa na Serikali, Bungeni.

(c) Katibu Mkuu Kiongozi kuwa Mamlaka ya Nidhamu kwa Makatibu Wakuu haiondoi ukweli kuwa Waziri Mkuu pamoja na kusimamia Mawaziri wengine Bungeni, yeye ni kiungo kati ya Wabunge na Watendaji wote

wa Serikali nje ya Bunge. Aidha, Waziri Mkuu alitoa Kauli Bungeni kuwa Serikali italifanyia kazi suala la Ndugu David Kitundu Jairo na ahadi hii ya Serikali ndiyo iliwezesha "hali ya hewa" Bungeni kutulia. Hivyo, Waziri Mkuu alikuwa na wajibu wa kurudi Bungeni kutoa taarifa ya utekelezaji wa suala hilo na hadi sasa hajafanya hivyo. *(Makofi)*

(e) Katika misingi ya Utawala Bora, licha ya kwamba dhana ya Mgawanyo wa Madaraka *(Separation of Powers)* inataka Mihimili isiingiliane katika kazi, ni muhimu Mihimili hiyo iheshimiane na kushirikiana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kubaini kama Utaratibu huo Umeathiri Dhana ya Haki na Madaraka ya Bunge Dhana ya Haki na Madaraka ya Bunge: Dhana ya "haki za Bunge" ni pana. Waandishi mbalimbali wa masuala ya Kibunge wamewahi kutoa tafsiri ya dhana hii. Mmoja wa Waandishi hawa ni Kaul ambaye amefafanua maana ya "haki za Bunge" kama ifuatavyo naomba kunukuu:-

> *"In parliamentary language, the term "privilege" applies to certain rights and immunities enjoyed by the House of Parliament and Committees of the House collectively and by Members of the House individually. The object of parliamentary privilege is to safeguard the freedom, the authority and the dignity of Parliament. Privileges are necessary for the proper exercise of the functions entrusted to Parliament by the Constitution."* Mwisho wa *quotation.*

Madaraka na haki za Bunge la Tanzania vimeainishwa katika Ibara ya 100(1) na (2) ya Katiba inayosomeka kama ifuatavyo:-

> "100 (1) Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na Chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali pengine nje ya Bunge.
>
> (2) Bila ya kuathiri Katiba hii au masharti ya Sheria nyingine yoyote inayohusika, Mbunge yeyote hatashtakiwa au kufunguliwa shauri la madai mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge au alilolileta Bungeni kwa njia ya maombi, Muswada, Hoja au vinginevyo."

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 101 inalipa Bunge uwezo wa kutunga Sheria ili kuhifadhi na kutilia nguvu uhuru wa majadiliano na shughuli za Bunge kwa ujumla kama inavyotakiwa na Ibara ya 100. Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 *(The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, Cap. 296)* na Kanuni za Bunge zimetaja baadhi ya haki na kinga hizo kama ifuatavyo:-

(i) Haki ya kutoa adhabu;

(ii) Kuweka utaratibu wa namna ya kujiendesha;

(iii) Kulinda mamlaka na heshima ya Bunge; na

(iv) Kulinda uhuru wa mawazo. *(Makofi)*

Hivyo, haki za Bunge kama Taasisi na Mbunge mmoja mmoja zimelindwa kikatiba na kisheria. Aidha, pamoja na Katiba, Sheria na Kanuni kutaja haki na kinga za Wabunge imekubalika miongoni mwa nchi za Jumuiya ya Madola kwamba haki na kinga hizo hazijitoshelezi *(not exhaustive)*, hivyo katika kushughulikia suala hili, mila, desturi na mazoea ya Mabunge ya *Commonwealth* zitafuatwa.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick M. Werema, katika kukubaliana na hilo alisema; naomba kunukuu:-

> "Haki za Bunge hazipo *exhaustive* kwenye Sheria. Yaani ukisoma Sheria unachoona kwenye Sheria siyo haki zote za Kibunge. Kuna nyingine zinatokana na desturi na mazoea ya Mabunge haya ya *Commonwealth."*

Mheshimiwa Spika, suala hili la haki zote kutopatikana kwenye Sheria lilizungumziwa pia na Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mstaafu, Mheshimiwa Andrew Chenge, (Mb.) ambaye alifafanua kuwa Waandishi wengi wa masuala ya Katiba kwenye eneo hili wamekubaliana kwamba huwezi kukuta haki zote zimeainishwa (codified) na

ndiyo hali ilivyo sasa ukiangalia katika nchi nyingi za Jumuiya ya Madola. Kwa maneno yake Mheshimiwa Andrew Chenge, (Mb.) alisema, naomba kunukuu:-

> "… *there is no closed list* ya *classes* ya makosa ambayo Bunge linaweza kusema umenifanyia, huwezi kusema ni haya tu, ukafunga mlango. Mazingira yanabadilika na yanakuwa *very dynamic,* mambo ambayo ulitegemea jana yasiathiri haki na madaraka ya Bunge, leo yanaweza kuja katika sura tofauti yakawa." *(Makofi)*

Kamati Teule imeona kwamba Kifungu cha 12(1) cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296 kinaakisi Hoja hizi na kinasomeka: Nanukuu:-

> "… *Subject to the Constitution and the Standing Orders of the Assembly, the Assembly has all such powers and jurisdiction as may be necessary for inquiring into, judging and pronouncing upon the commission of any Act, matter or thing, not amounting to an offence under this Act, which is a breach of Parliamentary privileges."* Mwisho wa kunukuu.

Kwa hiyo, suala la haki za Bunge kimsingi limeachwa kwa Bunge lenyewe kuamua ni mambo gani yakifanyika yatasababisha Bunge na Wabunge kuvunjiwa haki zao kwa kutegemea mazingira ya wakati husika bila kuathiri masharti ya Katiba.

Iwapo utaratibu uliotumiwa na Katibu Mkuu Kiongozi umeathiri Dhana ya Haki na Madaraka ya Bunge: Kamati Teule imebaini kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002 na Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003 baada ya Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kuahidi kulishughulikia suala hili, utaratibu uliotumiwa na Katibu Mkuu Kiongozi kulichunguza ni sahihi.

Baada ya Katibu Mkuu Kiongozi kukamilisha Uchunguzi wa Awali, utaratibu alioutumia wa kutoa taarifa ya matokeo ya Uchunguzi huo kupitia Vyombo vya Habari na maneno aliyotumia wakati wa uwasilishaji wa matokeo ya Uchunguzi wa Awali ndiyo yaliyosababisha hisia ya kuingiliwa kwa dhana ya haki na madaraka ya Bunge. Aidha, Mapokezi ya Ndugu David Kitundu Jairo Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini siku aliporudi kazini nayo yalichangia kujenga sura ya ushindani na mapambano baina ya Mihimili miwili ya Dola.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kutoa Taarifa ya Uchunguzi kupitia kwenye Vyombo vya Habari kimeibua makundi mawili, moja likisema kimeathiri na lingine likisema hakijaathiri dhana ya haki na madaraka ya Bunge.

Msingi wa mtazamo wa Kundi la Kwanza ni kwamba hapakuwa na Hoja mahususi ya kutaka taarifa hiyo irudishwe Bungeni.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Werema katika hili anasema:-

> "Utaratibu huu sioni kama umeathiri dhana ya Haki na Madaraka ya Bunge kwa sababu nilivyoelewa ni kwamba kulikuwa hamna Hoja ambayo iliamuliwa na Bunge ambayo Bunge lilitaka lijulishwe Serikali imefanya nini."

Mtaalam mmoja wa masuala ya Katiba wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alifafanua kwamba, kwa sababu Katibu Mkuu Kiongozi hakuagizwa na Bunge, kisheria hakulazimika kuripoti Bungeni ingawa kisiasa ingefaa aripoti. Kwa hiyo, kama amedhalilisha heshima ya Bunge ni kisiasa na siyo kisheria. Alisisitiza kwa kusema:-

> *"I think he had a political responsibility at least to inform you the results."*

Mmoja wa Makatibu wa Bunge Wastaafu, akifafanua suala hilo alisema, kitendo hicho hakijaathiri dhana hiyo kwa vile Katibu Mkuu Kiongozi alikuwa anafanya uamuzi ambao ulikuwa na maslahi kwa Umma. Kwa hiyo, Umma nao ulikuwa na haki ya kujua na vilevile Katibu Mkuu Kiongozi hana mamlaka ya kwenda Bungeni na hapa alisisitiza kwa kusema, nakuu:-

> *"Chief Secretary* hana kitu tunakiita locus stand ya yeye kuja Bungeni … anaye-appear Bungeni ni Waziri Mkuu… yeye hawezi kuja kutoa taarifa Bungeni, lakini kutoa sehemu nyingine anatoa kwa mujibu wa mamlaka aliyonayo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Kundi la Pili lina msimamo kwamba kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kutoa maelezo kwenye Vyombo vya Habari huku akifahamu wazi kuwa Serikali kupitia Waziri Mkuu imetoa ahadi Bungeni, kimeathiri haki ya Bunge ya kupata taarifa na zaidi kama Waziri Mkuu hakufahamishwa naye hakutendewa haki kwa vile kauli yake aliyoitoa Bungeni mpaka sasa haijatimizwa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Akisisitiza hili, mmojawapo wa Mawaziri alikuwa na haya ya kusema:-

> "… Waziri Mkuu hakutendewa haki, kwamba maneno yale ya Serikali hakuyasema majibu yake ambayo alipaswa kuyatoa yeye Bungeni hakupata nafasi ya kuyasema… Naomba kurudia. "… Waziri Mkuu hakutendewa haki, kwamba maneno yale ya Serikali hakuyasema majibu yake ambayo alipaswa kuyatoa yeye Bungeni hakupata nafasi ya kuyasema na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu walimtegemea Waziri Mkuu awajulishe kwanza, yaani wananchi wapate taarifa ile kupitia Bunge. Kwa hiyo, nao hawakutendewa haki." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Spika Mstaafu, Mheshimiwa Pius Msekwa akikubaliana na Hoja kwamba kitendo hicho kimeathiri haki za Bunge alisema kwa kunukuu.

> "… kwa hiyo, utaratibu uliotumiwa na Katibu Mkuu Kiongozi kwa maoni yangu ulikiuka taratibu za mfumo wa Bunge kuihoji Serikali na Serikali kujibu Hoja hizo … Hoja za Wabunge zinaelekezwa kwa Serikali iliyoko ndani ya Bunge." *(Makofi)*

Mheshimiwa Pius Msekwa alimalizia kwa kusema, kitendo cha maamuzi kutolewa na kutekelezwa kabla ya Taarifa kurudishwa Bungeni, hapo ndipo dhana ya haki za Bunge ilikiukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule iliwasiliana na Katibu wa Bunge la Uingereza *(The House of Commons)* kwa kuwaandikia barua kutaka kupata uzoefu wao katika changamoto kama hii. Katika majibu yake, Katibu wa Bunge aliweka wazi ukweli kwamba katika suala la mawasiliano baina ya Bunge na Serikali, hakuna Serikali yoyote makini ambayo itaruhusu mawasiliano kati yake na Bunge kwa namna ambayo italiudhi Bunge, kwamba:-

> "*…it is rarely good policy for any government to act in a way that annoys Members of the Legislature…(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wao Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu walisema kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kwenda kwenye Vyombo vya Habari kujibu Hoja iliyoanzia Bungeni kimeingilia wajibu na haki za Bunge kama zilivyoelezwa katika Ibara ya 63(2) na (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Bunge limenyang'anywa haki ya kupokea taarifa na kujiridhisha kwa kuhoji na kuuliza maswali hasa ikizingatiwa kuwa Bunge katika kuisimamia Serikali ni pamoja na kuhoji matumizi ya fedha za Wananchi kama ilivyokuwa katika suala hili. *(Makofi)*

Mmoja wa Wanasheria Wakuu Wastaafu alieleza kuwa, kitu ambacho kinaonesha kwamba Bunge limedhalilishwa ni pale ambapo Katibu Mkuu Kiongozi alitoa taarifa bila kuwasilisha matokeo ya uchunguzi huo Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nitawaomba Waheshimiwa Wabunge waendelee kusoma maelezo mbalimbali ya watu mbalimbali waliokuja kutoa maoni yao katika jambo hili kama inavyoonekana kwenye taarifa.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kwamba suala hili lazima likemewe ili lisirudie tena kwa maslahi ya taifa na mambo ya siasa waachiwe wanasiasa na watumishi wa umma waendelee kufanya kazi zao na kufuata maadili ya utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ili kufahamu undani wa suala hili Kamati Teule ilifanya mahojiano na wahusika wakuu wawili ambao ni Waziri Mkuu na Katibu Mkuu Kiongozi. Katika mahojiano na Katibu Mkuu Kiongozi, Kamati pamoja na mambo mengine ilitaka kufahamu kama kulikuwa na mawasiliano kati yake na Waziri Mkuu kabla hajatoa

Taarifa yake ya Uchunguzi kwa Vyombo vya Habari na kama alitoa taarifa hiyo huku akijua kuwa Waziri Mkuu alitoa kauli Bungeni na kwamba Bunge lilikuwa linasubiri majibu, Katibu Mkuu Kiongozi aliieleza Kamati Teule kuwa suala la nidhamu ya watumishi wa umma linaendeshwa kwa Sheria za Utumishi na sio suala la kisiasa na hicho ndicho alichokifanya. Kwa maneno yake Katibu Mkuu Kiongozi alisema:-

> "… mimi nilichofanya nilichukua Sheria, nikachukua Kanuni, taratibu na mamlaka niliyonayo nikafanya niliyofanya. Hiyo ya Waziri Mkuu kwamba atayarudisha Bungeni hilo sikuwa na uhakika sana kama ninaelewa vizuri…"

Kamati ilihoji pia namna suala hili lilivyofika mezani kwa Katibu Mkuu Kiongozi; iwapo alipelekewa na Waziri Mkuu baada ya kuibuliwa Bungeni au alichukua uamuzi yeye mwenyewe baada ya kusikia likizungumzwa Bungeni lakini haikuweza kupata majibu kutokana na maelezo kwamba mawasiliano kati yake na uongozi wa ngazi za juu ni *highly classified.* Aliendelea kusema:-

> "…hilo kwa kweli siwezi kulisema, kwa sababu ni mambo ya ndani mno, itoshe tu kwamba mimi ninayo Sheria iliyotungwa na Bunge naitekeleza…"

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wake Waziri Mkuu aliieleza Kamati Teule kwamba ni kweli alilieleza Bunge kuwa analipeleka suala la Ndugu David Kitundu Jairo kwa Rais kwa kuwa kimahusiano Waziri Mkuu na Rais ni watu ambao wanawasiliana kwa karibu sana. Kamati Teule ilipotaka kufahamu iwapo Waziri Mkuu alimpa taarifa Mheshimiwa Rais kama alivyoliahidi Bunge, alisema:-

> "…alipokuja, nililazimika kumwarifu kwamba kumetokea nini, naye akatupa maelekezo, ambayo nilidhani ni mazuri tu …kwamba ni vizuri mzingatie taratibu maadam umelitoa huko ukaamua kulileta huku…katika kulisimamia hamna budi mrudi kwenye sheria zetu zinazotawala utumishi…"

Waziri Mkuu alieleza pia kwamba walishauriana na Katibu Mkuu Kiongozi namna ya kushughulikia suala hilo. Kamati Teule ilipotaka kufahamu iwapo Waziri Mkuu alipewa taarifa baada ya Katibu Mkuu Kiongozi kukamilisha Uchunguzi wa Awali ambao katika hatua za mwanzo walishauriana, Waziri Mkuu alijibu kwamba hakupata taarifa hizo kabla na kwamba na yeye alizisikia baadaye. Kwa maneno yake Waziri Mkuu alisema:-

> "…kimahusiano sisi hata bila kujali huo mfumo wa kisheria, mamlaka haya ni ya kwake angeweza kufanya hivyo, lakini bado kama angeamua tu kwamba … Bwana, Waziri Mkuu muda wote tunawasiliana naye, hata katika hili tuliwasiliana naye, ameniwezesha nimeweza kulisimamia, bado angeweza akarudi kwangu na kusema Bwana, nimemaliza kazi yangu vizuri, sasa nataka niende nikafanye moja, mbili, tatu. Pengine na mimi busara nyingine zingenijia na ningesema sawa tu, lakini hebu ngoja kidogo, pamoja na kwamba ni mamlaka yako hayo, unaweza kisheria ukafanya hivyo, lakini hebu ngoja kwanza na mimi nione kama kuna namna nyingine ya kuweza kufanya, kwa sababu wenzangu wananingoja huku kuweza kujua nini kimetokea katika mchakato mzima. Sasa kwa sababu alikwenda kwa mamlaka yake, mimi nimekuja nikazipata baadaye. Sasa baada ya pale ndiyo inakuwa maji yameshamwagika, kuyazoa tena inakuwa siyo rahisi sana. Kilichohitajika pale ni hilo tu ni namna ya kutafuta ushauri kabla hujakwenda mbali sana. Naweza kusema it is unfortunate kwamba, halikujitokeza at that material time…"

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule haikuweza kuthibitisha kuwa, kitendo cha taarifa kutolewa kwa kutumia Vyombo vya Habari wakati bado Bunge halijapewa taarifa kimeathiri dhana ya haki na madaraka ya Bunge kisheria. Hata hivyo, kwa kuwa suala hili lilianzia Bungeni, na kwa kuwa kulikuwa na mawasiliano kati ya Waziri Mkuu na Katibu Mkuu Kiongozi kabla ya kuanza kwa mchakato wa Uchunguzi wa Awali; hivyo basi, Katibu Mkuu Kiongozi alikuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba Bunge kupitia kwa Waziri Mkuu linapata Taarifa ya matokeo ya Uchunguzi wa Awali kabla hajaitoa kwa Vyombo vya Habari.

Ikumbukwe kwamba Wabunge walisitisha mjadala husika wa utaratibu wa Wizara kuchangisha Taasisi fedha kwa sababu suala hilo lilikuwa linafanyiwa kazi na Serikali kama Waziri Mkuu alivyoliomba Bunge, na Wabunge walitegemea kuwa baada ya uchunguzi kukamilika wangepewa taarifa rasmi ili waamue kuendelea au kuachana nalo.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa mambo ambayo yalielezwa na baadhi ya watu waliofika mbele ya Kamati Teule kuwa yameathiri dhana ya haki na madaraka ya Bunge ni maneno aliyotumia Katibu Mkuu Kiongozi

siku alipotoa Taarifa ya Uchunguzi wa Awali kwa Vyombo vya Habari. Hili lilitiliwa mkazo na mchangiaji mmoja aliposema:-

> "…utaratibu uliotumiwa ni kweli umekiuka haki na madaraka ya Bunge kwa maana ya *substantively* lakini vilevile hata tone iliyotumika, maneno yaliyotumika na Katibu Mkuu Kiongozi, yalionesha defiance na kiburi kwa Bunge…"

Mheshimiwa Spika, maneno yanayozungumzwa hapa ni pale Katibu Mkuu Kiongozi aliposikika akisema Ndugu David Kitundu Jairo kuwa anaweza kuchukua hatua kwa kuwashtaki kwa defamation waliomharibia jina, akitoa mfano kwamba hata Waandishi wa Habari wamewahi kuwalipa watu mbalimbali kutokana na kosa hili. Kwa maneno yake alisema:-

> "…sasa hii mimi namwachia mwenyewe Jairo kama yeye ataamua kupeleka mbele ya safari, vyombo vipo, anayo haki ya kufanya hivyo. Anayo haki kwamba mimi nimedhalilishwa. Si mmeona watu wengine mmewahi kuwaandika kwenye magazeti, wengine si mmewahi kuwalipa watu hapa kwa sababu ya *defamation?..."*

Kauli ya kwamba Ndugu David Kitundu Jairo anaweza kushtaki kwa defamation imetafsiriwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi alimaanisha Ndugu David Kitundu Jairo anaweza kuwashtaki Wabunge kwa kile kilichosemwa Bungeni tarehe 18 Julai, 2011. Mtazamo huu uliungwa mkono na mmoja wa wahojiwa ambaye alisema:-

> "…Sasa ile ni threatening na kutisha Waheshimiwa Wabunge… Mheshimiwa Beatrice Shellukindo alisema yale maneno yake ndani ya Bunge na …tuna *immunity* …Katibu Mkuu Kiongozi kusema kwenye Vyombo vya Habari kwamba Mbunge huyu anaweza kushtakiwa ni sehemu ya kuingilia Bunge."

Mheshimiwa Spika, suala la kinga ya Wabunge kutoshtakiwa kwa kauli wanazozitoa Bungeni pia liliungwa mkono na kufafanuliwa na Mtaalam wa Masuala ya Katiba wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mchangiaji mwingine ambaye alisema:-

> "…Hawawezi kushtaki kwa *defamation* …sioni hapo amekuwa *defamed* vipi. Hii ni barua, ni *fact* ipo na imekuwa *tabled,* ni halisi…pale hajadhalilishwa."

Tofauti na mtazamo kuwa maneno ya Katibu Mkuu Kiongozi yalimaanisha kuwa Ndugu David Kitundu Jairo anaweza kuwashitaki Wabunge, wapo waliosema kuwa Katibu Mkuu Kiongozi hakumaanisha hivyo badala yake alimaanisha kuwa amwandikie Mheshimiwa Spika kuonesha kutoridhishwa kwake kwa kutumia Kanuni ya 64 na 71.

Kamati Teule iliona ni vyema pia kusikia kutoka kwa mhusika ni nini hasa lilikuwa lengo la kauli yake hiyo. Katibu Mkuu Kiongozi alifafanua kuwa alimaanisha Ndugu David Kitundu Jairo anaweza kupeleka malalamiko kwa Mheshimiwa Spika, kwamba:-

> "…ile *defamation* niliyozungumza nilikuwa nawazungumzia wale Waandishi wa Habari wenyewe kwamba ninyi si mmewahi kushtakiwa kwa *defamation*…siyo kwamba Bunge ndiyo lishtakiwe kwa *defamation*…"

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ina maoni kwamba, kwa kutumia maneno "vyombo vipo" Katibu Mkuu Kiongozi alimaanisha kwamba Ndugu David Kitundu Jairo angeweza kwenda kwenye chombo chochote cha haki kumshtaki Mbunge kinyume na matakwa ya Katiba kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 100 na Kifungu cha 3 cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inaona maneno haya yameathiri dhana ya haki na madaraka ya Bunge kwa vile kwa mujibu wa Ibara ya 100(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296, Kifungu cha 3, msisitizo ni kuwa majadiliano ya Wabunge hayatahojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au katika Mahakama au mahali penginepo nje ya Bunge. Aidha, Ibara ya 100(2) inaelekeza kwamba Mbunge hatashtakiwa kwa jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge. Kumshauri Ndugu David Kitundu Jairo kwenda kwenye chombo chochote ni kukiuka Ibara hizo na hivyo kuathiri uhuru wa majadiliano ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, maneno mengine ya Katibu Mkuu Kiongozi ambayo yanalalamikiwa ni pamoja na kauli kwamba mtu aliyetoa barua kwa Mbunge "ikithibitika atapewa haki yake…" kwamba inaweza kuathiri haki ya Wabunge kupata habari na hata kutishia raia wema kutoa nyaraka kwa Wabunge hata zile ambazo zinaonesha maovu kwa kuwatisha watoa habari na hivyo kuwafanya Wabunge washindwe kutekeleza wajibu wao wa kuisimamia Serikali. Maneno ya Katibu Mkuu Kiongozi kuhusu hili ni kwamba mpaka sasa wanaendelea kutafuta nani alitoa barua kwa Mbunge au kwa Wabunge; ikithibitika atapewa haki yake na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Kwa upande mwingine mmoja wa wanazuoni wa masuala ya Katiba na Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alisema kuwa kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kusema Mbunge alipata wapi Nyaraka za Serikali ni kulidharau Bunge. Alisema:-

> "…Waziri Mkuu kabeba mzigo, halafu wewe unasema alipata wapi Nyaraka … *I don't think he should have said that…*"

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati Teule kuwa badala ya kulalamika na kutishia Whistleblowers, Watendaji Wakuu wa Serikali sasa wanatakiwa kutumia taratibu za ndani kutatua tatizo la kuvuja kwa Nyaraka za Serikali ambalo limekuwa likijitokeza mara kwa mara hadi kushusha heshima ya Serikali. Aidha, Kamati Teule inaona umuhimu wa kutungwa kwa Sheria ya *Whistleblower's Protection Act* ambayo itasaidia kushughulikia suala hili.

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 Agosti, 2011 Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini alirudi kazini kama alivyoelekezwa na Katibu Mkuu Kiongozi, na alipokelewa kwa mapokezi makubwa ikiwa ni pamoja na gari lake kusukumwa, yeye kuvishwa shada la maua na kuimbiwa nyimbo. Vilevile Waandishi wa Habari walikuwepo na kurekodi matukio yaliyoendelea. Wengi wa watu waliofika mbele ya Kamati Teule walitoa maoni kuwa kitendo hicho sio cha kimaadili ya mtumishi wa umma kwa kuwa picha iliyojitokeza ni kuwa katika suala hili kulikuwa na mashindano kati ya Serikali na Bunge, na kwamba Bunge lilikuwa "linazomewa" kuwa limeshindwa.

Akitoa maoni yake kuhusu hili Mwanasheria Mkuu wa Serikali alisema:-

> "…halivunji Sheria, lakini ni jambo la hovyo kwamba sasa unarudi unasukumwa na gari, watu wanakupokea kwa mbwembwe, ni jambo la hovyo…"

Mmoja wa Makatibu wa Bunge Wastaafu alisema, kitendo kile ni kulidharau Bunge na kinaonesha kuwa Watendaji wa Serikali wameingia kwenye siasa. Kwa maneno yake alisema: -

> "…baada ya kutangazwa uamuzi huu kesho yake alipokelewa kule Wizarani … kwa shangwe, gari lake likasukumwa …Vyombo vya Habari vilikuwa pale *which means* jambo lenyewe lilikuwa limepangwa… watumishi wengi walikuwa pale chini …kwa mtu civil servant ukiona anasukumwa…*now this thing is being politicized…it is in bad test…*"

Mchangiaji mwingine alisema, mapokezi yale yalishangaza wengi hasa kwa vile limetokea kwenye Ofisi ya Umma. Kiongozi wa umma kusukumwa ndani ya gari, watumishi kuacha kazi kwenda kwenye mapokezi, ni dalili ya kwamba ndani ya Utumishi wa Umma kuna mmomonyoko wa maadili kiutendaji, kwamba:-

> "…hatujazoea sisi kuona *civil servants* wakiwa wanafanya mikutano kama hiyo. Kazi hiyo ni ya wanasiasa, lakini *openly* imeonekana inafanyika. Kwa hiyo, kuna mmomonyoko mkali sana wa maadili ya kiutendaji kwenye *Public Service* ambayo pia nayo inabidi iwe *addressed*…"

Kamati Teule imebaini kuwa kitendo cha mapokezi ya Ndugu David Kitundu Jairo kimeashiria yafuatayo:-

- Matumizi mabaya ya muda wa kufanya kazi kwa vile kwa kipindi chote hicho kazi hazikufanyika na hivyo umma kukosa huduma.

- Uvunjifu wa maadili ya Utumishi wa Umma kinyume na Kifungu cha 47(3)(b) cha *Public Service Scheme, 2003* kinachosomeka kama ifuatavyo:-

*"Every Public Servant shall not conduct himself in a way which:-*

*(b) is improper ..."*

Kamati Teule inaona kuwa mapokezi yale na yote yaliyojiri ni *"improper"* kwa mtumishi wa umma.

- Kulidharau Bunge kwa kuonesha kwamba kulikuwa na mashindano na mshindi kapatikana, wakati ukweli ni kwamba Bunge lilikuwa katika wajibu wake wa kuihoji Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kwamba, suala hili lazima likemewe ili lisijirudie tena kwa maslahi ya Taifa na mambo ya siasa waachiwe wanasiasa na watumishi wa umma waendelee kufanya kazi zao na kufuata maadili ya Utumishi wa Umma.

Kuangalia nafasi ya mamlaka ya uteuzi kwa ngazi ya Makatibu Wakuu katika kushughulikia masuala ya nidhamu ya anaowateua:-

Mheshimiwa Spika, Hadidu ya Rejea ya Nne iliitaka Kamati Teule kuangalia nafasi ya Mamlaka ya Uteuzi kwa ngazi ya Makatibu Wakuu katika kushughulikia masuala ya nidhamu ya anaowateua.

Katika kushughulikia Hadidu hii, Kamati ilifanya yafuatayo:-

(a) Kupitia Katiba, Sheria ya Utumishi wa Umma, 2001 na Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003.

(b) Kufanya mahojiano na mashahidi wa aina mbalimbali.

Misingi ya Katiba, Sheria na Kanuni za Utumishi kuhusiana na Mamlaka ya Uteuzi kwa Makatibu Wakuu:-

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 36 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inampa Rais mamlaka ya kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Aidha, Rais ana madaraka ya kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka ya uongozi wanaowajibika kuweka Sera za Idara na Taasisi za Serikali na Watendaji Wakuu wanaowajibika kusimamia utekelezaji wa Sera za Idara na Taasisi hizo katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002 inaelekeza kwamba kutakuwa na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye atateuliwa na Rais na atakuwa Mkuu wa Utumishi wa Umma na Katibu wa Baraza la Mawaziri. Aidha, Kifungu 5(1)(a) kinaainisha kwamba, kutakuwa na Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu mbalimbali ambao watateuliwa na Rais. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

*"5(1) Except where the President determines otherwise, there shall be appointed by the President –*

*a Chief Executive Officer in respect of each Ministry, extra ministerial department, region or local government authority, in the Government of the United Republic, who shall be known as the Permanent Secretary for that Ministry, the Head of that extra ministerial department or Regional Administrative Secretary for the Region or the Director of the Local Government Authority as the case may be ..."*

Katiba inampa Rais mamlaka ya kutekeleza madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yeye mwenyewe moja kwa moja au kukasimu madaraka hayo kwa watu wengine. Miongoni mwa madaraka ambayo Rais amekasimu ni yale ya kushughulikia masuala ya kinidhamu kwa watumishi wa umma kama inavyoelezwa hapa chini. Hata hivyo, Rais haruhusiwi kukasimu madaraka ya kumuachisha kazi mtumishi yeyote kwa maslahi ya umma.

Mamlaka ya Nidhamu kwa Watumishi wa Umma wanaoteuliwa na Rais:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wa umma wanaoteuliwa na Rais ni Katibu Mkuu Kiongozi kama inavyofafanuliwa katika Kifungu cha 4(3)(d) kama ifuatavyo:-

*"4(3) The Chief Secretary shall, as head of the Service, provide leadership, direction and image to the service and shall:-*

*(d) be a disciplinary authority in respect of public servants appointed by the President."*

Kitendo cha Rais kukasimu kwa Katibu Mkuu Kiongozi madaraka ya kushughulikia nidhamu ya watumishi anaowateua hakimuondoi moja kwa moja katika kushughulikia nidhamu yao, kwa sababu kulingana na masharti ya Ibara ya 36(4) Rais ana mamlaka wakati wowote kuchukua hatua za kudhibiti nidhamu ya watumishi na utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

Rais pia ni Mamlaka ya Rufaa kwa mtumishi yeyote wa umma ambaye Mamlaka yake ya Nidhamu ni Katibu Mkuu Kiongozi. Hivyo, mtumishi asiporidhika na uamuzi wa Katibu Mkuu Kiongozi ana haki ya kukata rufaa kwa Rais ambaye anaweza kuuthibitisha, kuurekebisha au kuutengua uamuzi wa Katibu Mkuu Kiongozi. Kifungu cha 25(1) kinafafanua kama ifuatavyo:-

*"25(1) Where –*
*(a) The Chief Secretary exercises disciplinary authority in respect of a public servant who is an appointee of the President by reducing the rank other than reversion from the rank to which the public servant has been promoted or appointed on trial or reduces the salary or dismisses that public servant may appeal to the President against the decision of the disciplinary authority and the President shall consider the appeal and may confirm, vary or rescind the decision of that disciplinary authority…"*

Taratibu za Kushughulikia Masuala ya Kinidhamu kwa Watumishi wa Umma Wanaoteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003 zimefafanua kwa kina taratibu hizi kama ilivyoelezwa awali katika Taarifa hii, Kanuni ya 36 inaelekeza kwamba pale inapobidi hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya mtumishi wa umma Mamlaka husika ya Nidhamu inalazimika kufanya Uchunguzi wa Awali *(Preliminary Investigation)* ili kuthibitisha kama mtumishi mtuhumiwa ana kesi ya kujibu au la.

Iwapo Uchunguzi wa Awali utathibitisha kuwa mtumishi mtuhumiwa ana kesi ya kujibu, na kwamba uzito wa kesi yenyewe unaweza kusababisha mtumishi husika akapewa adhabu ya kufukuzwa kazi, kushushwa cheo au kupunguzwa mshahara, Kanuni zinaelekeza kwamba Mamlaka ya Nidhamu italazimika kumpatia mtumishi mtuhumiwa notisi na hati ya mashitaka inayoainisha tuhuma dhidi yake, na kumtaka atoe maelezo ya utetezi wake ndani ya muda utakaoainishwa.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 45 inaelekeza kwamba mtumishi mtuhumiwa akishindwa kutoa maelezo ya utetezi ndani ya muda aliopewa au akitoa maelezo yasiyojitosheleza, Mamlaka ya Nidhamu itateua Kamati ya watu wawili au zaidi kwa ajili ya kufanya uchunguzi *(Inquiry Committee).*

Sifa kuu za watumishi wanaoweza kuteuliwa katika Kamati ya Uchunguzi, pamoja na sharti la kuzingatia jinsia, ni kuwa mtumishi husika awe Afisa Mwandamizi na zaidi *(Senior grade and above)* na katika ngazi ya juu kumzidi mtumishi mtuhumiwa. Hata hivyo, kwa upande wa watumishi wa umma wanaoteuliwa na Rais Kanuni ya 46(2) inaelekeza kama ifuatavyo:-

*"…where the appointing authority of the accused public servant is the President, no person shall be appointed a member of an Inquiry Committee for conducting an Inquiry into a charge or charges against such public servant unless he is a Judge, the Permanent Secretary, a head of Independent Department, a Regional Administrative Secretary, a Senior or a Principal Resident Magistrate…"*

Taratibu zitakazotumiwa na Kamati ya Uchunguzi katika kuendesha kazi zake zimefafanuliwa katika Kanuni ya 47. Aidha, Kanuni ya 48 inaelekeza kwamba, Kamati ya Uchunguzi itakapokamilisha kazi yake itawasilisha Ripoti kwa Mamlaka ya Nidhamu ikielezea, pamoja na mambo mengine, iwapo kwa mtazamo wa Kamati tuhuma dhidi ya mtumishi mtuhumiwa zimethibitishwa ama la. Isipokuwa Kamati ya Uchunguzi haitakiwi kutoa mapendekezo yoyote kuhusiana na adhabu kwa kuwa hilo ni jukumu la Mamlaka ya Nidhamu.

Mheshimiwa Spika, Kanuni pia zinaelekeza kwamba iwapo Mamlaka ya Nidhamu itamtia hatiani mtumishi mtuhumiwa basi mtumishi huyo atapewa adhabu ambayo utekelezaji wake utaanza mara moja. Kanuni ya 48(8) inafafanua:-

*"Where the disciplinary authority finds the accused public servant guilty, he shall proceed to award punishment.*

*Provided that where the accused public servant is punished by dismissal, his dismissal shall take effect from the date upon which the Disciplinary Authority found the accused public servant guilty."*

Mheshimiwa Spika, ufuatao ni uchambuzi wa yaliyojitokeza:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia Katiba, Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002 na Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003 na mahojiano na watu mbalimbali Kamati imebaini yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002 na Kanuni zake za Mwaka 2003 zimeonesha wazi kuwa zaidi ya kuwa Mamlaka ya Rufaa, Rais hana nafasi kubwa sana kwenye masuala ya nidhamu ya anaowateua. Sheria zimetoa madaraka makubwa kwa Katibu Mkuu Kiongozi kufanya Uchunguzi wa Awali na kuendelea na kutoa adhabu ya kumpunguzia mshahara mtuhumiwa bila hata kuhusisha Mamlaka ya Uteuzi (Rais). Hakuna mahali popote kwenye Sheria au Kanuni panapomlazimisha Katibu Mkuu Kiongozi kuwasiliana na Mamlaka ya Uteuzi kabla ya kutoa maamuzi yake. Hata kama ziko taratibu za kiutawala, ombwe hili *(vacuum)* kwenye Sheria linaweza kusababisha matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Spika, hofu hii ya matumizi mabaya ya madaraka inatiliwa nguvu na kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kumrudisha kazini Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na kesho yake (Mamlaka ya Uteuzi) kumrudisha tena likizoni, inaonesha wazi hapakuwa na mawasiliano ya kiutawala kati yao. Kwa mujibu wa Taarifa ya Ikulu kwa Vyombo vya Habari ya tarehe 26 Agosti, 2011 uamuzi wa Rais wa kumsimamisha kazi Ndugu David Kitundu Jairo haujatokana na shinikizo la Bunge, na kwamba Ndugu David Kitundu Jairo asirudi kazini mpaka atakapoamua namna gani ya kurudi, lini na wapi, kama kungekuwa na mawasiliano Katibu Mkuu Kiongozi asingemrudisha kazini Ndugu David Kitundu Jairo na kesho yake Rais anamsimamisha kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile kuitaarifu Mamlaka ya Uteuzi ni hiari tu ya Mamlaka ya Nidhamu au ni suala linalofanyika kiutawala, bado inatia shaka katika sakata hili kama Mamlaka ya Uteuzi ilitaarifiwa kwa kuwa kama ingetaarifiwa si rahisi kuruhusu Taarifa ya Uchunguzi itolewe kwenye Vyombo vya Habari huku ikielewa fika kuwa Serikali kupitia Waziri Mkuu ilikuwa imetoa ahadi Bungeni, hivyo ilipaswa kurudi Bungeni.

Mheshimiwa Spika, inatia shaka kama kweli Mamlaka ya Nidhamu iliishirikisha Mamlaka ya Uteuzi na Mamlaka hiyo ikaruhusu taarifa ya nidhamu ya mtumishi wa umma itolewe hadharani wakati inafahamika siku zote kwamba, masuala ya kinidhamu kwa Watumishi wa Umma ni SIRI. Kiutaratibu Ndugu David Kitundu Jairo angepewa tu taarifa kama ilivyofanyika mara ya pili aliporudishwa likizoni kwani haikusikika kwenye Vyombo vyovyote vya Habari hadi pale Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge, alipouliza swali kwa Waziri Mkuu Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 35(1) inaeleza kuwa, shughuli zote za utendaji za Serikali ya Jamhuri ya Muungano zitatekelezwa na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais; Ibara ya 52(3) inaelekeza kuwa, katika utekelezaji wa madaraka yake, Waziri Mkuu atatekeleza au kusababisha utekelezaji wa jambo lolote au mambo yoyote ambayo Rais ataagiza kwamba yatekelezwe.

Hata hivyo, katika masuala ya nidhamu ya watumishi wa umma wanaoteuliwa na Rais, nafasi ya Waziri Mkuu haionekani moja kwa moja. Katiba, Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma vinamuondoa kabisa Waziri Mkuu katika kushughulikia masuala ya nidhamu kwa watumishi hao. Kutokana na mjadala huo hapo juu, Kamati Teule ina maoni kwamba Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma zifanyiwe mapitio ili kubaini maeneo zaidi yanayohitaji marekebisho ili kuondoa migongano, kuweka wigo mpana wa haki kutendeka na kuongeza ufanisi wa kazi katika Utumishi wa Umma. Kwa mfano, kwa kuwa suala la nidhamu ya wateule wa Rais ni nyeti na pana si vyema suala hilo kuwa mikononi mwa mtu mmoja. Ni vyema Serikali ikafikiria mojawapo ya njia zifuatazo:-

- Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wa umma wanaoteuliwa na Rais inaposhughulikia masuala ya nidhamu ifanye hivyo kwa kumshirikisha Waziri Mkuu ambaye ni msimamizi wa shughuli za siku kwa siku za Serikali.

- Kuunda Chombo maalum cha kushughulikia masuala ya nidhamu kwa watumishi wa umma wanaoteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 36 inayohusu Uchunguzi wa Awali *(Preliminary Investigation)* ina upungufu kama ifuatavyo:-

- Haitoi maelekezo maalum kwa Mamlaka ya Nidhamu kuhusiana na mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya Uchunguzi wa Awali kwa mfano namba ya wajumbe na sifa zao, tofauti na ufafanuzi unaotolewa katika Kanuni ya 46 kuhusu Kamati ya Uchunguzi *(Inquiry Committee).*

- Tafsiri inayopatikana ni kuwa, Mamlaka ya Nidhamu ina ridhaa ya kuona namna sahihi ya kupata ukweli wa awali kuhusu tuhuma zinazomkabili mtumishi anayehusika.

- Upo uwezekano wa Mamlaka ya Nidhamu kufanya uchunguzi huo yenyewe na kufanya maamuzi iwapo kuna kesi ya kujibu au la.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa “ridhaa” hii unaweza kuleta utata mfano, kwa suala la Ndugu David Kitundu Jairo inaelezwa kwamba Katibu Mkuu Kiongozi alimtumia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya Ukaguzi Maalum kwa vile hata kama suala husika linahusu fedha na Sheria ya Ukaguzi inaruhusu mtu yeyote kuomba Ukaguzi Maalum *(Special Audit)* bado kuna mashaka kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pekee asingeweza kutoa majibu kuhusiana na masuala ya kinidhamu kwa upana wake.

Mheshimiwa Spika, Mambo Mengine Yenye Uhusiano Na Masuala Haya.

Katika sehemu hii ya Taarifa, Kamati Teule inayatolea ufafanuzi masuala kadhaa yanayohusiana na Hadidu za Rejea zilizotangulia. Masuala hayo ni pamoja na; Uvujaji wa Nyaraka za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imelazimika kulitolea maoni suala la uvujaji wa nyaraka za Serikali kwa sababu suala lililosababisha kuundwa kwa Kamati yenyewe linagusa uvujaji wa nyaraka za Serikali. Nyaraka za Serikali zaweza kuwa za wazi *(unclassified)* au za siri *(classified)*. Nyaraka za wazi ni wazi kwa matumizi ya ofisi husika tu na endapo zitavuja hazina madhara kwa Serikali, ni mawasiliano ya kawaida ndani ya Wizara/Idara za Serikali. Kimsingi ni nyaraka ambazo hazina usiri ndani yake ingawaje hazitakiwi kusomwa na watu wasiohusika isipokuwa tu wanapozipata kwa njia zinazoruhusiwa. Akisisitiza hili wakati wa mahojiano, Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Umma alisema:-

> “…katika utendaji wa Serikali kuna majalada yanayoitwa open files yenye masuala ya kawaida…ambayo hayana usiri ndani yake…mawasiliano ambayo kwa namna moja au nyingine hayawezi kuleta athari kwa upande wa Serikali…pamoja na kwamba yanaweza kuwa filled kwenye open files, bado ninaamini kwa dhati kabisa kwamba katika Serikali taarifa si vyema ikawa accessed na mtu ambaye haruhusiwi na kama inatoka basi itoke kwa njia ambayo Serikali imeweka…”

Mheshimiwa Spika, vilevile mawasiliano au taarifa yoyote Serikalini haitakiwi kwenda kwenye Vyombo vya Habari au kwa umma isipokuwa taarifa ambazo zinasaidia katika kujadili masuala ya jamii hazitakiwi kuzuiliwa labda kama taarifa hizo ni za siri. Suala hili limefafanuliwa katika Kifungu C.15 cha Kanuni za Utumishi wa Umma, 2009 Toleo la Tatu kinachosomeka:-

> *“(1) no correspondence which has passed between Ministries, Independent Departments, Regions, Local Government Authorities or between the Public and Ministries/Independent Departments/Executive Agencies/Regions/Local Government Authorities may be communicated to the press or any member of the public without the approval of the Chief Executive Officer concerned, but information of the general nature which may be of material assistance in discussing local questions need not be withheld, provided that such information is not of the confidential nature of likely to infringe the privacy of others.*
>
> *(2) unauthorized disclosure of official information shall make a public servant liable to disciplinary action or criminal prosecution.”*

Mheshimiwa Spika, aidha, utoaji wa taarifa za Serikali bila kibali utafanya mtumishi aliyetoa taarifa hizo kushtakiwa kwa makosa ya kinidhamu au kufunguliwa mashtaka ya jinai.

Mheshimiwa Spika, Nyaraka za Siri *(Classified Documents)* zinafafanuliwa na Sheria ya Usalama wa Taifa, Sura ya 47, katika Kifungu cha 3 kuwa ni taarifa au kitu chochote ambacho mamlaka husika imetamka kuwa ni siri. Kifungu hicho kinasomeka:-

*"…any information or thing declared to be classified by an authorized officer…"*

Mheshimiwa Spika, nyaraka hizi ziko za aina tatu kama ifuatavyo:-

(a) Siri Kuu *(Top Secret)* ni zile ambazo endapo zitavuja zitasababisha madhara makubwa sana *(grave damage)* kwa usalama wa Taifa.

(b) Siri Sana *(Secret)* hizi ni zile ambazo endapo zitavuja zitasababisha madhara makubwa *(serious damage)* kwa usalama wa Taifa.

(c) Siri Ndogo *(Confidential)* hizi ni zile ambazo endapo zitavuja madhara yake sio makubwa sana kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ili kuzitofautisha nyaraka hizi huwa zinagongwa mihuri kulingana na usiri wa nyaraka husika. Kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Taifa, Sura ya 47, kutoa nyaraka hizi kwa mtu asiyeruhusiwa ni kosa. Kifungu cha 5 kinasomeka kama ifuatavyo:-

*"Any person who communicates any classified matter or causes the leakage of such classified matter to any person other than a person to whom he is authorized to communicate it or to whom it is in the interest of the United Republic his duty to communicate it shall be guilty of an offence and liable on conviction to imprisonment for a term not exceeding twenty years."*

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo hayo hapo juu, Kamati Teule imebaini kwamba mawasiliano yote ndani ya Serikali ni ya siri ingawa viwango vya usiri vinatofautiana na kwamba jinsi ya kuzipata nyaraka za mawasiliano hayo ni kwa kibali maalum pekee.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa pamekuwepo na malalamiko ya uvujaji wa Nyaraka za Siri za Serikali. Mmoja wa wachangiaji aliyefika mbele ya Kamati Teule alisema:-

"…katika miaka ya hivi karibuni nyaraka za Serikali tena sensitive kabisa zimekuwa zinaonekana kwenye mitandao ya *internet,* nyingine zinachapishwa kwenye magazeti …"

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa Nyaraka za Serikali zilizopata kuvuja hivi karibuni na kulalamikiwa ni barua ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwenda kwenye Taasisi zilizo chini ya Wizara yake akiziomba zichangie fedha ili kufanikisha uwasilishaji wa Bajeti ya Wizara Bungeni. Katibu Mkuu Kiongozi wakati akitoa matokeo ya uchunguzi kwenye Vyombo vya Habari alipoulizwa kuhusu uhalali wa barua iliyosomwa Bungeni alisema:-

"…mpaka sasa sisi tunaendelea kutafuta nani alitoa taarifa, nani alitoa barua kwa Mbunge au kwa Wabunge. Ikithibitika atapewa haki yake na kuchukuliwa hatua za nidhamu zinazopasa."

Mheshimiwa Spika, kauli hii ya Katibu Mkuu Kiongozi inadhihirisha kwamba barua iliyosomwa Bungeni ni siri ya Serikali na haikupaswa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilitaka kujiridhisha kuwa barua iliyowasilishwa Bungeni na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mbunge, inaangukia katika kundi lipi la nyaraka za Serikali. Kwa kuwa barua hiyo haikuwa na muhuri wa aina yoyote kati ya mihuri mitatu iliyoelezwa hapo juu. Katibu Msaidizi kutoka Tume ya Utumishi wa Umma alitoa maoni yake kwamba barua ile inaangukia kwenye kundi la confidential (siri ndogo) kwa sababu ni mawasiliano kati ya Katibu Mkuu na Watendaji. Aidha, alieleza kuwa kwa utaratibu wa kawaida ilitakiwa igongwe muhuri. Kwa maneno yake alisema:-

"Kwa maoni yangu hii ina-*fall* kwenye *confidential* (siri ndogo)…naweza kushindwa kujua moja kwa moja kwa nini mamlaka husika haikupiga muhuri wa *confidential* juu ya barua hii lakini ninachofahamu ni

kwamba information yoyote ambayo haitakiwi kuwa *open* kwa mtu asiyehusika whether ni ndani ya Wizara husika inatakiwa igongwe muhuri kwa sababu once isipogongwa muhuri basi mtu yeyote hata yule ambaye haruhusiwi kui-*access* anaweza akai-*access* kana kwamba ni *document* ya kawaida...”

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa barua iliyowasilishwa Bungeni na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo ni nyaraka ya kawaida ya Serikali na sio miongoni mwa nyaraka za siri *(classified document)* kwa kuwa haikugongwa muhuri wowote wa siri.

Mheshimiwa Spika, katika mahojiano na mashahidi mbalimbali, Kamati Teule imebaini kwamba baadhi ya sababu zifuatazo huchangia sana uvujaji wa nyaraka za siri za Serikali:-

(a) Baadhi ya Watendaji ndani ya Serikali kutoridhishwa na baadhi ya mambo ambayo yanafanyika katika Idara zao kinyume na utaratibu na hivyo kutaka yarekebishwe. Kwa kuwa Bunge limejijengea heshima na kuaminiwa, watendaji hao huwapatia Wabunge nyaraka zenye vitendo viovu kama vile ubadhirifu wa fedha za umma, wakiamini kufanya hivyo kutasaidia kukomesha vitendo hivyo.

Sababu hii inaungwa mkono na maneno ya mchangiaji mmoja aliposema:-

“...wapo watu kwenye Serikali ambao wanaona vitu ambavyo siyo sahihi, na kwa sababu Bunge limejenga heshima na kuaminiwa, watu wanawaamini Wabunge kwamba ukimpa Mbunge hili Bwana atasaidia kulisema na litarekebishwa. Mimi nadhani ni jambo la muhimu kuendelea kutoa fursa hiyo...”

(b) Baadhi ya watumishi kutoridhishwa na mfumo wa kushughulikia matatizo ama masuala mbalimbali Serikalini hivyo kutafuta msaada kwa Wabunge au kwa vyombo vya habari.

(c) Baadhi ya Watendaji kutoridhishwa na mishahara au marupurupu wanayopewa na hivyo kugeuza nyaraka za Serikali kuwa biashara ili kujiongezea kipato kwa kuziuza kwa watu mbalimbali ambao huzihitaji kwa maslahi yao. Msisitizo katika hili ulitolewa na mmoja wa wahojiwa kwa kusema:-

“...Nyaraka za Serikali zinavuja kwa njia nyingi. Kuna wengine sasa wanafanya biashara...ni ukweli ulio wazi baadhi ya nyaraka za Serikali zinauzwa hata kwa bei mbaya...sasa watumishi wa Serikali wengine wanakuwa *tempted* kuuza baadhi ya nyaraka ili wajipatie kipato...”

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati Teule kwamba, barua aliyosoma Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mbunge, Bungeni ni kielelezo cha watumishi kutoridhishwa na kitendo cha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuzichangisha Taasisi zilizo chini ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule katika uchunguzi wake ilibaini changamoto zifuatazo katika suala zima la nyaraka za Serikali:-

(a) Utaratibu uliowekwa wa kupata taarifa kupitia nyaraka za Serikali kutoka mamlaka husika mfano Watendaji Wakuu hauwawezeshi wale wanaozihitaji kwa nia njema kuzipata kwa urahisi kwa kuwa Watendaji Wakuu hao hao wanaweza kuwa ndiyo wahusika wa maovu yanayotafutwa.

(b) Wigo wa Nyaraka za Serikali kuwa siri ni mpana kiasi ambacho kila jambo linalofanyika linatafsiriwa kuwa ni siri wakati mambo mengine ni ya kawaida tu. Hili ni tatizo kubwa ambalo husababisha mambo maovu kutojulikana mapema na kuliingizia hasara Taifa.

(c) Sheria iliyopo ni ya kutoa adhabu kwa mtoa taarifa inayohusiana na nyaraka za Serikali lakini hakuna Sheria ya kumlinda mtoa taarifa *(Whistleblower Protection Act)* huyo pindi anapotoa taarifa inayosaidia Serikali kubaini maovu na kuyazuia au kuyarekebisha.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto zilizoainishwa hapo juu, Kamati Teule ina maoni yafuatayo:-

(a) Ni vyema nyaraka nyeti *(sensitive)* za Serikali zikaendelea kubakia kuwa siri. Hata hivyo, ni vyema usiri wa nyaraka za Serikali usitumike vibaya kama vile watendaji wa Serikali wasio na maadili kujificha nyuma yake na kutenda maovu.

(b) Serikali ifanye utafiti na uchambuzi ili hatimaye ilete Bungeni Muswada wa Sheria ya Kumlinda Mtoa Taarifa *(Whistleblower Protection Act).*

(c) Utaratibu wa upatikanaji wa nyaraka za Serikali ufanyiwe uboreshaji kwa kuwaruhusu wanaohitaji nyaraka hizo kuziomba katika ngazi za juu ikiwa watapata ugumu katika ngazi ya Watendaji Wakuu *(CEOs)* au ngazi nyingine yoyote husika.

Mheshimiwa Spika, kufuatia maoni ya baadhi ya mashahidi na wachangiaji katika mahojiano, Kamati Teule imebaini masuala kadhaa ambayo Serikali inapaswa kuyazingatia ili kuboresha hatua mbalimbali zinazotumika Serikalini katika kujaza nafasi za uteuzi, taratibu za ajira na kuboresha mpango wa kurithishana madaraka na nafasi za kazi ili kuleta tija. Kamati Teule imebaini kwamba kuteua na kuajiri kwa kuzingatia zaidi upeo, sifa, uzoefu na aina ya taaluma katika nafasi mbalimbali zikiwemo za uongozi katika Idara, Taasisi au Vitengo na kadhalika. kutaongeza uzalishaji na kuboresha utoaji huduma na utekelezaji wa majukumu kwa tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika michango yao wachangiaji mbalimbali waligusia maeneo yafuatayo katika kusisitiza Hoja hizo:-

(a) Kwamba baadhi ya Watendaji wakiwemo wale walioko katika ngazi za maamuzi wanakosa umakini katika kufanya maamuzi na badala yake hutegemea ushauri pekee kutoka kwa watendaji walioko chini yao bila kupima ubora na athari za ushauri huo. Jambo hili linatafsiriwa kuwa kwa kiasi kikubwa linatokana na kukosa taaluma, ujuzi na uzoefu katika nafasi walizonazo, sifa ambazo wakati mwingine watumishi walioko chini yao huwa nazo.

(b) Kwamba ajira zenye kuzingatia taaluma, ujuzi na uzoefu zitakuwa endelevu kwa kuwa zitasababisha ushindani wa wazi miongoni mwa jamii/watumishi na kutoa fursa sawa katika kurithishana nafasi na madaraka na hivyo ushindani huo kuwa chachu katika kuleta maendeleo kwa Taifa.

(c) Kwamba kwa baadhi yao kukosa taaluma husika *(relevant profession)* husababisha kutotii maadili ya taaluma husika kwa kuwa wanaofanya kazi za taaluma bila kuwa na sifa za taaluma hizo hawawajibiki katika taaluma hizo na maadili yake hivyo kufanya maamuzi ambayo husababisha utendaji mbovu na kulisababishia Taifa hasara kubwa, bila kuwepo utaratibu mahususi wa kuwachukulia hatua za kitaaluma ambazo kwa kawaida ni za haraka na zinazofaa zaidi *(more effective).*

(d) Kwamba kukosekana kwa uwajibikaji na kuwepo kwa mmomonyoko mkubwa wa maadili miongoni mwa watumishi wa Serikali na jamii kwa ujumla ndiyo husababisha kutoheshimu na kutotii Sheria, Kanuni na taratibu hivyo kujiingiza katika vitendo visivyofaa kama vile wizi wa mali ya Umma zikiwemo fedha na nyaraka za Serikali.

(e) Kwamba watumishi kutozunguka katika Wizara, Idara na Vitengo mbalimbali wakati wa utumishi wao kunawanyima fursa ya kupata uzoefu mtambuka katika mfumo wa Serikali na kuwafanya wabobee. Aidha, kukaa katika sehemu moja kunawafanya wadumae na pia kuendelea kurudia makosa wanayoyafanya siku hadi siku kwa kutumia mazoea badala ya uzoefu wakidhani hivyo ndivyo sahihi au hufanya makosa kwa makusudi ili kukidhi manufaa yao binafsi.

Mheshimiwa Spika, wakiendelea kutoa michango yao baadhi ya mashahidi walitolea mifano uteuzi katika ngazi za juu na mmoja wao alisema:-

> *"... Accounting Officer* ana sifa gani ndiyo hapo pa kuanzia. Mimi nikasema tu, naweza nikasema pamoja na kwamba naonekana mdogo, lakini ni kati ya watu ambao tulipikwa. Mimi nimekuwa *Head* wa *Section* kwa miaka mitano na nusu, nimekuwa Kamishna kwa miaka mitatu, nimekuwa Naibu Katibu Mkuu *almost three years.* Unajua tofauti na shuleni, yaani kazi za *civil service you learn in the process."*

Nimefanya kazi na Makatibu Wakuu wengi sana, tena wale *the best, I say so.* Nimefanya kazi na akina marehemu Rutihinda, Mzee Fulgence Kazaura, Peter Ngumbulu, nimejifunza mengi pia na Bwana Peniel Lyimo na Bwana Mutalemwa tena wakati huo unajua. Kwa hiyo, sasa *is a learning process,* kama kweli ambition yako ni kufanya vizuri, *there is a lot of best practices.* Unaangalia maneno mazuri ya viongozi wako kwa sababu ukiwa na cheo ni vizuri ukifurahie, unakikalia vizuri kiti chako halafu unakuwa *comfortable.* Na siyo kwenda Dodoma ndiyo unahangaika, inakuwa ni *process* ya mwaka mzima.

Sasa *I would say* kwamba, kuna hii *aspect* ya kujifunza halafu unakomaa unakuwa Afisa Masuuli umetulia. *You know what you are supposed to do. You believe in yourself...."*

Mheshimiwa Spika, aidha, mmoja wa Viongozi Wakuu wastaafu naye aliieleza Kamati kuwa:-

"...Uteuzi wa watu katika nafasi mbalimbali; iwe upande wa Serikali na hata upande wa siasa ni vyema ukafanyika kwa kuzingatia zaidi uwezo kitaaluma, kiutendaji na kimaadili *(Performance, professional and ethical competence).* Ni vyema tukafuata kitu kinachoitwa *meritocracy..."*

Mheshimiwa Spika, kutokana na michango hii, linajitokeza fundisho kwamba zipo changamoto nyingi zinazoikabili Sekta ya Utumishi wa Umma kwa sasa na zinazohitaji kushughulikiwa. Kwa mfano, ili mtu afuzu kuteuliwa katika Utumishi wa Umma, hususan katika kada za juu *(senior and executive grade)* anapaswa kuwa na sifa stahiki katika elimu, uzoefu na uadilifu katika Utumishi wa Umma, ikiwa ni pamoja na kuzingatia maadili ya Taifa na uzalendo.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilipata mfano wa Marekani, ambako mtumishi kabla hajateuliwa katika nafasi yoyote kubwa anapitia kwenye Mtandao wa Vyuo vinavyoitwa *Strategic Studies Institutes,* ambavyo kazi yake ni kufundisha Maadili ya Taifa, Sera za mambo mbalimbali, Uzalendo na mengineyo yenye mtazamo au sura ya kitaifa bila kujali itikadi. Utaratibu huu unafanana na ule wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa na vyuo vingine mahususi kwa mafunzo ya Uongozi, utaratibu ambao ni mzuri na Taifa letu linapaswa kuongeza kasi ya kuufufua na kuuendeleza.

Mheshimiwa Spika, madhara yanayotokana na kuwepo kwa watumishi wasiokidhi vigezo vya kitaaluma, uzoefu na uadilifu ni mengi ikiwa ni pamoja na:-

(a) Ushauri usiofaa wa baadhi ya Wataalamu kwa Wakuu wao wa Kazi. Kwa mfano, katika suala la Wizara ya Nishati na Madini kuendesha michango kwenye Taasisi zilizo chini yake, upo ushahidi kwamba Mkurugenzi wa Sera na Mipango alitoa ushauri usiofaa na wa upotoshaji kwa Katibu Mkuu huku akijua fika, kwa taaluma na uzoefu wake, kwamba kufanya hivyo ni kinyume na Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha. Kwa upande wa Wahasibu wa Idara, Kamati Teule imebaini kwamba licha ya kuhusika kwa namna mbalimbali katika matumizi ya fedha zilizokusanywa walifanya hivyo bila kuzingatia taratibu za fedha kama wataalam.

(b) Baadhi ya Watendaji Wakuu kushindwa kupima ushauri wanaopewa na hatimaye kufanya maamuzi yasiyo sahihi. Kwa mfano katika suala hili lililosababisha kuundwa kwa Kamati Teule, kama ilivyoelezwa hapo juu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini alishauriwa na watendaji wake kuendesha uchangishaji, lakini alishindwa kupima mantiki ya ushauri huo kuwa ni kinyume na Kanuni za Fedha za Umma, 2001. Katika mahojiano na Kamati Teule Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini alitumia maelezo ya kwamba alishauriwa na wataalam kama utetezi pekee.

(c) Matumizi ya fedha za umma kwa namna ambayo haiipatii Serikali thamani ya fedha hizo badala yake huiletea hasara na hatimaye kurudisha nyuma jitihada za Serikali katika kuinua na kuimarisha uchumi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia Hoja mbalimbali kama zilivyotolewa hapo juu, Kamati Teule ina maoni yafuatayo:-

(a) Ni vyema Watumishi wakawezeshwa ili wazifahamu vizuri zaidi kazi zao, wazipende, wawe mabingwa na wabobee ili kuleta tija na ufanisi Serikalini, lakini pia kukuza fursa zao katika Soko la Ajira la Afrika Mashariki na duniani kote *(World class standards);* lakini ni muhimu zaidi kwa Watumishi wa Umma kuwa wazalendo, waipende Nchi yao na wafanye kazi zao kwa kuzingatia maadili na kuweka mbele maslahi ya Taifa.

(b) Kuhusu maadili ya taaluma *(Professional Ethics)* kwa wataalamu mbalimbali wakiwemo Wanasheria, Wahandisi, Wahasibu, Wataalamu wa Sekta ya Afya, Utawala na kadhalika ili kudhibiti changamoto zinazotokana na kusaini mikataba mibovu na kufanya maamuzi mengineyo yanayoligharimu Taifa, wakati umefika sasa kwa Serikali kutumia vizuri zaidi Mabaraza, Bodi na Jumuiya mbalimbali za kitaaluma zilizoanzishwa kisheria ili watumishi wataalamu hao wanaokiuka maadili ya taaluma zao wabanwe.

Taasisi hizi zina mamlaka ya kisheria ya kuchukua hatua hata za kunyang'anya leseni ikithibitika ukiukaji huo ni wa kiwango cha kupindukia na pindi mtaalamu anaponyang'anywa leseni anapoteza sifa za kuajiriwa katika nafasi hiyo. Jambo hili linaweza kuwa muafaka kwa hatua za haraka wakati taratibu nyingine za kisheria zikiwa zinafuatia kwa kuwa hizo zina mlolongo mrefu na huchukua muda mrefu zaidi.

(c) Namna nzuri ya kuendelea kuwatumia wastaafu na waliobobea katika utendaji Serikalini sio kuwaacha katika ajira rasmi kwa kuongeza mikataba; badala yake ni vyema zaidi kuwatambua na kuwaandaa kuwa waajiri wapya katika Sekta Binafsi ili waendelee kushiriki katika ujenzi wa Taifa kupitia utaratibu wa *Public Private Partnership (PPP)* ambao ni kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano chini ya Dira ya Taifa ya 2025.

Kuwatumia wastaafu kwa utaratibu huu kutapunguza woga wa watumishi kustaafu, kutaongeza ajira Serikalini hasa ajira kwa vijana, kutaongeza ajira katika Sekta Binafsi, kutawaongezea fursa za ajira rasmi vijana wahitimu kutoka Vyuo Vikuu na vinginevyo na kutaacha urithi kwa waajiriwa wapya *(back up).*

Mheshimiwa Spika, ushauri huu ukizingatiwa utakuza, kuimarisha na kuboresha utendaji na mchango wa Sekta Binafsi katika maendeleo ya Taifa. Hii ni kwa sababu watumishi hawa wastaafu na waliobobea na wanaotokea Serikalini watakuwa wanazijua na watazingatia Sheria, Kanuni na taratibu na miongozo mbalimbali ikiwemo miiko n.k hivyo kuongeza tija katika malengo mbalimbali ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mahojiano na mashahidi mbalimbali Kamati Teule imebaini changamoto kadhaa katika utendaji wa Wizara ambazo zinahusu uhusiano wa kikazi baina ya Mawaziri na Makatibu Wakuu. Ili kuweza kutoa maoni na mapendekezo kuhusiana na suala hili Kamati Teule ilifanya utafiti kuhusu kazi za Makatibu Wakuu na Mawaziri na mahusiano yao ya kikazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 5(1)(a) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002 kinaelezea uteuzi wa Makatibu Wakuu wa Wizara *(Permanent Secretaries)* unaofanywa na Rais. Katibu Mkuu ni Mtendaji Mkuu wa Wizara na kwa maana hiyo ndiye mshauri mkuu wa Waziri katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Hivyo basi, Katibu Mkuu katika Wizara ana majukumu yafuatayo:-

(a) Kuwa Afisa Masuuli wa Wizara *(Accounting Officer).*

(b) Kuwa Mkuu wa Watumishi wote wa Umma walioko Wizarani.

(c) Kushauriana na Waziri juu ya mambo yote yanayohusu Baraza la Mawaziri.

(d) Kuandaa na kutekeleza Sera, Sheria, Mikakati, Mipango na Programu za Sekta yake.

(e) Kuandaa Rasimu ya nyaraka zote za Baraza la Mawaziri zinazohusu Wizara.

(f) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi yote ya Baraza la Mawaziri yanayohusu Wizara na kuandaa Taarifa za Utekelezaji na kuziwasilisha katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, kila robo ya mwaka na kila zinapohitajika.

(g) Kuandaa orodha ya masuala muhimu yanayotarajiwa kuwasilishwa katika Baraza la Mawaziri toka katika Wizara kila baada ya miezi sita na kuiwasilisha katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

(h) Kuwasilisha kwenye Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mapendekezo ya Programu ya Miswada inayotarajiwa kuwasilishwa Bungeni kwa mwaka mzima mwanzoni mwa kila mwaka.

(i) Kuhudhuria vikao vyote vya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu *(IMTC),* Kamati Ndogo za *IMTC* na Vikao vya Kazi.

(j) Kushauriana na Waziri mambo yote yanayohusu Wizara.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 55(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaelezea uteuzi wa Mawaziri unaofanywa na Rais. Kazi za Mawaziri *(Ministers)* zinaainishwa katika Mwongozo wa Baraza la Mawaziri kama ifuatavyo:-

(a) Msimamizi Mkuu wa Wizara katika utekelezaji wa maamuzi na shughuli za Serikali ikiwa ni pamoja na Sera, Mikakati, Mipango na Programu.

(b) Akiwa ni mwakilishi wa Rais Wizarani, Waziri ndiye mlinzi na mtetezi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(c) Waziri ni msemaji Mkuu wa Wizara. Aidha, Waziri anawajibika kwa Rais, Waziri Mkuu na kwa Bunge kuhusu uendeshaji wa Wizara anayoiongoza.

(d) Waziri pia anawajibika kuwasilisha kwenye Baraza la Mawaziri mapendekezo ya masuala ya Kitaifa yatakayojadiliwa katika ngazi ya Kimataifa na ambayo yanahitaji msimamo wa nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mwongozo wa Baraza la Mawaziri Kamati Teule imeridhika kwamba, mahusiano ya kikazi baina ya Mawaziri na Makatibu Wakuu yamewekwa bayana, kwa lugha inayoeleweka na kukidhi haja ya kuwafanya Mawaziri na Makatibu Wakuu watekeleze majukumu yao kwa ufanisi na kwa tija. Kwa mfano, kama ilivyoelezwa hapo juu Waziri ndiye msimamizi mkuu wa Wizara katika utekelezaji wa maamuzi na shughuli za Serikali ikiwa ni pamoja na Sera, Mikakati, Mipango na Programu. Wakati huo huo miongoni mwa kazi kubwa za Katibu Mkuu ni kuandaa na kutekeleza Sera, Sheria, Mikakati, Mipango na Programu za Sekta yake. Vilevile imeainishwa kwamba Katibu Mkuu atashauriana na Waziri juu ya mambo yote yanayohusu Wizara. Aidha, Katibu Mkuu ndiye Afisa Masuuli wa Wizara *(Accounting Officer).*

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imechambua Kazi za Mawaziri na Kazi za Makatibu Wakuu kama zilivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Baraza la Mawaziri. Vilevile Kamati Teule imechambua Sheria ya Fedha za Umma, 2001 *(The Public Finance Act 2001 Act No. 6, 2001)* na kubaini Kifungu cha 8(1) cha Sheria hiyo ambacho kimeweka wazi nafasi ya Katibu Mkuu katika kutekeleza majukumu yake ya masuala ya fedha pasipo kumshirikisha Waziri ambaye ndiye msimamizi mkuu wa Wizara. Kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo:-

> *8(1) There shall be appointed by name and office and in writing by the Paymaster-General an accounting officer in respect of each expenditure vote, who shall control and be accountable for the expenditure of money applied to that vote by an Appropriation Act and for all revenues and other public monies received, held or disposed of, by or on account of the department or service for which the vote provides.*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maudhui ya Mwongozo wa Baraza la Mawaziri, Katibu Mkuu ndiye mtekelezaji wa Sera, Sheria, Mikakati, Mipango na Programu, na kwamba chini ya Mwongozo huo Katibu Mkuu atafanya hivyo chini ya uongozi wa Waziri ambaye ni Msimamizi Mkuu wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo. Hata hivyo, yakikosekana mawasiliano mazuri kati ya Waziri na Katibu Mkuu kinyume na matakwa ya Mwongozo wa Baraza la Mawaziri na Katibu Mkuu akatumia madaraka yake kama yanavyoainishwa katika Kifungu cha 8(1) ni vigumu sana kwa Waziri kusimamia utekelezaji wa maamuzi na shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Spika, uchangishaji wa Shs 22,000,000.00 kwa Taasisi Nne chini ya Wizara ya Nishati na Madini kwa ajili ya Semina ya Wabunge.

Mheshimiwa Spika, katika uchunguzi wake, Kamati Teule ilibaini kuwa, utaratibu wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kuchangisha Idara zilizo chini yake haukutumika kwenye suala la uwasilishaji wa Bajeti pekee. Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu David Kitundu Jairo, aliziandikia pia barua Taasisi nne kuomba mchango kwa ajili ya Semina ya Waheshimiwa Wabunge iliyofanyika tarehe 26 Juni, 2011 katika Ukumbi wa Pius Msekwa, Dodoma. Katika barua hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini aliainisha kuwa ushiriki wa

Wizara pamoja na kukodisha Ukumbi ungehitaji Shs 39,000,000.00 na ushiriki wa Waheshimiwa Wabunge Shs 46,000,000.00; kwa mchanganuo huo, mahitaji halisi ya Semina yalikuwa Shs 85,000,000.00.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa barua iliyotajwa hapo juu, kila Taasisi ilitakiwa kuchangia Shs 22,000,000.00 na kwamba kiasi hicho kilipwe kwa Bi. Hawa Ramadhani, Mhasibu wa Wizara. Taasisi hizo ni *REA, EWURA, TANESCO* na *TPDC*. Taasisi zote zilichanga kama ilivyotakiwa na jumla ya michango ilikuwa Shs 88,000,000.00.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha hizi zilizochangwa (Shs 88,000,000.00) yalikuwa kama ifuatavyo:-

| Na. | Matumizi | Kiasi cha Fedha (Shs) | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Posho kwa Waheshimiwa Wabunge | 15,840,000.00 | 18% |
| 2. | Posho kwa watubalimbali | 57,539,800.00 | |
| 3. | Mafuta ya magari | 5,040,000.00 | 82% |
| 4. | Chakula | 4,194,200.00 | |
| 5. | Vifaa vingine | 5,386,000.00 | |
| | **JUMLA KUU** | **88,000,000.00** | **100%** |

Tanbihi: Posho kwa watu mbalimbali ililipwa kwa:-

(i) Watumishi wa Ofisi ya Bunge;
(ii) Watumishi wa Wizara ya Nishati na Madini;
(iii) Waandishi wa Habari;
(iv) Watumishi wa Afya; na
(v) Askari Polisi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, kwa mujibu wa barua ya maelekezo iliyotolewa na Ofisi ya Bunge juu ya Semina ya Wabunge kuhusu Sekta ya Umeme, viwango vya posho vilielekezwa kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| (a) | Viongozi wa Bunge | Shs. | 250,000.00 |
| (b) | Wabunge (Vikao) | Shs. | 80,000.00 |
| (c) | Wabunge (usafiri) | Shs. | 30,000.00 |
| (d) | Wakuu wa Idara au Kazi maalum | Shs. | 80,000.00 |
| (e) | Maofisa | Shs. | 50,000.00 |
| (f) | Watoa huduma wengine | Shs. | 20,000.00 |

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia nyaraka za matumizi ya michango hiyo ya Shs. 88,000,000.00, Kamati Teule ilibaini kwamba baadhi ya viwango vya malipo ya posho vilikuwa tofauti na maelekezo kutoka Ofisi ya Bunge. Kwa mfano, wakati Waheshimiwa Wabunge walilipwa Shs. 110,000.00 kila mmoja, ilionekana kuwa mtumishi wa ngazi ya mhudumu alilipwa Shs. 120,000.00 badala ya Shs. 20,000.00; Wakurugenzi walilipwa Shs. 180,000.00 badala ya Shs. 80,000.00; na Maofisa wengine walilipwa Shs. 150,000.00 badala ya Shs. 50,000.00.

Mheshimiwa Spika, baada ya kujitokeza utata huo, Kamati Teule ililazimika kufanya mahojiano na Mhasibu wa Wizara ya Nishati na Madini aliyehusika kulipa posho hizo, ambaye alieleza kwamba aliagizwa kwa mdomo na kiongozi wake kuwa amuongezee kila mtumishi Shs 100,000.00 ikiwa ni bonus kwa kazi waliyofanya ya kudurufu makabrasha ya Semina. Nyongeza hiyo ndiyo ilisababisha posho zilizolipwa kwa watumishi zisomeke kuanzia Shs 120,000.00, 150,000.00 na Shs 180,000.00 badala ya Shs 20,000.00, Shs 50,000.00 na Shs 80,000.00.

Hata hivyo, baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Bunge wanaohusika na kuratibu shughuli za semina za Wabunge walipohojiwa na Kamati Teule walikana kuhusika na malipo ya viwango vya posho vya Shs 120,000.00, 150,000.00 na Shs 180,000.00 na kwamba wao walilipa Shs 20,000.00, Shs 50,000.00 na Shs 80,000.00 kufuatana na maelekezo ya Ofisi ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, ukweli uliothibitika katika suala hili ni kama ifuatavyo:-

(a) Wakati Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini alidai kutenga Shs 39,000,000.00 kwa ajili ya ushiriki wa Wizara na kukodisha ukumbi, Kamati Teule imethibitisha kuwa Ukumbi wa Pius Msekwa huwa haukodishwi.

(b) Kufuatia mahojiano kati ya Kamati Teule na baadhi ya mashahidi waliolipwa, Watumishi waliotajwa kwamba wamelipwa Shs 120,000.00 walilipwa Shs 20,000 tu; watumishi waliotajwa kwamba wamelipwa Shs 150,000.00 walilipwa Shs 50,000.00 tu na wale waliotajwa kwamba wamelipwa Shs 180,000.00 walilipwa Shs 80,000.00 tu. Kwa maana hiyo, malipo ya nyongeza ya Shs 100,000.00 yaliyooneshwa kwa kila mtumishi si halisi bali ni ya kughushi. Kutokana na kughushi huko, jumla ya fedha kiasi cha Shs 13,900,000.00 ambazo ni asilimia 15% ya jumla ya fedha zilizokusanywa (88,000,000.00) ni malipo hewa.

(c) Baadhi ya watumishi walioorodheshwa kuwa walipokea malipo hayo hawakuwepo Dodoma siku hiyo.

(d) Hata kama agizo la malipo ya bonus lingekuwa ni la kweli haiwezekani shughuli ya kudurufu nyaraka za semina ifanywe na Wakurugenzi wote, Maofisa wote na wahudumu wote. Hii inaoyesha kwamba namba ‘1’ iliongezwa baada ya malipo halali kufanyika.

(e) Tarehe 25 Juni, 2011 yalifanyika manunuzi ya Mikoba *(Bags)* 310 kwa ajili ya kuwekea makabrasha ya Semina ya Waheshimiwa Wabunge. Mikoba ilinunuliwa kwa fedha taslimu kinyume na masharti ya Kanuni 86(1) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 kwa kutoambatisha bei shindanishi.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya mchakato wa kukusanya Shs 88,000,000.00 na kuzitumia kwenye Semina ya Wabunge kwa kiwango kikubwa hayatofautiani na mazingira yaliyotumika kuchangisha Shs 140,000,000 kutoka Taasisi za Wizara na kuzitumia katika shughuli ya maandalizi na uwasilishaji wa Hotuba ya Bajeti Bungeni kama ilivyobainika hapo awali katika Taarifa hii. Tofauti iliyopo ni kwamba michango ya Shs 88,000,000.00 ilipelekwa moja kwa moja kwa mtumishi wa Wizara bila kuingizwa kwenye Akaunti ya Wizara ya Nishati na Madini wala Akaunti ya *GST.*

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inaona kwamba utaratibu wa sasa wa uendeshaji wa Semina za Wabunge unatoa mwanya kwa watendaji wasio waaminifu kufuja fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati Teule inafanya mahojiano na watu mbalimbali, Hoja kadhaa zinazohusu mgawanyo wa madaraka na uhusiano wa kikazi wa Mihimili ya Dola hususan Bunge na Serikali, zilijitokeza. Baadhi ya Hoja hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kilichotokea Bungeni tarehe 18 Julai, 2011 ni Bunge lilikuwa likitekeleza wajibu wake wa kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba.

(b) Katiba yetu haitoi mgawanyo bayana wa madaraka *(Clear Separtion of Powers)* baina ya Mihimili mitatu ya Dola hususan Bunge na Serikali tofauti na ilivyo katika nchi nyingine kama vile Kenya. Chini ya Katiba mpya ya Kenya Serikali haimo ndani ya Bunge; Mawaziri sio Wabunge na Mwanasheria Mkuu wa Serikali pia sio Mbunge.

(c) Taratibu za mgawanyo wa madaraka zipo katika Katiba lakini wakati mwingine zinasahaulika na kutofuatwa ipasavyo.

(d) Dhana ya mgawanyo wa madaraka haimaanishi utengano, yaani mamlaka haya hayahodhiwi na Chombo kimoja tu, isipokuwa uangalifu unahitajika kwa namna ya kutenganisha kazi za Mihimili hii mitatu vinginevyo uko uwezekano mkubwa wa kugongana.

(e) Bunge limeanza kuingia katika shughuli za utendaji badala ya kuisimamia Serikali, kwa mfano Kamati za Kudumu za Bunge badala ya kushughulika na Wizara zinakwenda moja kwa moja kwa Taasisi.

(f) Kazi hii inayofanywa na Kamati Teule ya Bunge ya kuchunguza suala lililofanywa na Serikali inaonesha kuwa Bunge sasa linaingilia kazi za utendaji (Bunge linaingia jikoni) badala ya kubaki na kazi yake ya kuisimamia Serikali.

(g) Katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Wabunge kazi yao ni kuratibu, kuhoji na wakati mwingine kuibana Serikali ili ifanye kazi kulingana na malengo ya Katiba. Serikali inawajibika Bungeni na mambo yote yanayofanywa na Serikali hususan yale yanayohusu fedha ni lazima yawe wazi ili Bunge liweze kuchunguza kama matumizi ya fedha yanaendana na taratibu, Kanuni na masharti yanayowekwa na Sheria.

(h) Ni muhimu Bunge na Serikali vifanye kazi kwa utaratibu ambao ni wa maelewano.

(i) Mawanda *(scope)* ya Ibara ya 63(2) inayohusu Bunge "kuisimamia na kuishauri Serikali" hayako wazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hoja zilizotajwa hapo juu, Kamati Teule imeona izungumzie, kwa ufupi, uhusiano miongoni mwa Mihimili ya Dola, hususan changamoto zilizopo na namna ya kuzishughulikia. Hata hivyo, changamoto hizo zitahusu mahusiano ya kikazi kati ya Serikali na Bunge tu kwa kuwa jambo lililosababisha kuundwa kwa Kamati Teule lilihusisha Mihimili hiyo miwili. Ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 pamoja na mambo mengine, inaelezea dhana ya mgawanyo wa madaraka *(Separation of Powers)* baina ya Mihimili mitatu ya Dola ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Serikali ina mamlaka ya utendaji, Bunge lina mamlaka ya kutunga Sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma na Mahakama ina mamlaka ya kutekeleza utoaji haki. Aidha, Ibara hii inasisitiza kwamba:-

> "Kila Chombo kilichotajwa katika Ibara hii kitaundwa na kutekeleza majukumu yake kwa kufuata masharti mengine yaliyomo katika Katiba hii."

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa madaraka ya kila Mhimili, Ibara ya 35 inaelekeza kwamba shughuli zote za utendaji za Serikali ya Jamhuri ya Muungano zitatekelezwa na watumishi wa Serikali kwa niaba ya Rais. Ibara ya 62 inaanzisha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kufafanua kwamba Bunge litakuwa na sehemu mbili; Rais na Wabunge. Ibara ya 63(2) inaweka wazi kwamba Sehemu ya Pili ya Bunge ina madaraka, kwa niaba ya Wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba.

Kwa upande wa Mahakama, Ibara ya 107A inaelekeza kwamba mamlaka yenye kauli ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama, na kwamba katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, Mahakama zote zitakuwa huru na zitalazimika kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, Katiba inafafanua kwamba wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote, na kwamba Serikali itawajibika kwa Wananchi. Kufuatana na misingi ya demokrasia ya uwakilishi, mamlaka ya wananchi ya kuiwajibisha Serikali yanatekelezwa na Bunge, na kama ilivyoelezwa hapo awali, jukumu kubwa la Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali kwa niaba ya Wananchi. Katika kutekeleza jukumu hili Bunge linawauliza Mawaziri maswali kuhusu mambo ya umma ambayo yako ndani ya wajibu wa Waziri husika, linajadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bajeti, linajadili na kuidhinisha mpango wa muda mrefu au mfupi unaokusudia kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga Sheria ya kusimamia utekelezaji huo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kuisimamia Serikali, Bunge kama sauti ya wananchi, lina wajibu wa kuzungumzia jambo lolote linalohusu uendeshaji wa Serikali yakiwemo matumizi ya fedha za umma. Mipaka ya Bunge kufanya kazi zake za kuihoji na kuisimamia Serikali na kutunga sheria ipo ndani ya Katiba na imefafanuliwa katika Kanuni za Bunge. Kwa mfano, katika kutunga Sheria, Bunge linatakiwa kuzingatia masharti yaliyowekwa na Sehemu ya Tatu ya Katiba (Haki na Wajibu muhimu), pamoja na Ibara za 64, 98 na 99. Vilevile Kanuni za Bunge zimeweka miongozo ya uendeshaji wa mijadala Bungeni. Jambo ambalo Kamati Teule imelibaini katika suala hili ni kuwa kila Mhimili unataka kufanya kazi wenyewe na kukumbatia mamlaka yake kiasi kwamba inapotokea Mhimili mwingine unahoji inaonekana kama vile Mhimili huo unataka kuingilia madaraka ya mwingine. Hii ni kinyume na ukweli kwamba kulingana na mfumo wa utawala wa nchi yetu hakuna *absolute separation of powers.* Katika suala hili Serikali inadai kwamba jukumu la kusimamia nidhamu za utumishi wa umma ni la kwake na sio la Bunge, na ndiyo msingi wa madai kwamba kitendo cha Bunge kuunda Kamati Teule kuchunguza suala ambalo kwa mtazamo wa Serikali linahusu nidhamu ya watumishi wa umma ni kuingilia madaraka yasiyo ya kwake. Akitoa maelezo yake mbele ya Kamati Teule, Katibu Mkuu Kiongozi alisema:-

"…lipo tatizo la tafsiri, mamlaka na mipaka ya mihimili hiyo, *particularly* Mihimili hii miwili; Bunge na *Executive* kwa maana ya Serikali. *We have a problem, a serious one…* leo Mhimili mmoja unahojiwa na Mhimili mwingine kwa uamuzi wake; *it is a very serious problem!..."*

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine msimamo wa Bunge ni kuwa suala la Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu David Kitundu Jairo siyo la kinidhamu pekee bali linahusu nidhamu na matumizi ya fedha za umma, na kwamba kwa kuwa Katiba imetoa mamlaka kwa Bunge kuidhinisha fedha zote zitakazotumika na kusimamia matumizi yake, hivyo Bunge lina wajibu wa kuingilia kati pale inapoonekana kuwa kuna vitendo vinavyoashiria matumizi mabaya ya fedha za umma. Na kwamba Katiba imelipa Bunge mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali katika mambo yote yanayohusu Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imebaini pia kuwepo kwa changamoto za kimawasiliano miongoni mwa Viongozi Wakuu ndani ya Serikali. Katibu Mkuu Kiongozi ni Mkuu wa Utumishi wa Umma na Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wa umma wanaoteuliwa na Rais. Waziri Mkuu ana madaraka juu ya udhibiti, usimamiaji na utekelezaji wa siku hadi siku wa kazi na shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Waziri Mkuu pia ni kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Spika, changamoto hii ya mawasiliano hafifu baina ya viongozi hawa imejidhihirisha katika kulishughulikia suala la Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu David Kitundu Jairo. Suala hili liliibuka Bungeni, na kama tulivyoeleza hapo awali baada ya mchakato wa kulishughulikia kukamilika kulitakiwa kuwepo mawasiliano kati ya Katibu Mkuu Kiongozi na Waziri Mkuu. Hata hivyo, Katibu Mkuu Kiongozi alieleza kwamba alichukua hatua ya kushughulikia suala la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Ndugu David Kitundu Jairo, kama Mamlaka ya Nidhamu na kwamba hana uhakika kama Waziri Mkuu alilieleza Bunge kuwa Serikali ingerudisha majibu Bungeni. Kwa upande wake Waziri Mkuu aliieleza Kamati Teule kwamba:-

"… kwa mujibu wa mamlaka yake alifanya hivyo. Lakini kama nilivyokuwa nimesema kwamba, angeweza vilevile kutumia ile niliyosema yaani uhusiano na hekima ambazo zimekuwa zikitumika hapa na pale katika kupima suala gani ujumuike na viongozi wenzako. Katika jambo hili angeweza vile vile akaamua kwamba ah, katika hili ngoja nimshirikishe Waziri Mkuu… lakini ukienda tu kwa mtazamo wa Sheria moja kwa moja, wakati mwingine tunaingia kwenye matatizo ambayo yanaweza kuleta tatizo katika uendeshaji wa shughuli za Serikali…"

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inaona kuwa pamoja na kwamba kila Mhimili una kazi zake, lengo kubwa ni kumhudumia mwananchi, kitendo cha Mihimili kuvutana kina athari kwa misingi ya utawala bora na kinaweza kukwamisha maendeleo. Ni maoni ya Kamati Teule pia kwamba dhana ya mgawanyo wa madaraka haimaanishi mamlaka yamehodhiwa na Chombo kimoja au mtendaji mmoja tu, bali Mihimili inatakiwa ishirikiane, iheshimiane na kukosoana *(checks and balances).*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hiari *(Discretionary Powers)* kwa Makatibu Wakuu wa Wizara na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, katika lugha ya kawaida *"discretionary powers"* ni mamlaka ya hiari ya kuchukua hatua au kufanya maamuzi kwa namna ambayo mhusika ataona inafaa *(one's own judgment).* Mamlaka ya namna hii hutolewa kwa viongozi au watendaji katika nyanja mbalimbali kwa lengo la kuwezesha shughuli kufanyika kwa ufanisi bila vikwazo visivyo vya lazima. Mara nyingi *discretionary powers* hutolewa kwa Majaji, Mahakimu, Viongozi wa Kisiasa na Watendaji Wakuu Serikalini na katika Taasisi za Umma na hata Taasisi Binafsi. Katika uchunguzi wake, Kamati Teule imebaini kuwa kuna upungufu katika matumizi ya fedha za umma unaotokana na discretionary powers wanazopewa Watendaji Wakuu katika Wizara na Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imebaini kuwa baadhi ya malipo ya stahili mbalimbali kwa Viongozi na Watumishi wa Umma hayajawekewa masharti wala viwango ambavyo vinatakiwa kuzingatiwa. Taratibu na viwango vya malipo husika hutolewa na Watendaji Wakuu kwa kadri kila mmoja anavyoona inafaa. Mfano wa stahili ambazo Kamati Teule imearifiwa kuwa hazijatolewa viwango rasmi vya malipo ni Posho ya Takrima *(Entertainment Allowance).*

Mheshimiwa Spika, Kanuni L.14 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009, Toleo la Tatu inayohusu Posho ya Takrima *(Entertainment Allowance)* inasomeka kama ifuatavyo:-

*"L.14(1) All Accounting Officers are allocated funds for entertainment under their respective items for "Government Hospitality." This is the only provision from which an Accounting Officer is required to meet his expenditure on any form of entertainment.*

*(2) The objective of providing funds for entertainment is to afford every Accounting Officer the ability to offer Government hospitality to the public servants directly concerned with his field of responsibility ...*

*(3) It is not possible to foresee or set out all the circumstances or occasions, which would justify the use of funds from the government hospitality vote. This is left to the good judgment and discretion of Accounting Officers ...*

*(4) A commuted entertainment allowance may be granted from the central entertainment vote to a public servant who is regularly called upon to extend hospitality on behalf of the Government."*

Mheshimiwa Spika, wakati kukiwa hakuna mwongozo wowote uliotolewa juu ya namna ya utekelezaji wa Kanuni hii, hali ni tofauti kwa Kanuni L.32 inayohusu Posho ya Vikao *(Sitting Allowance).* Kanuni hii inaainisha kwamba kutakuwa na Posho ya Vikao ambayo italipwa kwa kibali cha Katibu Mkuu (Utumishi) kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu, Katibu Msaidizi na Wajumbe wa Tume, Bodi au Kamati iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria au iliyoundwa kwa agizo la Rais au Waziri Mkuu. Aidha, Kanuni L.33 inasomeka: -

*"L.33 Sitting Allowance shall be payable per day of the sitting at a rate to be determined from time to time, by the Permanent Secretary (Establishments)."*

Mheshimiwa Spika, katika kuweka mwongozo wa viwango vya Posho hii kama inavyoelekezwa na Kanuni L.33, Katibu Mkuu (Utumishi) amekuwa akitoa Waraka mara kwa mara. Waraka unaotumika hivi sasa ni Waraka wa Utumishi wa Serikali Na. 2 wa Mwaka 2010 kuhusu Posho ya Vikao *(Sitting Allowance)* wa tarehe 11 Februari, 2010 ambao umeanza kutumika tarehe 1 Julai, 2010.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya kutokuwa na Waraka maalum unaofafanua viwango na taratibu za Posho ya Takrima *(Entertainment Allowance)* ni kuwa, Wizara zimekuwa na viwango na taratibu tofauti za kulipa posho hii kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri hususan wakati wa Mikutano ya Bunge, Dodoma. Katika mahojiano na Viongozi na Watendaji mbalimbali wa Wizara, Kamati Teule imekuwa ikihoji utaratibu na viwango vinavyotumika na mara zote majibu yamekuwa yakitofautiana kati ya Mtendaji mmoja na mwingine.

Mheshimiwa Spika, alipoulizwa na Kamati Teule kama kuna Mwongozo wowote unaofuatwa na Wizara yake katika kuwalipa Waziri na Naibu Waziri Posho ya Takrima *(Entertainment Allowance),* Mmoja wa Makatibu Wakuu wa Wizara alisema kuwa malipo hayo yanategemea hali ya fedha, na kwamba:-

"...kuna kipengele kinasema discretion ya Katibu Mkuu, inategemea kutokana na hali ya fedha, kwa hiyo, sisi tumezoea tukienda kule tunajua Waziri atakuwa na wageni ... mara nyingine unaweza tu ukawanunulia... maji, juisi, lakini hatuna fedha ... ni ngumu kumpa fedha au kumpelekea vitu vingi..."

Mheshimiwa Spika, kauli hii inalingana na majibu ya Waziri mmoja ambaye alieleza kwamba hajawahi kuona Waraka unaoonesha kuwa anastahili kulipwa kiasi fulani cha Posho ya Takrima *(Entertainment Allowance)*; hivyo inategemea na hali ya fedha wakati mwingine anapata, wakati mwingine hapati.

Mheshimiwa Spika, Waziri mwingine alipoulizwa utaratibu unaotumika na Wizara yake kuwalipa Posho ya Takrima *(entertainment allowance)* yeye na Naibu Waziri wake alisema:-

"...kuna Mwongozo ambao umetolewa, kwa mfano, Waziri akienda kwenye Bunge la Bajeti fedha atakazolipwa kwa ajili ya *entertainment allowance* ni Shs. 500,000.00 na Naibu Waziri Shs. 400,000.00 ...kwenye Bunge la kawaida tunapewa Shs. 200,000.00. Hii ni kwa nyakati zile ukiwa Bungeni, kule unaweza kutembelewa na mgeni...anakuja kuzungumzia juu ya barabara yake...huwezi ukamwangalia tu, itabidi umnunulie soda ..."

Mheshimiwa Spika, Waziri mwingine tena alisema hajawahi kupewa posho hiyo na kwamba:-

"…kwa ngazi ya Waziri ninavyojua ni kwamba, huwa kuna vitu vinaitwa kama chai, ambavyo ni vya Ofisi yake, lakini sijawahi kuona inakuwa ni kama fedha *as such*… nimekuwa Waziri sijawahi kushika fedha kwamba hii ndiyo allowance yako, mara nyingi Ofisi ile ndiyo inasimamia, wageni wamekuja leteni juisi, kuna wageni wanapewa…"

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Nishati na Madini Kamati Teule iliona katika nyaraka na pia kwa maelezo ya Watendaji wa Wizara kuwa, kati ya tarehe 18 Julai hadi 26 Agosti, 2011 wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge (Juni – Agosti, 2011) Waziri na Naibu Waziri walilipwa Shs 4,000,000.00 kila mmoja kama Posho ya Takrima *(Entertainment Allowance).* Katika kufafanua sababu na vigezo vya Wizara hii kulipa kiasi hiki cha fedha, Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Nishati na Madini alieleza:-

"…Katibu Mkuu wa Wizara anayo mandate ya kutoa *entertainment allowance* kwa Maofisa hata viongozi … kwa msingi huo nilimshauri Katibu Mkuu kwamba atoe *entertainment allowance*, na mara nyingi Katibu Mkuu anaweza kutoa kiasi chochote ambacho anafikiria. Lakini tuliona kwa kipindi ambacho kilikuwa kimebaki Mawaziri wetu pamoja na matatizo ambayo yalikuwa yametokea wasijisikie wapweke sana waweze kuendelea kufanya kazi zao kwa amani…"

Mheshimiwa Spika, baada ya kubaini kuwepo kwa tofauti kubwa ya viwango vya posho ya Takrima vilivyolipwa na Wizara hii ikilinganishwa na Wizara nyingine Kamati Teule ililazimika kufanya mahojiano ya kina zaidi na Mkurugenzi huyu kama ifuatavyo:-

"Swali: Huu utaratibu ni wa Wizara ya Nishati na Madini peke yenu kwa sababu bahati nzuri tumeongea na Wizara nyingi na hawana utaratibu kama huo. Wewe unasema nini kuhusu hilo?

Jibu: Huu siyo utaratibu wa Wizara ya Nishati na Madini peke yake, upo kwenye Wizara nyingi na Katibu Mkuu anaangalia na kama nakumbuka hiyo *Circular* au Sheria nadhani inasema "na kama Fungu linaruhusu."

Swali: …Kwa hiyo Shs. 4,000,000.00 maana yake kila siku ni shilingi ngapi?

Jibu: Shilingi laki tano.

Swali: Shilingi laki tano kwa siku?

Jibu: *Entertainment per day.*

Swali: Hesabu hizo ni shilingi ngapi?

Jibu: Kwa siku nane Shs. 4,000,000.00 kila mtu.

Swali: …huoni kwamba huu ni ubadhirifu kwa kiasi fulani? Kwa sababu wenzako wa Wizara zingine ni Shs. 500,000.00 kwa muda wote na wengine hawana kabisa…?

Jibu: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria au Kanuni hiyo inayotumika inasema kama analo fungu…Katibu Mkuu anayo mamlaka ya kuweza kutoa viwango kulingana na Fungu alilonalo na ameangalia mazingira …"

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wizara ya Nishati na Madini pamoja na matumizi haya ya kuwalipa Mawaziri Posho ya Takrima *(Entertainment Allowance)* inayotofautiana na Wizara nyingine kwa kiwango kikubwa sana kwa kutumia *discretion* ya Katibu Mkuu, Kamati Teule pia imebaini kuwa ni Wizara hii pekee iliyoiarifu Kamati kwamba watendaji wake wakienda kwenye Vikao vya Bunge, Dodoma wanalipwa Posho ya Kikao *(Sitting Allowance)* pale wanapokaa kuchambua Hoja za Wabunge. Wakati wa Mkutano wa Nne wa Bunge kwa muda wa siku tano kuanzia tarehe 14 Julai hadi 18 Julai, 2011, Wizara ilitumia jumla ya Shs 127,820,000.00 kuwalipa *Sitting Allowance* Watendaji wa Wizara na Taasisi waliokuwa Bungeni, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule ilipitia pia Kanuni za Fedha za baadhi ya Taasisi na kubaini kuwa zipo ambazo zinatoa mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za umma. Kwa mfano, Kanuni za Fedha za *REA* na *EWURA* (Kanuni 16.4 na 16.4.1) zinaeleza kwamba hakuna shughuli au matumizi yatakayoruhusiwa nje ya Mpango

Kazi wa Mwaka na Bajeti isipokuwa tu kwa idhini ya Mtendaji Mkuu au Bodi. Kanuni hizi zinafanana neno kwa neno na zinasomeka kama ifuatavyo:-

> *"…No activity may be carried out or expenditure be incurred without its prior inclusion in the annual plan and budget except approval has been obtained from the DG or Board."*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipotaka kupatiwa ufafanuzi kuhusiana na kiasi cha fedha nje ya Bajeti ambacho Mtendaji Mkuu anaweza kuidhinisha kwa mujibu wa Kanuni iliyotajwa hapo juu, iliarifiwa kuwa hakuna ukomo, isipokuwa tu baada ya matumizi taarifa inabidi itolewe kwa Bodi.

Mheshimiwa Spika, hatari na athari za kutoa uhuru mkubwa kama huu ni kuwa, inapotokea Taasisi kuongozwa na Kiongozi mbinafsi upo uwezekano wa yeye kutumia fedha za umma kwa maslahi binafsi kwa kisingizio cha kuwepo kwa mahitaji muhimu ambayo yanajitokeza nje ya Mpango Kazi na Bajeti hivyo yeye kutumia mamlaka yake na kuyaidhinisha. Pamoja na matumizi ya fedha kama ilivyofafanuliwa hapo juu, Kamati Teule imebaini kuwa Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma wana uwezo hata wa kupindisha maamuzi ya Makatibu Wakuu kwa madai hayo hayo ya *"discretionary powers."* Mfano, wakati wa maandalizi ya kwenda Dodoma kwa ajili ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, Katibu Mkuu wa Wizara alitoa maelekezo kuhusiana na idadi ya watendaji wanaotakiwa kwenda Dodoma kwenye Mkutano wa Bunge la Bajeti. Katibu Mkuu alielekeza kwamba Maofisa 44 kutoka Wizarani na 17 kutoka kwenye Taasisi ndiyo wameidhinishwa kwenda Dodoma. Hata hivyo, idadi ya watendaji waliokwenda Dodoma waliongezeka kutoka jumla ya Watendaji 61 walioidhinishwa hadi kufikia 243.

Mheshimiwa Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Taarifa ya Ukaguzi Maalum anaeleza kwamba hapakuwa na idhini kwa Maofisa walioongezeka kwa kuwa kila Mkuu wa Taasisi alikuwa na uamuzi wa kuwaita Maofisa wa ziada kadri alivyoona inafaa. Aidha, watumishi wote waliokwenda Dodoma bila kujali idadi yao wala shughuli iliyowapeleka walilipwa posho za vikao.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mahojiano na Kamati Teule kuhusu *Discretionary Powers,* Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alieleza kutoridhishwa kwake na miongozo ambayo inatoa mamlaka makubwa kwa Watendaji Wakuu na kwamba miongozo hiyo ina mianya ambayo inaweza kusababisha ubadhirifu wa fedha za Umma. Akitoa maelezo yake mbele ya Kamati Teule, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alisema:-

> "…katika kaguzi zangu hata huko nyuma nimeshauri kwamba, kuna haja kusema kweli Utumishi kuwa *more explicit* katika kutoa Miongozo yao kwa sababu kuna Miongozo ambayo inaachia too much power kwa *Accounting Officer. Issue* ya *honorarium, issue* ya *entertainment allowance, issue* ya ni kikao kipi, ukisoma ule Mwongozo wa Utumishi uko *loose and therefore* ni Mwongozo ambao unaweza ukawa *misused…"*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo juu, Kamati Teule inaona umuhimu kwa Watendaji Wakuu kupewa uhuru na mamlaka ya kuamua mambo kwa kiwango fulani kwa kutumia busara zao. Hata hivyo, Kamati Teule inapendekeza kuwa Serikali ihakikishe kwamba *discretionary powers* zinawekewa utaratibu na mipaka maalum ili zisiwe chanzo cha matumizi mabaya ya madaraka na fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa muda iliyopewa na kwa kukidhi mahitaji ya Hadidu za Rejea ilizopewa, Kamati Teule imepitia Taasisi chache tu za mfano lakini Serikali ikifanya utafiti zaidi kuhusiana na Kanuni za Fedha na utendaji wa Taasisi za Umma, inaweza ikagundua mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Kamati Teule imekamilisha uchunguzi kuhusu utaratibu uliobainika wa kukusanya fedha kwa ajili ya maandalizi na uwasilishwaji wa Hotuba za Bajeti za Wizara Bungeni. Kamati Teule imekamilisha jukumu hilo kwa kufanya mahojiano na watu 146, kupitia Katiba, Sheria, Kanuni na nyaraka mbalimbali, kupitia na kuchambua Taarifa ya Ukaguzi Maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kukusanya taarifa mbalimbali kwa njia ya Dodoso kama ilivyoonyeshwa katika utangulizi wa Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya uchunguzi huu yamebainisha kwamba utaratibu wa Wizara kuchangisha fedha kwa ajili ya kuwasilisha Hotuba ya Bajeti yake Bungeni haukuwa wa kawaida na haukujengwa katika misingi yoyote ile kisheria. Halikadhalika, fedha zilizokusanywa zilitumika kwa ajili ya matumizi ambayo yasingehitaji uchangishaji kwa sababu yangeweza kugharimiwa na kasma zilizopo za Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kamati Teule imebaini kuwa licha ya kuonesha upungufu wa aina mbalimbali katika kuendesha zoezi la uchangishaji na matumizi ya fedha hizo, Taarifa hiyo haikuweza kuweka bayana kama uchangishaji huo ulikuwa halali au vinginevyo katika kutoa ushauri na hitimisho. Aidha, pamoja na upungufu wa Taarifa hiyo Katibu Mkuu Kiongozi hakuitumia ipasavyo na kusababisha kumsafisha Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine Kamati Teule ilibaini kuwa kitendo cha Katibu Mkuu Kiongozi kufanya Uchunguzi wa Awali kuhusu suala la Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini Ndugu David Kitundu Jairo kilikuwa sahihi kwa kuwa yeye ndiye Mamlaka yake ya Nidhamu. Kuhusu suala la kutoa taarifa kwa Vyombo vya Habari, Kamati Teule haikuweza kuthibitisha kuwa, kitendo cha taarifa kutolewa kwa Vyombo vya Habari wakati bado Bunge halijapewa taarifa kimeathiri dhana ya haki na madaraka ya Bunge kisheria.

Hata hivyo, kwa kuwa suala hili lilianzia Bungeni, na kwa kuwa kulikuwa na mawasiliano kati ya Waziri Mkuu na Katibu Mkuu Kiongozi kabla ya kuanza kwa mchakato wa Uchunguzi wa Awali, hivyo basi, Katibu Mkuu Kiongozi alikuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba Bunge kupitia kwa Waziri Mkuu linapata Taarifa ya matokeo ya Uchunguzi wa Awali kabla hajaitoa kwa Vyombo vya Habari.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nafasi ya Mamlaka ya Uteuzi kwa ngazi ya Makatibu Wakuu katika kushughulikia masuala ya nidhamu ya anaowateua, Kamati Teule imegundua upungufu katika Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake. Upungufu huo unahusu madaraka makubwa ya Katibu Mkuu Kiongozi katika mchakato mzima wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa Makatibu Wakuu bila kuishirikisha Mamlaka ya Uteuzi ambaye ni Rais, na Waziri Mkuu ambaye ni Msimamizi wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule pia imepitia masuala mengine mbalimbali yanayohusiana na Hadidu za Rejea kama ilivyoainishwa katika Sehemu ya 7.0 ya Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati Teule; Utaratibu wa uchangishaji wa fedha uliofanyika katika Wizara ya Nishati na Madini haukuwa na uhalali wowote kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Fedha za Umma. Vilevile, uchangishaji huo ulisababisha Taasisi kubebeshwa mzigo kwa kuwa hazina kasma mahususi kwa ajili ya kuichangia Wizara kwa ajili ya maandalizi na uwasilishaji wa Bajeti Bungeni. Kamati Teule imeridhika pia kwamba huo siyo utaratibu wa kawaida kama ilivyoelezwa na Katibu Mkuu Kiongozi katika Taarifa yake kwa Umma kupitia Vyombo vya Habari kuhusu Uchunguzi wa Awali.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imeridhika kwamba Taasisi zilizochanga hazikuwa na kasma mahususi, badala yake zimetoa fedha kwenye kasma zisizohusika kwa matumizi hayo. Kwa mfano, *TANESCO* ilitoa fedha kutoka katika kasma ya *Donations and Subscriptions, TPDC* ilitoa kwenye kasma ya *Gas Revenue, REA* ilitoa kwenye *Preparation of REA Business Plan and Budget* na *EWURA* ilitoa kwenye kasma ya Elimu kwa Umma. Ni dhahiri kwamba, kasma zilizotoa fedha hizo hazikuweza kukamilisha majukumu yaliyokusudiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Nyaraka za matumizi halisi zinaonesha kuwa fedha zilizokusanywa zimetumika kwa ajili ya malipo ya posho ya kujikimu kwa watumishi 69 wa Wizara, posho ya vikao kwa watumishi 243 waliokuwa Dodoma, manunuzi ya chakula, manunuzi ya vifaa vya kuandikia, malipo ya Takrima kwa Waziri na Naibu Waziri na manunuzi ya mafuta kwa ajili ya magari, matumizi ambayo yangeweza kugharimiwa na kasma husika za Wizara bila kuhitaji kuchangisha. Aidha, Nyaraka zilizowasilishwa hazikuonesha kuwepo kwa malipo kwa Waheshimiwa Wabunge ambayo yangeashiria rushwa.

Vilevile imethibitika kuwa, licha ya fedha hizo kukusanywa kinyume cha taratibu, fedha zilizochangwa zimetumika kwa matumizi yasiyo ya lazima na kwa ubadhirifu.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa ushauri na hitimisho la Taarifa yake, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hakujibu Hadidu ya Rejea kuhusu uhalali wa michango hiyo na matumizi ya fedha zilizokusanywa kama alivyopewa na Katibu Mkuu Kiongozi. Badala yake alihitimisha na kutoa ushauri wa Taarifa yake kwa kujikita

kwenye idadi ya Taasisi kuwa siyo 20 na kiasi cha fedha kilichochangwa kuwa siyo Shs 1,000,000,000.00. Hatua hii ilikuwa ni ya upotoshaji mkubwa wakati Taarifa ilikuwa na maudhui ambayo yangeweza kuonesha makosa ya kinidhamu kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini. Aidha, Taarifa hiyo haikuweza kubainisha matumizi ya jumla ya Shs 190,823,120.00 ambazo zimebainishwa na Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wake Katibu Mkuu Kiongozi alitumia hitimisho hilo lililotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuacha sehemu kubwa ya maudhui yaliyomo kwenye Taarifa ya Ukaguzi Maalum ambayo kama yangetumika vizuri yangebainisha makosa ya kinidhamu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Kamati Teule imeridhika kwamba Katibu Mkuu Kiongozi alitumia hitimisho hilo lisilokidhi haja kwa makusudi ya kumsafisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na kuupotosha umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imeridhika kwamba hatua ya kufanya Uchunguzi wa Awali iliyochukuliwa na Katibu Mkuu Kiongozi dhidi ya Ndugu David Kitundu Jairo ni sahihi kwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi ndiye Mamlaka ya Nidhamu kwa Makatibu Wakuu wote kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, 2002 na Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni alichukua hatua ya kuhamisha suala la Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini Ndugu David Kitundu Jairo kutoka Bungeni ili likafanyiwe kazi na mamlaka husika na Wabunge kuridhia hatua hiyo. Ni maoni ya Kamati Teule kwamba Katibu Mkuu Kiongozi angetumia busara ya kawaida kuona umuhimu wa kuliarifu Bunge matokeo ya Uchunguzi wa Awali kupitia Waziri Mkuu kabla ya kutoa matokeo hayo kwa Vyombo vya Habari kwa kuzingatia kuwa suala hili liliibuliwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, Katibu Mkuu Kiongozi angeendeleza dhana ya kuimarisha mahusiano mazuri, kuheshimiana, kuelewana na kuaminiana baina ya Mihimili hii miwili ya Dola. Kitendo cha kutoliarifu Bunge kimesababisha Waziri Mkuu abakie na deni la kuliarifu Bunge matokeo ya hatua zilizochukuliwa na Mamlaka ya Uteuzi.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati Teule kuwa kitendo cha Taarifa kutolewa kwa kutumia Vyombo Vya Habari wakati Bunge halijapewa taarifa kimeathiri dhana ya haki za Bunge kwa kuwa Bunge limepokonywa haki ya kupata taarifa na kukamilisha suala lililolianzisha na ambalo kwa kiasi kikubwa limehusu matumizi ya fedha za umma ambayo usimamizi wake kwa mujibu wa Katiba ni jukumu la Bunge. Aidha, kitendo hicho hakikumtendea haki Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni kwa kuwa alikuwa ametoa kauli Bungeni kuwa atalifikisha suala hilo kwa mamlaka za juu na Bunge lilikuwa bado linasubiri majibu yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa vile Katibu Mkuu Kiongozi alitumia maneno “vyombo vipo” wakati alipokuwa anajaribu kufafanua juu ya uwezekano wa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini kuchukua hatua dhidi ya Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mbunge, kwa *defamation,* Kamati Teule imeridhika kwamba, maneno hayo yalimaanisha chombo zaidi ya kimoja, kwamba Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini angeweza kwenda mahakamani au kwenye chombo kingine chochote nje ya Bunge. Pamoja na kwamba ni haki kwa kila raia kwenda mahakamani maneno haya ambayo yalionekana kuwa ni ushauri kwa Katibu Mkuu wa Nishati na Madini yalikuwa yanachochea ukiukwaji wa Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu cha 3 cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura ya 296.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati Teule kwamba, kwa kuwa suala la nidhamu ya wateule wa Rais ni nyeti na pana, si vyema suala hilo kuwa mikononi mwa mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inaona kuwa kuna wigo mpana sana wa Nyaraka za Serikali zinazoitwa za siri jambo ambalo limetoa nafasi kwa baadhi ya watendaji wasio waaminifu kufanya maovu kwa kujificha katika mwamvuli huo wa usiri. Aidha, Kamati imeona kuwa kukosekana kwa Sheria ya kuwalinda watoa taarifa *(Whistleblowers)* kunalinyima Taifa fursa ya kubaini na kuyashughulikia maovu hayo kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inaona kwamba kuna haja ya kuzingatia zaidi upeo, sifa, uzoefu, taaluma, maadili na uzalendo katika nafasi za uteuzi. Vile vile vijana wenye sifa wapewe nafasi katika ajira mpya na wastaafu kwa upande wao waandaliwe na kuhamasishwa kuanzisha shughuli katika Sekta binafsi zitakazozalisha ajira.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa sasa wa kila Wizara au Taasisi kugharamia na kuendesha Semina kwa Wabunge unatoa mwanya kwa wanaoratibu semina hizo wasio waaminifu kutumia fursa hiyo kama njia ya kujipatia na kutumia fedha hizo kwa manufaa binafsi.

Mheshimiwa Spika, inapotokea Mihimili kuvutana kunakuwa na athari katika misingi ya utawala bora, hali ambayo inaweza kukwamisha maendeleo hasa ikizingatiwa kwamba dhana ya mgawanyo wa madaraka haimaanishi Mhimili mmoja kuhodhi madaraka hayo na kuweka kuta kati yake na Mihimili mingine badala yake ni dhana ya Mihimili kushirikiana, kuheshimiana na kukosoana *(Checks and Balances).*

Mheshimiwa Spika, Sheria, Kanuni na Taratibu zinazotoa mamlaka ya hiari *(Discretionary Powers)* zinawaachia Maofisa Masuuli mwanya, ambao unaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha za umma na kuisababishia Serikali hasara.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule imeona kwamba ni muhimu mahusiano ya kikazi baina ya Waziri ambaye ni Msimamizi Mkuu wa Wizara na Katibu Mkuu ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Wizara yawe mazuri ili kuleta ufanisi ndani ya Wizara na Serikali kwa ujumla. Hii itawezekana tu kama viongozi hawa watafanya kazi kwa kuwasiliana, kushauriana na kushirikiana kama Mwongozo wa Baraza la Mawaziri unavyoelekeza, tofauti na ilivyofanyika katika suala la kuchangisha fedha katika Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, katika suala la uchangishaji wa fedha uliofanywa na Wizara ya Nishati na Madini, Kamati Teule baada ya kukamilisha uchunguzi kwa kupitia nyaraka mbalimbali na kufanya mahojiano na watu mbalimbali, haikuweza kuthibitisha moja kwa moja ushiriki wa Waziri au Naibu Waziri katika kubariki au kuidhinisha uchangishaji huo. Hata hivyo, kutokana na kazi za Waziri kama zilivyoainishwa katika Mwongozo wa Baraza la Mawaziri, Waziri alipaswa kufahamu kilichoendelea Wizarani kwake kwa sababu yeye ndiye Msimamizi Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Kamati Teule:-

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inapendekeza Bunge likemee kwa nguvu zote utaratibu wa uchangishaji huu uliofanywa na Wizara ya Nishati na Madini na kwamba uchangishaji wa fedha wa aina yoyote lazima uzingatie Sheria, Kanuni na Taratibu za fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inapendekeza kwamba Serikali ichukue hatua za kinidhamu kwa Ndugu David Kitundu Jairo kwa matumizi mabaya ya madaraka, kukusanya na kutumia fedha za Serikali kinyume cha Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha za Umma na kuruhusu matumizi mabaya ya fedha za Umma. Vilevile Serikali iwachukulie hatua za kinidhamu, kwa mujibu wa Sheria, watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini waliotajwa kwenye Taarifa hii kushiriki kwa namna mbalimbali katika mchakato wa uchangishaji na matumizi ya fedha hizi za umma. Aidha, kwa kuwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Baraza la Mawaziri Waziri ndiye Msimamizi Mkuu wa Wizara, hivyo suala la uchangishaji halikupaswa kufanyika bila yeye kufahamu, Kamati Teule inapendekeza Serikali ichukue hatua zinazofaa kwa Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa William Ngeleja, Mbunge.

Mheshimiwa Spika, katika suala la Ndugu David Kitundu Jairo, Kamati Teule imesikitishwa sana na jinsi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alivyoshindwa kutekeleza wajibu wake kikamilifu, hususan katika kutoa ushauri na hitimisho katika ripoti yake na jinsi alivyotoa taarifa kwenye Vyombo vya Habari. Kwa kufanya hivyo, ameshindwa kulisaidia Bunge na Umma kwa ujumla, badala yake amekuwa ni sehemu ya kuficha maovu. Hivyo, Kamati Teule inapendekeza Serikali ichukue hatua zinazofaa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upotoshaji huo.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu Kiongozi kwa makusudi aliamua kumsafisha Ndugu David Kitundu Jairo kwa kuficha ukweli wa Taarifa ya Ukaguzi Maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuamua kwamba Ndugu David Kitundu Jairo hakuwa na kosa la kinidhamu, kitendo ambacho kimeupotosha Umma wa Watanzania. Kamati Teule inapendekeza Serikali ichukue hatua zinazofaa kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inapendekeza kwamba, kwa kuwa tunakaribia kuingia katika Mchakato wa mapitio ya Katiba, Wananchi wajadili kwa kina na kuainisha taratibu zinazotakiwa kuzingatiwa na Mihimili mitatu ya Dola nchini katika kutekeleza majukumu yao, hususan:-

(a) Muundo wa Bunge kuhusu utaratibu wa sasa wa Serikali kuwa ndani ya Bunge (Mawaziri kuwa Wabunge) au vinginevyo.

(b) Mawanda *(Scope)* ya Mamlaka ya Bunge kuisimamia na kuishauri Serikali.

(c) Mawasiliano baina ya Mhimili mmoja na mwingine hasa katika mambo yanayogusa haki na madaraka ya Mhimili zaidi ya mmoja.

(d) Mipaka na ushirikishwaji wa mamlaka mbalimbali ndani ya Mhimili mmoja wa Dola katika utekelezaji wa majukumu.

(e) Taratibu za Mihimili ya Dola kusimamiana, kurekebishana na kukosoana bila ya kuathiri masharti ya Sheria na Katiba *(Checks and Balances).*

Mheshimiwa Spika, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo zifanyiwe marekebisho ili kutoa nafasi kwa Makatibu Wakuu kuwashirikisha Mawaziri *(consultation)* katika maamuzi ya kiutendaji hasa katika matumizi ya fedha. Hatua hii itawapa fursa Mawaziri kuweza kutekeleza vizuri zaidi majukumu yao wakiwa kama wasimamizi wakuu wa maamuzi na shughuli za Serikali Wizarani.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifanye mapitio ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake ili kurekebisha maeneo yote ambayo yameonekana yana upungufu. Kwa mfano, Kanuni ya 36 ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2003 ifanyiwe marekebisho ili:-

- Kuweka wazi utaratibu wa Mamlaka ya Nidhamu *(Disciplinary Authority)* kufanya Uchunguzi wa Awali *(Preliminary Investigation).*

- Kuonesha wazi muundo na idadi ya wajumbe wa chombo kinachopaswa kufanya Uchunguzi wa Awali kama ilivyo kwa Kanuni ya 46 inayohusu Kamati ya Uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kanuni ya 46 Kifungu kidogo cha (3) hakipo, badala yake kuna 46(1), (2), (4) na (5) hivyo Kanuni hii iangaliwe na kurekebishwa kama inavyofaa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la nidhamu kwa Wateule wa Rais ni nyeti na pana Kamati Teule imeona kuwa si vyema suala hilo kuachwa mikononi mwa mtu mmoja kama ilivyo sasa katika Sheria ya Utumishi wa Umma. Kamati Teule inapendekeza:-

(a) Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wa umma wanaoteuliwa na Rais inaposhughulikia masuala ya nidhamu ifanye hivyo kwa kumuarifu Rais ambaye ni Mamlaka ya Uteuzi na Waziri Mkuu ambaye ni Msimamizi wa siku hata siku wa kazi na shughuli za Serikali; au

(b) Serikali iunde Chombo maalum cha kushughulikia masuala ya nidhamu kwa watumishi wa umma wanaoteuliwa na Rais.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inapendekeza Bunge lijadiliane na Serikali kuhusu namna bora ya kuendesha semina kwa Wabunge ikiwemo kutenga kasma mahususi ndani ya Mfuko wa Bunge na kusisitiza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu waraka namba tatu wa mwaka 2011 wa Katibu Mkuu wa Hazina na mlipaji Mkuu wa Serikali, Kamati Teule inapendekeza kuwa Serikali isisitize Maofisa Masuuli wote wazingatie wazingatie maudhui ya waraka huo ikiwa ni pamoja na kutoendesha uchangishaji wa fedha bila kibali cha Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule inapendekeza kuwa Serikali itoe mwongozo kuhusu malipo posho ya takrima, yaani *entertainment allowance* na *honorarium* ili kuainisha viwango vya posho hizo. Mwongozo huo utolewe mara kwa mara kulingana na hali halisi. Kwa upande wa Taasisi za Wizara, Serikali ifanye uchambuzi wa kanuni zao za fedha kubaini upungufu unaotokana na matumizi ya kanuni hizo kuweka utaratibu wa kuziba mianya ya matumizi yasiyofaa. Aidha, Kamati Teule inapendekeza kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria

ndogo, iongezewe uwezo na muda kupitia kanuni hizo ili kubaini upungufu kwa wakati na kupendekeza marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe mwongozo kuhusu idadi ya maofisa wanaopaswa kwenda Dodoma kwa ajili ya mikutano ya Bunge na katika mwongozo huo Serikali isisitize matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano na TEHAMA, yakiwemo matumizi ya simu na barua pepe ili kupunguza idadi ya watumishi na kubana matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani kwa Bunge letu Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu na kupitisha Azimio la kuundwa kwa Kamati hii Teule. Vilevile kwa moyo wa dhati kabisa nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kutuamini na kutupatia heshima kubwa kwa kututeua kuwa wajumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuchukua fursa hii kumshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Kayanza Peter Pinda Mbunge, ambaye pamoja na shughuli nyingi na ratiba ngumu alikubali kutenga muda wake na kuitikia wito wa kuja mbele ya Kamati Teule. *(Makofi)*

Napenda pia kuwashukuru sana watendaji wakuu na watumishi wote wa Wizara ya Madini na taasisi zake kwa kutupa ushirikiano wa dhati uliotuwezesha kufanikisha uchunguzi wa suala hili. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa watumishi wote wa umma katika ngazi mbalimbali waliokuja mbele ya Kamati ya Teule, wanazuoni waliobebea katika masuala mbalimbali yanayohusiana na mada ya uchunguzi huu.

Spika wa Bunge Mstaafu, Mawaziri Wakuu Wastaafu, Mawaziri, Wabunge, Makatibu wa Bunge Wastaafu, Makatibu Wakuu, Asasi za Kiraia na wengineo kwa kutupatia ushirikiano katika mahojiano na mashauriano wakati wa kipindi chote cha uchunguzi uliofanywa na kamati hii. Shukrani zangu ziende pia kwa Makatibu wa Bunge la Uingereza *(House of Commons),* na Bunge la Australia House of Representatives kwa mchango wao ambao umekuwa wa manufaa katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu napenda kutoa shukrani za dhati kwa Katibu wa Bunge Dkt. Thomas D. Kashililah, kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi yake vizuri na kuikamilisha kwa wakati. Aidha, kwa namna ya pekee kwa niaba ya Kamati Teule napenda kumshukuru Katibu wa Kamati Ndugu Nenelwa Mwihambi Wankanga, pamoja na wasaidizi wake, Ndugu Lukago Alphonce Madulu, Ndugu Asia Paul Minja na Ndugu Msigwe Dickson Bisile. *(Makofi)*

Napenda pia kuwashukuru wafuatao; Ndugu Ashura Kalikwendwa Waijaa, Ndugu Feliciana Lawrent Mabada, Ndugu Jemina Mpozi Magohe, Ndugu Amon Kasyanju, Ndugu Abdullah Seleman Mwinyipembe na Ndugu Shaban Mussa, pamoja na Wajumbe wote wa sekretarieti kwa ujumla, kwa kushirikiana na Kamati hii katika shughuli za siku hata siku na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu liyapokee, liyaridhie na kuyaazimia mapendekezo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, walioomba kuchangia mpaka sasa ni 26 na taarifa hii ni ya Kamati Teule. Kuna hatari ya watu kujirudia rudia, Kanuni zinakataa kujirudia rudia. Kwa hiyo, nitaanza kuwaiteni mhakikishe hamrudii rudii, jielekezeni kwenye mapendekezo

Tunaanza, sasa ninamwita Mheshimiwa Martha Umbulla, atafuatiwa na Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Felix Mkosalimali, atafuatiwa na Mheshimiwa Ezekia Wenje na Mheshimiwa Agripina Buyogera na Mheshimiwa James Lembeli ataendelea. Tutaendelea kutaja majina kadiri tunavyoendelea.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nami ninatanguliza kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuwa na uzima na afya njema, kwa kipindi chote hicho cha kazi yetu hii muhimu na nyeti kwa mustakabali wa Taifa letu. Aidha, ninakushukuru wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika, kwa kuniteua kuwa Mjumbe wa Kamati yako Teule ya Bunge; na ninapenda kukuhakikishia kwamba, nimefanya kazi hii kwa uaminifu na uadilifu, kama ambavyo taarifa yetu imeonesha na mimi mwenyewe nimepata fursa ya kujifunza mambo mengi, lakini vilevile kufanya uchunguzi. Ninaweza kusema kwamba, sikuwa najua hii kazi kwa jinsi ambavyo imekuwa lakini nimepata uzoefu na kuweza kuchambua, lakini pia kufanya maamuzi kulingana na Sheria, Kanuni na Taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama si kwa kurudia lakini kwa kusisitiza tu katika maeneo fulani fulani na pengine kufanya ufafanuzi. Nikianza na hadidu ya rejea ya kwanza, suala la uhalali wa kukusanya fedha hizi zilizokusanywa kutoka kwenye Taasisi za Wizara ya Nishati na Madini na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, chimbuko lake ni barua ambayo imeangukia mikononi mwa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, ambaye kwa nafasi hii pia ninaomba nimshukuru na kumpongeza sana kwa ujasiri wake. *(Makofi)*

Kwa jinsi ambavyo ameibua hoja ambayo imepelekea sasa pengine kuziba mianya na ubadhirifu mkubwa uliokuwa unafanyika katika Wizara na hatimaye pia kurekebisha miongozo na taratibu mbalimbali kwa nia ya kudumisha Utawala Bora katika nchi yetu. Kwa hiyo, ninampongeza kwa moyo wa dhati.

Katika suala la uhalali, sipendi kurudia lakini suala hili limeleta bonde kubwa, tukilitazama katika Taasisi zile zilizochangishwa imeonekana wazi kwamba, hakukuwa na kasma ambazo zilikuwa zinalenga uwasilishwaji na ukamilishaji wa bajeti Bungeni na kwa hiyo pia haikuwa na ridhaa ya Taasisi ambazo zimechangishwa, kwa sababu haikuridhiwa na Viongozi wa Taasisi zenyewe na wala hazikuridhiwa na Bodi zenyewe za Taasisi. Kwa hiyo ni wazi kabisa kwamba, Taasisi zile zinapata uzito na mzigo mkubwa wa kutekeleza shughuli zao kwa kuwa kasma zile ambazo zimechangishwa zimetoka kwenye maeneo ambayo zilikuwa na shughuli tofauti na kwa hiyo ninadhani hili suala siyo la Wizara ya Nishati peke yake.

Ukaguzi na uchambuzi wetu haukuweza kubaini Wizara nyingine yoyote, lakini pengine Wizara nyingi zina Taasisi zilizopo chini yao, pengine suala hili linafanyika hatuwezi kusema haiwezekani. Kwa nafasi hii ni fundisho kwa Wizara kuweza kuangalia kwamba ni utaratibu ambao unakiuka kabisa taratibu za fedha za Serikali za Umma. Kwa hiyo ni suala ambalo limeweza kurekebisha mifumo mbalimbali ili Wizara zetu ziweze kutenda kazi kwa ufanisi kadiri Bunge linavyoidhinisha bajeti hapa Bungeni.

Kwa nini ile barua ya Mheshimiwa Beatrice ilileta mtafaruku ama kwa jinsi ambavyo imeibua hisia ya Wabunge kwamba huenda kuna rushwa, lakini ni wazi kwamba wakati ule Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ilikuwa na matatizo ya kwamba nchi ipo kwenye giza na kwa hiyo lolote ambalo lingeweza kutokea wakati ule, watu wangehisi kwamba Wizara inajaribu kuwahonga Wabunge ili bajeti hiyo iweze kupitishwa. Tumekuja kutafakari hilo halikuweza kubainika kusema kweli, lakini ni wazi kwamba Waswahili wanasema siku za mwisho ni arobaini. *(Makofi)*

Kwa nini barua ile imetoka kwenye Wizara ya Nishati na Madini ikaletwa hapa Bungeni; mtu unaweza ukajiuliza kwamba pengine watu wamechoshwa na tabia iliyokuwa inaendelea katika Wizara na kwa hivyo wakaona hakuna njia nyingine ni kuweza kupenyeza hii ili Umma wa Watanzania likiwemo na Bunge letu Tukufu, liweze kuliona hili na kuipiga marufuku na kwa hiyo nadhani ndiyo ilikuwa sababu hiyo kwamba watu wamechoshwa. *(Makofi)*

Cha kushangaza, Viongozi wetu ambao walichukua jukumu la kushughulikia suala hili, Katibu Mkuu Kiongozi akasema hakuona suala la kumwajibisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa sababu aliona ni suala la kawaida. Alisema ni utaratibu wa kawaida na ni kweli Mheshimiwa Spika ilikuwa inafanyika miaka ya nyuma na hata mwaka huu; kwa hiyo, ni utaratibu wa kawaida.

Suala zima hata ule utaratibu wa kawaida; je, ni halali kuchangisha na matumizi ya hizo fedha ni halali kutumika ilivyotumika kama ambavyo tuliona kwamba ni kuupotosha umma na kusema kwamba ni utaratibu wa kawaida na ikatosha kumsafisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini? Kwa hiyo, ninadhani kwa nafasi hii pia, kama Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini aliukuta utaratibu huu na yeye akauendeleza; ni wazi kwamba hakuwa mwadilifu, alipaswa kuliona hilo kwamba, hakupaswa kuendeleza utaratibu ambao ameukuta

na hauendani na taratibu za fedha, yeye badala ya kuendeleza angeweza kuukatisha na kuupiga marufuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuliona kwamba suala hili lilitosha kumwajibisha na jinsi ambavyo tumetoa maoni yetu na mapendekezo ninadhani Bunge lako Tukufu litaamini kwamba, tulifanya kazi hiyo kwa uaminifu na ndivyo tulivyoona kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye hadidu ya rejea ya pili, kuhusu Taarifa ya Ukaguzi, tuliona kwamba, ni mlolongo ule ule wa uovu kwa sababu Katibu Mkuu Kiongozi alipomtumia *CAG* kufanya uchunguzi, alikuwa na nia njema ya kubaini tatizo liko wapi na kuhakikisha kwamba analirekebisha. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ililenga maeneo mawili ya kusema kwamba, hakukuwepo na Taasisi 20 na wala hizi fedha hazikuwa bilioni moja. Sasa suala hilo alilofanya ni sahihi, lakini tatizo linakuja kwamba ni kweli kwamba suala la kutokuwa na Taasisi 20 na kutokuwa na shilingi bilioni moja linatosha kumsafisha Katibu Mkuu kwamba hakuwa na kosa la kinidhamu; ni wazi kwamba, kuna mwenzetu mmoja tulipomhoji alisema ukiwa na ng'ombe 100 ukaibiwa ng'ombe wako wote lakini ukatembea ukakuta ng'ombe watatu miongoni mwa walioibiwa wapo kwa mtu fulani; unaweza ukasema yule siyo mwizi? *(Makofi)*

Kwa vyovyote vile suala hazikuwa Taasisi 20 wala shilingi bilioni moja, suala ni kwamba kulikuwa na uhalali wa kuchangisha na zile fedha na zilitumikaje. Kwa hiyo, ninadhani suala hili lilitosha kumwajibisha na kumwona *CAG* kwamba katika kutoa uamuzi huu katika uchunguzi wa awali, hakutenda kikamilifu wajibu wake wa kuutaarifu umma kwamba lile lilikuwa kosa la kinidhamu na kwa hiyo hilo anaweza akaliona kwamba ni upotoshaji wa umma na hasa ilipotoka kwenye vyombo vya habari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulichunguza sana katika matumizi ya hizi fedha zilizotumika, tuliona kwamba fedha hizo zilitumika kiubadhirifu mkubwa sana; kwa mfano, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, aliidhinisha watu 61 tu kuja kwenye uwasilishaji wa Bajeti Bungeni. Katika matumizi ya zile fedha, idadi ikaongezeka mpaka kufikia watu 243; ongezeko la watu 180 na kitu, sasa tukaona kwamba haieleweki kabisa. Kwa nini idadi kubwa ya watu ije Bungeni katika uwasilishaji wa Bajeti?

Vilevile tumetoa mapendekezo kwamba ni wakati mwafaka kuona sasa hivi tuna teknolojia, kama kuna suala ambalo linatakiwa litolewe ufafanuzi kutoka katika Wizara, mtu anaweza akatuma *email,* akapiga simu au akapata maelezo akiwa kule kule Wizarani, badala ya kuleta rundo la watu kubwa namna hiyo kuja Bungeni kutumia zile fedha kiubadhirifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona kwamba ni wazi pia hiki kitendo kilikuwa cha ufujaji wa fedha za Serikali; ukiangalia magari 15 yalikuja hapa Bungeni kutoka Wizara moja na zaidi sana katika kuchunguza utakuta gari moja limewekewa mafuta lita 230 kwa siku moja na tulipoitisha *log book* tuliona kwamba gari hilo hilo halikutoka hapa Dodoma kwa siku hizo. Sasa hizo lita 230 zilizotumika na gari moja yapo magari 15 kwa muda ule kusema kweli inatosha kuonesha kwamba Wizara hiyo ilikuwa na ubadhirifu wa kutumia hizo fedha. *(Makofi)*

Taasisi nyingi zilikwishaona na ndiyo maana hata nyaraka hizo za siri zikaanza kuvuja; kwa mfano, Taasisi ya *EWURA,* walipoambiwa wachange shilingi milioni 50 wakajua kwamba hawawezi kufuatilia hizi fedha na kwa hiyo wakakataa kuchanga wakasema sisi tutachangia chakula, vinywaji na tafrija. Matokeo yake wakachanga wakalipia hiyo tafrija kwa jumla ya shilingi milioni tisa tu na kwa hiyo wakaona kwamba wangetoa milioni 40 na imetumika milioni tisa wame-*save* fedha hizo ambazo wasingeweza kuzifuatilia. *(Makofi)*

Kwa hiyo; ni wazi kwamba, Taasisi zenyewe zilikwishaona kwamba huu si utaratibu mzuri lakini kwa sababu mkubwa akishasema hakuna namna ya kukataa, inaonekana kwamba ni kutowajibika. Kwa kweli kama tulivyoainisha kwenye Ripoti yetu, katika masuala yote ambayo tumetolea ufafanuzi, tumezingatia Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 iliyorekebishwa mwaka 2004 na Kanuni zake. Vilevile tumetumia Katiba, Ibara ya 136, kwa kuwa fedha zote zinazotolewa ni lazima ziidhinishwe na Bunge, Kanuni ya 53 inaonesha kwamba, fedha hizi za Umma ni lazima zikaguliwe. Kutoa fedha katika Taasisi na kupeleka moja kwa moja kwenye Akaunti ya *GST* ni wazi kwamba hapa katikati ime-*lose track* kwamba, asingeweza kukaguliwa ama kufanyiwa *audit*. Ndiyo maana tuliona kwamba hizi fedha mtu yeyote asingeweza kuzifuatilia, hazikupita kwenye Mfuko wa Hazina, hazikupita kwenye Vitabu vya Serikali na kwa hiyo hakukuwa na namna yoyote ya kuzi-*audit.*

Vilevile kama ilivyoainishwa kwenye Ripoti, tulijiuliza hivi huu uwasilishaji wa bajeti ulihitaji shilingi ngapi? Tulibaini kwamba, ulihitaji shilingi milioni 207, lakini kasma iliyopaswa kuhusika ilikuwa na shilingi milioni 35, lakini siku chache baada ya barua ile iliyoangukia mikononi mwa Mheshimiwa Beatrice kutolewa ya kuomba michango, Wizara ikatoa shilingi 171 milioni, kwa hiyo, ukijumlisha 35 na 171 ilikuwa 207; kwa hiyo, ilitosha kabisa kukamilisha bajeti. Tuliona kwamba, Katibu Mkuu hakuwa na sababu ya kuendelea kuchangisha lakini aliendelea kuchangisha na aliendelea kutumia hizo fedha, tuliona huo ni ukiukwaji wa utaratibu na suala ambalo linapaswa kukemewa kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, katika hadidu ya rejea ya tatu, tulichambua mifano mbalimbali ya hoja zinazoibuliwa Bungeni na kadiri Mwenyekiti alivyowasilisha au taarifa inavyoelekeza, tuliona kwamba Waziri Mkuu aliliondoa hili suala Bungeni na akalipeleka juu; na tuliona kwamba ni dhahiri kadiri ilivyoelezwa kwamba ingepaswa kurudi katika utaratibu ule ule ili Bunge liweze kuarifiwa na kwa hiyo Bunge kutendewa haki katika suala zima la mfumo wa utoaji taarifa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja na ninakushukuru sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, mbele ya *Speaker's Gallery* tunao wageni wafuatao; tumepata heshima ya kufikiwa na Mheshimiwa Mke wa Makamu wa Rais, Dkt. Bilali, Mama Bilali; ninaomba asimame, karibu. *(Makofi)*

Vilevile wamefuatana na Mke wa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi, Balozi Seif Iddi. Tumefurahi kwa kuja na ninadhani mtashirikiana na sisi hapa.

Waheshimiwa Wabunge, lakini la pili napenda niwatambue wafuatao, kuna wageni wetu wa jana wa *TAPAC* wameondoka, lakini pia tuna wanafunzi wa *CBE* wengine walikuwepo jana na leo kuna wengine, tafadhali wasimame. *(Makofi)*

Lakini pia tuna wageni wa Mheshimwa Zabein M. Muhita na Mheshimiwa Juma Nkamia, ambao ni Maafisa Watendaji na ni Wanafunzi wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Halafu kuna wageni wa Mheshimiwa Lediana M. Mng'ong'o ambao ni Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, wakiongozwa na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri. Pia yupo Kaimu Mkurugenzi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kesho saa 3.00 asubuhi kutakuwa na semina ya *TAPAC* kwa hiyo, Wabunge wote wanakaribishwa na anasema, anaomba niwatangazie wanachama wa Umoja wa Wabunge wa Kupambana na UKIMWI kwamba watakuwa na semina kesho, saa tatu asubuhi, katika Ukumbi wa Msekwa.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii Mheshimiwa Jenista J. Mhagama, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 5.00 watakuwa na kikao Chumba namba 231, sasa sijui wanajigawa namna gani.

Halafu Katibu wa Chama cha Wabunge wa *CCM* Bungeni, anaomba niwatangazie kwamba leo watakuwa na kikao cha Wabunge wote wa CCM, *Saint Gasper,* saa 12.00 jioni.

Katika orodha yangu ya wachangiaji, sijaangalia vizuri kumbe Mheshimiwa Mbowe yupo. Kwa hiyo, ningependa baada ya Makamu Mwenyekiti wa Tume basi Mheshimiwa Mbowe aweze kuchangia.

Mheshimiwa Tundu Lissu ulikuwa na nini?

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kuulizia Kiongozi wangu wa Kambi ya Upinzani kwa nini hajatamkwa kuchangia, lakini naona umeshaona. Nashukuru sana.

**SPIKA :** Ahsante nilikuwa sijaona msururu wa majina. Mheshimiwa Mbowe!

**MHE. FREEMAN A. MBOWE :** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nichangie mambo machache sana ya msingi. Kwanza, naomba niipongeze kabisa Kamati ya Teule ya Bunge kwa kazi nzuri waliyoifanya. Kwa kweli kwa taarifa ilivyowasilishwa sina tatizo nayo napenda kuiunga mkono na naomba vile vile nikubaliane na mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati Teule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda ku-*register* jambo moja ambalo pengine nilifikiri katika siku za usoni kuna umuhimu wa kulitafakari sana hasa katika hatua za awali za uundaji wa Tume kama hizi. Ni vema kwa mtu aliyetoa wazo la msingi akawa ni sehemu ya Kamati Teule na kwa maana hiyo Mheshimiwa Zitto Zubeir Kabwe ambaye ndiye aliyetoa hoja ya msingi kuhusu umuhimu wa kufanya uchunguzi huu ingekuwa vema angekuwa amejumuishwa kwenye Kamati Teule na hapo angeweza kutoa mchango wake moja kwa moja kwa kipindi chote ambacho Kamati imefanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pamoja na kwamba kuna hadidu za rejea maalum kwa ajili ya jambo hili, lakini tuliangalie kwa upana zaidi hasa katika uwajibikaji na utendaji ndani ya Serikali. Kwamba Kamati hii na hili sakata la Wizara ya Nishati na Madini, liwe limetupa fursa ya kuangalia kwa upana wake matatizo yaliyopo katika uendeshaji wa Serikali, ufujaji wa fedha uliokithiri ndani ya Serikali na siyo kwa Wizara moja bali ni kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Umma yakiwemo Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, nina mfano rahisi ambao ningependa nirejee, nao ni kuhusiana na semina ya Wabunge iliyofanyika Dodoma katika Ukumbi wa Msekwa, semina ambayo Kamati kwa kweli imetupa taarifa za kina sana kuhusu ni nini kilijiri. Sisi kwa upande wetu tumekuwa tunaangalia jambo lenyewe la Wizara kuchangisha fedha kutoka kwenye asasi zilizo chini yake, lakini ndani yamefumuka mambo mengine mengi ambayo yanaonesha upana wa wizi, upana wa ubadhirifu na mfano ambao ni halisi kabisa ni semina ya Wabunge ambayo ilifanyika Dodoma.

Mheshimiwa Spika, hili linanikumbusha wakati tulipokuwa tukijadili bajeti kwenye masuala ya posho, nilitahadharisha kwa Waheshimiwa Wabunge nikasema kwamba, Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukawa kweli tunahitaji tulipwe posho za vikao, hilo ni jambo lingine, lakini tuna wajibu wa kuangalia kwa kina Serikali na kwa maana hiyo Taifa hili linapata hasara kiasi gani kwa sisi kuendekeza vitu kama hivyo bila kuangalia upande wa pili ni watu wangapi wana-*take advantage* ya Wabunge kuchukua na basi kuweza kufuja fedha nyingi sana za Serikali bila hata aibu.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwenye hoja ya semina, ukifanya hesabu za haraka haraka ni kwamba, semina imefanyika Ukumbi wa Msekwa, ukumbi ambao unatolewa bure, lakini kwenye hesabu za Wizara ukumbi unaonekana umelipiwa. Ukumbi wa Msekwa hauchukui zaidi ya watu 300 lakini ukikokotoa orodha ya watu waliohudhuria semina ni zaidi ya 440, unajiuliza waliingia katika ukumbi gani?

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo semina ilikuwa ni ya siku moja kwa mujibu wa taarifa, lakini imetumia zaidi ya shilingi milioni 88, shilingi milioni 88 kwa semina ya siku moja ambayo Wabunge waliopigiwa hesabu kushiriki ni Wabunge 350, lakini ukiangalia hesabu ya Wabunge waliosaini ni Wabunge 195. Wabunge wengine waliobakia wamekwenda wapi na fedha zao zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile unaangalia fedha zilizolipwa kwa Katibu Mkuu katika muda wa siku tatu ambazo amefanya kazi, amelipwa malipo mbalimbali ambayo ni zaidi ya shilingi milioni nne kwa semina ya siku moja ya Wabunge. Tunakwenda wapi Watanzania? Hizi fedha zimetoka *TANESCO*, *EWURA* na kwenye Taasisi za umma zilizokuwa chini ya Wizara ya Nishati na Madini. Sasa kesho gharama za umeme zikipanda tunashangaa inakuwaje gharama za umeme zinapanda. Ni kwa sababu tuna gharama nyingi ambazo zinakuwa *associated* na Taasisi ambazo zipo chini ya Wizara zinaongeza *operational cost* ya Wizara na hatimaye inabidi kuzifidia kwenye malipo anayolipa mtumiaji wa umeme na nishati nyingine ili kuiwezesha Wizara na Serikali kujiendesha.

Mheshimiwa Spika, nashangaa mpaka leo watu wako Serikalini, nashangaa mpaka leo watu wapo maofisini na hoja sasa siyo kumjadili Bwana Jairo au Katibu Mkuu, ni hoja ya kujadili watumishi wengine mbalimbali wa Serikali ambao walishiriki pamoja na Katibu Mkuu kuona kwamba kuna wizi wa kiwango hiki unatendeka, kwa sababu Katibu hakufanya mambo haya peke yake na kama Katibu Mkuu anaagiza wasaidizi wake washiriki kwenye mambo ambayo ni kinyume cha taratibu haistahili kushtakiwa ama kuhukumiwa Katibu Mkuu peke yake ni lazima Katibu Mkuu aondoke na mfumo wake mzima ambao ulikuwa unamlinda au unamsaidia katika kukwapua fedha za umma.

Waheshimiwa Wabunge, mkifanya hizi hesabu mpaka unaona aibu, kama nilivyosema mimi mwenyewe ukiangalia malipo ambayo yanalipwa kwa Katibu Mkuu eti watu wanakaa Wizarani wanasema Katibu Mkuu apewe shilingi milioni tatu, anapewa posho ya shilingi milioni tatu ambayo haina maelezo yaani ni posho maalum. Halafu Wizarani wanaandikia tena barua kwamba Waziri apewe shilingi milioni nne na Naibu wake apewe shilingi milioni nne na wanapewa na wanasaini na watu wanaona ni jambo la kawaida, hapana! Hatuitendei Serikali haki wala hatulitendei Taifa haki!

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hii ni *tip of a nice bag* yaani kwamba ni jambo dogo tu lakini linapanua wizi ambao unafanyika kitaasisi ndani ya Serikali na wizi ambao kwa upana wake unaweza usiweze kuguswa na Ukaguzi wa Mdhibiti Mkuu wa Serikali kwa maana ya *CAG*. Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye ni Kiongozi wa Serikali Bungeni, nimetambua kabisa kwamba Kamati vile vile imeona kwamba Mamlaka ya Waziri Mkuu yanakuwa *tested* kwa sababu pengine Waziri Mkuu hapewi mamlaka ya kufukuza yaani Mamlaka ya nidhamu kwa Waziri Mkuu hayapo *clear* sana, matokeo yake watu wanaweza wakafanya mambo ya mzaha mzaha wakati Waziri Mkuu yupo na Waziri Mkuu anakosa nafasi ya kuchukua hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, suala la semina Bungeni, suala la semina kama sera ya Kitaifa linahitaji ufafanuzi, kupitia mikusanyiko ya semina na warsha tumezungumza mara nyingi kwamba kimekuwa ni chanzo kikubwa sana cha wizi wa kitaasisi ndani ya Serikali, ndani ya Mashirika ya Umma na vyombo vingine mbalimbali ambavyo vipo chini ya Serikali, matokeo yake fedha nyingi sana zinapotea na zinapotea kwa mtindo huo huo wa kuhalalisha semina. Waziri Mkuu ameshawahi kutoa tamko kwanza kwamba, wanalifanyia kazi suala hili. Pengine sasa ni wakati muafaka mkalitolea ufafanuzi wa kina kweli kweli kwa sababu jambo hili linaonekana linapuuzwa kwa sababu ni chanzo kikubwa cha watu kugawana fedha na chanzo ambacho kinashindwa kuthibitisha au kudhibitiwa. Kwa hiyo, pengine ni muhimu Serikali kupitia kwa Waziri Mkuu ikatoka na tamko maalum ambalo Wabunge wataweza kulielewa kwamba tunabana vipi matumizi ya Serikali katika mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ukurasa wa 122 wa taarifa hii kuna wizi ambao hata huwezi ku-*imagine* kwamba ni viongozi wa Serikali wanafanya, mtu analipwa posho ya shilingi 20,000/= lakini inaandikwa kwenye karatasi ambayo ni kughushi kwamba ni posho ya shilingi 120,000/= na watu bado wapo ofisini, hii Serikali ni Serikali gani isiyoweza kuwawajibisha watu ambao wanaliibia Taifa? Ndiyo sababu tunasema kwamba maisha ya wananchi yanakuwa ghali kwa sababu ya wizi mdogo mdogo ambao kwa ujumla wake unalisababishia Taifa hasara kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeshawahi kuzungumza kwamba utafiti uliwahi kufanywa na watu wa *DFID* wa Uingereza wanasema kati ya 35% - 40% ya bajeti ya Serikali ya Tanzania chini ya Chama cha Mapinduzi ni matumizi ambayo yangeweza yakaokolewa na kwenda katika shughuli za maendeleo, lakini ni pesa zinazopotea kwenye *recurrent expenditure* kwa sababu ya wizi mdogo mdogo kama huu ambao unafanyika siyo kwenye Wizara moja wala mbili lakini ni katika mfumo mzima wa Serikali na mashirika ambayo yapo chini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu, kitu ambacho nakiomba sana Serikali ifanye ni kwamba, Serikali ije na mpango wa makusudi kabisa wa kujaribu kubana matumizi ya Serikali. Nina hakika tungekuwa na mkakati wa makusudi wa bila kujiangalia sisi binafsi kama Wabunge na kama Mawaziri tunalipwa nini? Sisi tuangalie kwa ujumla kwamba je watu wanatumia fursa hii kiasi gani kujineemesha na kulitia hasara Taifa? Nina hakina tungeweza tukaokoa fedha nyingi na zikawapunguzia wananchi makali ya maisha. Huu upande mmoja wa semina, ni upande muhimu mno ambao unastahili kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa sana katika Wizara ambalo Mawaziri mara nyingi hawathubutu kukiri kwa sababu ya usiri wa Serikali. Lakini ni ukweli kwamba tunasikia malalamiko ya Mawaziri, kuna mgongano mkubwa sana wa kimamlaka kati ya Mawaziri na Makatibu Wakuu wenu, hili ni jambo ambalo hamlikubali lakini ukweli ndiyo huo. Kwenye Wizara Mawaziri mko pale lakini wenye Mamlaka ya mwisho ni Makatibu Wakuu na ni mara nyingi sana Mawaziri mnapuuzwa, mnakuja hapa sisi tunawakaanga ninyi lakini ukweli ni kwamba, wahusika wakuu wanaofanya ubadhirifu Serikalini ni Matibu Wakuu na wala siyo Mawaziri. Mawaziri wengine Makatibu wenu Wakuu wanawapuuza na sisi tunajua, mnalalamika na hamna sauti ndani ya Wizara zenu. Tunaomba Serikali ilifanyie kazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, Waziri Mkuu na Rais mliangalie hili, utendaji kazi wa Mawaziri na Makatibu Wakuu uhusiano wao ukoje? Kama leo tunaweza tukaletewa taarifa kwamba Katibu Mkuu wa Wizara aliamua mambo mazito kama haya bila kumshirikisha Waziri wake ni tatizo kubwa sana. Sasa Serikali inaongozwa

na Makatibu Wakuu ama inaongozwa na Mawaziri? Mawaziri najua hamtakiri lakini angalau mkubali kwa kuandika *note* kwa ku-*acknowledge* hilo kwa sababu najua hicho kilio ninacho kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, lazima Mamlaka ya Makatibu Wakuu ambao naomba nieleweke sina ugomvi na Makatibu Wakuu kwani nawaheshimu sana Makatibu Wakuu walio wengi na kwamba ni watu wazuri na waadilifu. Lakini haiondoi ukweli kwamba viongozi wa kisiasa ambao wamepewa Mamlaka ya kuongoza Wizara ndiyo wana dhamana za Wizara na siyo Makatibu Wakuu. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo ni kwamba ili Mawaziri tuweze kuwa-*take to task* kwa namna inavyostahili ni lazima kweli wawe na uhuru na uwezo wa kufanya maamuzi ndani ya Wizara zao bila kuhitaji msaada wa Katibu Mkuu na Serikali kupitia kwa Waziri kama kweli hamtawapa Mamlaka Mawaziri sisi tutaendelea kuwakaanga lakini ukweli ni kwamba wale ambao wanahusika na uchafu ndani ya Serikali wamekaa katika viti vya nyuma wanawaona Mawaziri wao wakikaangwa. Sasa hilo ni jambo lingine ambalo napenda kulieleza kwa uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo napenda kulieleza nikirudi kwenye mapendekezo ya Kamati. Ni kweli Katibu Mkuu hastahili kuendelea kuwepo katika nafasi hiyo kwa sababu ubadhirifu uliofanywa siyo tu wa kuchangisha fedha kinyume cha taratibu na hata matumizi katika Wizara yake yameonesha kabisa kwamba Kamati imepewa *forged document*, kumefanyika *efforts* za ku-*cancel* ukweli na ni lazima watu wote basi wanaohusika katika mtiririko huo waweze kuchukuliwa hatua ili Serikali ijisafishe mbele ya Umma.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana na sasa namwita Mheshimiwa Moses J. Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ili nami niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza kabisa naomba niunge mkono hoja iliyowasilishwa na Kamati Teule ya Bunge ikiwa ni pamoja na maazimio yote yaende kama yalivyo.

Jambo la pili, naomba ninukuu Ibara ya 100 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania halafu nitajielekeza kwenye hoja. Kifungu kidogo cha (1) juu ya uhuru wa majadiliano na utaratibu wa shughuli ndani ya Bunge, kinatuambia kwamba: “Kutakuwa na uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano au katika Mahakama au mahali pengine nje ya Bunge”.

Kifungu kidogo cha (2) kinasema: “Bila ya kuathiri Katiba hii au masharti ya Sheria nyingine yoyote inayohusika, Mbunge yeyote hatashitakiwa au kufunguliwa shauri la madai Mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema au kulifanya ndani ya Bunge au aliloleta Bungeni kwa njia ya maombi, Muswada, hoja au vinginevyo”. Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nimenukuu Ibara ya 100 (1) na (2)? Nataka kujielekeza kwenye kauli aliyoitoa Katibu Mkuu Kiongozi dhidi ya Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Beatrice Matumbo Shellukindo kwamba vyombo vipo, kwa hiy,o anaweza wakati mwingine Bwana Jairo ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini kwenda Mahakamani akamshtaki.

Sitaki kuamini kwamba Katibu Mkuu Kiongozi alipotoa kauli ya kumshauri au kumshawishi Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini ambaye sasa hivi yuko pembeni kwenda Mahakamani au kuchukua hatua za kisheria dhidi ya Mbunge mwenzetu kwamba Mheshimiwa Luhanjo hakuwa na akili au hakuwa na uelewa juu ya Ibara ya 100 ambayo inazuia suala la kumfungulia mashtaka Mheshimiwa Mbunge yeyote ambaye atatoa hoja ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Kitendo hicho ni uhuni uliokithiri na haupaswi kufumbiwa macho na yeyote ambaye anaona kwamba kwa kutumia lugha hii namwonea, huyu ndugu naomba tu avumilie kwani haya ni mawazo yangu. Huyu Katibu Mkuu Kiongozi ni kiongozi mkubwa. Narudia tena, Katibu Mkuu Kiongozi huyu ni msomi, ndiye alikuwa haelewi ukuu wa Katiba, kwamba haelewi Ibara ya 100 inasema nini juu ya kinga za Wabunge ndani ya Bunge, sitaki kuamini hivyo. Niombe…

**KUHUSU UTARATIBU**

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu Mheshimiwa Waziri! Naomba Mheshimiwa ukae kidogo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 64, pamoja na mjadala mzuri sana unaoendelea ningeomba mdogo wangu Machali kwa mujibu wa Kanuni hii ya 64 kifungu kidogo cha (j) ningemshauri Mheshimiwa anayesema sasa hivi atumie tu lugha ya kawaida inayoeleweka. Tumesikia wachangiaji wengi, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Umbulla, wamechangia lugha ile ile, maneno yale yale, lakini yanaeleweka. Kumwita mtu mhuni, ni lugha ya kihuni, nilifikiri neno uhuni linaudhi. *Message* itafika tu, taarifa hii, maazimio haya yatafika tu, lakini naomba neno hilo la kihuni si lugha ya Kibunge.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nakubaliana na ushauri huo. Angeweza akasema tu huo siyo ustaarabu ingekuwa vizuri kuliko tukianza kutumia maneno ambayo yanaonekana kama matusi matusi na sisi wenyewe tunakuwa *rated* hivyo hivyo. Mheshimiwa Machali, endelea tafadhali, naomba usijibu kuhusu hili.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba muda wangu pia tuuangalie wasi-*count* muda ambao ameutumia Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**SPIKA:** Sawa ndiyo utaratibu wetu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama Serikali iliyoko madarakani iko *serious* kweli na matatizo haya ya uhujumu wa uchumi, hawa watu walipaswa wakamatwe mara moja na wafikishwe mahali panapohusika na ikibainika, nimekuwa muumini wa utaratibu ambao unatumika katika nchi za Mashariki ya Mbali. Watu hawa walistahili wakamatwe na wanyongwe hadharani ili kusudi iweze kuwa fundisho kwa watu wengine. Kwa sababu gani? Tutaendelea kupiga ngoma ile ile, watu wanacheza wimbo ule ule, kila kukicha leo unasikia Wizara ya Nishati na Madini, hakuna hatua ambazo zinachukuliwa, kesho tutasikia Wizara ya Afya, kesho kutwa tutasikia Wizara ya Elimu, baada ya hapo tutasikia sijui Wizara gani! Haiwezekani! Hapa tunachezeana akili. Serikali kama mnasikia, hawa watu leo mnapaswa mtoe hati ya kuwakamata, wakamatwe wapelekwe kama wezi wengine wa kuku, wezi wengine ambao tumekuwa tukishuhudia wanafanya makosa madogo madogo na kufikishwa vituo vya Polisi na kuweza kuhifadhiwa mahabusu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wanachezea mamilioni ya Watanzania yanayotokana na kodi za Watanzania lakini taratibu ambazo zilipaswa kufuatwa zinakuwa kama vile za kuwalea lea. Naomba niipongeze Kamati hii kwa jinsi ambavyo wameweza kutuwasilishia taarifa ambayo ina ukweli ndani yake. Kazi kwenu Serikali kama hawa watu hamtawakamata, laana za Watanzania zitakuwa juu yenu. Narudia tena kusema laana za Watanzania zitakuwa juu yenu. Kwa hiyo, nashauri Katibu Mkuu Kiongozi, ashtakiwe kwa kosa la kuingilia uhuru wa Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naomba niwashauri Mawaziri wote wa Wizara ya Nishati na Madini wa-*take* kitu kinachoitwa *political responsibility.* Muwajibike tu ninyi wenyewe kwa uungwana. Kwa sababu gani! Wakati najaribu kuangalia kwenye kijitabu hiki cha viambatanisho ukurasa ule wa 88, Mheshimiwa William Ngeleja, amesaini malipo kwa ajili ya *entertainment allowance* shilingi milioni nne tarehe 18 Julai, 2011. Naibu Waziri, Ndugu Malima naye kasaini shilingi milioni nne wakati posho ya Waziri Mkuu hata angekusanya inawezekana mara tano isingefika huko. Shilingi milioni nane watu wanalipwa siku moja! Tunachezeana akili ndugu zangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama hawawezi wakaamua kuwajibika wao wenyewe, nina wasiwasi na uzalendo wao. Huwezi ukaenda kusaini shilingi milioni nne halafu kesho bado unang’ang’ania kuwa Waziri wa Nishati na Madini, au Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Tunawatania Watanzania. Ni rafiki zangu, lakini tunapokuwa kazini inabidi niwaambie ukweli. Nisipowaambia ukweli siwasaidii ninyi na vile vile siwasaidii Watanzania waliotupa dhamana ya kuwawakilisha ndani ya Bunge letu. Chukueni hiyo *political responsibility* na kama hamuwezi kuamua wenyewe kujiuzulu na Rais akaweza kuwafumbia macho, nitamshangaa na yeye nina-*suggest* ajiuzulu halikadhalika turudi kwenye uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, lakini sisi hapa ukienda kuanzia ule ukurasa wa 186 na kuendelea, Kamati yetu Teule imeweza kuwasilisha katika taarifa yake, ikitueleza waziwazi kabisa, wamewahoji hawa Watumishi wa Bunge ambao walitakiwa wapewe posho za shilingi 20,000/=, 50,000/= na 80,000/=. Taarifa zilizopo kwa mujibu wa taarifa hii ya Kamati Teule wamekataa, walilipwa kiwango hicho cha 20,000/=, 50,000/= na 80,000/= hapa kilichofanywa ni

nini! Pale penye shilingi 80,000 ina maana wameongeza moja. Hii ni *forgery*, laki moja na elfu themanini, laki moja na elfu hamsini. *Forgery* ni *criminal offence* kwa wale Wanasheria.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kuwa, watumishi hawa tunao na Kamati imewahoji na wamekataa, Serikali tunaomba tupate kauli yenu. Mnasubiri nini kama siyo Serikali nzima kuwawajibisha hawa watu? Kitendo cha kuwaacha huyu Bwana Jairo na wengine wote ambao wanahusika katika ku-*commit* hii *criminal offence* ya kughushi, natumia maneno ya ndugu yangu Kafulila, basi itakuwa ni Serikali legelege na itakuwa imechoka kweli kama mtaacha kuwashughulikia watu hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kama hapa kwenye shilingi 80,000/= wameongeza moja, moja mpaka mwisho na ni rahisi sana kweli, huu utakuwa ni uonevu mkubwa sana kwanza, kwa hawa Watumishi ambao wanalihudumia Bunge. Ni kuwadhalilisha watu hawa, umewapa shilingi 80,000/=, 20,000/= unakwenda kuongeza pale moja, moja kwa misingi gani? Ili kwamba wao ndiyo waje waonekane kwamba, wameshiriki katika wizi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama Rais Kikwete hawashughulikii Mawaziri wetu wawili na kuweza kuwawajibisha hawa watu, jiuzulu wewe ili kusudi aweze kuunda Baraza la Mawaziri lingine. Huu ni ushauri wa bure ambao nautoa kwako. Usiogope! Kwa sababu wewe ndiye ambaye tunakutambua kwamba, ni kiungo baina ya Bunge na Serikali, Kiongozi Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni. Kwa hiyo, kama haya yanafanyika ina maana kuwa na wewe unayaafiki kwa sababu ni mwakilishi wa Serikali, ni kiungo baina ya Bunge na Serikali. *Take that political responsibility* kwa maslahi ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndugu zangu kama tuko *serious* kweli na sisi wote Waheshimiwa Wabunge, tuweke pembeni itikadi zetu za Vyama, sijui CCM, sijui CHADEMA, sijui *NCCR*, sijui *CUF*, kama watu hawa hawawezi kuchukuliwa *appropriate initiatives* tukubali wote tuwajibike kwani Waheshimiwa Wabunge tutakuwa tumeshindwa kazi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Kwa mujibu wa Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, juu ya Madaraka ya Bunge, kifungu kidogo kile cha pili ambacho kinatwambia kwamba, sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itashindwa kuwachukulia hatua watu hawa na sisi Waheshimiwa Wabunge tunazidi kusema ni Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa tumeshindwa kutimiza wajibu wetu wa kuisimamia Serikali, tuwajibike kisiasa turudi tu kwenye uchaguzi kwa sababu haya ambayo leo hii yameonekana kwenye Wizara ya Nishati na Madini inaonekana yako mengi huko katika Wizara zetu mbalimbali, yamejificha tu bado hayajaweza kujidhihirisha waziwazi. Najua utakuwa ni uamuzi ambao ni mgumu sana kwa Waheshimiwa Wabunge, eeh, tuachie tena nafasi za Ubunge turudi kwenye uchaguzi? Tukubali! Hakuna sababu ya kuendelea kukaa hapa na wakati mamilioni ya shilingi yanatafunwa kila siku. Wenzetu huko wanawaza ni namna gani wanafunzi wa Vyuo Vikuu mikopo imekuwa ni matatizo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Eeh?

**SPIKA:** Muda umekwisha, kengele ya pili.

Wanasema anza wewe kwanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitumie Kanuni ya 60(5) (a) na (b): "Endapo maombi ya kuchangia hoja fulani yatakuwa mengi zaidi ya muda uliotengwa kwa hoja hiyo, Spika atatoa nafasi ya kwanza kwa Wabunge ambao: (a) hawajachangia katika hoja zilizotangulia na (b) wamechangia mara chache". Halafu bila ya kuathiri masharti ya Kanuni hii, hiyo tu inanitosha na Ibara ya (7) ile ya kutorudia rudia. Kwa hiyo, wale waliochangia jana nitawaruka na nitaendelea na wale wengine kwanza. Mheshimiwa Ezekiel Wenje, atafuatiwa na Mheshimiwa Agripina Buyorega.

**MHE. EZEKIEL D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata fursa hii nami niweze kuchangia katika hili suala muhimu linalohusu maslahi ya Taifa letu lililopo mbele yetu siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, kwanza napongeza Kamati Teule ya Bunge, kwa kazi kubwa waliyoifanya. Wamefanya kazi nzuri, wamefanya kazi kubwa kwa maslahi ya Taifa letu, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna masuala mawili tunayojadili; suala la kwanza tunajadili uhalali wa Katibu Mkuu na Wizara kukusanya fedha kutoka kwenye Taasisi nne zilizo chini ya Wizara. Lakini pia tunajadili jinsi matumizi ya hizo fedha yalivyotokea.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kwa mujibu wa hii taarifa, hizi fedha zimekusanywa kinyume na maelekezo ya Serikali na ukaguzi wa awali wa *CAG* ulionesha na kuna maswali matatu tunayojiuliza; moja Wizara kwenye hii taarifa inasema kwamba, walihitaji zaidi ya shilingi milioni 207 kufanikisha hii bajeti ambazo walipata kutoka kwenye *OC* zao, lakini bado wakaendelea kukusanya fedha zingine kutoka kwenye hizi Idara za Serikali ambazo ziko chini ya hii Wizara. Sasa tunajiuliza kwa kuwa, walikwishapata hizi fedha milioni 207 za kuja kufanikisha bajeti yao, kulikuwa na haja gani ya kuendelea kuitisha fedha kutoka kwenye hizi Idara? Hapa ndiyo unakuwepo mwanzo wa sisi kuanza kuuliza maswali mengi. Kulikuwa na haja gani ya hawa watu kuendelea kukusanya hizi fedha tena?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, hizi fedha ukiangalia hii taarifa, Idara hizi hazikushirikishwa kwenye kikao chochote cha kuhalalisha hayo makusanyo. *In fact* walitoa hizi fedha kwa hofu. Mheshimiwa Mwenyekiti, ametoa hii taarifa kwa Kiingereza alisoma ile taarifa ya watu wa *TPDC I think* ambao wanasema kwamba, tulikubali kutoa kwa sababu *you could not actually predict the unforeseen consequences* ambazo zingetokana na kutolipa. Ina maana hawa watu wamelipa kwa hofu na ina maana matendo kama haya yanaendelea kila siku Serikalini na hivyo ina maana kuna mambo ya ajabu yanatokea ambayo sisi hatujui. Tunamshukuru tu Mungu hii Wizara imefanya tukajua mambo yanayoendelea. Sasa kama Serikali inaendeshwa kwa utaratibu huu wa kupiga Wakurugenzi mkwara ili walete fedha kinyume na maelekezo ya Serikali, tunakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya ripoti ya awali ya *CAG* kuna maswali yaliulizwa pale, lakini bado Katibu Mkuu Kiongozi akaenda akaitisha Vyombo vya Habari akasema yeye haoni haja ya kuchukua hatua ya pili ya kinidhamu dhidi ya Jairo. Maana yake ni kwamba, yeye aliamua kum-*clear* Jairo. Pamoja na kwamba, bado kuna maswali yaliyojitokeza kwenye ripoti ya *CAG* ya awali, hii ni dharau kubwa kwa Bunge aliyofanya Katibu Mkuu Kiongozi, Mheshimiwa Luhanjo na lazima awajibike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini tunapiga kelele hapa Ngeleja awajibike? Ngeleja tunataka awajibike kwa sababu ya matukio makuu matatu:-

Moja, Ngeleja kama Waziri ndiye ana-*oversee operations* kwenye Wizara yake. Anapotwambia kwamba, hakushirikishwa, alipaswa ajishirikishe kama hakushirikishwa. Ina maana hii ni *evidence* kwamba hawa Mawaziri wameshindwa ku-*manage* Makatibu Wakuu wao, Wizara zao na hawajui wanachofanya, bora waachie ngazi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kitendo cha Ngeleja kurudi siku ile kumpokea Jairo kwa mbwembwe na yeye alikuwepo ofisini, hii inaonesha kwamba, anaelewa nini kiliendelea siku ile Jairo anasukumwa, gari inasukumwa, imebadilika uwanja wa siasa Ngeleja alikuwepo ofisini tumeona kwenye Vyombo vya Habari anampokea Jairo, hili alielewa.

Mheshimiwa Spika, kwa kitendo cha Ngeleja kukubali kusaini shilingi milioni nne kama posho eti *honorarium*, *honorarium* ni ya nini? *Four million, a lot of money* hii lazima awajibike, anajua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye taarifa ya Kamati Teule inaonesha Mawaziri waliohojiwa aidha hawaelewi basi hata *circulars* za Serikali zikoje na hawaelewi hata sheria ambazo wao wanazisimamia. Kuna Mawaziri wengine wanasema kwamba, hakuna *circular* ya Serikali ambayo inaidhinisha hizo *honorarium* wanazolipwa. Kwenye hayo majibu ya Kamati kuna wengine wanasema, aah, ni Katibu Mkuu atakavyoamua, wengine wanasema kuwa ni

shilingi 500,000/= kwa kipindi chote cha Bunge, wengine wanasema kwenye Bunge la Bajeti shilingi 500,000/= kwa Waziri na shilingi 400,000/= kwa Naibu Waziri na kwenye kipindi cha Bunge la kawaida ni shilingi 200,000/=.

Lakini Mheshimiwa Ngeleja kwa kujua haya yote kwamba, kuna maelekezo ya Serikali wao wamekubali kupokea shilingi milioni nne, nne yeye na Naibu Waziri wake *this is conspiracy,* wanajua wamehusika na lazima wawajibike. Hatumwajibishi Ngeleja kwa sababu yeye ni mtu wa CCM, ni kwa sababu ameshindwa kusimamia majukumu aliyopewa na Rais wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nchi hii ina historia na inaeleweka, kuna Mawaziri waliwahi kuwajibika. Mwinyi aliwahi kuwa Waziri na aliwajibika. Aliwajibika siyo kwamba, yeye ndiye alitenda makosa hayo *direct*, aliwajibika kwa sababu hayo makosa yalifanyika *under his watch*. Kwa hiyo, Waziri unapowajibika siyo kwamba, wewe ndiye umeiba moja kwa moja, ni kwa sababu kosa limefanyika *under your watch* na kama kiongozi muadilifu na mtu anayependa nchi yake, lazima uwajibike kuweka mfano wa utawala bora. Kuna Mawaziri wengi waliishawahi kuwajibika nchi hii, tunajua. Kwani kuna kosa gani Ngeleja kuachia ngazi? Kuna tatizo gani? Kila siku tunajadili hii Wizara. Jana kulikuwepo na *fraud* kubwa *same Ministry*, leo *same Ministry, what is happening?*

Mheshimiwa Spika, tunachukua muda wote wa Bunge asilimia 80 kujadili Wizara moja *where are we going?* Inafikia wakati watumishi wa umma wanaleta mpaka *this is doctoring*. Ukiangalia matumizi ya fedha hizi unagundua kwamba *the whole process is fraudulent;* kila kitu *is doctored,* ripoti hizi wanazoleta hizi ni *doctored* na jamaa eti wamesema wameleta watumishi 243 eti kuja kusimamia bajeti Dodoma niambie watu 243 ni sawa na idadi ya Wabunge unaowaona humu sasa hivi. Hao wote kutoka Dar es Salaam ulete hapa wafanye nini. Hii haiwezekani, ni wizi ambao hata kipofu anaona, hii haiwezekani. Wakati umefika lazima kama Taifa tujifunze kufanya maamuzi magumu. Mheshimiwa Ngeleja hata kama una *dream* kubwa na siasa ya nchi hii, kuwajibika leo haiwezi ikafanya usiwe Rais miaka 20 ijayo kama unataka. Nakupa ushauri wa bure na sitaki unilipe kwenye huu ushauri ninaokupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hii ripoti ni kweli kuna makosa mengi yamefanyika na Mheshimiwa Luhanjo, Mheshimiwa anayeitwa Jairo, hii kugushi nyaraka tunaita *this is a criminal offence,* lazima hawa watu wachukuliwe hatua na sio tu ya kuwaachisha kazi bali wapelekwe Mahakamani, wafungwe kwa sababu ushahidi tunao na haki ya mama msipowafunga, msipowapeleka Mahakamani sio laana, tunajipanga upya.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Buyogera atafuatiwa na Mheshimiwa James Lembeli.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Kwanza kabisa, naomba niungane na wenzangu kuipongeza Kamati Teule ya Bunge kwa kazi nzuri na takatifu mliyoifanya. Pili, naomba nimpongeze Mbunge mwenzangu ndugu yangu, Kamishna mwenzangu, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo kwa uaminifu mkubwa wa kubeba dhamana na kujenga heshima ya Bunge kama tulivyopewa dhamana na Wabunge wenzetu, nakupongeza sana kwa ujasiri wako. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kukubali uteuzi wa Kamati ile na kukemea kauli iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi ya kumrudisha au kumsafisha Ndugu Jairo, nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Spika, hasa kwa kauli yake aliyoitamka siku ile ya kuunda Kamati Teule: "Kwamba kama mnadharau zenu, dharau zenu zifanyike huko huko Serikalini sio humu ndani Bungeni". Nampongeza sana Naibu Spika. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukilalamika kwa muda mrefu Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuonesha ni jinsi gani Wabunge tunavyodharauliwa na Watendaji wa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leo umepata kielelezo sahihi kutoka kwa Bwana Jairo. Leo ni uthibitisho wazi wa jinsi gani Viongozi wa Serikali, Watendaji wa Serikali wanavyolindana katika matatizo na ufisadi mbalimbali unaofanyika katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Bunge lilidharaulika kwa kiasi kikubwa na mbaya zaidi sisi tunaamini kwamba, Mheshimiwa Rais anamwamini sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na tunaamini kwamba Waziri Mkuu ndiye Mshauri Mkuu wa Serikali kwa maana ndiyo Mshauri Mkuu wa Mheshimiwa Rais. Lakini kilichotokea siku ya mjadala

ule Mheshimiwa Waziri Mkuu alilithibitishia Bunge kwa uchungu mzito kwamba angekuwa yeye ndio mwenye mamlaka ya mwisho siku ile ile angetamka jambo.

Mheshimiwa Spika, sasa kinachonisikitisha ni kuangalia kauli ya Waziri Mkuu, baada ya muda kauli ya Katibu Mkuu Kiongozi hawa watu ni watu wazito sana ambao ndio *defence* ya Mheshimiwa Rais wetu. Unapoona matamshi yanagongana kwa Viongozi wakubwa kama hawa ni hatari kwa Serikali yetu. Bila ya kusahau, naomba niungane na Wabunge wenzangu waliotangulia kusema kwamba, hatua za haraka za kinidhamu na iwe mfano kwa Watendaji wengine zichukuliwe bila ya kuangalia sura ya mtu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hatutafanya maamuzi ya uhakika katika hili niungane na wenzangu kwamba itabidi Waziri Mkuu ajiuzulu na ili Waziri Mkuu asijiuzulu namwomba Waziri Mkuu abadili utaratibu kabisa. Kama ni mpole, upole wake unamponza na mwisho wa yote watamfikisha kwenye hatua mbaya hawa Watendaji anaowalinda. Dalili zimejionesha humu Bungeni kwa maana ya watu kufanya mambo ya aibu kwa Watanzania. Kwa hiyo, naungana na wenzangu kabisa kwamba utaratibu ufanyike na ikiwezekana Waziri Mkuu akae na Watendaji na Washauri wake wazuri waweze kuzipitia hizi Wizara upya, wawachunguze hawa Makatibu wa Wizara zote upya, wale wote walio na matatizo wakae pembeni tuweke Makatibu wengine kwa maslahi ya Taifa letu. Nayasema haya kwa nini?

Mheshimiwa Spika, leo tunamjadili Bwana Jairo na kwa upande wa Bwana Jairo kwa kweli lazima ashughulikiwe ili Watanzania waweze kujenga imani kwa Serikali yao. Lakini tunakumbuka Bunge letu hili tulijadili Wizara ya Maliasili katika upotevu wa wanyama wetu hawa wanaosafirishwa bila ya Watanzania kujua, lakini majibu yaliyokuwa yanatoka kwenye Wizara yanaangamiza. Mpaka leo hatujajua hatima ya yale mambo yanakwenda wapi. Kila tatizo Watendaji wapo tofauti na Mawaziri. Leo unaweza ukashangaa Wabunge hapa tunajenga hoja, Mheshimiwa Maige utakuwa shahidi yangu, nimejenga hoja hapa kilio cha wananchi wa Wilaya ya Kasulu ni namna gani wananyanyasika, ni jinsi gani tuweze kuwa wawakilishi wazuri. Mheshimiwa Maige ameahidi tutalishughulikia na uliyoyaahidi yalikamilika, uliagiza Mkurugenzi akaja Kasulu, lakini matokeo yake kwa sababu Watendaji wanakuwa na ajenda ya siri ya kujua ni nini wanachokifanya, nikiwa Jimboni yeye aliongea na Watendaji wa Halmashauri wakaenda *site* kwenda kufanya kazi wanayoijua, hatimaye akarudi ofisini ametumia fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge niliwasilisha hoja ile, hakunishirikisha mpaka leo Watanzania kule wanalala kwenye miti kama Wakimbizi, lakini Mheshimiwa Maige huna makosa. Ukiangalia tatizo ni Watendaji wanaokuzunguka, Watendaji wako kwenye Wizara wana nguvu kuliko wewe na hili nafikiri ninapozungumza *Hansard* inaweka rekodi, tutakuomba ushauriane na Waziri Mkuu naamini nyie ni Washauri wazuri kulingana na uzoefu wenu, mshauri Mheshimiwa Rais amwongezee Manaibu Waziri, Mheshimiwa Maige. Tatizo ni kwamba, suala hili tunaangalia Makatibu, tunajua mkanda wa Bwana Jairo utaeleweka kwani Kamati Teule imeshamaliza na kwa kuwa Wabunge wote tunaochangia tunakubaliana na Maazimio yaliyotolewa na Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, haya mambo yanauma sana. Nina hakika ni salamu kwa Bunge lako kujipanga vizuri ili tujue kabisa kilio kinacholalamikiwa na wananchi, mambo ya ufisadi, ufisadi sasa ni kielelezo tosha kwamba ufisadi kweli upo na ndiyo maana Katibu Mkuu Kiongozi alikuwa ameamua kumsafisha Bwana Jairo ili kupoteza ule ukweli kwa sababu haya mambo ya ufisadi hayafanyiki kwenye Wizara ya Nishati na Madini tu, yanafanyika katika Wizara nyingi. Kwa hiyo kwa sababu ni tatizo kubwa ndio maana ameamua kumsafisha ili mambo yaishe. Sasa Waswahili wanasema “Ukificha ugonjwa kifo kitakuumbua”. Sasa Katibu Mkuu Kiongozi alitaka kuficha ugonjwa, leo kifo kinamuumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nimalizie kwa kusema tena na namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu awe mkali ili Watendaji kwa kweli waweze kubadili tabia. Lakini kubwa zaidi naungana na Wabunge wenzangu waliozungumza kwamba upitiwe utaratibu upya ili Mawaziri, Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wasiwe Wabunge ili Bunge liongezewe nguvu ya kusimamia vizuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

**SPIKA:** Ahsante, sasa nitamwita Mheshimiwa James Lembeli, atafuatiwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ambayo umenipa, nafasi ambayo binafsi nilikuwa naisubiri kwa hamu kubwa sana. Bila ya kuchelea nasema, naunga mkono Maazimio yote yaliyotolewa na Kamati Teule kwa asilimia mia moja. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitatumia muda mchache sana, lakini nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu maneno ambayo nimeyasoma katika gazeti moja la wiki hii la kila siku ambalo lilimnukuu Baba wa Taifa. Kwa heshima na taadhima nakuomba uniruhusu nisome nukuu hiyo.

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa miaka takriban 15 iliyopita alikuwa anazungumzia suala la rushwa, alisema: "Sasa tumetikiswa ufa mmoja mkubwa sana, rushwa ya Tanzania siku hizi haina aibu", haya ni maneno ya Baba wa Taifa. Natembeatembea hivi watu wananiheshimu kidogo huko nchi za nje kwa sababu tulijenga Taifa hapa lenye heshima kubwa sasa pananuka." Baba wa Taifa alisema. "Serikali ya wala rushwa haikusanyi kodi, itabaki kufukuzana fukuzana na vijitu vidogo vidogo mabarabarani basi". Sasa Tanzania inanuka kwa rushwa.

Mheshimiwa Spika, tunachokizungumza hapa ni rushwa tu na iko Serikalini. Sasa imepiga hodi mpaka pale Ikulu. Ikulu ni mahali patakatifu, mtu hapa ametuhumiwa kwamba amekusanya fedha isivyo kihalali, anachomoka mtu pale Ikulu anamsafisha kwa misingi gani haieleweki na jambo baya zaidi rushwa hii pia imepiga hodi kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Mahesabu ya Serikali. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hivi vitabu haiingii akilini kwamba Ofisi ya Bwana Utuoh inatoa taarifa ya kumsafisha mtu ambaye dhahiri kabisa ni mwizi. Sasa ni *cancer*, ni UKIMWI ambao unalimaliza Taifa hili. Nchi hii sasa imebaki mifupa tu minofu yote wamekula na wanaokula minofu hii ni wakubwa kule Serikalini na kwenye Mashirika ya Umma. Nimesema sitasema maneno mengi, lakini nataka kusema nakubaliana kabisa na Maazimio yote, lakini lugha iliyotumika sikubaliani nayo. Kwa mfano, wanasema "Kamati Teule inapendekeza Serikali ichukue hatua zinazofaa kwa Katibu Mkuu Kiongozi", hapana lugha inayopashwa kutumika hapa afukuzwe kazi. Namheshimu sana Mzee Luhanjo, nimefanya naye kazi wakati akiwa Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, hakuwa hivi tena ana mvi kama mimi, lakini kwa mambo aliyoyafanya na kejeli aliyoifanya dhidi ya Bunge hili afukuzwe.

Mheshimiwa Spika, lazima tutoe mfano Wabunge hapa kila siku tunalaumiwa watu wanapiga kelele tunajikusanyia mapesa, pesa zenyewe ziko wapi ni hizi hapa wanaiba wao wenyewe. Ukipiga hesabu ya zile shilingi laki moja, moja walizoongeza kwenye shilingi hamsini, ishirini na kadhalika huyo mtu amekusanya si chini ya shilingi milioni 15, lakini yuko pale Nishati na Madini, kwa sababu wametengeneza mtandao pale Wizarani, sijawahi kuona Katibu Mkuu anasukumwa na wafanyakazi. Katibu Mkuu anayesimamia sheria sijui na nini gari lake linasukumwa. Namsikitikia ndugu yangu Ngeleja na yeye alikuwemo ofisini akapigwa picha anamkumbatia, anasherehekea, unasherehekea nini?

Mheshimiwa Spika, rushwa hii na Serikali yetu kama sikivu basi iwasikie Wabunge hapa, tusilindane, na iko siku sisi ambao tunaolindanalindana tutakuwa upande mwingine Tutaanza kupiga kelele hivi hivi hawa watu lazima wachukuliwe hatua, wafukuzwe na wapelekwe Mahakamani ni wezi.

Mheshimiwa Spika, kwa ndugu yangu Ngeleja nimesoma ukurasa wa 200 na ngapi, kimsingi Katibu Mkuu katika hili hakumshirikisha Ngeleja. Lakini Ngeleja anawajibika kwa sababu alipopelekewa shilingi milioni nne aliuliza zinatoka wapi? Sasa ndugu zangu Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Malima cha msingi hapa leo busara itumike kulinda heshima zao, heshima ya familia zao, heshima ya Chama cha Mapinduzi, lakini wampe heshima pia aliyewateua, inakuwaje kila Bunge tunapokutana hapa Wizara ya Nishati na Madini mpaka lini na nyie mpo hapo hapo haiwezekani. Nitakuwa wa kwanza kumshauri Mheshimiwa Ngeleja aachie ngazi. Wapo wanaosema hamna, mimi sijui, ni lazima tuwatetee Watanzania. Kama sisi humu ndani tunalindana, basi hatupaswi kuwa humu ndani. Nchi hii ni yetu sote na tuangalie historia jamani.

Mheshimiwa Spika, nchi za wenzetu wamefikia hatua gani kwa masuala haya haya madogo madogo ya rushwa. Naamini hata wanaokwenda mitaani kule ni kwa sababu wanatusikiliza na wanatuangalia, wakati sisi tunaendesha magari makubwa wao wanasota mitaani, lakini akikamatwa ameiba kuku, amepora simu mbili, kama atabahatika kufika Polisi, atapona, asipobahatika anachomwa moto. Sisi huku mtu anaiba mabilioni ya pesa, tunasema Sheria itachukua mkondo wake, kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mweleze Rais kwamba, hawa watu hawatoshi. Kwa sababu najua tatizo hili haliko Nishati na Madini tu, lipo karibu Wizara zote. Sasa usiposafisha mji wako unasubiri mtu aje akusafishie? Lazima Serikali ikubaliane na hali halisi kila Bunge tutakapokuja hapa kutakuwa na Kamati Teule kwa nini?

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine naunga mkono maazimio yote ya Kamati Teule, nawaomba Ndugu zangu Mheshimiwa Ngeleja na Mheshimiwa Malima watumie busara tu. Mzee Mwinyi alishawahi kujiuzulu, Mheshimiwa Ngasongwa aliwahi kujiuzulu kuhusu minofu na baadaye akarudishiwa Uwaziri wake, lazima mlinde heshima yenu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa nipende kusema tu kwamba, namshukuru Mungu sana kwa siku hii ya leo. Namshukuru Mungu kwa nini? Nataka nisikie taarifa hii. Ukweli kwa jinsi nilivyoiona leo ni kwa mara ya kwanza na sikuwa na sababu ya kufuatilia kwa sababu ilikuwa ni hoja ya Bunge. Kabla sijasema hivyo niseme pia, nachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Tanzania. Tangu siku nilipoibua hoja hii hapa Bungeni ikapokelewa na Bunge zima na ikawa ya Bunge zima nimepokea simu na *massage* takriban 1,215 na nimezirekodi zote na hakuna hata moja ambayo ilisema tofauti. Zote zilikuwa zinashukuru na kupongeza na kueleza mambo ya kutisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza hapa tujue kwamba *this is more serious* kuliko tunavyofikiria. Kwa wananchi ni jambo lingine kabisa. Nichukue fursa hii kuwapongeza sana viongozi wa dini zote hasa Masheikh wangu kule Kilindi ambao usiku na mchana wamekuwa wakifunga kwa ajili yangu. Wachungaji mmekuwa mkisali kwa ajili yangu na kwa ajili ya Bunge hili. Jamani nasema tunaweza tukashangaa mbona yanajitokeza sasa hivi na ni ya muda mrefu? Mungu ana jambo anafanya Tanzania na kama ametuchagua humu humu ndani kulifanya tusiogope vitisho. Kwa sababu neno la Mungu linasema kazi yake ni gharama yake, ukishaifanya yeye ndiye atakulinda. Sikuwa na hofu, kuna kipindi nikaambiwa tukupe walinzi, nikasema walinzi wa nini? Mungu wangu yu hai. Kwa kweli, nasema tunachofanya ni kazi ambayo Mungu ametuleta kwayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja. Kwanza kabisa napongeza Kamati Teule. Kwa kweli nilivyoitwa siku ile pale kwenye ile Kamati nilielewa *how serious they were.* Tangu ile *search, search* mlangoni, acha pochi, acha simu, acha kila kitu mpaka unaingia ndani, unakula kiapo kama upo Mahakamani na mahojiano yote yanarekodiwa ili usije ukasema hukusema. Nawapongeza sana pamoja ni Wabunge wenzangu lakini kwa dakika zile ambazo nilikaa takriban saa moja hapakuwa na Ubunge pale. Nawashukuru sana, nawapongeza kwa kazi ambayo wameifanya na ambayo ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, Watanzania mmeshuhudia. Watanzania kwa masuala ya itikadi hayapo tunapozungumzia maslahi yenu. Tunapozungumzia masuala ya maendeleo ya Watanzania hatuna cha itikadi. Hapa wote tunazungumza lugha moja. Haya mambo ya itikadi tuachieni, ni siasa na lazima iwe hivyo ilivyo. Lakini kwa masuala ya maendeleo tuko kitu kimoja na tutahakikisha tunapambana, tufikie yale ambayo tumejipangia. Niseme tu namshukuru sana Mheshimiwa Umbulla kwa kusema kwamba, suala ambalo hasa anahisi ni chimbuko, mimi hoja hii nimeibua si kwa sababu ya Jairo au nani.

Mheshimiwa Spika, nimeibua suala hili kuonesha mambo ambayo lazima tuyakemee. Watanzania wamechoka jamani. Natoka kwenye Jimbo mojawapo ambalo watu wako nyuma sana kikipato, wanaishi kwa kilimo cha msimu mmoja. Mzee ukimpa shilingi 1,000/=, anakubariki kana kwamba umempa milioni moja. Sasa ukija ukiona hapa hela zinavyofujwa kwa kweli haiwezekani na hii ipo nchi nzima. Kwa hiyo, niseme kwamba, nia yangu ilikuwa ni kuonesha mambo yaliyopo ili yakemewe na yasimame, kama haiwezekani, hatua stahiki zichukuliwe, hatuvumilii tena hata sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nimeshukuru sana, watumishi wazalendo na waaminifu ambao wanatoa taarifa na kwa kweli niseme ni katika wale ambao tunasubiri kwa hamu sana huo Muswada ambao utaletwa kuhusu haki ya mtoa taarifa, *Whistle Blower's Protection Act*. Kwa sababu nashangaa eti mtu kuibua ukweli au ufisadi anaanza kupewa vitisho. Nimekwenda pale Wizara ya Nishati na Madini muda mchache baada ya lile tukio, hamwezi kuamini, nafika pale hata wale waliokuwa wananipa taarifa wamenikakukia hawanisalimii. Mlangoni masharti kibao, ingia, saini, subiri mpaka tumpate, unapelekwa ukifika hata ofisi ya mhusika huendi. Tunaficha nini. STK 9429 imewekewa mafuta lita 230 kwa siku moja na haikutoka hapa Dodoma. Ndiyo maana walisukuma magari,

wanajua wanachokifanya, ndiyo maana mnatununia. Nawaambia pale Wizarani acheni upuuzi wenu hatukuja kupendana au kufarijiana, fanyeni kazi yenu.

Mheshimiwa Spika, kama ni masuala ya ubadhirifu nitaendelea kuyasema na watanihudumia na walinihudumia kweli. Unaona kabisa watu wana nidhamu ya woga hatuwezi kwenda namna hiyo. Ndiyo maana hata *TPDC* wengine wameshasema sitaki kurudia, wamesema kwamba ukiacha kulipa hii athari zake zinajulikana. Kwa nini tuache hivyo, watu wamekuwa vitisho tunawaangalia tu. Kwa kweli niko sawa na wenzangu, hawa ambao wanahusika ni hatua moja kwa moja. Huu mtindo wa kusema kwamba apumzike, kwa nini tunawapooza pooza? Mbona watu wadogo wanachukuliwa hatua hapo hapo ni mbaya kupita maelezo, kwa nini inapokuja wakubwa tunakuwa tunarembaremba, tunaremba nini? Tunalinda nini tunachokijua? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli niseme mengi yamenishinda. Sina mengi ya kusema kwa sababu yote yameshasemwa. Lakini huu ubadhirifu ambao umekithiri mpaka Bodi zinaogopa *forgery* za kutisha. Kwa mfano, hapa kwenye ukurasa 176 mtaona kwenye hili jedwali kubwa; kuna posho za kujikimu Maofisa wa Wizara kwenye Semina ya Wabunge, mtaona pale 80,000/- kwa siku nne halafu eti kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma *on transit,* eti ni shilingi 80,000/=. Jamani haya mambo ni ya kawaida hayo? Kasaini pale kuanzia Katibu Mkuu, Maofisa na nani na nani. Maofisa shilingi 80,000/= *on transit, on transit* gani masaa manne kutoka hapa na Dar es Salaam, lakini vilevile utashangaa watumishi wamebambikwa majina. Kuna watumishi wamebambikwa majina na siku ile watumishi 92 walilipwa posho. Pale naona mpaka majina ya Wakurugenzi wa Bunge, shilingi 180,000/=, watumishi wote mpaka wahudumu na wengine nadhani walikuwa *maternity leave* wako pale. Tunafanya nini, sisi hatuwezi kuachia mambo kama haya, tunachafuana bila sababu.

Mheshimiwa Spika, niombe kusema kwamba, kwa kweli kabisa *GST* nadhani kuna haja ya kuwasaidia. Sikupumzika na pamoja sikuwa kwenye Tume nilikuwa nafanya kazi kwa utaratibu wangu. Pale nina hakika kuna pesa nyingi ambazo zimekuwa zikipitishwa. Utaratibu wa mfumo wa Bajeti ya Serikali ni kwamba, ukiingiza hela ambazo haziko ndani ya bajeti ile inakataa. Sasa wakaona tupeleke wapi ambako hela zitatoka kwa urahisi, ndiyo wakakimbiza kule *GST* ambako wamekuwa wakipitisha na nadhani ukiongea na uongozi Profesa Abdulkarim Mruma na wengine watakwambia ukweli. Pale imekuwa kama ni pitishio. Lazima tusimamie hili.

Mheshimiwa Spika, pia katika upelelezi wangu nimekutana na Mawaziri wengine wengi, lakini hayo tutayaibua kwa kadiri tunavyokwenda kwa sababu hatuwezi kuacha jiwe hata moja halijageuzwa. Watanzania sasa wamechoka. Jamani mnavyoona taarifa zinatoka kama hivi mjue huko ndani hakukaliki. Kuna watu hawana *Godfathers*, hawana mtu wa kumsaidia, yupo yeye ni yeye, hawa ndiyo wanaohisi uchungu. Wengine ni wazalendo kupita maelezo, wanaona jinsi nchi inavyokwenda. Hatuwezi kunyamaza kwa kuogopa ni lazima tuseme ukweli na hata kama kuna wengine humu ndani ambao wana tabia hizo, hatuwezi kunyamaza mtatusamehe, tumekuja hapa na kura za wananchi kutetea maslahi na ndicho tutakachokifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe tu kusema na pengine nitakuwa tofauti kidogo lakini msema kweli na mara nyingine mtu ni vyema aseme maoni yake. Sina sababu yoyote ya kusema na ninyi mnajua kabisa mimi sihongeki, sishauriki yaani kubembelezwa kuwa *colluded*. Mimi huwa nasema kile ambacho nakiamini. Niseme na hili sikutaka kusema lakini nimeona limejitokeza sana. Ukiangalia ukurasa wa 119 wa hiki kitabu kidogo mpaka 120 utakuta pale mamlaka ambayo wamepewa Makatibu Wakuu ni makubwa mno kiasi kwamba sio lazima wahusiane na Mawaziri. Kwa kweli napata uchungu na napenda niseme ukweli kabisa, sina nasaba yoyote na Ngeleja wala nini. Mimi ni msema ukweli hata kama na yeye anakosea namwambia. Lakini ukiangalia madaraka kama haya si lazima amwambie.

Mheshimiwa Spika, sasa hapa tukisema Mawaziri wajiuzulu ndugu zanguni, naheshimu kabisa na napenda haki lakini watajiuzulu wangapi? Tatizo la pembejeo limekuwa shida, mtasema Maghembe ajiuzulu leo. Masuala ya wauzaji wanyamapori mtasema leo ajiuzulu Waziri wa Maliasili? Haiwezekani, lazima ifike mahali tuchunguze chimbuko. Jana Mheshimiwa Shibuda alisema vizuri, utachukua huku juu lakini chini uozo uko palepale.

Mheshimiwa Spika, hivi tujiulize leo Ngeleja na Malima akitoka ina maana tatizo limekwisha? Tatizo litakuwa halijapungua wala nini kwa sababu uozo uko palepale. Wenye mamlaka wako pale, taratibu zetu ndiyo sio sahihi. Nimefurahi wengine wamesema ziangaliwe kwa kasi na mabadiliko yafanyike ili tuone kwamba kazi inafanyika. Wawe wanahusishwa hapo tunaweza tukawa-*take to task* kwamba jamani hapa mmekosea. Mimi niseme hata hiyo milioni nne kwa mfano, huyu Katibu Mkuu ana-*discretion* ya kusema wape hela kiasi fulani. Mimi nilikwenda kuulizia ndiyo maana nasema na yule Mhasibu akasema *discretion* wanayo, wanampa kwa kipindi cha miezi

mitatu ya Bajeti. Unakwenda Dodoma Mheshimiwa hii hapa *entertainment* yako. Kwa sababu ni lazima anakutana na watu kwa ajili ya bajeti yake. Anatoa zile shilingi milioni nne. Niwaombe sana wapendwa, nawaombeni sana Waheshimiwa, kweli kama ni suala la kusema ajiuzulu basi tufanye haki, kama ni kujiuzulu ni wengi wa kujiuzulu. Lakini sio kusema kwamba nawatetea.

Mheshimiwa Spika, hata suala la hii barua naomba niseme, chukieni msichukie, lakini ndiyo maoni yangu, lazima myaheshimu kwa sababu kila mtu ana maamuzi yake. Nasema hata hizi barua siku hiyo sikutaka kabisa kuwaonesha hawa watu kwa sababu nilijua wanaweza wakaniona wakaanza kufikiria labda nini. Nilifanya kimya kimya, tunacheka kwenye *corridor,* nikaja nikaibua barua hapa. Sasa niseme, mambo mengine hawayajui. Sasa mkianza kuwa-*take to task* kila mmoja kwa kweli naona si sahihi. Siwatetei lakini nasema kama watalazimika kujiuzulu wajiuzulu kwa mengine. Lakini kwa msingi wa suala hili tunalolizungumzia naona *it is not fair*.

Mheshimiwa Spika, najua nitakuwa nimewakwaza wengi, lakini nimewakwaza kwa kusema ukweli ambao nauamini. Naomba niseme hivi na naomba niwaambie watumishi wa Tanzania na wananchi wa Tanzania kupitia jukwaa hili; kwamba msiogope, mambo ni mengi machafu yanaendelea na hatutasita kuyafichua lakini ukweli tutafanya haki, pale tunapoona haki inatakiwa kufanyika. Lakini kusema kukurupuka tu na nyie mnaogopa sijui nininini, kwa kweli hapana.

Mheshimiwa Spika na Wabunge wa Bunge hili, nawashukuruni sana kwa mshikamano ambao tumepeana kwa pamoja, naheshimu mawazo yenu, naomba tuendelee kuwa pamoja lakini naomba pia taarifa zinapopatikana tushirikiane kwa pamoja ili kuona haki inatendeka. Hatujali nani mkubwa na nani mdogo. Mabadiliko ya Katiba yanakuja, ni lazima tuhakikishe kwamba Katiba yetu inakuwa safi ambayo itakidhi na haitaacha *loopholes* kama hizi ambazo zimetokea.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru na naunga mkono hoja isipokuwa hiyo moja ya kusema kwamba Waziri pengine apewe masuala… lakini sio awajibishwe. Hilo la kuwajibishwa nalikataa kwa upande wangu hata mkisema nini. Mimi Beatrice Matumbo Shellukindo, Mbunge wa Kilindi nasema hilo siliafiki ni kuwaonea bure na kama ni hivyo tuwaonee wote lakini sio wao tu. Ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge, mtu akipewa nafasi yake hakuna sababu ya kuzomea, mwacheni amalize anavyoona yeye. Sasa namwita Mheshimiwa Mchungaji Natse, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi kama Mjumbe wa Kamati Teule nitoe maoni machache. Moja kati ya wale tuliowahoji alisema kwa uzito kwamba Serikali imeoza na tena ni Mjumbe mwenye taaluma kubwa katika nchi hii na mimi nilitafakari yale maneno yake kwa uzito "*Serikali Imeoza*."(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nukuu ya Maandiko Matakatifu inasema hivi: "Wote wameoza na kupungukiwa na utukufu wa Mungu", wanahitaji kutubu. Sasa nikiunganisha maneno hayo na mambo yote ambayo tumeyajadili na bahati nzuri tumeichambua Serikali, Ikulu, Wizara na Taasisi zake kwa umakini. Ndiyo maana mara nyingine wengine wanafikiri tumekuwa *lenient* katika kutoa mapendekezo, hapana. Unaweza ukaambiwa mshenzi wewe, kumbe mshenzi ina maana *positive* kwamba katika mambo fulani na ujanjaujanja. Ni kweli Serikali inahitaji kujitafakari upya katika yote yanayotendeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niseme hivi ni muda muafaka ambao Mungu amependa tuione Serikali ya Tanzania sasa *through* Wizara ya Nishati na Madini, tuangalie Wizara nyingine zote. Maana haya ambayo yametendeka katika Wizara ya Nishati na Madini kimsingi yapo Wizara zote na maovu kabisa.

Moja ni Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara zingine zote. Sasa je, tuendelee kutenda dhambi ili neema iongozeke? La hasha! Ni lazima tufike mahali sasa Watanzania Serikali yetu ambayo inapaswa kusimamiwa na Bunge ifike mahali iwajibike. Nafikiri kwa nia nzuri kabisa, tumeangalia ni kweli na tumependekeza haya mamlaka ya hiari ambayo wamepewa *Permanent Secretaries* na *Director Generals,* Serikali iangalie upya maana yanatumika vibaya katika mfumo mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa nini sasa Waziri awajibike? Ni lazima Waziri awajibike kwa sababu ndiyo msimamizi mkuu wa mambo yote ya Wizara. *Failure to that* Waziri mwambie aliyekuteua kwamba kwa sababu umenitengenezea mazingira haya, naomba Mheshimiwa Rais chukua kiti chako, sitaweza kufanya. Lakini kwa sababu tunalea na kukubali mzigo huo, *consequences* zake kama Waziri lazima pia uzikubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, imetushangaza sana Wizara ya Nishati na Madini, Waziri wake anasema amesikia kwa mara ya kwanza barua ikisomwa na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo hapa Bungeni sawa na Mbunge mwingine.

Naomba nitoe mfano mdogo sana ndugu zangu Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chukua baba nyumbani na mama na watoto. Binti bahati mbaya akapata ujauzito, baba anakuja kugundua siku moja tumbo liko hivi.

*(Hapa Mzungumzaji alionyesha ishara ya tumbo kutuna mfano wa mimba)*

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Kwanza atamwuliza mama kulikoni na imekuaje hapa? Mama ulikuwa wapi? Kwa Kiafrika kwa haraka tu ni mama atalaumiwa na atabebeshwa mzigo huo. Lakini unafikiri je, huyu mama alimwagiza kweli huyu mtoto afanye alivyofanya? La hasha. Lakini sasa huyu mama awajibishwe?

Wajibu wake, tena angesema tangu mwanzo, baba fulani mwenendo wa binti yetu sasa sio mzuri yuko hivi na hivi. Basi baba atajua ukweli, lakini mama akifichaficha mpaka siku ya mwisho, mama lazima awajibike. Kwa hiyo, Waziri na Naibu wake lazima wawajibike na wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe pia na *Chief Secretary,* kwa maana kwamba, Rais amwajibishe *Chief Secretary,* kwanza kwa kulidharau Bunge na kuudanganya Umma wa Watanzania kwamba Ndugu David Kitundu Jairo, hana kosa la kinidhamu. Taarifa ya *CAG* inaonesha makosa ya nidhamu yaliyo wazi. Lakini akatumia kwa makusudi kuudanganya Umma. *Chief Secretary* ni mtu mkubwa sana katika nchi hii. Tunamheshimu; yeye ni Katibu wa Baraza la Mawaziri, anafahamu kila kitu.

Nimechukua mhimili mdogo, nitazameni hapa. Kichwa Rais, mkono wa kulia Waziri Mkuu, mkono wa kushoto *Chief Secretary*. Mamlaka haya ndiyo yanayotenda kazi kwa pamoja ili nchi iweze kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa imejidhihirisha kwamba kuna kama kuonyeshana mimi zaidi kuliko, mimi zaidi kuliko. La hasha! Mihimili ikifikia hatua hiyo, nchi inaporomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi niseme hivi, tunayo bahati, nchi hii Mungu anaipenda. Hata hili kuibuka, ni kwamba Tanzania tujiangalie kwa upya. Tujiangalie kwa upya na tuone tunakwendaje ili kukosoana, kuheshimiana, kuhudumiana katika mihimili mitatu. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba mapendekezo ambayo Kamati tumeyatoa, yafanyiwe kazi mara moja kwa mustakabali wa Tanzania na kwa afya ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imesikitisha mhimili huu wa Bunge unatuhumiwa na Serikali kuonekana kwamba nao unashiriki katika ubadhirifu wa fedha za umma kwa njia ya kuandaa semina. Wamezungumza, tumeuliza, shilingi 20,000/= kwa huyu mhudumu, 50,000/= kwa maofisa, 80,000/=, sasa iko 120,000/=, 150,000/=, 180,000/=. Watumishi wengine wa Bunge wala hawakuwepo, lakini fedha zimetumiwa. Hawa tuliwauliza imekuwaje?

Mheshimiwa Spika, wanasema ni *topping allowance*, 100,000/= kwamba baada ya kazi yote kufanyika vizuri, bosi mmoja kutoka Wizara ya Nishati na Madini akaagiza walipwe hawa watu *topping allowance* ya laki laki! Jamani, ni haki 20,000/=, *topping allowance* 100,000/=, inaingia akilini hiyo hesabu? Ni haki 50,000/=, *topping allowance* 100,000/=! Aha, huu ni wizi, wizi! Kwa hiyo, ilitakiwa hatua ya kushitakiwa Mahakamani na siyo kubembelezwa tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kusema hivi; mmoja wa Mawaziri Wakuu Wastaafu tuliowahoji alisema hivi: "Mimi nashawishika kukubaliana nayo kwamba Bunge letu ni dhaifu, Bunge ni dhaifu, haliwezi kusimamia Serikali." Hili ni kweli na katika michango yangu siku moja nilisema; Mbunge kama mwakilishi wa wananchi anakuwa Waziri, akishakuwa Waziri, anaacha ile hali ya kuwawakilisha wananchi, amekuwa kitu kingine. Hii ni shida! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kweli Bunge lipate meno yake sawa sawa na ndiyo kazi yake. Lisimamie Serikali, hii itasaidia sana kuhakikisha kwamba wananchi wa Tanzania waiamini Serikali yao, waamini Bunge lao na chombo cha Mahakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote naomba nichukue nafasi hii, kwanza kuishukuru Ofisi yako kwa kupitia Kamati Teule yetu kuliwezesha Bunge lako sasa kufanya kazi yake ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya taarifa mbili; ya jana na leo ni uthibitisho kwamba sasa Bunge linatimiza majukumu yake vizuri na tunaomba tu sasa Mfuko wetu ule wa Bunge uwezeshwe ili kazi ya Bunge ya kuisimamia vizuri Serikali ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili; naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, wakati wa Bajeti nilisema hizi shilingi trilioni 13 tunazobajeti hapa, hii fedha ni nyingi na hatukuwa na sababu ya kuwa na *deficit* tuliyonayo, lakini bado mfumo wetu wa Bajeti una matatizo na unahitaji kuangaliwa upya. Haya ni matokeo ya maneno ambayo niliyasema wakati ule kwamba zipo fedha nyingi sana zinatumika nje ya utaratibu na ndiyo maana tumefika mahala mpaka leo hatuna Bajeti ya kujitosheleza wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili lazima tulisimamie kama Wabunge, tupitie Kamati zetu kuhakikisha Serikali inatumia fedha ambazo zimepitishwa na Bunge na si vinginevyo. Huu ni utangulizi wangu wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu; taarifa ni nzuri sana na Kamati imefanya kazi nzuri sana. Mimi ni mmoja kati ya waliobahatika kuitwa kwenye Kamati na nilisema na nitaendelea kusema kuwa tunalo tatizo la kusimamia sheria tunazozipitisha katika Bunge letu hili. *Law enforcement* imekuwa *very very poor in this government,* na hili lazima tukubali kwamba ni tatizo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma Taarifa ya Kamati Teule, ukurasa wa 133, inasema; "Katibu Mkuu wa Wizara anayo *mandate* ya kutoa *entertainment allowance* kwa maofisa hata viongozi. Kwa msingi huo nilimshauri Katibu Mkuu kwamba atoe *entertainment allowance* na mara nyingi Katibu anaweza kutoa kiasi chochote ambacho anafikiria."

Mheshimiwa Spika, ninavyofahamu mimi, Bunge hili likishapitisha Bajeti kwa vifungu vyake, hakuna mwingine mwenye mamlaka ya kufanya vinginevyo! Hakuna, hilo la kwanza. Lakini, la pili; anayesimamia matumizi ya Serikali na anaye-*appear* kwenye Kamati za Bunge ni *Accounting Officer* ambaye ni Katibu Mkuu. Hatujapata katika Kamati zote za Bunge kumwita Waziri katika suala la matumizi, tunamwita Katibu Mkuu, ndiye *Accounting Officer* aliyepewa mamlaka kisheria. Nalo hili ni vizuri tukalizingatia, na ndiyo maana Waziri unapofika mahala ukaona mambo hayaendi sawa na hili lilitokea Mheshimiwa Spika, unamchukua Katibu Mkuu wako, unakwenda kwa Rais aliyemteua na aliyekuteua, unamwambia Mheshimiwa, sote wawili umetuteua, lakini mimi hatuendi sawa na huyu mwenzangu, uamuzi ni wa kwako. Kwa sababu wewe una *political responsibility*, yeye ana wajibu wa kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikuarifu wewe unafahamu tulilifanya mwaka 1984 pale *Home Affairs*. Tulikuwa na Katibu Mkuu *very efficient*, lakini alikuwa *too slow*. Basi, tukaenda kwa Mwalimu, tukamwambia, sisi sote umetuteua wewe, huyu mwenzetu *speed* yake na yetu haiendi sawa sawa. Hilo tu! Uaminifu, kazi, *he is very good, but very slow* kiasi cha kwamba tunagongana kutokana na *speed* tu. Basi akauliza wewe umekaa muda gani pale kazini? Akasema nimekaa miaka mine, siku ya pili akamtangaza akamfanya kuwa *RDD,* akaondoka Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *the appointing authority* lazima ichukue hatua ndiyo nchi itakwenda. Lipo tatizo la kutokuchukua maamuzi kwa ajili ya watu wanaovunja utaratibu. Mimi nilipokwenda kwenye Kamati, baada ya kuisikia kauli ya Waziri Mkuu ndani ya Bunge inayosema kama yeye angekuwa na madaraka, angeweza kuchukua hatua, "lakini nitashauriana na mwenye mamlaka." Inatosha kabisa, inapofika Waziri Mkuu kutoa kauli hiyo ndani ya chombo hiki, muhimili mkubwa, inatosha kuiambia *authority* kwamba huyo mtu ana matatizo! Inatosha kabisa! Wala mimi nisingetafuta jambo lingine! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliwaambia kwenye Kamati kwamba kwa matokeo yale pale, yanatosheleza kabisa kuchukua hatua bila ya jambo lolote lingine. Anakwenda Katibu Mkuu Kiongozi, ambaye anawajibika moja kwa moja kwa Rais, na kwa maana hiyo anawajibika kwa Waziri Mkuu, maana ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali, sikutegemea jambo lingine. Nilitegemea lolote litakalofanyika lazima Waziri Mkuu atakuwa ameshirikishwa kikamilifu ili aiambie taasisi anayoisimamia ndani ya Bunge kwamba jamani, maamuzi yangu na nilivyosema ndani ya Bunge, nitamshauri bwana mkubwa huko, haya ndiyo maamuzi. Nilitegemea hilo, siyo kwenda kwenye vyombo vya habari. Serikali haifanyi kazi kwa vyombo vya habari, inafanya kazi kwa karatasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo halikutokea. Kwa hiyo, nasema tunalo tatizo la *enforcement of law*. Hili lazima lisimamiwe na Serikali. Lakini nataka nirudie walilolisema Waheshimiwa Wabunge kwamba uozo ni mkubwa. Matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali ni makubwa sana. Jana tumeshuhudia kwenye mradi wa gesi, tutashuhudia na miradi mingine. Wenzangu walitishwa juzi kwenye gesi hapa, na mimi nikawaambia Bunge lililopita lile, nilitishwa na *Williamson Diamond* kwamba ukituchunguza sisi wakubwa, utashika adabu yako. Nikasema, mtu anakufa mara moja tu, ninaamini kama Yesu atarudi, wengine hatuwezi kurudi. Amempaisha, siku yake ikifika atarudi tena, naye ataondoka vilevile. Nikawaambia *we die only once!* Hizi *multinational companies* zilizopo hapa zitatufilisi, zitatumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa haingii akilini, unakuja na wafanyakazi 230 kwa kazi gani? Ya kupitisha Bajeti ya Wizara!? Haiwezekani! *A responsible person* ambaye ni *Accounting Officer* alitakiwa awajibike na haya haraka tena iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne; nyaraka nyingi zinatolewa na *Pay Master General*, lakini haziheshimiki. Lakini la kusikitisha zaidi, taasisi ambayo Serikali na Watanzania wanaiogopa na kuiamini ni Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, ndiyo matumaini yetu wote, hata Kamati zetu za Bunge zikikaa, tunaitegemea ofisi hii ndiyo itatupa taarifa zilizo sahihi, na itakuwa imefanya uchambuzi wa kina juu ya masuala yanayohusika. Kama *CAG* kapelekewa taarifa ya uchunguzi, haishii tu mambo ya juu juu. Ndiyo kuna *forgery* ndani ya uchunguzi wake. Hajasema hata mtu mmoja apelekwe Mahakamani, hakuna! Kwanza, kwake yeye ni *advantage*, akiambiwa fanya uchunguzi, haishii kwa taarifa ile maana ndiyo kazi yake. Anaichukua kama ni *opportunity* ile ya kufanya zaidi ya hapo na hata tunapomwagiza katika Kamati za *PAC* na *POAC*, anafanya kazi zaidi ya pale tulipomwambia. Sasa leo kama kaishia kwa kufunika funika mambo, *credibility* ya ofisi hii kubwa tunayoiheshimu, tungependa iwe *very efficient* kwa sababu ndiyo inayolisaidia Bunge hili, ndiyo kioo chetu katika mapato na matumizi ya Serikali. Napo kuna walakini mkubwa sana. Bunge hili litashindwa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati zetu za *oversight* zinaitegemea sana taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kama yenyewe imeanza kazi ya kubabaisha babaisha, tutakuwa katika hatari kubwa sana. Kwa hiyo, mimi nasema mapendekezo ya Kamati yetu juu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, hili ni kosa kubwa sana. Tunaliona kama dogo, ni kubwa. Ni kubwa kwa sababu yeye ndiye mchunguzi wa mwisho, tumemwambia hata Benki Kuu ndiye mwenye *authority* kusema nani akaichunguze Benki Kuu, Kisima cha Serikali. Kama leo ameshindwa hili jambo dogo kutupa uwazi na kuiambia Kamati taarifa iliyowazi, tutakwenda wapi katika Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania ni maskini sana, wanaendelea kuwa maskini. Rasilimali za nchi bado hazitumiki vizuri, rasilimali za nchi bado zinachukuliwa na wageni hovyo. Ukiangalia dhahabu na migodi mingine inavyotoka hapa nchini, huwezi kuamini. Bunge hili lina kazi kubwa sana. Wala Wabunge tusijibebeshe lawama ya kutaka tujiuzuru, tuli-*strengthen* Bunge letu kufanya kazi, kuiwajibisha Serikali. Katiba hii inatupa mamlaka ya kuiwajibisha Serikali hata Rais, Katiba hii inatupa mamlaka hayo. Tutumie madaraka yetu, tutumie Kanuni zetu tuiwajibishe Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naungana kabisa na mapendekezo ya Kamati. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu. Lakini nianze kwa kukupongeza wewe kwa umadhubuti wako, kwanza, wa kukubali na hatimaye kuwezesha Kamati zetu zote mbili ziweze kufanya kazi, Kamati ya Nishati iliyokuwa inashughulika na masuala ya gesi ambayo ripoti yake imesomwa jana, lakini pia kuiwezesha Kamati hii Teule na Bunge lako Tukufu kufanya kazi ambayo mimi binafsi, napenda kuwapongeza sana Wajumbe wa Kamati hii Teule kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi kwa Kamati Teule kwa kazi nzuri iliyofanya, niende kwenye ukurasa wa 146 wa mapendekezo ya Kamati Teule. Inasema hivi; "Katibu Mkuu Kiongozi kwa makusudi aliamua kumsafisha Ndugu David Kitundu Jairo kwa kuficha ukweli wa taarifa ya ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na kuamua kwamba Ndugu David Kitundu Jairo hakuwa na kosa la kinidhamu, kitendo ambacho kimeupotosha umma wa Watanzania. Kamati Teule inapendekeza Serikali ichukue hatua zinazofaa kwa Katibu Mkuu Kiongozi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu Kiongozi ni Katibu wa Baraza la Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi kuanzia saa 1.30 mpaka jioni anafanya kazi Ikulu, Ikulu ambayo muasisi wa Taifa hili alisema ni mahali patakatifu na akasema yeye hakuchaguliwa kupafanya Ikulu kuwa pango la wanyang'anyi. Ikulu hii kwa sasa inakaliwa na Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwa ridhaa ya Watanzania, na sina mashaka na uadilifu wa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete. Nampongeza sana kwa hatua alizozichukua za kumwajibisha Jairo, kumweka pembeni. Lakini matumaini yangu leo na matumaini ya Watanzania, kwa kasi ile ile iliyomfanya Mheshimiwa Rais kumweka Bwana Jairo pembeni ili uchunguzi ufanyike, natarajia atawatendea haki Watanzania, leo ikiwezekana, kama si leo, kesho kuhakikisha kwamba Ikulu inaendelea kubaki kuwa tumaini kwa Watanzania kwa kuondoa watu ambao wanachafua taswira ya Ikulu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inapaswa watendaji waadilifu ambao wamethibitisha kwa vitendo vyao na ambao rekodi yao haitiliwi mashaka juu ya utendaji wa haki, ndiyo wapewe nafasi ya kwenda Ikulu. Ikulu ikiongozwa na mtendaji ambaye uaminifu wake na uadilifu wake unatiliwa mashaka, inaharibu taswira nzima ya Ikulu hata kama Rais aliyepo pale ni mwadilifu na mchapakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vitendo vya Katibu Mkuu Kiongozi Ndugu Philemon Luhanjo vya kuficha ukweli na kuwakingia kifua watendaji wa Serikali wasiokuwa waadilifu, inaharibu taswira ya Ikulu yetu na ninamwomba Mheshimiwa Rais amweke pembeni Ndugu Luhanjo. Lakini siyo kumuweka pembeni tu, awamu ya nne imeweka rekodi ya kuwafikisha baadhi ya watendaji wasio waaminifu na waliotumia ofisi za umma vibaya kuwafikisha Mahakamani. Sioni ni kwa namna gani Ndugu Luhanjo na Ndugu Jairo watakosa kutendewa haki hii ya kufikishwa katika vyombo vya dola, kufikishwa Mahakamani ili waweze kuwajibika kwa matendo yao ya kutumia ofisi ya umma vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuacha kumfikisha Luhanjo na Jairo Mahakamani kwa matumizi mabaya ya ofisi ya umma itakuwa ni kuendelea kuwakingia kifua, ni kuwalea na kitendo hiki Watanzania hawatafurahia na mimi mwenyewe nasikitika kwamba nitakuwa mmoja kati ya watu watakaolipigia kelele jambo hili mpaka haki hii itendeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 52(1) Waziri Mkuu amepewa madaraka au mamlaka, juu ya udhibiti na usimamizi wa utekelezaji wa sheria na udhibiti na utekelezaji wa shughuli za kila siku za Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Nilitarajia kwamba baada ya kwamba jambo hili liliibuliwa Bungeni na kulikuwa na deni la Waziri Mkuu kuendelea kuleta taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge, ili waweze kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa Ibara ya 63, nilitarajia kwamba Katibu Mkuu Kiongozi angetambua nafasi hiyo ya Waziri Mkuu iliyopo kwa mujibu wa Ibara ya 52 na angetambua pia madaraka aliyonayo Waziri Mkuu, kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni na kwa maana hiyo ripoti hiyo angeileta kama ilivyo na ushauri kwa Waziri Mkuu ili Waziri Mkuu kwa niaba ya Serikali aweze kuitolea kauli Bungeni na Bunge hili liweze kutimiza wajibu wake wa kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu Luhanjo hakufanya hivyo kwa sababu ambazo anazijua yeye, na ambazo kwa sasa hazijajificha bali ni kwa sababu ya kumkingia kifua Jairo ambaye kwa pamoja wamekaa Ikulu ile, wakijidai wanamsaidia Rais kutimiza wajibu wake, lakini kwa bahati mbaya wakiwa ni wahujumu wakubwa wa maslahi ya Taifa hili, na wahujumu wa dhamana walizopewa na Rais, Jakaya Mrisho Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka awaombe radhi Watanzania na amwombe radhi Rais na wawajibike jioni ya leo kukabidhi barua zao za kujiuzulu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakisubiri Taasisi ya TAKUKURU, naitarajia TAKUKURU iwatendee Watanzania haki kwa ajili ya wizi uliopo bayana hapa, kuwafikisha wahusika wote mahakamani bila kujali kwamba walikuwa na nyadhifa zipi, wala bila kujali kwamba walikuwa wameongezewa muda wa utumishi baada ya muda wao wa umri wao kutumikia Serikali hii, kuwa umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kwamba kama Serikali itachukua hatua hizo kwa kiwango hicho, Serikali itakuwa imejipambanua na kuwathibishia Watanzania kwamba waliyoyafanya hao, wameyafanya wao na kwa kweli Ikulu na wakubwa wetu hawahusiki.

Mwandishi mmoja wa habari na Mwandishi wa Makala mbalimbali ninayemheshimu sana Jenerali Ulimwengu, aliwahi kuandika kwenye makala yake mojawapo akisema naomba kunukuu; "Haiwezekani kuwa na Taifa ambalo watu wachache kwa kutumia ofisi za umma wanaishi maisha ya raha na anasa za kupindukia, na walio wengi wanaishi maisha yanayokaribiana na maisha ya hayawani, yaani umaskini uliotopea, halafu ukatarajia kuwa na amani na mshikamano katika Taifa la aina hiyo." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi hiki cha ukwapuaji wa mamilioni ya fedha za Watanzania, tunatengeneza Watanzania wachache wanaoishi maisha ya raha na anasa, wakati wengine walio wengi wakiishi katika umaskini uliotopea, ni matarajio yangu kwamba hao watachukuliwa hatua, ili kuhakikisha kwamba tunalinda heshima ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Taifa si mkusanyiko wa watu ambao kila mmoja ana ajenda yake, bali ni watu walio katika nchi moja, wanaochangia historia na utamaduni, kumbukumbu za machungu na matamu na wenye matarajio ya pamoja ya siku za usoni. Kwa vitendo hivi vya wenzetu hawa, matarajio ya pamoja ya siku za usoni hayapo na hasa ukizingatia kwamba wanachukua kile ambacho kingeweza kuwasaidia Watanzania kuondoa na kupunguza umaskini wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye hoja inayomhusu Waziri ukurasa wa 145, Aidha, kwa kuwa kwa mujibu wa Mwongozo wa Baraza la Mawaziri, Waziri ndiye msimamizi Mkuu wa Wizara, hivyo suala la uchangishaji halikupaswa kufanyika bila yeye kufahamu, Kamati Teule inapendekeza Serikali ichukue hatua zinazofaa kwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa William Ngeleja.

Lakini Kamati Teule kwenye ukurasa wa 119 inasema kwamba Kifungu cha 8(1) cha *Public Finance Act*, kwa mujibu wa kifungu hicho kimeweka wazi nafasi ya Katibu Mkuu katika kutekeleza majukumu yake ya masuala ya fedha pasipo kumshirikisha Waziri ambaye ndiye msimamizi mkuu wa Wizara, kifungu hicho ndivyo kinavyosema kwamba Waziri ndiye msimamizi wa Wizara, kwamba Katibu Mkuu anafanya maamuzi yanayohusiana na fedha bila kumshirikisha Waziri. Najua kufa kufaana, Ngeleja akijiuzulu, Adamu Malima akijiuzulu nafasi za Baraza la Mawaziri zitakuwa wazi na Rais atatafuta wa kujaza kutoka miongoni mwa Wabunge waliopo kwenye nyumba hii au atawateua zile nafasi kumi. Lakini waswahili wanasema mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina utetezi katika shilingi milioni nne walizopewa Mawaziri, lakini katika hili la ukwapuaji wa milioni 418 ambazo Katibu Mkuu Kiongozi ndiye anayetafuta kwa njia alizozitafuta, njia halali na haramu, na akazitumia kwa njia haramu, utakapomwajibisha Waziri katika hili mimi kama ndiyo busara ya wengine mimi binafsi naona kama mtakuwa mmewaonea vijana hawa, kwa sababu katika hili tukio hilo limetendeka na kama mtaendelea kung'ang'ania hilo, mtafukuzana kila kukicha. Tatizo lililopo ni mfumo wa mawasiliano kati ya Makatibu Wakuu na Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nalizungumzia pia jambo moja la watendaji wa taasisi hizi ambazo zimetakiwa zipeleke fedha zao kwa David Kitundu Jairo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini. Hawa wamepeleka bila kupenda na kama una Katibu Mkuu wa Wizara ambaye anakuagiza wewe *EWURA* lete fedha, wewe *TANESCO* lete fedha, *TPDC* lete fedha, na wewe unataka uwepo kazini na unajua kabisa Jairo anafanya haya akiwa na uhakika wa kulindwa na Luhanjo, hivi wewe utafanyaje? Inabidi labda wewe umeamua tu kufukuzwa kwa sababu mamlaka ya nidhamu ya watumishi ni Katibu Mkuu Kiongozi, ukiwa na Katibu Mkuu wa aina hii ambaye kesho anaweza kumpendekeza mdogo wake au haka yake, kuwa mrithi wa nafasi wa Katibu Mkuu Kiongozi kwa Rais, kutokana na ameshaonesha, kama unaweza kumbeba Jairo kwa nini usimbebe dada yako, kaka yako kesho kumpendekeza kwa Rais awe Katibu Mkuu Kiongozi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nasema maazimio yote yaridhiwe na wote wawajibike, wapelekwe mahakamani ili waache. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nilisema nitamwita Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Anne Kilango.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Taarifa.

**SPIKA:** Jamani, tungemaliza, taarifa unamtaarifu nani sasa? Tuendelee kwanza na Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Anne Kilango atafuatia.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba nipongeze kazi nzuri ya Kamati Teule ya Bunge lako Tukufu iliyoifanya kama inavyooneshwa katika ripoti ya Kamati pamoja na ushahidi mkubwa ambao Kamati imeuonesha katika viambatanisho vinavyokuja na ripoti hii. Niseme kwamba naunga mkono *findings* pamoja na *recommendations* zote za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumnukuu Baba wa Taifa letu katika kitabu chake cha Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania na kama nitapata muda nitamalizia mchango wangu kwa kumrudia Baba wa Taifa vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa katika kitabu chake alisema hivi katika ukurasa wa 52 wa Kitabu hicho; Waingereza wana msemo, *nature hates vacuum* (hulka huchukia ombwe) hata siasa huchukia ombwe. Kama uongozi ni mbovu upo kama haupo, au upo kwa maslahi ya yenyewe, watatokea watu waujaze uwazi uliopo, hauwezi kuachwa wazi hivi hivi. Lakini uongozi mbovu ni kama mzoga, una tabia ya kukaribisha fisi na inzi. Tusidhani kuwa hulka ya siasa yetu ni tofauti na hulka ya siasa ya watu wengine, kwamba sisi tunaweza kuvumilia uongozi mbovu na tusivune matunda ya hulka ya uongozi mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ambayo taarifa ya Kamati Teule ya Bunge lako Tukufu imeyaonesha ni matunda ya hulka ya uongozi mbovu. Tunavuna *the whirlwind* kwa sababu tumeruhusu uongozi mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ripoti ya Kamati pamoja na michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge imewakaanga sana Katibu Mkuu David Jairo na Katibu Mkuu Kiongozi Philemon Luhanjo na ni sahihi kabisa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matendo waliyoyafanya ni matendo ya wahalifu, ni *criminal acts, they should be treated as criminals.* Kwa hiyo, ni sahihi kabisa kama walivyokaangwa. Lakini si David Jairo wala Philemon Luhanjo peke yake ambao wameshiriki katika *criminal acts*, kwa mujibu wa taarifa ya Kamati ya Bunge lako Tukufu, siyo wao tu na ninaomba niseme kwamba siyo wao tu ambao wameshiriki katika uhalifu huu. Wakuu wa Taasisi na Mashirika yote yaliyochanga hizo fedha na wao wameshiriki katika *criminal acts and they should be treated as criminals*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tangu tarehe 7 Machi, 2011 Wizara ya Fedha ilishatoa Waraka unaokataza Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kuchangia Wizara fedha. Na ninaomba niseme maneno yaliyopo katika hiki kitabu kikubwa cha ushahidi; Wizara haipaswi kupewa fedha za ziada kupitia Mashirika na Taasisi zilizo chini yake, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Mashirika na Taasisi za Umma wanaagizwa, kuacha mara moja, utaratibu wa kukopa au kukopesha nje ya taratibu za kisheria zinazosimamia utunzaji wa matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma watakaoshindwa kuzingatia maelekezo hayo watachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa kanuni zilizopo. Kwa hiyo, siyo tu David Jairo na siyo tu Philemon Luhanjo ni pamoja na hawa wengine waliotoa hizi fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika hali hii, ni kweli kaka yangu William Ngeleja, ni kweli katika mazingira haya, *classmate* wangu William Ngeleja, kuna watu walihoji nimesomea wapi, sikusomea chini ya mti, nimesoma na William Ngeleja.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya aina hii, *classmate* wangu utapata wapi uwezo, *moral authority* ya kuendelea kujiita Waziri kesho!, Katika mazingira haya kaka yangu Adam Malima unawezaje kesho ukaendelea kujiita Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo tu kwa kutokujua fedha zinaibiwa, lakini vilevile kwa kupokea malipo ambayo *you should have known better*, mlitakiwa mjue vizuri. Unapokeaje shilingi milioni nne kwa ajili ya *entertainment* ya watu wako wa Jimboni na wageni wako wengine wakati una *entertainment allowance* ya Serikali, unapokeaje *per diem*

ya shilingi 400,000/= wakati ukiwa Bungeni unapata *per diem* ya Serikali. Unawezaje ukapokea pesa zote hizi bila kujiuliza *its for propriety*.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu Mawaziri wetu hawa kama bado wana-*any of semblance of integrity left* kesho wasijiite Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ripoti ya Kamati ya Bunge lako Tukufu inazua maswali mengine makubwa zaidi, katika mpango wa maendeleo ya miaka mitano ya Taifa, 2010 - 2015 Serikali imesema kwamba utaratibu wa malipo ya posho unaharibu mfumo mzima wa malipo ya Serikali. Mpango wa Taifa wa miaka mitano umependekeza utaratibu wa malipo ya posho uondolewe, ripoti hii inathibitisha *with evidence* ukweli na busara ya hayo maneno kwenye mpango wa maendeleo ya miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna ushahidi humu kwamba kwa siku moja Tarehe 14 Julai, 2011 Maafisa wa Serikali pamoja na Mawaziri wao wamejilipa posho kwa siku moja shilingi milioni 73, wanalipana *per diem*, posho ya kujikimu ya kati ya shilingi 315,000/= hadi 640,000/= kwa siku. Mtu anaitwa Mrusuri amepokea *per diem* ya shilingi 640,000/=. Mwingine anaitwa Dkt. Dalaly Kafumu 560,000/= kwa siku moja. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Mbunge.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Sijui kama ni Mbunge. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mnyonge wako. *(Kicheko)*

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:**Mheshimiwa Spika, ripoti hii inatupa fursa nyingine ya kurudi kwenye busara ya mpango wa maendeleo wa miaka mitano, utaratibu wa posho unatuangamiza, kama inafanyika hivi katika Wizara ya Nishati na Madini, hebu tujiulize Wizara ya Fedha kuna nini? Tujiulize ofisi ya Waziri Mkuu kuna nini? Tujiulize katika Wizara zote za Serikali wizi ukoje? Ubadhirifu ukoje! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watoto wetu wanahangaika hawana hela ya kusoma, akinamama wanazaa chini ya sakafu hakuna hela za dawa, lakini tuna fedha za kutoa posho ya kujikimu kwa afisa mmoja wa Serikali kwa siku moja shilingi 640,000/=, *shame on them! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utendaji wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Ibara ya 143(2)(b) inamuelekeza Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali namna ya kufanya kazi. Hajafanya kama maelekezo ya Katiba yanavyotaka, kwa sababu hiyo, ushauri wangu kwa Waziri Mkuu, naomba Waziri Mkuu amshauri Rais atumie mamlaka yake chini ya Ibara 144(2) amsimamishe kazi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, amuundie Tume ya Uchunguzi ili hii *ground* ambayo Katiba inasema aondolewe kwa tabia mbaya, ichunguzwe na hatua husika zichukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi tena kwa Mwalimu Nyerere nimalizie, Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania, Mwalimu anasema, na nilisema uongozi mbovu, sasa Mwalimu anasema; "Lakini hatulazimiki kuendelea na uongozi mbovu wa chama na Serikali, wala tukiendelea na hali hii bila kubadili uongozi wa chama na Serikali, sina uhakika kama tutafika huko salama, masuala muhimu ya nchi yetu hayatashughulikiwa, na masuala mengine muhimu ya uchumi, huduma za umma, rushwa na kadhalika yataachwa yajitatue yenyewe. Nasema katika hali kama hiyo sina hakika kama tutafika salama, na tukifika salama, tukiwa na uongozi huu huu wa chama na Serikali mbele yetu itakuwa ni giza tupu, majuto ni mjukuu, huja baadaye." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Watanzania wafanyie kazi wito wa Baba wa Taifa, hatulazimiki kuendelea na uongozi wa aina hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, nilimwita Mheshimiwa Anne Kilango Malecela atafuatiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi na nitaingia upande wa pili baadaye. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu, lakini kwanza pia nichukue nafasi hii nishukuru sana Kamati yetu Teule, Kamati ya Bunge. Kamati hii imefanya kazi nzuri sana na kuna watu wengine wameanza kuihoji hii Kamati, kuna watu wamefikia hatua wakasema oh! Kamati hii, hapana Kamati hii imefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo ambalo nawasihi Wabunge wote mnisikilize bila kujali itikadi zetu, mwaka 2007 kuliundwa Kamati Teule ya Richmond. Kamati Teule ni za Bunge, ile ni Kamati Teule ya Bunge, hii ni Kamati Teule ya Bunge. Mwenyekiti wa Kamati Teule hii ni Mheshimiwa *Engineer* Ramo Makani, maazimio tutakayoyatoa hapa ni maazimio ya Bunge. Maazimio tutakayoyaunga mkono naomba yachukuliwe kwamba siyo ya Mheshimiwa *Engineer* Ramo na wala siyo ya Mheshimiwa Martha, ni maazimio ya Bunge Zima. Kamati hii ni Kamati Teule ya Bunge. Naomba isije ikabadilisha jina ikaitwa Kamati Teule ya *Engineer* Ramo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, binadamu wote tunaishi kwa hisia, tumeanza vizuri kwenye Kamati Teule ya Richmond, tumeanza vizuri ilikuwa ni Kamati Teule ya Bunge, tukafika tukatoa maazimio hapa ya Bunge, baadaye yaligeuka ikaitwa kamati ya Mwakyembe, Kamati ya akina nani isifanyike hivyo tena tutaharibu Bunge hili. Hii ni Kamati Teule ya Bunge, maazimio tutayaunga mkono hayo ni maazimio yetu wote bila ya kujali itikadi zetu na hii ripoti ni ripoti ambayo imeletwa Bungeni. *(Makofi)*

Sasa naomba kuchangia, kila tukisimama tunalalamika jamani, Tanzania siyo maskini, tunaonekana tuna mdomo, Tanzania siyo maskini. Hii ni nyumba moja tu tumefungua mlango wakaingia watu waka-*search* wametoka na haya. Hebu tufungue nyumba zote ndio mtakapogundua kwamba Tanzania siyo maskini. Lakini mimi nazungumza huku roho inaniuma sana. Nina watoto wanne nina wajukuu wanne, mimi ni mtu mzima Watanzania wanaibiwa mno tena mnawaibia Watanzania bila ya kuwaonea huruma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi naomba nimesimama siku 70 kwenye jukwaa nikiitetea Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ikamate nchi. Lakini naomba nisimame sasa hivi, niikosoe Serikali ya CCM. Serikali kuna mahali mmetoa mwanya. Wizara kubwa kama hii ya Nishati na Madini, Wizara kubwa kama ya Maliasili na Utalii, Wizara zote zina fedha za wananchi, mnakwenda kumwekea huyu kiongozi wa kiasi mbali na zile fedha mnamwambia Katibu Mkuu wewe peke yako simamia hizi fedha, kosa. Lazima hilo tukubali Serikali kwamba mfumo huu tuuondoe mara moja, japo Waziri ashauriane na Katibu Mkuu lakini iwapo tutamuacha Katibu Mkuu yeye ndiye anayekumbatia fedha zote na Wakurugenzi wake huku chini na viongozi wote watendaji huku chini, haya mambo yataendelea kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina uhakika mambo yanayofanywa kwenye Wizara zetu na Makatibu Wakuu na Wakuu wa Idara ndio yote yako hivi hivi. Ninasema Mwenyezi Mungu unisaidie tufungueni hizi nyumba zote, hizi hapa mtakuta haya mambo yako hivi hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima ikae ione hili lililojitokeza hapa nyumba moja tuliyoifungua hii iangalie irudi mfumo wa jinsi utendaji kazi kwenye hizi Wizara ni mbovu. Tunaweza tukamwambia Ngeleja ajiuzulu ni kweli atajiuzulu, tutakuwa hatujafanya kitu chochote. Jiuzulu leo Ngeleja tutakuwa tumetatua tatizo? Hatujatatua kwa sababu ukienda Wizara ya Maliasili na Utalii utayakuta hayo hayo. Waziri kasimama hivi, Katibu kasimama hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa najihoji hivi kwa nini Mawaziri na Makatibu Wakuu wengi wao hawapatani? Leo ndio nimepata jibu ni mfumo mbovu wa Serikali. Waziri unampeleka pale yeye hana kauli na fedha ya nchi yake. Lakini unamwambia wewe Waziri ndio mkubwa wa Wizara hii, lakini hajui mambo ya fedha, eti ni kubembeleza. Utakuta Makatiba Wakuu wamesimama hivi hivi, hawa wote hapa wananyamaza kimya, hawana kauli kwenye Wizara zao wote hawa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali yangu niilaumu, mmetoa mianya lakini Mawaziri walio waadilifu wangekuwa wana nafasi ya kuangalia matumizi ya fedha wangeokoa mambo mengi. Lakini wapo kando ndio maana inafika mahali akipewa kaposho anapokea, ehee! Anapokea. Mimi nasema hivi, Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Waziri Mkuu kakae na Rais muangalie kasoro hii, kila siku mtasikia Waziri huyu, Makatibu Wakuu hapa ndani na Mawaziri wengine hawasemi. Watafanyaje kazi hawa? Katibu Mkuu na Waziri unaambiwa hawasemi, mimi nakumbuka Maliasili na Utalii, Waziri yule aliyeondoka na mwenzie walikuwa hawasemi. Kwa nini hawasemi, ahaa, mambo huko ndani. Serikali ya Chama cha Mapindunzi jamani, Wizara zimebeba fedha za wananchi. Wekeni mifumo ambayo itafanya fedha zilindwe vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nirudi kwa hawa watendaji wadogo, nyie mnawadharau hawa Wakuu wa Idara hawa sijui Wanyamapori, sijui idara gani ndio wenye fedha. Katibu Mkuu ndiye ameshika Wizara. Mimi sisemi kwamba Makatibu Wakuu nawapiga vita, naupiga vita mfumo. Tena naupiga vita mfumo na nitaomba

Serikali mje mtueleze kwamba hivi kweli nyie mnaona huu mfumo ni sahihi? Hawa Mawaziri wamenyamaza wamejikunyata lakini hawana kauli. Tutabaki kila siku jiuzulu na Waziri Mkuu naye pale huenda ni hivi hivi, huenda naye Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu naye huenda ni hivi hajui fedha zinavyokwenda ni mfumo gani huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nitoe maoni yangu mfumo huu ubadilishwe kuwe na mahusiano katika matumizi ya fedha, kuwe na mashauriano, kuwe na mazungumzo. *At least* ifike mahali wote wawili tukisema haya ondokeni wote tunawapeleka Mahakamani tukiwa tuna nguvu. Leo hapa Jairo tuna nguvu zaidi kuliko yule pale hatuna nguvu naye sana. Yule tutasema ni *political* anajiuzulu kisiasa, lakini ajiuzulu Ngeleja leo tumetatua matatizo? Hatujatatua matatizo, mnajuaje huko upande wa Maliasili na Utalii, mnajuaje Mifugo, mnajuaje Fedha? Tufungueni nyumba zote mkute vituko.

Mheshimiwa Spika, mimi ninachoomba kuhusu fedha za Watanzania hakuna msalia Mtume. Wote wachukuliwe hatua za kisheria. Tunapiga makelele Luhanjo, tarehe 1 Desemba, nasikia anastaafu kwa hiyo, achukuliwe hatua nyingine maana anastaafu, maana yake tuangalie mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya maazimio Serikali msije mkatuzungusha nayo, myachukulie umuhimu kama ambavyo na sisi tunachukulia umuhimu rasilimali za wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kusema sana la kwangu ambalo nalisimamia na nalililia Serikali badilisheni mfumo wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba anayeongoa na Waziri Mkuu aniachie kidogo, Waziri Mkuu anisikilize. Waziri Mkuu hanisikilizi ulisema watu wasiongee na Waziri Mkuu naomba. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nundu tunakusema wewe. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu mfumo mlionao wa utendaji kazi katika Wizara siyo sahihi. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Bado anaongea.

**MHE. ANNA K. MALECELA:** Jamani unayeongea na Waziri Mkuu niachie. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ni Waziri.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Hata kama ni Waziri mimi niko kazini pia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa sababu mambo haya yanahusu Serikali, sasa Waziri Mkuu kama hasikii sisi tutaelewaje? Haya mambo yanahusu Serikali. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, hili naomba Waziri Mkuu akiwa Mtendaji Mkuu wa Serikali alichukue na akae na Rais, waangalie mfumo wa utendaji wa kazi kwenye Wizara hizi. Katibu Mkuu amepewa madaraka makubwa mno kuhusu fedha za Watanzania. Watumishi wanamheshimu Katibu Mkuu kuliko Waziri. Waziri yeye ni *briefcase* tu na hili gari mnaloliona hapa hamna kitu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri Mkuu hili ulichukulie uzito na Bunge lijalo utujibu. Bunge lijalo tujibiwe kuhusu mfumo wa utendaji ndani ya Wizara zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu, hoja ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchunguza uhalali kwa utaratibu wa Wizara kuchangisha fedha kwa ajili ya kupitisha Bajeti Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba na mimi nichukue nafasi hii niwashukuru sana wafuatao wa kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Beatrice Shellukindo aliyeibua jambo hili hapa Bungeni. Lakini niwapongeze pia na wale watoa habari kwa Mheshimiwa Shellukindo. *(Makofi)*

Nawapongeza hawa kwa sababu waliotoa habari hizi wapo Serikalini. Wanapotoa habari maana yake wamechoka na yale yanayoendelea Serikalini. Mimi nawaomba wale watendaji ambao wapo Serikali na wanaona mambo yanakwenda ndivyo sivyo wasisite kututumia Wabunge ambao tunaweza tukasema ndio tukaiarifu Serikali kwamba yanayoendelea Serikalini ndivyo sivyo. Kwa hiyo, nawapongeza sana wale watoa habari wala wasikate tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Kabwe Zitto, nadhani ndiye aliyetoa hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule. Kamati Teule kwa uzoefu wangu niliokaa Bunge la Tisa zinatusaidia sana kuibua mambo maovu yanayofanyika Serikalini. Mimi naomba pamoja na kwamba inaweza ikawa inaleta ufa kwa upande wa Serikali yanapokuja mambo mazito usisite kuziunda Tume za namna hii ili tuweze kuhakikisha tunaisimamia Serikali inavyopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini shukrani nyingine ni kwa Kamati Teule. Naomba niipongeze sana Kamati Teule uliyoiunda Mheshimiwa Spika, yalisemwa mambo mengi sana ulipoiunda Kamati hii na wewe ni shahidi watu walisema umeunda Kamati watu ambao hawana majina, watu hawana uzoefu. Kwa hiyo, walibeza Kamati na mimi nilikuwa nasoma kwenye vyombo vya habari. Lakini Kamati hii na wewe imekupa jina kubwa kwamba uliteua watu ambao wamefanya kazi kinyume na Watanzania walivyotegemea. Niwapongeze wote kutoka pande zote ambao tuko hapa Bungeni wamefanya kazi bila kujali tofauti zao za kisiasa na huo ndio uzalendo niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi naomba niseme kwamba naungana na wenzangu wote waliochangia bila kujali upande walikotoka. Wote wamechangia kuiunga mkono hoja hii na mimi napenda niseme naunga mkono mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati Teule ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda moja tu ambalo ningependa niliseme kwenye taarifa ya Kamati kuna fedha ambazo hazijulikani zimefanya kazi gani. Kuna fedha ambazo tuliambiwa zilifanya kazi kwa ajili ya kuandaa upya randama wakati Wizara iliporudia Bajeti yake. Lakini Kamati imetueleza kwamba fedha hizo hazikuwa na nyaraka na fedha nyingine ambazo zilifanya kazi ambazo hazikueleweka. Ninaomba kiongezwe kifungu kingine pale mwishoni katika mapendekezo ya Kamati kwamba fedha zile zote ambazo zilionekana zimetumika vibaya au hazina nyaraka ninaomba wahusika kwa namna yoyote itakavyoonekana inafaa wakatwe hizo fedha na zirejeshwe Serikalini hili halikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba fedha hizo zirejeshwe Serikalini kwa wale wote ambao inawezekana walizilipa sambamba/sanjali na hatua nyingine za kinidhamu ambazo zimependekezwa na Kamati Teule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nizungumze jambo moja ambalo wenzangu wamerudia lakini ni kama kusisitiza lakini nipitie kurasa katika taarifa ya vielelezo. Nina uhakika Waheshimiwa Wabunge wote tunazo nyaraka. Naomba hapa Serikali itusaidie ukifungua ukurasa 176 wa taarifa hii kuna malipo yaliyolipwa kwa David Jairo pale shilingi 400,000 ni tarehe 25 mpaka 28 inaitwa posho ya kujikimu, ukienda ukurasa wa 178 kuna shilingi 400,000 kwa tarehe hiyo hiyo ya 25 mpaka tarehe 28 ambayo inaitwa posho ya kikao kwa maafisa. Ukienda ukurasa 181 zimelipwa shilingi milioni tatu kwa David Jairo inaitwa posho maalum ya Katibu Mkuu tarehe hizo hizo. Ukienda ukurasa 182 Jairo amelipwa shilingi 800,000 malipo maalum kwa viongozi kwa tarehe hizo hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali ifafanue tofauti ya malipo na majina haya na mimi naanza kuelewa Wabunge wanapozungumza haya malipo ya posho ninadhani tunakwenda ndivyo sivyo. Posho nyingi zimekuwa nyingi mno kwa mtu mmoja huyo huyo kwa siku hiyo moja mtu anaweza akalipwa posho za milioni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo kubwa, ninaomba Serikali itoe maelezo sahihi sana katika malipo kwa sababu Watanzania wanapoyaona mambo haya na sisi Wabunge wa Bunge la Jamhuri tupo hapa ndani na kama walivyosema wenzangu wapo Watanzania ambao kwa kweli wanaishi katika mazingira magumu sana na watu wakalipwa hivi hii si sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, adhabu iliyopendekezwa kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na ambaye asimamishwa Kamati imesema achukuliwe hatua za kinidhamu na mimi napendekeza kama Kamati ilivyosema lakini iweke mkazo kwamba kwa kweli Jairo hapaswi kurejea katika uendaji wa kazi Serikalini. Kama akirejea basi itaonekana Bunge lako linatwanga maji kwenye kinu. Hapa Bunge lako litaendelea kudharauliwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niseme Wabunge hatulumbani tu na watendaji wa Serikali, kila mtu anatimiza wajibu wake. Wabunge tunatimiza wajibu wetu wa kuisimamia na kuishauri Serikali. Nina hakika watumishi Serikalini wanapoona Wabunge wanazungumza haya wanafikiri kwamba wanaonewa, wala hatuna sababu ya kumuonea mtu kwa sababu tuliapa kuitii Katiba yetu kwa hiyo, tunaishauri na kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi hainiingii  akilini kwamba Mawaziri hawa ndio wasimamizi wakuu wa Wizara zao. Lakini inakuwaje Waziri huyu au Mawaziri hawa hawajui yanayoendelea ndani ya Wizara za kwao. Hapa ni kitendawili kikubwa sana.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, atuambie kwamba kuna udhaifu au akiri kwamba kuna udhaifu mkubwa ndani ya utendaji kazi Serikalini. Kwa maana hayo na mimi unaweza ukaona hamna sababu katika hali hiyo ya kuwa na Mawaziri, Mawaziri wanafanya nini Wizarani kama mambo haya mazito yanaweza yakaendelea, Mawaziri wapo, sioni sababu ya kuendelea kuwa na Mawaziri Wizarani. *(Makofi)*

Lakini pia Mawaziri kama Wabunge hapa ndipo wanapopakwa matope kwa sababu wanajigawa vipi wakati gani wanaisimamia Serikali na wao wenyewe huku wakiwa ndani ya Serikali? Inakuwa ngumu sana. Niseme kwamba Ngeleja hakujua na kweli Katibu hakuwa na sababu ya kumfahamisha Ngeleja kwa sababu ya madaraka aliyonayo na Waziri atawajibika kwa mambo ambayo hakuyatenda.

Ninaomba Serikali iangalie hilo na kwa sababu yameshazungumzwa sana, mimi sitaki kuchukua upande, Serikali iangalie yale yaliyozungumzwa jinsi ya utendaji kazi katika Wizara ulivyo na bahati mbaya sana Wizara ya Nishati na Madini imekuwa inazungumzwa sana ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bunge la Tisa ilizungumzwa sana, Bunge la Kumi inazungumzwa sana, namuonea huruma sana Waziri Ngeleja na Naibu wake. Kwa hiyo, wakati mwingine ni vizuri Serikali ikatafakari juu ya mambo ambayo yanaendelea ndani ya Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba yamezungumzwa mambo kuhusiana na *TPDC* na taasisi zilizochangia wapo Wabunge ambao wamesema na taasisi zilizochangia na zenyewe zichukuliwe hatua kwa sababu zilichangia kwa makosa, lakini mimi nataka tu niseme tunaishukuru hata taasisi ya *TPDC* hata kwa kuchangia *under protest*, wamechangia zile pesa bila hiyari yao, lakini wakaenda kuripoti kwenye Bodi kwamba hatukuwa na namna, ilibidi tu tutii agizo. Kwa hiyo, inaonyesha kwamba watu wanachanga fedha Serikalini lakini hawajaridhika, ni mfumo uliopo Serikalini ambao unapaswa urekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sioni namna ambavyo Katibu Mkuu Kiongozi anaweza akatoka katika hili na hili ndilo tatizo la kufanya kazi kirafiki ndani ya Serikali, maana yake mimi nakiona ambacho Mheshimiwa Luhanjo alikuwa anakifanya pale kwanza ni urafiki uliopo kati yake na Jairo kwa sababu tu ya kufanya kazi kwa muda mrefu pamoja, lakini ni kwa sababu tu ya kulindana na kufadhiliana ndani ya Serikali, haya ndiyo yanayouwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine mimi huwa nasema kwamba tunawapa hoja Wapinzani kusema. Kwa sababu wakati mwingine wakisema mambo ambayo yanaonekana Serikalini na kama Serikali tukisema haya, halafu hatua hazichukuliwi basi watasema Serikali imeendelea kufuga wezi, kufuga mafisadi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba mambo mengine Mheshimiwa Waziri Mkuu, hayahitaji hata hawa watu kwenda Mahakamani ni Serikali kwamba tunawaondoa tu kwenye *system* ya Serikali yetu na Watanzania ambao wengi wanaelekea kukata tamaa na utendaji ndani ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi kama Serikali itachukua maamuzi mara moja mimi nina hakika wananchi wa Tanzania walio wengi wataendelea kurudisha imani ndani ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Lakini kinyume chake tutakuwa tunaendelea kujichimbia kaburi na haya hatuhitaji kuendelea kuhutubiwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chombo kimojawapo ambacho kilikuwa na heshima sana katika nchi ni Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Mheshimiwa ndugu yetu Ludovick Utouh alipata heshima sana lakini hili inaonekana limemchafua, limeondoa imani ile kwa Wabunge wengi na Watanzania ambao walikuwa nayo juu ya chombo hiki. *(Makofi)*

Inaonekana *CAG* ndugu yangu Utouh alifanya kazi kwa kuelekezwa na mamlaka zilizopo, lakini akiwa kama ofisi ambayo imeanzishwa chini ya mamlaka na sheria maalum ya Bunge, Utouh hakupaswa asifanye kazi katika mazingira aliyofanya kazi na mimi naungana na wale wanaosema ni vizuri kikaundwa chombo kingine cha kuangalia mwenendo wa namna gani Ofisi ya *CAG* ilivyoshughulikia suala hili maana ilishughulikia kinyume kabisa na utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba kama nilivyosema mapendekezo yaliyotolewa na Tume, tunapokuja kwenye Mkytano wa Saba, nadhani itakuwa ni Mkutano wa Saba, ni Mkutano wa Sita eeh! Mkutano wa Sita, ninaomba Serikali ije na majibu ya kutosha juu ya mapendekezo haya bila kusubiri Wabunge tuje tuibue mambo mengine makubwa hapa.

Kwa hiyo, ni vizuri kwamba Serikali ikaja kwamba nimeona kwa mujibu wa mapendekezo haya kwa sababu hayakuwa *numbered* yameanzia kifungu cha 9.2 lakini ukiya-*number* mwenyewe pale unafika nayo karibu 12 na lile ambalo nimetoa pendekezo hapa kwamba pesa zilizoibiwa ambazo hazikueleweka matumizi yake na hakukuwa na nyaraka na zenyewe zifanyiwe tathmini ziweze kurejeshwa. Kwa hiyo, mapendekezo yote haya, yafanyiwe kazi na Serikali ije na majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Kamati yako kwa kufanya kazi bila kuchoka na hatimaye kutuletea hapa Bungeni. Pamoja na taarifa hiyo ni kwamba Sheria ya Fedha ni bora ikafanyiwa marekebisho kama si kubadilishwa kabisa.

Mheshimiwa Spika, kama Waziri hata akitaka kwenda Jimboni ni lazima aombe pesa kwa Katibu Mkuu kama sio ruhusa, na kama Katibu Mkuu akikataa basi Waziri hana ujanja. Pia hata kama mtumishi akikosea Waziri hana uwezo hata wa kumkaripia, huu ni udhalilishaji kwa Mawaziri wa Serikali na sheria hii imepitwa na wakati, ni vyema sasa Makatibu Wakuu wanapofanya maamuzi washirikiane na Mawaziri na sio Makatibu hao kujenga viburi hata kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Waziri ajulishwe na ushauri ufanyike japo Waziri asijihusishe na mambo ya utendaji. Ni wakati muafaka kurekebisha sheria hiyo. Na si vizuri sana kusema Ngeleja ajiuzulu wakati yeye ni Waziri ambaye hana meno, kwani kazi yake ni kusurubiwa humu Bungeni kwa kosa ambalo linatendwa na Makatibu Wakuu wao.

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwe makini na vipi kufanya marekebisho ya sheria. Ahsante.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja na mapendekezo yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja naomba nichangie baadhi ya maeneo kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuamini kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alishindwa kubaini mapungufu ya wazi na taarifa yake kutumika kupotosha umma, huu ni udhalilishaji mkubwa wa taaluma ya uhasibu kwamba na *anormalities* hizi na zikaweza kubainishwa kiurahisi na Kamati Teule kwa mujibu wa viambatanishi. Hivyo naunga mkono pendekezo la Kamati Teule ya Bunge jinsi ilivyomuona Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kutumika kupotosha umma.

Mheshimiwa Spika, mfumo mzima wa kiutendaji Serikalini kwa maana ya Wizara ni vema ukatizamwa upya kwani Makatibu Wakuu wamekuwa na madaraka makubwa katika maamuzi ya matumizi ya fedha na madaraka ya kinidhamu kiasi cha kuwanyima madaraka ya kutoa maamuzi ya kuwawajibisha.

Mheshimiwa Spika, mfumo mzima uangaliwe upya kwani haya ndiyo yanayojitokeza mpaka kwenye Halmashauri zetu.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikupongeze wewe mwenyewe pamoja na Kamati hii Teule uliyoiunda kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pole kwa kazi hii ngumu. Kimsingi tunachojifunza ni kuwa mmomonyoko huu wa matumizi ya pesa hasa katika taasisi zetu, wakati tunaleta hoja yetu ya Kamati Teule iliyopita tulisema, ipo haja sasa ya kufuatilia kwa umakini jinsi gani uwajibikaji wetu hauangaliwi tu katika ngazi zetu za juu. Kwani walimu wa ubadhirifu huo ni hao hao kiasi kwamba kila anapoondoshwa mkubwa akija mwingine naye anafundishwa kufanya tena uovu. Nashauri Wizara hii ifanyiwe *reshuffle* kuanzia chini huko na taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, hivyo Wizara hii ni sugu na itaendelea kuleta tatizo katika nchi. Lakini pia na kwa Waheshimiwa Wabunge basi tupige tu marufuku kwa Wizara yoyote au Taasisi kutufanyia semina au kikao cha kulipwa posho, badala yake kama mtu au taasisi wanataka kusaidia, basi ipitie mfuko wa Bunge ili kuleta heshima ya Bunge kwani kweli viposho bado vinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 120, naona *Accounting Officer* ni Katibu Mkuu hivyo hapo sioni likijitokeza vizuri suala la hawa Mawaziri na hasa kama hakuna mwongozo kamili wa utoaji wa *honorarium.*

Mheshimiwa Spika, na kwa kweli ndani ya Serikali ni vema kuangalia kwa mapena kuwa jambo hilo limesambaa kwa kiasi gani katika Wizara nyingine, huenda kila mtu amejipangia na kujichukulia, inatisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote, kwa kuwa Mheshimiwa Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu na *CAG* ni viongozi waliotumikia nchi hii kwa muda mrefu na wamefanya vizuri katika baadhi ya majukumu yao nashauri busara na hekima zitumike kuwapunguzia adhabu na mamlaka husika, hasa kama hili ni kosa lao la kwanza.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuchangia hoja ya Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naanza kwa kuipongeza Kamati Teule ya Bunge kwa kazi nzuri na makini iliyofanya kwa niaba yetu na Watanzania kwa ujumla. Napendekeza kwa sababu ya yote tuliyoletewa na Kamati Teule, kwanza Bunge kupitia Kamati ndogo ya Katiba na Sheria ipitie sheria zote za utumishi wa umma na kanuni ili kuboresha na kuondoa sheria na kanuni ambayo inaleta matatizo na kutokuwa na uwazi katika utendaji wa kazi. Sheria mpya iweke bayana na kwa uwazi, na adhabu kwa mtumishi atakayekiuka miiko na maadili ya kazi. Pia Sheria ya Fedha katika ofisi ya umma na taasisi ya umma zipelekwe kwa kutoa elimu kwa wananchi na watumishi na wakielewa vizuri haya matumizi mabaya hayatakuwepo. Pia sheria mpya ya kulinda wote katika maeneo mbalimbali watakaotoa ushahidi katika mambo ya usalama, ubadhirifu na matumizi mabaya ya ofisi za umma walindwe kwa nguvu zote.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza hatua kali za kinidhamu na za kisheria zichukuliwe dhidi ya wote waliokosea utaratibu na kusababisha hasara kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nashauri maoni ya Kamati ya kumwajibisha Waziri wa Nishati na Madini nitoe maoni yangu, siamaini kuwa ni sahihi kwa sababu sheria na kanuni hakukosea yeye, *Accounting Officer* ni Katibu Mkuu, watajiuzulu na kutolewa kafara wangapi? Bila kubadilisha mfumo mzima wa matumizi ya fedha na nidhamu katika kazi hatutasonga mbele.

Mheshimiwa Spika, pia pawe na uwazi katika masuala ya fedha za umma, isiwe siri, fedha za umma ziweze kukaguliwa na mtu yeyote kwa kufuata taratibu.

Mheshimiwa Spika, pia Bunge liazimie kuwa hatua kali zichukuliwe kwa mtumishi yeyote wa umma ngazi ya vijiji hadi Taifa kwa matumizi mabaya ya fedha, ofisi na kuleta hasara katika mali ya umma. Hii ndiyo njia pekee ya kurudisha imani ya Serikali kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani mbali na kutumia ofisi vibaya, kutumia fedha na mali ya umma vibaya hata kashfa yoyote katika masuala yake binafsi ya maisha hujiuzulu ili kuleta imani ya viongozi waadilifu katika Serikali na umma. Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Serikali, pia inabidi iangaliwe upya, wananchi watapoteza imani na ofisi hiyo *(CAG),* kwa sababu haikufanya kazi yake inavyopaswa basi walio husika wawajibike hii ndiyo fursa na Bunge liazimie na kuweka mkakati wa kuboresha mfumo wa utawala na fedha.

Mheshimiwa Spika, elimu kwa umma juu ya maadili ya viongozi iwe ni kipaumbele kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nieleze kuwa mimi ni mmoja wa Wabunge tuliohojiwa na vyombo vyote viwili kuhusu uhalali wa utaratibu wa Wizara ya Nishati na Madini kuchangisha fedha kwa ajili ya kupitisha Bajeti hiyo Bungeni. Tarehe 29 Julai, 2011 nilihojiwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na tarehe 19 Oktoba, 2011 nilihojiwa na Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mahojiano hayo, nimepitia taarifa na kuona kwamba imezingatia sehemu kubwa ya maoni niliyoyatoa. Hata hivyo, kuna suala moja ambalo Ofisi ya Ukaguzi na Kamati Teule ya Bunge haikulizingatia. Naomba kupitia mchango huu Bunge ilizingatie na Serikali ilitolee majibu suala hili ni rushwa ya kitaasisi *(institutional corruption)* pamoja na ukiukwaji wa sheria wenye sura ya jinai katika hatua mbalimbali na matumizi ya fedha zilizotokana na uchangishaji uliofanyika katika hatua zote nieleze suala la Wizara ya Nishati na Madini kutoa fedha kwa Wabunge wakati Bajeti ya Wizara husika ilipokuwa inajadiliwa katika hatua ya Kamati. Aidha, nilieleza kwamba kuna ufisadi wa kitaasisi katika ulipaji wa posho za semina na vikao. Taarifa ya Kamati Teule imedhihirisha jambo hilo katika Kiambatisho XVII ambacho kinaonyesha nyaraka za malipo ya posho zimeghushiwa.

Mheshimiwa Spika, pia kipengele cha 2.4 kuhusu uchunguzi, kuhusu matumizi halisi ya fedha zilizokusanywa umeonyesha kuwa bado kuna utata wa matumizi ya kiasi cha shilingi 126,044,480/=. Hivyo, Bunge liazimie kwamba vyombo vya dola hususani TAKUKURU na *DCI* wafanye uchunguzi wa masuala yote ya tuhuma za rushwa, kughushi na matumizi mabaya ya fedha makosa ambayo ni ya jinai.

Aidha, kabla ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 144, kwa kuwa Ibara ya 143(6) imemlinda na kumpa uhuru; apewe nafasi ya kurekebisha udhaifu wa kiutendaji aliouonyesha. Udhaifu huo wa kiutendaji unaashiria kwamba alikubali kupokea maagizo ya kulinda uozo toka kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Ushahidi wa kimazingira ni kwamba inaelekea kulikuwa na mazungumzo kati ya Luhanjo na Kaimu Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Ndugu Mshihiri tarehe 19 Julai, 2011 kabla ya Katibu Mkuu Kiongozi kuandika barua ya hadidu rejea ya tarehe 20 Julai, 2011 yenye Kumb. Na. *CAB/40/476/01.* Hivyo, *CAG* aagizwe na Bunge kuendelea na hatua ya ziada ya kufanya uchunguzi wa kijinai *(forensic audit)* kwa mujibu wa sheria ili aweze kupendekeza hatua nyingine.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii ya Kamati Teule imedhihirisha nilichoeleza Bungeni wakati wa kuchangia mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Bunge liazimie kumshauri Rais ambaye ni sehemu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba Ibara 62(1) ili aweze kuchukua hatua za kuisafisha Ofisi ya Rais ikiwemo Ikulu. Ukiondoa Katibu Mkuu Luhanjo, Kauli za watendaji wengine ikiwemo Msemaji wa Ikulu Salva Rweyemamu na watendaji wengine zinaonyesha uozo katika mfumo wa utawala. Rais atumie mamlaka yake kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 34, 35, 36 kutengua uteuzi wa watuhumiwa na kufanya mabadiliko Ofisi ya Rais, Ikulu na Baraza la Mawaziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kidogo na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Kwanza kabisa naomba niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ile Teule kwa kufanya kazi nzuri, nashukuru sana na kuja na taarifa nzito, ya kina na ndefu. Taarifa hii ina kurasa 150 na ina kiambatisho chenye kurasa 212 ni taarifa nzito na inahitaji tuitafakari kwa kina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema kwa niaba ya Serikali ni kwamba tunaipokea taarifa hii na tumeyachukua maoni yenu yote yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ni maoni mazuri yenye nia nzuri ya kujenga. Kwa sababu ya ukubwa na uzito wa taarifa hii, ni vigumu kuitolea majibu yote hapa hapa, ninachoweza kufanya ni kuipokea kama hivi tunavyoipokea na kama tulivyoipokea taarifa ile nyingine ya Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini kuhusu sekta ndogo ya gesi na yenyewe pia tutakapokuja katika Mkutano wa Sita, tunategemea kuleta majibu ya hoja zilizomo kwenye taarifa hizi na hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezitoa zote. Serikali tunaomba tuseme tutafanya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nisemee moja tu hili la uwajibikaji; majukumu ya Waziri akiwa Wizarani pale yanatajwa katika muongozo wa Baraza la Mawaziri lakini pia katika ile *GN* ambayo Rais anaitoa kwamba Waziri atakuwa na majukumu yafuatayo. Kwa hiyo, Waziri anafanya kazi zile ambazo zimo katika mfumo wa Serikali. Hayo yaliyomo ndani ya mfumo wa Serikali, lazima Waziri ayajue. Mambo yakifanywa nje ya mfumo wa Serikali ni vigumu kwa Waziri kuyajua, ni vigumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mambo yatafanywa ambayo hayamo katika utaratibu wa kawaida wa Serikali, yakafanywa na kiongozi mwingine ndani ya Wizara ile, Waziri hawezi kuyajua na si rahisi kwa Waziri kwenda kuchungulia kwenye *entries* za Makatibu Wakuu, Makamishna, Wakurugenzi na kadhalika, hawezi kufanya hivyo, sasa yale ambayo yamefanyika ndani ya mfumo wa Serikali na ya utaratibu wa kawaida wa Serikali Waziri anatakiwa kuwajibika, lakini yale ambayo kwa kweli yanafanywa nje ya utaratibu wa kawaida wa Serikali utamuonea Waziri yeyote yule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka kutoa *clarification* hiyo na kusema kwamba tumeipokea taarifa hii na nitawaomba Waheshimiwa Wabunge watupe nafasi na sisi kama Serikali tuipokee, tuichukue, tukaitafakari, tukaitafutie majibu, tukachukue zile hatua ambazo tunaweza kuzichukua kwa haraka kwa mambo ambayo ni dhahiri, yale mengine tutakuja kuwapa taarifa tumefanya nini na mengine tutawaambia tutayafanyia nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru tu kwa kunipa nafasi hii kwa niaba ya Serikali, nasema tunaipokea taarifa hii, tunawapongeza walioandika taarifa hii. Wameandika taarifa nzuri na sisi tunadhani yaliyomo humu yatatusaidia katika kufikia maamuzi ya haki kwa wahusika wote. Naomba sana nikushukuru. *(Makofi)*

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nitatumia muda mfupi iwezekanavyo ili niweze kutoa *summary* tu ya yale ambayo ni ya muhimu kabla sijafanya kile ambacho ni cha muhimu zaidi cha kutoa hoja baada ya mjadala ulioendelea, kufuatia taarifa ambayo nimeisoma mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Kwanza nakushukuru sana kwa namna ambavyo umeweza kulishughulikia suala zima hili kwa namna ambavyo umeweza kutufanya sisi Kamati Teule tuweze kulishughulikia suala hili hadi kufikia wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru pia kwa *support* ambayo umetupa katika kipindi chote ambacho tumefanya kazi hii kwa sababu ni kwa namna hiyo peke yake ndiyo tumeweza kumudu kukamilisha kazi hii kwa namna tulivyoifanya.

Nichukue pia nafasi hii kuweza kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia kama ifuatavyo: Nianze na wale waliochangia kwa njia ya maandishi Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa John Mnyika na Mheshimiwa Josephat Kandege. *(Makofi)*

Pia wafuatao wamechangia kwa kuongea nianze na Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Moses Machali, Mheshimiwa Ezekia Wenje, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Tundu Lissu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Godfrey Zambi. Kama kuna mtu nimemsahau, basi itakuwa *it's a slip of a pen*, lakini nafikiri nimeweza kuwakamilisha wote kwa utaratibu huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama ametokea mwingine aliyesahaulika naomba nae pia atambulike kama ni mtu ambaye ametoa mchango wake. Ooh! alitakiwa kuwa mwanzoni mwanzoni kabisa hapa Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaliyojitokeza kwa ujumla wakati Waheshimiwa Wabunge wanapata nafasi ya kuchangia ni mengi, lakini niseme tu yote kwa ujumla wake yalikuwa ni ya kuweza kuboresha mapendekezo ambayo yametolewa na Kamati Teule. Kimsingi mimi kwa upande wangu kama Mwenyekiti wa Kamati naweza kusema machache kama ifuatavyo; jambo kubwa kabisa ambalo limejitokeza katika taarifa ambayo tumeiweka mbele ya Bunge lako Tukufu, mimi naweza kusema kwa maoni yangu masuala mengi ni ya kisheria, lakini upande mwingine masuala haya ni ya uzalendo zaidi, tumefika mahali sasa tunatakiwa kuwa wazalendo zaidi ya vile tulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria ni upande mmoja tu, sheria zipo lakini sheria haziwezi ku-*address* kila kitu ambacho kimo ndani ya maisha, lakini hata kama utachukua sheria moja moja, hakuna sheria ambayo hata katika jambo hilo ambalo sheria hiyo ina *address* hakuna sheria ambayo inaweza ikafanya hivyo kwa ukamilifu, hivyo utakuta kwamba wakati mmoja au wakati mwingine unahitaji *either* kuandika sheria ambayo haipo ama unatakiwa kuiangalia upya sheria ambayo ipo kwa sababu ya mapungufu ambayo yatakuwepo, naambiwa hakuna neno mapungufu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, unafanya nini wakati ambapo una sheria ambayo haitoshelezi na inahitaji uboreshaji? Maisha hayasimami, maisha yanaendelea, sasa utafanya nini katika kipindi ambacho unasema sasa natakiwa kuiangalia upya sheria fulani? Utafanya nini katika kipindi ambacho una jambo mbele yako na unatakiwa ulishughulikie lakini hakuna sheria inayo *address* suala hilo? Ni dhahiri kwamba kuna wakati tutapaswa kutumia busara na hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hiyo au baada ya kusema hayo niseme kwamba nilitangulia kusema wakati nikiwa nawasilisha taarifa yangu au taarifa ya Kamati Teule nikasema kwamba na kwa kusisitiza kabisa nikasema kwamba maoni na mapendekezo ya Kamati Teule hasa yale mapendekezo yatazingatia zaidi utawala wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeseme hivyo kwa sababu maeneo mengi na hata baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliosimama hapa wamesisitiza au wamesikitishwa sana na maeneo ambayo baadhi ya watendaji wameonekana kabisa kutotii sheria. Lakini pia hata katika kushughulikia masuala ya msingi na masuala muhimu, mahali pengi sana tunakiuka hata sheria ambazo zipo na hata kama zina *address* vizuri masuala hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Kamati Teule haikuona kama ni busara na yenyewe ika- *address* au ikatoa maoni yake na mapendekezo hayo kwa kukiuka sheria zilizopo. Basi naomba nirejee tena kusema kwamba Kamati Teule inapokea mapendekezo na maoni yote ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge ili kuboresha mapendekezo yake, lakini mapendekezo hayo kama yalivyoorodheshwa kwenye *report* yetu au kwenye taarifa yetu kama Kamati Teule, nayo pia na mimi niungane kabisa na Waheshimiwa Wabunge waliosema kwa umakini mkubwa kwamba sasa tunaitaka Serikali, licha ya kuchukua au kuyapokea na kusema itayazingatia maoni haya na mapendekezo haya basi Serikali ifanye hivyo kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi pamoja na Wanakamati wenzangu na Waheshimiwa Wabunge nimesikia wakisema kwa msisitizo kabisa kwamba Bunge lijalo, tukija hapa basi tuje tukiwa tunategemea kuja kupata utekelezaji wa mapendekezo kama yalivyoorodheshwa na kama yalivyoboreshwa na wachangiaji, Waheshimiwa Wabunge wakati wa mjadala ulioisha hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mnataka msiunge mkono?

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, naomba Bunge liazimie mapendekezo yaliyomo kwenye taarifa hii ili yaweze kufanyiwa kazi na Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mnyika. Naomba mchukue vitabu hivyo na ninaambiwa wengine hawakupata, Katibu ona wanapata. *(Makofi)*

## Mapaendekezo ya Mabadiliko ya Hoja

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja, naomba sasa Bunge lijadili mapendekezo ya mabadiliko ya hoja kwa mujibu wa Kanuni 57(1, 2) na Kanuni ya 119(4) ili kuongezea maneno yafuatayo kwenye maazimio.

Mheshimiwa Spika, kwanza katika ukurasa wa 145 wa mapendekezo ya Kamati, kwenye aya ya tatu, kwenye mchango wangu na michango ya Waheshimiwa Wabunge wengine, Wabunge wamerejea nyuma kwenye uchambuzi wa Kamati kuhusiana na kupitia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu uchunguzi uliyofanyika na taarifa hii kama ambavyo Kamati imeipitia kwenye ukurasa wa 32 kuna kifungu kinazungumza uchunguzi kuhusu matumizi halisi ya fedha zilizokusanywa.

Mheshimiwa Spika, ukiruka ukurusa wa 32 ukienda ukurasa wa 38 inaonyesha kwamba katika ukokotoaji wa matumizi kuna kiwango cha shilingi milioni 126 ambacho matumizi yake hayakuweza kubainika. Kamati ikaitaka Serikali ama Wizara husika ijieleze kwa maandishi kuhusu matumizi hayo, Wizara ikaeleza kwenye ukurasa wa 38 kwa sababu ya muda nisingependa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba ninukuu ukurasa wa 39 baada ya Kamati kupokea maelezo ya Wizara, ikaonekana hata hivyo maelezo yaliyotolewa na Mkurugenzi, kwa maana ya Mkurugenzi wa Wizara, hayakukubaliwa na Kamati Teule, hakukuwa na mchanganuo wowote wa matumizi wa nyaraka za uthibitisho wa malipo wa hizo pesa shilingi milioni 126, lakini pili kuna kitu kikubwa zaidi kiasi cha shilingi milioni 50 kilichoonyeshwa katika matumizi ya kurekebisha na kuwasilisha randama inaendelea kama ilivyoonyeshwa, kimeonyeshwa mara mbili matumizi yale yale. Kwa hiyo, ni *double accounting*, sasa *double accounting* kiuhasibu ni kosa kubwa sana kiuhasibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa ajili ya kushughulikia jambo hili, napendekeza baada ya aya ya tatu kwenye ukurasa wa 145, kuongezewe aya nyingine iwe na maneno yafuatayo:-

*"Pia Serikali ichukue hatua zaidi juu ya matumizi ya shilingi milioni 126,044,480 ambazo Kamati Teule imekataa maelezo yake, ikiwemo kuagiza kufanyika kwa ukaguzi wa kiuchunguzi (forensic audit)".*

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili litazingatia vilevile Sheria ya *Audit* ambayo inataka popote pale penye kuonyesha mashaka ya kijinai ama mashaka ya sura nyingine, Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kabisa kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi kwa maana ya *forensic audit* ili hatua za ziada ziweze kuchukuliwa. Hii itasaidia kwa hatua za msingi kuweza kuchukuliwa kama ambavyo binafsi nimependekeza na Wabunge wengine wamependekeza.

Mheshimiwa Spika, lakini pendekezo lingine la pili linahusu ukurasa wa 148, kwenye aya ya kwanza, Kamati Teule inapendekeza Bunge lijadiliane na Serikali kuhusu namna bora ya kuendesha Semina kwa Wabunge ikiwemo kutenga kasma mahsusi ndani ya Mfuko wa Bunge na kusisitiza uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika matumizi ya fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa ukirudi nyuma kwenye maelezo ya Kamati, kwenye kifungu cha saba ambacho kinahusu mambo mengine yenye uhusiano, kifungu cha 7.4 ambacho kimerejewa na ukurasa wa 120 wa Ripoti ya Kamati, kinazungumzia kuhusu uchangishaji wa shilingi milioni 22 kwa taasisi nne chini ya Wizara ya Nishati na Madini kwa ajili ya Semina ya Wabunge. Baada ya hapo kuna maelezo ambayo sitayanukuu kwa *interest* ya *time,* yapo ukurasa wa 121, 122 mpaka ukurasa wa 123 ambayo kwa muhtasari yanasema kwamba viwango vya posho ambavyo Bunge liliidhinisha watumishi wake walipwe, vikatajwa pale kwenye ukurasa wa 121 kwamba ni shilingi 20,000, shilingi 50,000 na shilingi 80,000 kulingana na ngazi ya mtu. Lakini ukurasa wa 122, Kamati imebaini na ushahidi uko bayana kabisa kwenye kabrasha hili la vielelezo kwamba tofauti na maelezo, wakati watu wamelipwa kwa mujibu wa maelekezo, *accounting* iliyofanyika *(retirement)* inaonyesha kwamba wa shilingi 20,000 wamelipwa shilingi laki moja na ishirini, wa shilingi themanini wamelipwa shilingi laki na themani. Kwa hiyo, maana yake kuna mtu hapo katikati baada ya watu kuwa wameshalipwa kiwango kidogo akaghushi *form* za malipo hapo katikati, akaongezea *figures* na akaweza kujinufaisha ambapo kimsingi ni ufisadi.

Mheshimiwa Spika, sasa pendekezo ambalo nalitoa *in a spirit* ya mchango wangu wa maandishi na mchango wa Waheshimiwa Wabunge wengine ili Serikali iweze kuchukua hatua zinazostahili, ukiondoa pendekezo la Kamati ambalo naliunga mkono, chini ya Azimio hilo la ukurasa wa 148, aya ya kwanza yaongezwe maneno yafuatayo:-

*"Aidha, Serikali iagize Vyombo vya Dola kufanya uchunguzi juu ya tuhuma za kughushi na ubadhirifu zilizoelezwa ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa kwa watakaobainika".*

Mheshimiwa Spika, tafsiri ya kifungu hiki sasa itaruhusu moja kwa moja Serikali kuagiza kama ni TAKUKURU, kama ni Ofisi ya *DCI* kupitia hivi vielelezo ambavyo tayari Kamati ya Bunge ilishavifanyia kazi na imebaini uozo na hatua zikachukuliwa kwa wote waliohusika na ufisadi huo.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba mabadiliko hayo yafanyike sambamba na Maazimio mengine ambayo yameshapendekezwa na Kamati.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Sawa! Sisi tulikuwa tunaangalia pendekezo la kwanza linalosema, pia Serikali ichukue hatua zaidi, hizi karatasi mnazo Waheshimiwa, juu ya matumizi ya shilingi milioni 126 ambayo Kamati Teule imekataa maelezo yake ikiwemo kuagiza kufanyika kwa ukaguzi wa kiuchunguzi *(forensic audit).* Halafu tuendelee palepale, aidha, Serikali iagize Vyombo vya Dola kufanya uchunguzi juu ya tuhuma za kughushi na ubadhirifu zilizoelezwa ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa kama ilivyoelekezwa. Tunasema hii yote ikae pamoja, uchunguzi ule wa *Controller* lakini pia na hii *forensic audit*, huna sababu ya kusambaza kwa sababu ukiangalia mapendekezo ya hawa siyo *clustered*, kwa hiyo, unaweza kuyaweka pamoja yakaingia vizuri.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, sina tatizo na haya mapendekezo kuwekwa pamoja isipokuwa itabidi sasa lile Azimio la Pili liwekwe maneno matumizi ya shilingi milioni 88 ya Semina ya Wabunge. Kwa sababu hizi shilingi milioni 126 za juu, ni za matumizi tofauti na ni kesi tofauti na hii ya chini ya kughushi ya shilingi milioni 88 zilizokuwa zimechangishwa kwa ajili ya Semina ya Wabunge. Kwa hiyo, hili Azimio la chini sasa ili liweze kuwa *into context,* liongezwe hayo maneno ninayoyazungumza la sivyo likikaa kule litahusiana moja kwa moja na semina. Ikiwekwa upande mwingine, itabidi kuwe na maneno yanayohusisha na shilingi milioni 88 za Semina ya Wabunge.

**SPIKA:** Kwa maana hiyo hiyo ndiyo tunachosema usiwa-*limit* hawa, tunachosema kughushi *let them go further*, tusiwa-*limit* kwa shilingi milioni 88 tu. Neno kughushi *is a more serious thing* kuliko kitu chochote kile.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mabadiliko ya Mapendekezo ya Kamati Teule kuongeza maneno yaliyoletwa na Mheshimiwa John J. Mnyika yalikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, maneno haya yataingia ramsi katika mapendekezo ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli za Kamati zimekwisha na kama tulivyoagiza, tuhakikishe Serikali inayachukulia haya mambo kwa uzito. Hii ni Kamati Teule ya kwanza na kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge, wajibu wa Bunge hili ni kuhakikisha tunaiangalia Serikali kwa undani sana. Hii ni *transition,* yaani tuko kwenye *transition*, kwa hiyo, Wabunge ni lazima wafanye kazi yao vizuri. Kwa hiyo, hii haitakuwa ya kwanza, zitakuwepo nyingi na wala siyo moja. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi ninachoomba kwa upande wa Serikali, jiangalieni wenyewe kwanza. Hata kama kutakuwa na mambo mengine lakini angalau yale mnayoyaona waziwazi yawe yamekwisha. Kwa maana hiyo basi nasema Kamati hizi zitaendelea kuwepo nyingi. Nyie mnajua watu sasa wanashiriki sana kuweza kusaidia Bunge letu lifanye kufanya kazi vizuri.

Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Kamati Teule kama mnaiafiki au vipi.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, wote tumeafiki na mapendekezo ya Kamati yamekubaliwa. *(Makofi)*

**KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizopangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Tano wa Bunge kama zilivyokuwa zimeainishwa katika Kitabu cha Shughuli za Bunge, zimekamilika.

**KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika**,** kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu**,** Mwingi wa Rehema kwa kutufikisha salama siku ya leo tunapohitimisha Mkutano wa Tano wa Bunge lako Tukufu ulioanza tarehe 8 Novemba, 2011. Tuna kila sababu ya kumshukuru kwa kuwa tumetekeleza majukumu yote yaliyopangwa kwenye ratiba kwa amani, utulivu na ufanisi mkubwa. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuwa, kwa pamoja tumefanikisha Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** napenda nitumie nafasi hii ya mwanzo kabisa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge mpya wa Jimbo la Igunga, kwa kura nyingi kupitia Chama cha Mapinduzi katika Uchaguzi Mdogo uliofanyika tarehe 2 Oktoba, 2011. Kuchaguliwa kwake, kunadhihirisha imani kubwa waliyonayo wananchi wa Igunga kwake na kwa Chama cha Mapinduzi. Vilevile, kunadhihirisha kwamba Chama cha Mapinduzi bado ni Chama imara, Chama cha wakulima na wafanyakazi na Chama chenye mvuto mkubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Mohammed Said Mohammed, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Muungano kupitia Baraza la Wawakilishi la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu tulipohitimisha Mkutano wa Nne wa Bunge lako Tukufu, kumekuwa na matukio mbalimbali yaliyosababisha majeruhi na kupoteza maisha ya ndugu, jamaa na marafiki zetu. Napenda kutumia nafasi hii kuwapa pole wote walioathirika kwa namna moja au nyingine kutokana na matukio hayo. Aidha, kwa wale waliopoteza maisha, namwomba Mwenyezi Mungu aziweke Roho za Marehemu wote mahali pema peponi, Amen.

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kutumia nafasi hii pia kuwatakia kheri Waheshimiwa Wabunge wote ambao katika kipindi hiki wamepata misukosuko ya maradhi na baadhi yao bado wako hospitalini ndani na nje ya nchi kwa matibabu. Napenda kuungana na familia zao kumwomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka na awape nguvu ya kurejea katika afya zao ili waweze kujiunga na familia, wapiga kura wao na Watanzania wote kwa ujumla katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Tano, jumla ya Maswali ya Msingi 123 na ya Nyongeza 289 yalijibiwa na Serikali. Aidha, Maswali nane (8) ya Msingi na matano (5) ya Nyongeza yalijibiwa kwa utaratibu wa Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili Miswada ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2011 *(The Public Procurement Act, 2011)*; na

(ii) Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2011 *(The Constitutional Review Act, 2011).*

Mheshimiwa Spika, vilevile, katika Mkutano huu, zilitolewa Taarifa mbili ambazo ni Taarifa ya Kamati ya Nishati na Madini juu ya Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi Nchini na Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu pia, Serikali ilitoa Tamko kuhusu Fujo na Vurugu zilizojitokeza hivi karibuni katika Mikoa ya Mbeya na Tabora.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote walioshiriki katika Mijadala ya Miswada na Taarifa hizo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba aliyoitoa jana tarehe 18 Novemba, 2011 katika Ukumbi wa Karume, Viwanja vya Mwalimu Nyerere - Barabara ya Kilwa, Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais amefafanua kwa kina maeneo muhimu yanayohusu mwenendo wa uchumi katika nchi yetu, hususan mfumuko wa bei, kushuka kwa thamani ya shilingi na kupanda kwa bei ya mafuta na chakula katika Soko la Dunia. Vilevile, alielezea vizuri sana suala la matumizi ya fedha za kigeni katika ununuzi wa bidhaa na huduma mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Rais, suala la mdororo wa kiuchumi uliopo na kupanda kwa bei ya mafuta na chakula katika Soko la Dunia kumeathiri siyo Tanzania pekee, bali nchi nyingi Duniani zikiwemo za Ulaya na Afrika na hata jirani zetu. Ili kupata uelewa mpana kuhusu suala hili, tumekubaliana kwamba Gavana wa Benki Kuu ataandaa Semina kuhusu masuala hayo itakayofanyika wakati wa Mkutano wa Sita wa Bunge ambapo tutapata fursa ya kujadili kwa kina hali ilivyo ya mwenendo wa viashiria vya uchumi wa nchi yetu, athari zake na hatua zinazochukuliwa na Serikali.

Aidha, Serikali imedhamiria vilevile kuandaa Semina nyingine mbili na kama tutapata muda katika Bunge lijalo ili tuweze kujadili vilevile suala la utaratibu mpya wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja kwa kutumia meli za mafuta zenye uwezo mkuwa wa ujazo. Semina hii tunatarajia iwasilishwe na *EWURA* pamoja na *TPDC*.

Aidha, tunatarajia vilevile kuwa na Semina nyingine kuhusu hali ya nishati ya umeme nchini chini ya *TANESCO* na Wizara inayohusika kwa ujumla. Maeneo haya tumeona ni vizuri yakaunganishwa kwa kuwa yana uhusiano wa karibu sana na taarifa aliyoitoa Mheshimiwa Rais kuhusu hali ya uchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake, Mheshimiwa Rais alizungumzia pia kwa kina mchakato wa maandalizi ya mabadiliko ya Katiba ambapo Bunge lako Tukufu limepitisha Muswada wa Sheria wa Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 jana tarehe 18 Novemba, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kwa dhati kabisa, kuwa maelezo yale ya Mheshimiwa Rais yatatoa majibu sahihi na uelewa wa pamoja kwa Watanzania wenzangu kuhusu mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Uelewa huo wa pamoja, kwa maoni yangu, utatuwezesha Watanzania wote kujiandaa na kushiriki kwenye hatua zinazofuata katika mchakato huo kwa utulivu, amani, umoja na mshikamano.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kukushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika, kwa jinsi ulivyoongoza mjadala huu. Nawashukuru pia Wenyeviti wa Bunge kwa jinsi walivyosimamia na kuongoza mjadala pale ulipojadiliwa.

Mheshimiwa Spika, Muswada tulioupitisha ulisimamiwa kwa umahiri mkubwa na Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge. Kwa moyo wa dhati, naishukuru Kamati kwa kazi nzuri ya kuchambua na kutoa ushauri kwa Serikali na hivyo kuonesha njia iliyo bora katika kutekeleza jukumu hili muhimu tulilohitimisha jana.

Mheshimiwa Spika, kipekee, ninawashukuru Mheshimiwa Pindi Chana, Mbunge na Mwenyekiti wa Kamati na Mheshimiwa Angellah Kairuki, Mbunge na Makamu Mwenyekiti wa Kamati, kwa kuongoza na kusimamia mjadala wa kuandaa Muswada uliopitishwa jana na Bunge lako Tukufu. Hawa wote ni kina mama, kumbe akinana mama wakipewa nafasi wanaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii, kuishukuru kwa moyo wa dhati kabisa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa ushirikiano mkubwa iliyoutoa wakati wote wa mjadala huu kuhusu Muswada uliopitishwa jana.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, Mbunge wa Ulanga Mashariki na Waziri wa Katiba na Sheria; na Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kipindi chote cha maandalizi na majadiliano ya Muswada huo. Nawashukuru pia Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa utaalam na ushirikiano mkubwa waliouonesha ambao uliwawezesha Viongozi hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, Muswada huo ulipitiwa pia na Wasomi, Wanataaluma, Makundi mbalimbali ya Jamii na Wadau wengi ambao siyo rahisi kuwataja wote hapa. Itoshe tu kusema, Serikali inawapongeza Wadau wote kila mmoja kwa nafasi yake kwa namna walivyoshiriki katika kufanikisha mjadala wa Muswada uliopitishwa na Bunge lako Tukufu jana.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wao wameandika historia mpya katika kulitumikia Taifa letu kwa kufanikisha hatua ya mwanzo na ambayo ninaamini ilikuwa ngumu katika kuelekea uundaji wa Katiba Mpya. Katiba ambayo kama alivyosema Mheshimiwa Rais, itaendana na mafanikio na changamoto za miaka 50 ya Uhuru, miaka 47 ya Mapinduzi ya Zanzibar, miaka 47 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ambayo italipeleka Taifa letu miaka 50 mingine ijayo kwa utulivu, amani, umoja na mshikamano. Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kazi kubwa mliyoifanya katika kujadili Muswada huo na hatimaye kuupitisha. Kazi tuliyonayo mbele yetu sasa ni kutekeleza yale ambayo Mheshimiwa Rais ameyaelekeza kwa Watanzania wote kushiriki kikamilifu katika hatua zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwaomba Watanzania wote kwamba sasa tuungane kwa pamoja kutekeleza hatua itakayofuata ambayo ni kutoa maoni yetu kwa Tume itakayoundwa na Waheshimiwa Marais wetu wa pande zote mbili – Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, nawaomba Viongozi na Wanachama wa Vyama vyote vya Siasa kupongeza hatua iliyofikiwa na kukubali Muswada huu ambao tayari umepitishwa kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wito wangu kwa wananchi wote ikiwa ni pamoja na Vyama vya Siasa, ni kuungana kwa pamoja katika hatua muhimu inayokuja ambayo itahusisha Watanzania wote ya kutoa maoni ya Katiba tunayoitaka. Nawasihi Watanzania wenzangu kuzingatia yale yote aliyotuasa Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ili hatua zote kuelekea kuandika Katiba Mpya zifanyike kwa amani na utulivu. Kwa pamoja tutaweza kufikia lengo tulilojiwekea na kuandika historia mpya ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa ikikabiliwa na hali ya ukame wa mara kwa mara na kwa muda mrefu, hususan tangu mwaka 2006. Hali hii imesababisha upungufu wa chakula katika baadhi ya Mikoa ambayo imekuwa ikiathirika zaidi na ukame. Hata hivyo, chakula ambacho kimekuwa kinazalishwa katika maeneo yenye mvua za kutosha, kimewezesha nchi yetu kuendelea kujitosheleza kwa chakula, kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, katika mwaka 2010/2011 uzalishaji wa mazao ya chakula unakadiriwa kufikia tani milioni 12.81 ikilinganishwa na mahitaji ya jumla ya tani milioni 11.50 za chakula kwa mwaka 2011/2012. Uzalishaji huu unatosheleza mahitaji ya chakula kwa asilimia 111, sawa na ziada ya tani milioni 1.31. Ziada hiyo kwa kiasi kikubwa inatokana na mazao yasiyo ya nafaka. Hivyo, uhaba wa nafaka ni kiasi cha tani 410,000 nchini kote na upungufu huo wa nafaka upo zaidi kwenye baadhi ya Mikoa inayokabiliwa na ukame.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya kina ya hali ya Chakula na Lishe Nchini iliyofanywa mwezi Agosti na Septemba, 2011, inaonesha kuwepo kwa jumla ya watu 1,062,516 katika Wilaya 52 za Mikoa 15 wanaokabiliwa na upungufu wa chakula (*Acute Food Insecurity)* kwa viwango mbalimbali. Wananchi hao wanahitaji tani 38,843 za chakula cha msaada kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Oktoba hadi Desemba 2011. Hadi tarehe 31 Oktoba 2011, jumla ya tani 13,905 za chakula zilikuwa zimechukuliwa kutoka Maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* na kusambazwa katika maeneo hayo yenye uhaba wa chakula na kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihadi za Serikali za kupeleka chakula cha msaada katika maeneo yenye upungufu wa chakula, natoa wito kwa wananchi kwenye maeneo yaliyo na upungufu wa chakula kutumia mvua kidogo zinazonyesha nchini hivi sasa kulima mazao yanayostahimili ukame kama vile mtama, viazi na mihogo ili kujiongezea chakula.

Mheshimiwa Spika, Serikali inazingatia kuhakikisha kunawepo na akiba ya kutosha ya chakula kwa ajili ya kukabiliana na upungufu wa chakula nchini. Hadi tarehe 30 Juni 2011, Wakala wa Hifadhi ya Taifa ya Chakula *(NFRA)* ulikuwa na akiba ya tani 154,506 za mahindi na tani 1.96 za mtama. Wakala umelenga kununua tani 200,000 za mahindi katika kipindi cha msimu wa mwaka 2011/2012. Hadi kufikia tarehe 30 Oktoba 2011, Wakala ulikuwa umenunua jumla ya tani 114,117 kutoka Mikoa iliyozalisha ziada hasa ya Nyanda za Juu Kusini. Katika kipindi hicho, jumla ya tani 49,792 za mahindi zilikuwa zimepelekwa kwenye Mikoa yenye upungufu wa chakula inayohudumiwa na Maghala ya Wakala yaliyopo Arusha, Shinyanga na Dodoma na kazi hiyo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kununua, kuhifadhi na kusafirisha mahindi kutoka maeneo yenye ziada kwenda maeneo yenye upungufu, linakabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa bajeti, uwezo mdogo wa kuhifadhi nafaka zinazonunuliwa na kasi ndogo ya kusafirisha mahindi kutoka katika maeneo yenye ziada kwenda kwenye maeneo yenye upungufu.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyotengwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha 2011/2012 kwa ajili ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA)* haitoshi kutekeleza malengo ya Wakala. Kati ya tani 114,117 za mahindi ambazo zimepokelewa katika Vituo vya Ununuzi, Wakala umeweza kulipia tani 80,615 tu na kushindwa kulipia tani 33,492 zilizopokelewa. Kufikia tarehe 30 Oktoba 2011, Wakala ulikuwa unadaiwa jumla ya Shilingi Bilioni 13.62 na wakulima waliouza mahindi yanayohifadhiwa na Wakala katika Vituo vya Makambako, Songea na Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeiruhusu *NFRA* kukopa Shilingi Bilioni 20 kutoka katika Mabenki ya Biashara Nchini na mazungumzo na Mabenki hayo yanaendelea. Pamoja na hatua hiyo, Serikali pia imeiruhusu *NFRA* kuuza mahindi tani 50,000 kwa Shirika la Chakula Duniani *(WFP)*, ambapo tayari tani 10,000 zimenunuliwa. Pia *NFRA* imeruhusiwa kuuza tani 40,000 kwa Wafanyabiashara Binafsi hatua ambayo sasa inaendelea chini ya Wizara ya Kilimo. Hatua hizi zitawezesha Wakala kulipia madeni ya wakulima, kuendelea na ununuzi, uhifadhi na usafirishaji wa mahindi kwenda katika maeneo yenye upungufu wa chakula.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kasi ya kusafirisha mahindi, Serikali inaangalia uwezekano wa kuiwezesha Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* kuongeza kasi ya kusomba mahindi kutoka kwenye Maghala ya Sumbawanga na Mpanda kwenda Shinyanga. Aidha, Serikali inaangalia uwezekano wa kutumia magari ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania *(JWTZ)* katika usafirishaji wa mazao haya. Ni imani ya Serikali kuwa jitihada hizi zitasaidia kukabiliana na uhaba wa chakula kwenye maeneo yenye ukame.

Mheshimiwa Spika, ili nchi yetu ijitosheleze katika Chakula na Lishe na kuongeza kipato katika Kaya pamoja na kukuza uchumi wa nchi, Tanzania inatekeleza Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo na Usalama wa Chakula yaani *"Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan"* (*TAFSIP*). Huu ni Mpango wa Miaka 10 kuanzia mwaka 2011/2012 hadi 2020/2021 ambao unawaleta pamoja Wadau wote katika Sekta pana ya Kilimo Tanzania Bara na Visiwani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Mpango huu utaiwezesha Sekta ya Kilimo kukua kwa asilimia sita (6%) au zaidi kwa mwaka. Katika kufanikisha mpango huu, Serikali imeridhia kuongeza bajeti ya kilimo hadi kufikia asilimia kumi (10%) kwa kuzingatia utekelezaji wa Azimio la Maputo la mwaka 2003 ambapo Wakuu wa Nchi za Afrika ikiwemo Tanzania walikubaliana kuwa kila nchi itaongeza bajeti yake katika Sekta ya Kilimo angalau kufikia asilimia kumi (10%) ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wadau mbalimbali walishiriki kuandaa Mpango huu ikiwa ni pamoja na Taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi, Wadau wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi, Wanataaluma mbalimbali, Jumuiya za Uchumi za Kikanda, Umoja wa Afrika, Ubia Mpya wa Maendeleo ya Afrika (*New Partnership for Africa's Development-NEPAD)* na Programu ya Kuendeleza Kilimo Barani Afrika (*Comprehensive Africa Agriculture Development Programme-CAADP*). Aidha, mchakato wa kutengeneza Mpango huu ulihusisha mikutano mbalimbali ya kukusanya maoni katika Kanda zote Tanzania Bara na Visiwani ambapo wadau mbalimbali walipata nafasi ya kuchangia katika uundwaji wa Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Serikali, Wadau wa Maendeleo wa ndani na nje ya nchi, Sekta Binafsi, Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)*, Jumuiya za Uchumi za Kikanda na Wakulima wadogo kwa wakubwa, watashiriki katika utekelezaji wa Mpango huu. Katika kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016, Mpango huu unategemea kutumia kiasi cha Shilingi Trilioni 8.75, sawa na wastani wa shilingi trilioni 1.7 kwa mwaka. Uwekezaji huo utakuwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuongeza uzalishaji, tija na Kilimo cha Kibiashara (Shilingi Trilioni 6.22);

(ii) Kutekeleza Mipango ya Umwagiliaji na Matumizi Bora na Endelevu ya Ardhi na Maji (Shilingi Trilioni 1.2);

(iii) Kufanya Maboresho ya Sera na kujenga uwezo wa Taasisi mbalimbali (Shilingi Bilioni 681.13);

(iv) Kuendeleza Miundombinu ya Vijijini, Masoko na Biashara (Shilingi Bilioni 357.26);

(v) Kuwezesha kufikiwa kwa Usalama wa Chakula na Lishe (Shilingi Bilioni 211.4);

(vi) Kukabiliana na mabadiliko ya Tabia Nchi na Majanga ya Asili (Shilingi Bilioni 66.31); na

(vii) Kuendeleza Sekta Binafsi (Shilingi Bilioni 15.56).

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Mkutano wa Kazi (*Business Meeting*) kwa ajili ya Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo *(TAFSIP)* ulifanyika tarehe 10 – 11 Novemba, 2011, katika Hoteli ya Blue Pearl, Dar es Salaam. Mkutano huo uliongozwa na Mheshimiwa Dokta Mohammed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hapo tarehe 10 Novemba, 2011 na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 11 Novemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huo ulihudhuriwa na Wadau mbalimbali toka Wizara na Taasisi za Serikali, Taasisi za Wakulima, Sekta Binafsi, Mashirika ya Kiraia na Wabia wa Maendeleo. Katika Mkutano huo, makubaliano yalifikiwa kuhusu maeneo ya kipaumbele ya Mpango, gharama za Mpango na Ratiba ya utekelezaji wake. Katika Mpango huu, mbinu na msukumo mpya kupitia uratibu, ukusanyaji wa rasilimali na ushirikishaji wa Sekta Binafsi, vitatumika katika kuongeza kasi katika utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini (*Agricultural Sector Development Programme – ASDP*) pamoja na Miradi na Programu mbalimbali zinazoendelea kutekelezwa katika Sekta ya Kilimo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo katika utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini *(ASDP)* kwa upande wa Tanzania Bara na Mpango wa Sekta ya Kilimo *(ASP)* kwa upande wa Tanzania Zanzibar. Utekelezaji wa Programu hii utahusisha kwa karibu Mipango ya Maendeleo ya Wilaya kama ilivyo sasa. Ni matumaini ya Serikali kwamba utekelezaji wa Mpango huu utaiwezesha Sekta ya Kilimo kuchangia katika ukuaji wa uchumi nchini, kuongeza pato la mkulima na kuhakikisha kwamba Taifa linajitosheleza kwa Chakula na Lishe na kuongeza ajira hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya maandalizi muhimu ya msimu wa kilimo wa mwaka 2011/2012 ambapo imejikita katika upatikanaji na usambazaji wa mbolea na mbegu, maandalizi ya Vocha kwa ajili ya Pembejeo za Ruzuku na upatikanaji wa Madawa ya Kudhibiti uharibifu wa Mazao.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mbolea nchini yanakadiriwa kufikia tani 400,000 kwa mwaka. Hadi kufikia tarehe 3 Novemba 2011, jumla ya tani 246,454 za mbolea, sawa na asilimia 61.6 ya mahitaji zilikuwa zimesambazwa katika Mikoa mbalimbali nchini. Kati ya hizo, tani 81,294 ni mbolea ya kupandia ambayo inatosheleza mahitaji ya wakulima wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na Mikoa ya Kigoma, Kagera, Manyara na Mwanza ambayo wakulima huanza kupanda mwezi Novemba kila mwaka. Kwa wakulima wa Mikoa inayopanda mwezi Januari na Februari kila mwaka, tani 129,711 za mbolea ya kupandia zitakazotumika katika Mikoa hiyo zinatarajiwa kupatikana kabla ya mwisho wa mwezi Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya mbegu bora za Nafaka na Mikunde nchini yanakadiriwa kufikia tani 30,000 kwa mwaka. Hadi tarehe 3 Novemba 2011, jumla ya tani 23,437, sawa na asilimia 78 ya mahitaji zilikuwa zimesambazwa katika Mikoa mbalimbali nchini. Kiasi cha mbegu kilichopo kinatosheleza mahitaji ya wakulima wanaopanda mazao hayo katika mwezi wa Novemba kila Mwaka. Aidha, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika inaendelea kuwasiliana na Makampuni ya Mbegu ili kiasi cha mbegu kilichobaki kipatikane kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika msimu wa kilimo wa mwaka 2011/2012, jumla ya tani 18,157 za mbegu bora za mazao ya mpunga na mahindi zitasambazwa kwa wakulima kwa utaratibu wa Vocha. Vilevile, tani 180,000 za mbolea ya kupandia na kukuzia mazao hayo, zitasambazwa kwa utaratibu huohuo kwa wakulima 1,800,000. Mapendekezo ya mgawanyo wa vocha katika Mikoa 20 na Wilaya 96 zinazohusika na ruzuku hiyo, yamekamilika na wahusika wameshapatiwa taarifa.

Vilevile, ruzuku ya mbegu bora za mtama kiasi cha tani 356 zitatolewa kwa wakulima 127,300 wa Mikoa yenye ukame ya Singida, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Dodoma na Mara. Pia, ruzuku ya mbegu bora za zao la alizeti, kiasi cha tani 50 zitatolewa kwa wakulima 10,392 wa Mikoa ya Singida na Shinyanga. Jumla ya vocha 5,400,000 zitasambazwa katika Mikoa 20.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa hii, naomba nitumie fursa hii kutoa Taarifa ya Upatikanaji na Usambazaji wa Mbegu za Pamba kwa Msimu wa 2011/2012. Hadi kufikia tarehe 16 Novemba, 2011, tani 15,000 za mbegu za Pamba zimesambazwa Vijijini, kati ya tani 20,000 zilizopangwa kusambazwa msimu huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali hii, limejitokeza kundi la Walanguzi wa mbegu za Pamba katika Wilaya za Bariadi, Maswa, Magu, Meatu na Kishapu ambao wanapita Vijijini wakinunua mbegu za Pamba walizosambaziwa wakulima hasa wakulima wadogo kwa kuwapa bei kubwa ili kununua mbegu hizo na baadaye kuuza kwa bei kubwa kwa watu wenye uwezo zaidi. Kwa kuwa mkulima akishauza mbegu zake hawezi kupata mbegu zingine tena; jambo hili ni la hatari sana kwa wakulima, zao la Pamba na uchumi wa Taifa. Aidha, kwa mkulima mwenyewe, kuuza mbegu yake ya pamba ni kujiua yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, mbinu nyingine inayotumika ni kwa Walanguzi wa mbegu na baadhi ya viongozi kupanga watu wengi katika vituo vya kununulia mbegu wakijifanya kuwa ni wakulima, kumbe lengo lao ni kuwakusanyia mbegu nyingi ili waiuze kwa bei kubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea majina ya Walanguzi wengi wa mbegu katika Wilaya za Meatu, Bukombe, Bariadi, Bunda, Magu na Kishapu na operesheni ya kuwakamata inaendelea. Hivyo, Serikali inawatahadharisha wote wanaoshiriki katika hujuma hii, kuacha mara moja. Hatua kali za Kisheria zitachukuliwa kwa wote wanaouza na wale wanaonunua mbegu za Pamba kinyume cha Sheria. Vyombo vya Dola hasa Polisi wameagizwa kuwafikisha Mahakamani mara moja wale wote, baada ya uchunguzi, watakaobainika kuwa wanahusika na zoezi hilo. Tunachoomba ni ushirikiano wa karibu kutoka kwa Watanzania hasa wanaolima zao la Pamba, kushirikiana na Polisi kutoa taarifa za ukweli juu ya jambo hili ili tuweze kudhibiti wimbi hili la ulangauzi ambalo kwa kweli lengo lake ni kuwaumiza wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, hadi tarehe 3 Novemba, 2011, tayari lita 3,072 za Madawa ya kudhibiti Viwavi Jeshi, Lita 2,000 za Madawa ya kudhibiti Ndege aina ya Kwelea Kwelea na Kilo 1,200 za kudhibiti Panya zilikuwa zimesambazwa katika Mikoa mbalimbali nchini. Aidha, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, imeandaa zabuni itakayowezesha kuingizwa nchini Lita 4,000 za Dawa za kudhibiti Ndege aina ya Kwelea Kwelea; Lita 7,000 za kudhibiti Nzige Wekundu; Lita 5,000 za kudhibiti Viwavi Jeshi; na Kilo 1,400 za kudhibiti Panya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maandalizi hayo ya kilimo yaliyofanyika na ili kupata ufanisi katika uzalishaji katika msimu wa kilimo wa mwaka 2011/2012, suala la usimamizi wa dhati litazingatiwa. Viongozi kuanzia ngazi ya Wizara hadi ngazi ya Vijiji, wasimamie upatikanaji, usambazaji wa pembejeo na upatikanaji wa ushauri wa kitaalam kwa wakulima wetu Vijijini. Vilevile, Wataalam wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, TAMISEMI na Halmashauri zote nchini, wanapaswa kutoka Maofisini na kwenda Vijijini kufuatilia na kusimamia kilimo mashambani. Mikoa na Halmashauri zenye Maafisa Ugani wengi katika ngazi ya Makao Makuu wahakikishe wanawahamishia kwenye ngazi ya Kata na Vijiji ili kuwasaidia kwa karibu zaidi wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, Viongozi na Jamii kwa ujumla wamekuwa wakizungumzia tatizo la ajira hasa kwa vijana. Athari za ukosefu wa ajira hususan kwa vijana ni kubwa na ni mbaya katika mustakabali wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo hili linachangia kwa kiasi kikubwa umaskini nchini kwani yeyote asiyekuwa na ajira hana kipato. Watu wasio na ajira ni rahisi kujikuta wanaishi kwa njia zisizokubalika katika jamii zikiwemo za wizi, unyang’anyi, matumizi ya dawa za kulevya, uhalifu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2001, kiwango cha ukosefu wa ajira nchini kilikuwa asilimia 12.9. Kwa matokeo ya utafiti wa Nguvu Kazi na Ajira ya mwaka 2006, Nguvu Kazi nchini ilikuwa watu milioni 18.8. Kati yao, watu milioni 2.2 walikuwa hawana ajira sawa na asilimia 11.7 ya nguvu kazi yote nchini. Makadirio ya kiwango cha ukosefu wa ajira nchini katika mwaka 2011 ni asilimia 10.7 ya nguvu kazi ya Taifa ya watu Milioni 22.2. Kwa kiwango hicho, inakadiriwa kuwa idadi ya watu wasiokuwa na ajira kwa sasa ni Milioni 2.4. Takwimu pia zinaonesha kuwa mwaka 2006 wakati wa utafiti wa Nguvukazi (*Labour Force Survey*) watu Milioni 14.9 walikuwa wameajiriwa kwenye Sekta Rasmi na watu Milioni 1.7 walikuwa wameajiriwa katika Sekta Isiyo Rasmi. Kwa mwaka 2011, inakadiriwa kuwa watu Milioni 17.3 wameajiriwa kwenye Sekta Rasmi na watu 2.5 wameajiriwa kwenye Sekta Isiyo Rasmi. Sekta ya Kilimo ndiyo inayoongoza kwa kuajiri asilimia 75 ya nguvu kazi. Sekta Isiyo Rasmi inaajiri asilimia Tisa, Serikali asilimia 2.4 na Mashirika asilimia 0.4.

Mheshimiwa Spika, utafiti unaonesha pia kuwa ukosefu wa ajira unawaathiri zaidi vijana wa umri kati ya umri wa miaka 15 hadi 24 ambao wanamaliza Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu. Aidha, tatizo hili ni kubwa zaidi kwa wanawake kuliko wanaume. Ongezeko kubwa la watu wasiyo na kazi linatokana na kasi kubwa ya ongezeko la watu wenye umri wa kufanya kazi ikilinganishwa na kasi ndogo ya ongezeko la nafasi za ajira ambalo limekuwepo kwa miaka mingi sasa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, suala hili la ukosefu wa ajira siyo la Tanzania tu, bali ni la nchi nyingi Duniani. Kwa mfano, kwa mwaka 2011, wakati kiwango cha ukosefu wa ajira Tanzania ni asilimia 10.7, nchi ya Afrika Kusini ni asilimia 25.0, Hispania asilimia 21.5, Ureno ni asilimia 12.4, Iran ni asilimia 11.5, Ufaransa ni asilimia 9.5, na Marekani ni asilimia 9 kwa kutaja mifano michache.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa mahitaji makubwa ya ajira nchini. Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008, inatambua kuwepo kwa tatizo la ukosefu wa ajira. Sera hiyo inalenga pamoja na mambo mengine kuandaa mazingira wezeshi kwa wasiokuwa na ajira kujiajiri wenyewe na kuainisha maeneo ya kiuchumi yanayoweza kukuza ajira na kuweka mikakati ya kutumia maeneo hayo kukuza uchumi. Aidha, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010, inalitambua suala hili. Katiba Ibara yake ya 77, Ilani imeelekeza kwamba:-

> *"Chama cha Mapinduzi kinatambua kwamba katika kipindi hiki suala la ajira hususan ajira ya vijana imekuwa nyeti. Hii ni kwa sababu idadi ya Vijana wanaofuzu Elimu ya Msingi, Sekondari, Vyuo na Vyuo Vikuu kila mwaka ni kubwa sana. Idadi hiyo inakuzwa pia na Vijana wanaomaliza Mafunzo ya JKT. Vijana wote hawa ni nguvukazi ya Taifa ambayo inaweza kutumika katika kazi na shughuli halali za ujenzi wa nchi". (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, Ibara ya 78 nayo inaainisha mambo yanayotakiwa kushughulikiwa na Serikali ili kujenga fursa za ajira hasa kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya juhudi kubwa kukabiliana na tatizo hili. Serikali yenyewe imekuwa ni miongoni mwa waajiri wakubwa nchini na itaendelea kuajiri vijana wengi kadri hali ya kiuchumi itakavyoruhusu.

Aidha, Serikali itaendelea kujenga mazingira ya kupunguza ukosefu wa ajira kwa kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha Sekta ya Kilimo ambayo inaajiri asilimia kubwa ya nguvukazi na kuchangia katika kutoa huduma za ardhi, kupanda, kuvuna, kutunza na kuuza mazao. Hatua nyingine ni kupanua mafunzo ya *VETA*; kupanua na kuboresha Elimu ya Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ufundi na Vyuo Vikuu na kuimarisha Mitaala ya Elimu ili Wahitimu waweze kujiajiri.

Vilevile, wananchi watahamasishwa kujiunga katika *SACCOs* na *VICOBA* na kuwawezesha kimtaji, kuweka mazingira mazuri ya kukuza Sekta Binafsi na uwekezaji na kuvutia Wawekezeji wa ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali itandelea kuwahamasisha Waajiri na wale wanaotafuta kazi kupata taarifa za hali ya Soko la Ajira.

Ningependa tukumbushane tu kuwa tunapozungumzia ajira hatuna maana ya ajira za kulipwa mishahara tu bali ni pamoja na ajira binafsi katika kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara na kadhalika. Hivyo, suala la kupunguza ukosefu wa ajira si suala la Serikali pekee bali ni pamoja na Sekta Binafsi. Kila mmoja wenu afanye kila liwezekanalo kuongeza ajira nchini. Tukiwa na dhamira ya pamoja tutaweza.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama katika nchi yetu ni shwari ikiwa ni pamoja na maeneo ya mipakani na eneo la Bahari ya Hindi, licha ya kuwepo kwa matishio ya Uharamia katika Pwani ya Nchi za Afrika Mashariki. Tarehe 3 Oktoba, 2011, Maharamia wenye asili ya Somalia walivamia ufukwe wa Bahari ya Hindi eneo la Mafia kwa lengo la kutaka kuteka meli inayotumika katika utafiti wa mafuta. Jambo hilo lilidhibitiwa na Wanajeshi wetu wa Jeshi la Wanamaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika jaribio hilo, Maharamia Saba (7) walikamatwa na hatua za Kisheria dhidi yao zinaendelea kuchukuliwa. Vilevile, kulikuwa na matukio mengine matatu ya uharamia ambapo yalidhibitiwa na hakuna madhara yoyote yaliyotokea kwa upande wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii, kulipongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi nzuri linalofanya kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa kudhibiti vitendo vya Uharamia katika Pwani ya Nchi za Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mnavyofahamu, kwa sasa katika Ukanda wa Afrika Mashariki kumekuwa na matishio ya Ugaidi, hususan katika nchi jirani. Hivi karibuni kumezuka matishio ya Kigaidi nchini Kenya kufuatia Serikali ya Kenya kufunga mpaka wake na Somalia kama njia ya kupambana na Kikundi cha Wapiganaji wa Kundi la Al-Shabab. Kutokana na hali hii, nchi yetu imeimarisha ulinzi katika mipaka yake yote ambapo Idara ya Uhamiaji imewaelekeza Maafisa Uhamiaji wa Mikoa yote na Vituo vyote vya kuingia nchini kuimarisha doria na misako katika maeneo yao ili kuzuia Wahamiaji Haramu, hususan Raia wa Somalia wengi wao wakitokea Kenya kuingia nchini. Aidha, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na Vyombo vingine vya Dola wameweka mikakati ya kukubaliana na tishio hili, ikiwa ni pamoja na kuweka Boti za Doria katika Pwani ya Bahari ya Hindi na Askari wa Doria katika maeneo ya Mipakani.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa Watanzania wote, hasa wale wanaoishi maeneo ya mipakani mwa nchi yetu kutoa taarifa katika Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama pale watakapoona mtu au watu ambao nyendo zao zinatia mashaka. Aidha, niwatake Viongozi wa Serikali za Mitaa na Vijiji kuendelea na zoezi la kuhakiki watu katika maeneo yao na kuchunguza watu wanaokuja na kuishi katika Vijiji na Mitaa yao bila ya kutoa taarifa kwa Viongozi wa maeneo hayo. Kazi ya kulinda nchi yetu na mipaka yetu itafanikiwa endapo wananchi wote watashirikiana kwa karibu na Vyombo vya Ulinzi na Usalama na kutoa taarifa pale inapobidi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007, nchi yetu ilikumbwa na tatizo la imani za kishirikina kwamba Viungo vya Watu Wenye Walemavu wa Ngozi (Albino) vinaweza vikaleta utajiri. Imani hiyo potofu ilisababisha kuibuka kwa kasi kwa vitendo vya mauaji na unyama wa kukata viungo vya Ndugu zetu Walemavu wa Ngozi. Vitendo hivyo vilisikitisha sana, kuona watu wachache kwa tamaa za kupata utajiri wanawageuza binadamu wenzao kama wanyama. Suala hili lilichafua jina na sifa ya Tanzania ambayo siku zote imekuwa ni nchi ya amani, umoja na mshikamano.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, Taasisi mbalimbali za Ndani na Nje ya Nchi na Madhehebu ya Dini kwa pamoja tulisimama kidete kupambana na vitendo hivyo. Vilevile, Serikali kupitia Vyombo vya Dola ilichukua hatua kali dhidi ya wahusika. Kwa kuzingatia hilo, watuhumiwa 94 walikamatwa na Kesi 11 za mauaji ya Walemavu wa Ngozi zilifikishwa Mahakamani na kati ya hizo, Kesi Tisa (9) zimekwisha kusikilizwa na Kesi Sita (6) zimeshatolewa hukumu ambapo Watuhumiwa Nane (8) wamehukumiwa Kunyongwa. Kutokana na jitihada hizo, matukio ya mauaji na kujeruhiwa kwa Walemavu wa Ngozi yalionekana kupangua sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali, bado hivi karibuni kumeripotiwa matukio mawili ya uhalifu yaliyohusisha kukatwa kwa viungo vya watoto wawili Wenye Ulemavu wa Ngozi kwa nyakati tofauti. Matukio hayo yalitokea Mikoa ya Mwanza na Shinyanga ambapo tarehe 14 Oktoba, 2011, mtoto wa Darasa la Tatu, Adam Robert, mwenye umri wa miaka 13, mkazi wa Kijiji cha Nyaluguguna, Kata ya Nyijuda, Wilayani Geita alivamiwa na kukatwa vidole vitatu vya mkono wa kulia mbele ya wazazi wake na mhusika kutoweka navyo. Katika tukio la pili, tarehe 22 Oktoba, 2011, Mtoto Kulwa Lusana, mwenye Miaka 16, mkazi wa Kijiji cha Mbizi, Kata ya Mega Wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga, naye alikatwa mkono wa kulia na mhusika kutoweka nao. Watoto hawa wanaendelea kupata matibabu, mmoja katika Hospitali ya Wilaya ya Geita na mwingine Hospitali ya Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Spika, katika matukio haya mawili watu wa karibu na majeruhi hawa wanahisiwa kuhusika kwa namna moja au nyingine na matukio haya wakiwemo wazazi wao ambao wamekamatwa na upelelezi wa mashauri yao unaendelea. Unyama huu unaofanywa na watu wachache, wenye uchu wa utajiri wasiokuwa na utu, unachafua sana jina la Tanzania Duniani kote na kudhalilisha Watanzania wote. Hivyo, naomba kutoa wito kwa wadau wote kwamba tuendelee kukemea vitendo hivi na kuvilaani na kuhakikisha uhalifu huo unatokomezwa. *(Makofi)*

Tuwasihi na kuwaomba sana Watanzania katika maeneo yote ambako matukio haya yanatokea, washirikiane na Vyombo vya Dola kutoa taarifa za kweli ili wale wote wanaohusika waweze kukamatwa na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria

Mheshimiwa Spika, naomba kusisitiza tena kwamba Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi ni binadamu kama walivyo binadamu wengine. Wanastahili haki ya kuishi kwa amani na kufurahi katika nchi yao. Hakuna mtu, kikundi chochote ambacho kina haki ya kumfanya Mlemavu wa Ngozi aishi kwa wasiwasi au kwa hofu katika nchi yake kwa sababu yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, narudia kuvisisitizia Vyombo vya Dola kuongeza nguvu katika kuhakikisha vitendo vya uhalifu dhidi ya Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi vinadhibitiwa ipasavyo na wadau wote tushirikiane kuhakikisha Ndugu zetu hawa wanalindwa.

Aidha, naomba kutoa wito kwa wananchi wote, wazazi, vijana na wadau wengine kwamba suala la ulinzi wa Ndugu zetu Walemavu wa Ngozi ni letu sisi wote. Ni wajibu wa kila mmoja wetu kutoa taarifa juu ya watu wanaonesha kuwa na mwenendo unaotia mashaka kuhusiana na Ndugu zetu hawa. Tunahitaji ushirikiano katika suala hili, hata kama wanaohisiwa ni wazazi, tafadhali toeni taarifa. Viongozi wa Madhehebu mbalimbali ya Dini, Viongozi wa Serikali na Wazee Maarufu, katika maeneo yenu, endeleeni kukemea imani hii potofu inayosababisha mauaji ya Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi na kuwaeleza madhara ya imani za kishirikina kwa Ndugu zetu hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge kutoka Kanda ya Ziwa ambako ndiyo mauaji haya yanajitokeza mara kwa mara na nguvu sana, tumieni nafasi zenu wakati mtakapokuwa mnafanya ziara katika Vijiji kutoa elimu kwa wananchi waache uhalifu huu ambao hauna maana na kwa kweli ni kosa kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Vilevile, Viongozi wa Serikali za Mitaa, nao wana jukumu la kubaini Makazi ya Walemavu wa Ngozi na kujaribu kuwasaidia kuwapatia ulinzi kila itakapowezekana. Ni muhimu kupata namba za simu za wazazi/walezi wao ili waweze kufuatiliwa. Kwa upande wa Ndugu zetu Walemavu wa Ngozi, nawaomba ninyi pia toeni taarifa pale mnapoona kufuatwafuatwa na watu ambao mnahisi wana nia mbaya au za kutia mashaka.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote tunafahamu na kutambua kuwa Timu yetu ya Taifa ya Mpira wa Miguu – *TAIFA STARS*, ilicheza na Timu ya Taifa ya Chad huko N'djamena, Chad tarehe 11 Novemba, 2011. Matokeo ya mechi hiyo yalikuwa ni ushindi kwa timu yetu kwa kuifunga timu ya Taifa ya Chad Mabao 2-1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mechi ya marudiano ilifanyika Uwanja wa Taifa, Dar es Salaam tarehe 15 Novemba, 2011 na matokeo yalikuwa Chad 1 na Tanzania 0. Hata hivyo, kwa matokeo hayo, bado Timu ya Taifa imefaulu kusonga mbele na hivyo kuingia katika kundi C ambalo lina Timu za Morroco, Ivory Coast na Gambia. Mechi hizo ni muhimu sana kwa Taifa kwa kuwa ni maandalizi ya kufuzu kwa fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Brazil mwaka 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Timu yetu imefuzu kuingia katika Makundi, lakini ukweli ni kwamba safari yetu bado ni ngumu na ndefu. Timu tulizopangwa nazo ni ngumu na ni magwiji wa Soka Barani Afrika. Ili kukabiliana na Timu hizo na kupata ushindi, tunahitaji maandalizi ya kutosha na michezo ya kujipima nguvu kwa Timu yetu. Naomba kuwaasa vijana wetu kuwa, hata kama tungekuwa na Kocha mzuri kama kiasi gani, lakini kama hawatafanya mazoezi ya kutosha, kujituma kwa hali na mali, kutambua kuwa wanabeba Bendera ya Taifa, bado ushindi utakuwa mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa mechi za ugenini na zile ya nyumbani, Timu yetu inahitaji kutiwa moyo, kusaidiwa kisaikolojia na zaidi ya yote kuungwa mkono kifedha ili iweze kushinda. Niwasihi Watanzania

wenzangu tuiunge mkono Timu yetu ya Taifa kwani ushindi wa Timu yetu ni ushindi wa Taifa; ni ushindi wa Watanzania wote, ni njia ya kuitangaza Tanzania Duniani na sote kama Watanzania tutapata sifa na kujivunia ushindi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba Watanzania, kila mmoja kwa nafasi yake, tuisaidie Timu yetu kwa hali na mali ili iweze kuibeba na kuipeperusha bendera ya Tanzania kwa ujasiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee sana, kupitia Bunge lako hili Tukufu, Bunge ambalo najua lina Wabunge wapenzi sana wa mpira, tukuombe kupitia kwako Mheshimiwa Spika kama itakupendeza basi tufanye uamuzi wa pamoja tuone ni namna gani tunaweza tukachangia Timu hii kifedha ili waweze kuwa na muda zaidi wa kufanya mazoezi katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Mlima Kilimanjaro ambalo nalo pia haliwezi kuachwa hivihivi. Tutakumbuka kuwa miezi ya karibuni kulikuwa na kampeni ya kuupigia kura Mlima Kilimanjaro ili uweze kuchanguliwa na kuwa miongoni mwa Maajabu Saba Mapya ya Dunia. Kulikuwa na vivutio 28 vilivyochaguliwa kutoka vivutio 77 kutoka nchi 220 zilizoshindanishwa mwaka 2007. Tangu Julai 2009, kura zilikuwa zikipigwa na hatima yake ilikuwa ni tarehe 11 Novemba, 2011. Matokeo rasmi ya kura hizo yatatangazwa mwanzoni mwa mwaka 2012 lakini katika matokeo ya awali, Mlima Kilimanjaro haukupata nafasi ya kushinda na kuwemo katika Maajabu Saba ya Dunia. Hata hivyo, ulipata nafasi ya kupita katika mchujo wa kwanza na kuwa miongoni mwa vivutio 14 kati ya 28, vilivyoshinda kura za awali. Hili ni jambo la kujivunia na naomba nitumie fursa hii kuwashukuru Watanzania wote ambao walishiriki kutuma ujumbe mfupi wa maneno ama *emails* zao kuupigia kura Mlima Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Maajabu hayo Saba yalikuwa yameamuliwa kwa kura, ninaamini na ni maoni yangu kuwa Watanzania wengi hawakutumia nafasi hiyo vizuri kuupigia Mlima Kilimanjaro kura. Aidha, taarifa ya kushindanishwa kwa Mlima Kilimanjaro hazikutolewa na kutangazwa mapema na Wizara yenye dhamana na Taasisi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni changamoto kwetu sote lakini zaidi kwa Wizara ya Maliasili na Utalii ambayo kimsingi ilikuwa na jukumu la kuwa mstari wa mbele katika kuwaelimisha wananchi kuhusu mashindano hayo tangu suala hili lilipojulikana mapema mwezi Julai 2011. Lazima nikiri, hatukuwa tumewatendea haki Watanzania kwa kutokulichukulia jambo hili kwa uzito unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na kwamba hatukupata nafasi, naomba nichukue nafasi hii kuzipongeza Kampuni za Simu za *Airtel* na *VODACOM* kwa kukubali kufanyakazi na Serikali, kufikisha ujumbe kwa Watanzania kuhusu kuupigia Kura Mlima Kilimanjaro. Matarajio yangu ni kwamba Kampuni zingine nazo zitashiriki katika maeneo mengine ya maendeleo kwa nyakati zijazo endapo fursa kama hii itajitokeza.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza wananchi wote wa ndani na nje walioitikia wito wa kuupigia Kura Mlima Kilimanjaro. Aidha, nitumie fursa hii kuzitaka Wizara zote kujipanga vizuri wakati wote tunapotokeza Mashindano ya Kimataifa katika Sekta zao kwa kuweka Uzalendo mbele na kuweka maslahi mapana zaidi na kuwa tayari kuipigania nchi yao kwa hali yoyote ile. Ufahamu wa wananchi upewe kipaumbele na wananchi washirikishwe kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo makubwa ambayo kwa sasa Serikali inayafanyia kazi ni kutekelezwa kwa Mradi wa Vitambulisho vya Taifa. Mapema mwaka huu, Serikali ilisaini mkataba na mkandarasi aliyeshinda zabuni za kutengeneza vitambulisho vya Taifa. Hivyo, kazi kubwa iliyoko mbele yetu sasa ni kutengeneza mfumo wa kuweka utaratibu mzuri wa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa ili wananchi waweze kusajiliwa na hatimaye kupewa vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, mradi huu una faida nyingi kisiasa, kiuchumi, kiusalama, kiulinzi na kijamii na zipo faida kumbwa ambazo tunaweza kuzitaja kama ifuatavyo:-

(i) Utaratibu huu utasaidia kuboresha Daftari la Wapiga Kura. Iwapo zoezi la kutoa Vitambulisho vya Taifa litakamilika kama ilivyopangwa, Serikali itapunguza gharama zinazotumika katika kuboresha Daftari la Wapiga Kura kwani tayari tutakuwa na taarifa za Watanzania wenye sifa za kupiga kura. Vivyo hivyo, tatizo la

kughushi kadi ya kupigia kura litakwisha kwani kitambulisho kitaweza kutambulisha uhalali wa mtu kupiga kura au la. *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa Serikali sasa iko katika maandalizi ya utekelezaji wa zoezi la sensa litakalofanyika mwezi Agosti, 2012, kuwepo kwa Vitambulisho vya Taifa, kutahuisha takwimu za sensa kwani mbali ya kujua idadi, Taifa kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa litakuwa na idadi kamili ya Watanzania, shughuli zao na mahitaji yao ya msingi na hivyo kuirahisishia Serikali kazi katika kuweka mipango yake vikiwemo vipaumbele vya huduma za jamii.

(iii) Mfumo huu utauongezea Serikali wigo wa ukusanyaji mapato na hivyo kuboresha huduma muhimu za kijamii kama vile afya, elimu pamoja na ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

(iv) Kuanzishwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao hivi sasa ni muungano wa nchi tano ambazo ni Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda, kumeongeza kwa kiasi umuhimu wa kuwa na vitambulisho. Aidha, kuna makubaliano kwamba wananchi wa nchi hizi wawe wanaweza kutembeleana bila vikwazo na bughudha kwa kutumia Kitambulisho cha Uraia. Tanzania na Uganda ndizo nchi pekee katika Jumuiya ambazo hazina Vitambulisho vya Taifa. Hata hivyo, tayari nimearifiwa kwamba Uganda nao wameshaanza mchakato wa kuwa na vitambulisho vyao.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa nilizonazo, Vitambulisho vya kwanza vitatolewa kuanzia mwezi Aprili mwaka kesho wakati wa Maazimisho wa Sherehe za Muungano. *(Makofi)*

Ombi langu kwenu Waheshimiwa Wabunge, Viongozi wa Vyama vya Siasa na wananchi kwa ujumla, ni kuunga mkono jitihada hizi za Serikali na kuelimisha umma faida ya zoezi hili kiuchumi, kisiasa na kijamii. Suala la Kitambulisho cha Taifa halina Chama wala itikadi. Hivyo suala hili ni Taifa zima. Sisi sote tuungane pamoja kuhakikisha kwamba mafanikio ya zoezi hili yanapatikana kwa wakati uliopangwa.

Vilevile, niwaombe Watendaji wote kuanzia Serikali za Mitaa, ngazi za Vijiji, Kata, Wilaya, Mikoa hadi Taifa, kuwa wazalendo katika kuthibitisha nani ni Mtanzania na nani si Mtanzania kwa kutoa taarifa sahihi bila uonevu na kuzingatia misingi ya haki na sheria. Napenda kuwaasa Watanzania wote kuwa wakweli wakati wote wa kuandikisha na kutoa Vitambulisho ili kujiepusha na madhara ya udanganyifu na hatua kali zitachukuliwa kwa wale wote watakaobainika kudanganya zoezi hili. Nalisema hili kwa msisitizo mkubwa hasa kwa upande wa Mikoa iliyo mipakani, Mikoa ya Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Mara na Mikoa mingine ambayo imepakana na nchi jirani. Zoezi hili kwetu ni lazima tulipe uzalendo wa hali ya juu sana ili tuweze kuwa na uhakika nani anaishi miongoni mwetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, itafanya sensa ya watu na makazi, mwezi Agosti, 2012. Sensa hii itakuwa ya tano tangu tulipopata uhuru mwaka 1961. Sensa zilizotangulia zilifanyika mwaka 1967, 1978, 1988 na mwaka 2002. Lengo kubwa la sensa ya mwaka 2012, ni kuchangia katika uboreshaji wa maisha ya Watanzania kwa kutoa takwimu sahihi na kwa wakati kwa ajili ya kupanga mipango ya maendeleo. Taarifa hizi zitasaidia katika kutathmini na kufuatilia utekelezaji wa mipango na programu za maendeleo kama ifuatavyo:-

(i) Kutoa takwimu za idadi ya watu, taarifa za kiuchumi na kijamii katika ngazi zote za Mipango;

(ii) Kutathmini utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 na ile ya Zanzibar ya mwaka 2020;

(iii) Kutumika katika kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) – Tanzania Bara na MKUZA – Tanzania Zanzibar);

(iv) Kutumika kutathmini hali ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia ifikapo mwaka 2015;

(v) Kusaidia Serikali kufanya tathmini juu ya ongezeko la idadi ya watu, makazi yao, shughuli zao na athari zake kwa mazingira ili kuwezesha kuweka sera na mipango madhubuti ya uboreshaji wa Makazi ya watu na utunzaji wa mazingira na pia kusaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa kuainisha mahitaji halisi ya miundombinu na huduma nyingine za Kijamii kama vile Jiji la Dar es Salaam na Miji mingine; na

(vi) Kuimarisha utawala bora na ukuaji wa demokrasia nchini kwa kutumia takwimu hizo katika kuamua mipaka mipya ya Majimbo ya Uchaguzi pamoja na mipaka mingine ya kiutawala.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya sensa hii yalianza mwaka 2004 kwa kazi ya kutenga maeneo ya kuhesabia watu yajulikanayo kitaalamu kama *Enumeration Areas*. Lengo kubwa la kazi hii ni kuitenga nchi nzima katika maeneo madogo madogo ya kuhesabia watu ili ifikapo mwezi Agosti 2012 watu wote watakaolala nchini waweze kuhesabiwa mara moja tu. Hadi mwezi Oktoba 2011, kazi hii ilikuwa imeshakamilika kwa 85% na inategemewa kukamilika mwezi Februari, 2012 kama ratiba ya sensa inavyoonesha.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine ambayo imekamilika ni sensa ya majaribio iliyofanyika mwezi Oktoba, 2011 ambayo ilikuwa na lengo la kutathmini utendaji na muundo mzima wa kuendesha zoezi la sensa mwakani. Lengo lingine la zoezi hilo lilikuwa kutathmini mtiririko mzima wa maswali yatakayoulizwa kwa watu wote watakaolala nchini usiku wa kuamkia usiku wa sensa pamoja na teknolojia ya kisasa itakayotumika katika uchambuzi wa takwimu.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa tuliyo nayo tangu Serikali ianze maandalizi ya sensa hii mwaka 2004 ni gharama kubwa itakayotumika kujipanga kuhesabu watu na kuchukua taarifa zao muhimu zikiwemo taarifa za umri, uraia, elimu, hali ya kazi, uzazi, vifo, hali ya ulemavu na mahali waliposhinda kwa muda usiopungua siku tatu na hususan katika miji mikubwa. Serikali imejipanga kutenga rasilimali fedha za kutosha na kupata rasilimali watu ambao ni Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Lengo ni kujihakikishia kuwa wananchi hawapotezi muda mrefu kuwasubiri Makarani wa kuhesabu watu kuwatembelea katika kaya zao, hususan katika Jiji la Dar es Salaam. Serikali itajipanga vizuri kupitia Kamati Kuu ya Sensa ambayo inajumuisha Wizara zote na hususan Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuona namna ya kuweza kuwapata Walimu watakaohitajika.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kuwepo kwa baadhi ya sehemu nchini ambazo hazifikiki kwa urahisi, hasa sehemu zenye miinuko mikali, wanyama wakali, visiwa vingi vinavyokaliwa na wavuvi na sehemu zenye watu wanaohamahama. Juhudi zitafanyika kuandaa namna bora ya kufika sehemu hizo kwa kutumia nyenzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia ndege, magari maalum na vyombo vya kuaminika vya majini.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi kwa kushirikiana na Serikali katika hatua tuliyofikia ya maandalizi ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. Pia niwaombe tena, kuendelea na ushirikiano huo wa kuhakikisha sensa ya mwaka 2012 inafanikiwa ili kuiwezesha Serikali kupanga mipango endelevu ya maendeleo. Wito wangu kwa Waheshimiwa Wabunge wote ambao mpo karibu na wananchi ni kuwaomba kuwaelimisha wananchi katika Majimbo yenu kuhusu umuhimu wa sensa ya watu na makazi ili waweze kushiriki kwa kikamilifu katika sensa hii. Aidha, niwakumbushe Wakuu wa Mikoa na Wilaya kutimiza wajibu wao kama wasimamizi wakuu wa zoezi hili katika Mikoa na Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeridhia kujiunga na mpango wa ubia katika uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa uwazi yaani "*Open Government Partnership*". Mpango huu ambao ni juhudi mpya za kimataifa katika kuendesha Serikali kwa uwazi na ushirikishwaji mkubwa wa wananchi, ulizinduliwa rasmi na viongozi wa nchi za Marekani, Brazil, Indonesia, Mexico, Norway, Philippines, Afrika ya Kusini na Uingereza mnamo tarehe 20 Septemba, 2011, wakati wa Mkutano wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa huko New York, Marekani. Msisitizo mkubwa wa mpango huu ni kuongeza uwazi na uwajibikaji katika Serikali, kuwawezesha wananchi kupata taarifa sahihi na kuzitumia kwa maendeleo yao, kuzuia na kupambana na rushwa na ubadhirifu na wizi wa mali ya umma na kusisitiza matumizi ya teknolojia na ubunifu katika kuimarisha utawala bora. Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Nne imeamua kutekeleza kwa uwazi shughuli zake, tumedhamiria kushirikiana na wadau katika ngazi zote kuhakikisha kwamba habari muhimu za utendaji wa Serikali zinatolewa kwa wananchi na kuwashirikisha katika kufuatilia na kutoa taarifa katika ngazi husika pale wanapoona utendaji hauridhishi.

Mheshimiwa Spika, ili kuwa mwanachama wa mpango huo, nchi zinatakiwa kuunga mkono azimio la uwazi katika kuendesha Serikali; kuandaa mpango kazi kwa kushirikiana na wananchi na kuweka utaratibu wa uwazi wa kutoa taarifa za utekelezaji wa mpango kazi huo. Napenda kupitia Bunge lako Tukufu kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania wote kwamba maandalizi ya mpango kazi shirikishi umeanza kwa kushirikisha wadau mbalimbali. Tayari Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Utawala Bora amezungumza na Waandishi wa Habari na kueleza kwa undani kuhusu mpango huo. Vilevile, tarehe 15 Novemba, 2011, Serikali ilikutana na wadau kutoka sekta binafsi na asasi za kiraia ambapo kwa pamoja walijadili kwa uwazi aina ya mpango kazi wa kitaifa

wanaoutaka na kubainisha maeneo ya kuanzia ili kutekeleza mpango huo kwa uwazi. Mawasiliano zaidi na wananchi yataendelea kupitia njia za barua za kawaida, barua pepe, simu za mkononi na tovuti ambazo anwani zake zimeshatolewa kwa wananchi. Nawasihi wananchi washiriki kikamilifu kutoa maoni yao kwa uwazi ili hatimaye tuwe na mpango kazi wa kitaifa kwa manufaa yetu wote.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine naomba kupitia Bunge lako Tukufu kuwaomba waheshimiwa Wabunge, Serikali itakapowasilisha mpango huo kwenu tuujadili kwa uwazi zaidi na tuweze kuboresha kwa kadri itakavyowezekana ili tuweze kweli kukidhi mahitaji ya mpango kama ambavyo tumedhamiria kuufanya. Lengo ni kuendesha shughuli zetu kama Serikali kwa uwazi mkubwa zaidi kuliko ilivyo sasa. Nataka niwahakikishie Watanzania kwamba, maoni yenu yataheshimiwa na kuzingatiwa ipasavyo katika Mpango huo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolielezea Bunge lako Tukufu wakati wa Hotuba yangu ya Bajeti mwezi Juni 2011, Serikali imedhamiria kwa dhati kupambana na tatizo la lishe duni hapa nchini. Katika kutekeleza azma hiyo, tarehe 20 Septemba, 2011, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, aliungana na viongozi mbalimbali duniani kujadiliana juu ya kuboresha lishe hasa kwa nchi zinazoendelea. Katika Mkutano huo, viongozi hao walionesha dhamira ya kushirikiana na Serikali yetu ili kuongeza kasi ya kupambana na tatizo la lishe duni hasa kwa siku 1,000 za kwanza za maendeleo ya mtoto muda ambao kitaalam ni muhimu sana katika maendeleo yote ya msingi ya binadamu. Aidha, tarehe 19 Septemba, 2011, nilizindua mkakati wa kitaifa wa lishe ambao utakuwa ndiyo dira ya kutekeleza shughuli zote za kuboresha lishe hapa nchini. Hivi sasa unaandaliwa mpango wa utekelezaji wa mkakati huo utakaoweka malengo na viashiria vitakavyopimika na kuongoza ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia watanzania wote kwamba, suala la kuboresha lishe linapewa umuhimu mkubwa na kuanzia Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, kasma maalum ya lishe itaanzishwa kwenye bajeti zetu. Nataka niwasihi wananchi kushirikiana na Serikali katika ngazi zote, ili kukabiliana na tatizo hili la lishe duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Waheshimiwa Wabunge na wananchi wanavyofahamu tarehe 9 Desemba 2011, Taifa letu litahitimisha maadhimisho ya miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara kwa uzito unaostahili. Maadhimisho hayo yalianza mwezi Juni mwaka huu, ambapo Wizara, Taasisi, Mikoa pamoja na sekta binafsi zimekuwa zikifanya Maonesho kwenye maeneo yao na sehemu mbalimbali nchini kuelezea mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizojitokeza pamoja na matarajio ya miaka 50 ijayo kwa ajili ya kumbukumbu ya vizazi vijavyo. Utaratibu huo unafanyika kwa zamu baina ya Wizara na Mikoa na utaendelea hadi tarehe 30 Novemba 2011. Kuanzia tarehe 1 hadi 9 Desemba 2011, maonesho hayo yatahamia uwanja wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Dar es Salaam ambapo Wizara zote, Taasisi pamoja na wadau wengine watashiriki.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa mara nyingine tena kuwatakia Watanzania wote kheri na mafanikio katika kuadhimisha sherehe za Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Nawaomba wananchi kuendelea kutembelea maonesho yanayofanyika kwa sasa katika sehemu mbalimbali nchini ili kujielimisha juu ya mafanikio tuliyopata katika kipindi cha miaka 50 ya Uhuru wetu wa Tanzania Bara pamoja na kutambua changamoto zake. Tutambue kuwa tuna kila sababu kama Taifa kujivunia maendeleo tuliyoyapata kwa miaka 50 kwa kuwa tumethubutu, tumeweza na dhamira yetu kwa kweli ni kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha hotuba yangu kwa kurejea machache kama ifuatavyo: -

Kwanza, tunayo kazi kubwa iliyoko mbele yetu ya kuunganisha nguvu kukabiliana na athari za msukosuko wa uchumi duniani kwa kujenga uchumi tulivu na kuhakikisha kuwa tunadhibiti mfumuko wa bei na kushuka kwa thamani ya shilingi. Tushirikiane wote katika kila nyanja zikiwemo Taasisi za Fedha kwa kutekeleza maelekezo yatakayotusaidia kukabiliana na matatizo hayo.

Pili, jukumu la kuandaa Katiba ni letu sote Watanzania bila kujali kabila, rangi, jinsia, dini ama itikadi za kisiasa na vyama. Kwa hili, Watanzania wote tuungane kulinda umoja wetu, amani yetu, utulivu wetu na mshikamano wetu uliodumu kwa miaka 50 ya uhuru wetu. *(Makofi)*

Tatu, tumeanza vizuri katika maandalizi ya msimu wa kilimo wa mwaka 2011/2012. Tuwahimize wakulima na wote wanaohusika na upatikanaji na usambazaji wa mbolea, mbegu na pembejeo kuhakikisha kwamba

zinawafikia wakulima kwa wakati. Tuwahimize wakulima kutumia mvua zilizoanza kunyesha katika baadhi ya maeneo nchini kwa kupanda mapema, kwani mvua za kwanza ni za kupandia. *(Makofi)*

Nne, tunalo jukumu la kuvutia na kufanya uwekezaji mkubwa katika nchi yetu. Nawaomba tuunganishe nguvu zetu kutangaza fursa zilizopo kikanda kwa ajili ya uwekezaji katika maeneo yetu. Kila Mkoa utenge ardhi kwa ajili ya uwekezaji na kutangaza fursa zilizopo kikanda ili kuleta msukumo wa pamoja katika kuvutia wawekezaji kwenye maeneo hayo.

Tano, bado tunalo tatizo la vitendo vya uhalifu nhini, ikiwa ni pamoja na uhamiaji haramu na uhalifu kwa Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi. Nawaomba wananchi wote kushirikiana na Vyombo vya Dola kuongeza nguvu katika kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa. *(Makofi)*

Sita, Serikali imefikia hatua za mwisho za kukamilisha zoezi la kuandaa Vitambulisho vya Taifa. Tushirikiane kuwaelimisha wananchi umuhimu wa suala hilo ambalo halina Chama wala itikadi. Tuungane kuhakikisha kwamba mafanikio ya zoezi hili yanapatikana na kila Mtanzania anapata haki yake kwa kupata Kitambulisho cha Taifa. *(Makofi)*

Saba na mwisho, maandalizi ya sensa itakayofanyika mwezi Agosti 2012 mwaka kesho yanaendelea. Tushirikiane kuwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa zoezi hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwashukuru wote waliofanikisha Mkutano huu wa Tano wa Bunge. Nikushukuru kipekee wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa kutuongoza vizuri ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu. Namshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake kwa huduma mbalimbali ambazo zilifanikisha mkutano huu. *(Makofi)*

Ninawashukuru Maafisa wote wa Serikali pamoja na Madereva waliotuleta hapa salama na ambao watatururudisha kwenye maeneo yetu ya makazi na kazi. *(Makofi)*

Mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, ninaushukuru uongozi wa Mkoa wa Dodoma na Vyombo vya Dola kwa kutuangalia vizuri tangu tulipofika hapa Mkoani. *(Makofi)*

Nivishukuru kwa namna ya pekee Vyombo vya Habari ambavyo vimeendelea kurusha taarifa zote wakati wa kipindi chote cha Bunge hili, kwenu ninyi wote nasema ahsanteni sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii sasa kuwatakia wote safari njema kurudi katika maeneo yenu ya kazi. Vilevile, niwatakie wote maadhimisho mema ya miaka 50 ya Uhuru, sikukuu njema ya Krismas na kheri ya mwaka mpya wa 2012. Ninamwomba Mwenyezi Mungu atufikishe sote salama mwaka 2012 ili tuweze sote kukutana katika Mkutano wa Sita wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi siku ya Jumanne, tarehe 31 Januari, 2012, saa tatu asubuhi, litakapokutana katika Mkutano wa Sita hapa Mjini, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake ndefu na mimi pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa ushirikiano mlionipa katika kipindi chote hiki na ninawashukuru Wenyeviti wote, Wajumbe wa Tume ya Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote, tuondoke hapa kama ndugu, marafiki na watu ambao tunaweza kufanya kazi kwa pamoja bila mashaka yoyote. *(Makofi)*

Niwatakie kwanza sikukuu njema ya Jamhuri, niwatakie kheri ya Krismasi na mwaka mpya. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, tusimame tuimbe Wimbo wa Taifa.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Walisimama*
*na Kuimba Wimbo wa Taifa)*

*(Saa 9.45 Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 31 Januari, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*